

WAEBRANIA

na

Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Cornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders East Africa, Inc.
714 S. Summit St., Appleton, WI 54914
+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

2026

Dhumuni kuu la kitabu cha Waebrania ni ukuu wa kipekee wa Kristo: Yeye ni “mng’ao wa utukufu wake [Mungu] na uwakilishi halisi wa asili Yake” (Ebr. 1:3). Yeye siyo tu “aliumba ulimwengu” (Ebr. 1:2) lakini “hushikilia vitu vyote kwa nguvu ya Neno lake” (Ebr.1:3). Ni yeye ndiye “aliyefanya utakaso wa dhambi [na ame] keti mkono wa kuume wa Ukuu mbinguni” (Heb 1:3). Yeye ni “mrithi wa vitu vyote” (Ebr 1:1). Kwa hiyo, yeye ni mkuu kuliko malaika na Musa. Dhabihu aliyotoa ni kuu pasipo ulinganifu kuliko dhabihu zote zilizotolewa chini ya sheria ya Musa. Agano jipya ambalo Kristo alilianzisha ni kuu Zaidi kuliko Agano la Kale la Musa, ambalo sasa muda wake umeisha. Kristo ni kuhani wetu mkuu. Yeye ni utimilifu wa Agano lote la Kale, ambalo lilikuwa kivuli chake Yeye mwenyewe. Tukiwa tunajua hivyo, tunapaswa kuhusisha Agano Jipya na wokovu anaoutoa Yesu katika Maisha yetu kwa njia ya Imani. Tunatiwa moyo kuiishi Imani hiyo, hasa hasa katika utumishi na upendo wetu kwa wengine, na kuvumilia kwa sababu mateso na magumu hutumiwa na Mungu kutufundisha sisi na ni alama zinazotutambulisha ya kwamba sisi ni Watoto wake.

YALIYOMO

I. UTANGULIZI…..…….....2
A. Mwandishi……..…….....2
B. Tarehe……..…..….2
C. Usuli…….…….....….3
D. Maudhui……..……..3
E. Dondoo……..…….....4

II. ITIFAKI YA KITABU CHA WAEBRANIA.…….…….....5

I. Ukuu wa Kristo (1:1—2:18)……..…….…….....5
MASWALI YA MJADALA…….…..12

II. Kristo kuhani wetu mkuu wa pekee (3:1—8:5)……..….13
MASWALI YA MJADALA……....41

III. Agano Jipya ni bora kuliko Agano la Kale kwa sababu ya dhabihu ya Yesu Kristo.
(8:6—10:18) ……..….42
MASWALI YA MJADALA…….....50

IV. Tunadhihirisha Agano Jipya kwenye Maisha yetu kwa njia ya Imani (10:19-13:19)……..…..50
MASWALI YA MJADALA ……..….74

V. Hitimisho (13:20-25)…….…….....76
MASWALI YA MJADALA ……..….77

BIBLIOGRAFIA……..…..…..77

MWANDISHI…….….82

I. UTANGULIZI

A. Mwandishi

Katika kitabu cha Waebrania, mwandishi hakutajwa kwa jina. Kumekuwa na mabishano ya muda mrefu kuhusu mwandishi wa kitabu hiki. Rejea ya awali tuliyonayo kuhusu mwandishi wa kitabu ni kutoka kwa Clement wa Alekzandria. (tak.150-215) aliyedai kuwa mwandishi ni Paulo. Mtazamo huu ulikubaliwa na Origen (185-253), aliyekuwa mrithi wake kwa Kanisa la Mashariki, na wengine wengi, wakiwepo wanaojulikana sana miongoni mwa Watu wa Matengenezo, John Owen, na Kanisa Katoliki la Roma. Kwa upande mwingine, katika kanisa la Magharibi, Irenaeus (tak.125-202) na Hipoliti (tak.170-235) walipinga na kusema kuwa Paulo hakuwa mwandishi. Tertullian (155-220) aliweka msimamo kuwa Barnabas ndiye aliyeandika kitabu hiki. Mwishowe, pamoja na mashaka, wote wawili Jerome (tak.342-420) na Augustine (354-430) walikubali kuwa Paulo ndiye mwandishi, na wengi wa Magharibu walifuata msimamo huo. Wakati wa matengenezo ya Kanisa, Luther alitoa maoni yake kwamba Apolo ndiye mwandishi, na Calvin alitoa maoni kwamba Luka au Clement wa Roma na Wanazuoni wa kisasa hukataa Uandishi wa Paulo wa kitabu hiki (tazama Carson na Moo 2005: 600-4; Guthrie 1983: 17-22; Marshall, Travis, na Paulo 2002: 244-45; Morris 1981: 6-7; Owen 1969: 67-95).

Kuna sababu zinafanya ionekane kwamba mwandishi siyo Paulo. Sababu hizo tofauti ni matumizi ya maneno magumu, mtindo wa kiyunani, stadi za semi na muundo wa mawazo kati ya kitabu hiki na nyaraka za Paulo zisizo na shaka (Carson and Moo 2005: 602; Eusebius 1890: 6.25.11, akimnukuu Origen; Guthrie 1983: 20; Morris 1981: 6). Kwa mfano, usemi "Kristo Yesu" haujakutumika kabisa kwenye kitabu hiki, ambapo Paulo ameutumia mara 90; vile vile, semi "ndani ya Kristo" au "katika Kristo Yesu" hazijitokezi, ambapo Paul ametumia semi hizo mara 88. Zaidi ya hayo, uandishi wa Paulo huwa na salamu ambazo humfunua yeye kama mwandishi mwanzoni kabisa mwa waraka; salamu ya namna hiyo hatuioni kwenye waraka wa Waebrania. Ukuhani mkuu wa Yesu ambao ni kiini cha kitabu cha Waebrania, hatuuoni katika nyaraka zinazofahamika za Paulo, na msisitizo wa kuinuliwa kwa Yesu kupita ufufuo wake hauendi sawa na msisitizo wa Paulo mahali pengine (Carson and Moo 2005: 602; Guthrie 1983: 19-20; Marshall, Travis, na Paulo 2002: 245).Hatimaye, kama wanavyoeleza Carson na Moo, "Ni vigumu kuamini kwamba Paulo angejitambulisha kama mtu ambaye alisikia Injili kutoka kwa wale waliosikia na wala si kutoka kwa Bwana Yesu mwenyewe' ([Ebr] 2:3; ling. Gal. 1:11-12)" (Carson na Moo 2005: 602; pia tazama Guthrie 1983: 20).

Kinachoonekana wazi ni kwamba mwandishi alikuwa ni Mwamini wa Kiyahudi (n.y, ni myahudi aliyeathiriwa na utamaduni wa Kiyunani) aliyefahamu tafsiri ya Kiyahudi ya Agano la Kale. Pia alijulikana kama LXX), wakati hakuna hata moja ya nukuu hizi kutoka Agano la Kale ambazo zinategemea Kiebrania lakini kwa wingi zimepatikana katika Septuagint. Misamiati na Kiyunani ya mwandishi inaonyesha kuwa yeye ni msomi mzuri (Carson and Moo 2005: 6044; Marshall, Travis, na Paulo 2002: 245). Yeye ni mzoefu kwa Paulo na ni miongoni mwa wale waliokuwa pamoja na Paulo, na kwa kuwa anamnukuu mwananfunzi wa Paulo yaani Tim, katika **13:23**. Mwisho, "Yeye ni mtu aliyeelezea Zaidi kuhusu msimamo wa Kikristo kuhusu Agano la Kale" na "Anatupa ufafanuzi ulio wazi sana kuhusu mtazamo wa Kikristo kuhusiana na Agano la Kale na wa mwandishi yoyote wa Agano Jipya" (Guthrie 1983: 21-22).

Ingawa kulikuwa na mabishano kuhusu kuhusishwa na Kitabu cha Waebrania kwenye maandiko ya Matakatifu, viongozi wa kanisa la kwanza kama vile Clement wa Roma alikikubali kitabu hiki kuwepo miongoni mwa vitabu katika Maandiko Matakatifu. Kujumuishwa kwake katika nyaraka kuu kama vile Codex Sinaiticus kulionekana ni muhimu zaidi. Mwishoni, kujibu kuibuka kwa mambo kadhaa na upotofu, katika Maandiko ya Agano Jipya na katika kitabu cha Waebrania, "majibu yalipatikana katika Baraza la Hippo mwaka 393 CE, Sinodi ya Carthage mwaka 397 CE, na Baraza la Carthage mwaka 419 CE" (Dirks 2008: 43). "Kutatuliwa" ni neon la kiutendaji, kama Sproul anavyodokeza, "Kanisa lilitambua, lilikubali na kupokesa, na kukiwakilishwa kwenye mkusanyiko wa maandiko matakatifu. Neno Kanisa katika Baraza lilikuwa ni *tunapokea,* 'Tunapokea.'" (Sproul 1992: 23; tazama Owen 1969: 25-64 kwa ajili ya majadiliano ya kina mengi ya misingi ya sifa za kitabu cha Waebrania kuwepo katika maandiko matakatifu yaani canon.

B. Tarehe ya Kuandikwa kwake

Kitabu cha Waebrania inadiriwa kuandikwa kabla ya kubomolewa kwa Hekalu mwaka 70 BK. Hii inathibitishwa na misemo tofauti ndani ya kitabu chenyewe. **Ebr 10:1-2** inasema kwamba *"Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. 2Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma*

kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?"[1] **Ebr 9:6-10** pia anatumia wakati uliopo akirejea dhabihu zinazoendelea kutolewa hekaluni. Zaidi, **Ebr 8:13** inasema Agano Jipya *"amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka."* Lugha ya kwamba *"karibu kupotea"* inaeleza kuwa, ingawa Agano la Kale lilikuwa kuukuu, desturi zake bado zinaendelea kufanyika (zilikoma mwaka 70 BK wakati hekalu limebolewa tayari). Kwa sababu hii, kipengele cha muhimu kwenye kitabu hiki ni kuelezea utoshelevu wa kipekee wa dhabihu ya Kristo ili kuwazuia wakristo kurejea nyuma katika desturi za Agano la Kale. Lugha hapo juu inakosa maana kabisa ikiwa hizo ibada hazikuwa zikifanyika wakati huo kabla ya kuandikwa kitabu hiki. Kwa kuwa jambo hili linabeba kipengele cha muhimu sana cha kitabu hiki, kubomolewa kwa hekalu kungetajwa humu kama ulikuwa umetokea kabla ya kuandikwa kitabu. Kutokutajwa kwa tukio hilo kunadhihirisha wazi kwamba kitabu kiliandikwa kabla ya mwaka 70 BK, na wala siyo baada. Hatimaye, inakadiriwa 95 BK, Clement wa Roma ananukuu kutoka katika sehemu mbalimbali za **Ebr 1:3-13**, hivyo akionyesha kwamba anakijua kitabu hicho na kwamba anatambua mamlaka yake. (Clement c.95: 36). Hii inaonyesha kwamba kitabu kilifahamika vizuri kipindi hicho. Ingawa hili haitoshi kuelezea kwamba hakikuandikwa baada ya mwaka 70 BK, uwezekano wa kuandikwa baada ya hapo ni mdogo sana, tukijua kwamba muda baada ya mwaka huo usingetosha kuenea kwa kitabu na kukubalika kwake kama mamlaka halisi.

C. Usuli

Ni wazi kwamba kitabu hiki kimeandikiwa Wakristo, ambao wanatiwa moyo kudumu katika ungamo lao kwa Kristo. (mf., **3:6, 14; 10:23**). Nakala ya kwanza ya kitabu hiki ambayo ilitufikia sisi ina kichwa kinachosema, "Kwa Waebrania" (Carson na Moo 2005: 609; Guthrie 1983: 22). Hii ni kuonyesha kwamba huenda Waebrania ndilo jina walilopewa waamini wa Kiyahudi waliofanyika kuwa Wakristo. Hii inaonekana katika ukweli ambao kitabu imenukuu kutoka Agano la Kale kwa kuurudiarudia, kimsingi kutoka katika Septuagint, na mara kwa mara ikinukuu ibada za Agano la Kale. Kuna nukuu nyingi na kuhusisha AK katika Kitabu cha Waebrania kuliko kitabu chochote cha AJ, bila kugusia Kitabu cha Ufunuo. Hakuna rejea yoyote inagusia upagani. Kitabu kinaelezea wito wa Ibrahimu hadi kuingia kwake katika nchi ya Ahadi, na kiini cha mjadala wake ni ukuhani wa Lawi, mfumo wa dhabihu wa Musa na Agano la Kale na huweka wazi jinsi yote yalivyotimizwa na kwamba yote yamezidiwa na Kristo. Hata hivyo kitabu hiki kinatumika kwa wote kwa usawa pasipo kujali walikotokea na historia yao. Kinafunua kwa utajiri mkubwa ufahamu kuhusu Kristo ni nani na kile alichofanya, uhusiano kati ya Agano la Kale na Agano Jipya na umuhimu wa kutunza Imani na hatari ya upotofu. Kitabu hiki kinatoa mafunzo ikijikita kuelezea vifungu vya AK na kutia moyo.

Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania kwa hakika aliwafahamu wasomaji wake na mazingira yao. Alijua kuhusu wao. (**Ebr 6:9-12**); jinsi walivyovumilia mateso na kuwahurumia wafungwa (**10:32-34**); na hali ya kiroho ya wakati huo alipokuwa anaandika waraka huu (**5:11-14; 12:4**). Yeye kutaja habari za Tim kutolewa gerezani, na usemi wake *"akija upesi, nitakuja pamoja naye, nitawaona"* (**13:23**), inaonyesha ufahamu wa mwandishi kuhusu wasomaji wake na Tomtheo anafahamika kwao. Kitabu hakionyeshi hawa wasomaji wa karne ya kwanza waliishi wapi. Ingawa baadhi wanasema hawa wasomaji wa karne ya kwanza walikuwa Lexandria au Yerusalemu, mazingira yanakubaliana na Roma, na maelezo yaliyopo katika **13:24** yanayosema kwamba *"wale waliopo Italia wanawasalimu"* yanafunua kuwa washirika wa mwandishi wanatokea Italia na walitaka kutuma salamu nyumbani (Guthrie 1983: 27; Marshall, Travis, and Paul 2002: 243).

Kitabu hakina mwanzo uliozoeleka wa nyaraka za kitume (yaani, utambulisho wa mwandishi, wanaoandikiwa, na maneno ya salamu). Hakina hitimisho lililozoeleka. **Ebr 13:22** kinajiita chenyewe *"maneno ya faraja."* Usemi kama huo umetumika katika **Mdo 13:15** ukirejea kwenye maneno ya Paulo katika Sinagogi wakati wa safari yake ya kwanza ya kitume. Kutokana na sababu hiyo, wengi wanatoa maoni kuwa kitabu cha Waebrania ni mahubiri yaliyobadilishwa kuwa waraka. (mf., Marshall, Travis, and Paul 2002: 232-33).

D. Maudhui

Maudhui makuu ya kitabu cha Waebrania ni Ukuu mkamilifu wa Kristo: yeye ni *"Mng'ao wa [Mungu] utukufu wa na uwakilishi halisi wa asili Yake"* (Ebr**1:3**). Yeye *"hakuumba ulimwengu"* peke yake (Ebr **1:2**) lakini "hushikilia vitu vyote kwa neno la nguvu zake" (Ebr **1:3**). Yeye ndiye mwenye *"aliyefanya utakaso wa dhambi, [aliketi] mkono wa kuume wa Ukuu huko juu"* (Ebr **1:3**). Yeye ni *"mrithi wa yote"* (Ebr **1:1**). Kwa hiyo, yeye ni mkuu kuliko malaika na Musa. Dhabihu aliyoitoa hailingani kabisa kwa ukuu na dhabihu zilizotolewa chini ya torati ya Musa. Agano Jipya, ambalo Kristo alilianzisha ni kuu Zaidi kuliko Agano la Kale la Musa, ambalo sasa nafasi yake imechukuliwa. Kristo ni kuhani wetu mkuu wa kweli. Yeye ni utimilifu wa Agano la Kale lote, ambalo lilikuwa likimhusu yeye aliyekuwa akitarajiwa. Tukijua hilo, tunapaswa kudhihirisha kwa Imani wokovu na Agano

[1] Mpaka itapoelekezwa vinginevyo nukuu zote zinatoka kwenye New American Standard Bible (1995).

Jipya ambalo Kristo ametupatia katika maisha yetu. Tunatiwa moyo kuvumilia katika hiyo Imani, kwa kuwa hususan mateso na magumu hutumiwa na Mungu kutufunza na ni alama zinazoonyesha kwamba sisi ni watoto wake.

E. Dondoo

Kitabu kinaweza kugawanywa katika vipengele vifuatavyo:

I. <u>Ukuu wa Kristo (1:1—2:18)</u>

A. Kristo ni ufunuo wa Mungu (1:1-3)
B. Kristo ni mkuu kuliko malaika (1:4-14)
C. Yesu pekee hutoa wokovu (2:1-18)
    1. Ni lazima tuushikilie wokovu (2:1-4)
    2. Vitu vyote vipo chini ya utawala wa Kristo (2:5-8)
    3. Kristo hutupa wokovu kwa njia ya mateso na kifo chake (2:9-18)

II. <u>Kristo ni kuhani wetu mkuu aliye mkuu (3:1—8:5)</u>

A. Kristo ni mkuu kuliko Musa (3:1-6)
B. Tofauti na Isareli waliokosa utii, tukishikamana na uaminifu wetu, tutaingia katika pumziko la kweli la sabato. (3:7—4:13)
    1. Msiwe wasioamini kama walivyokuwa Waisraeli (3:7-19).
    2. Tunaingia kwenye pumziko letu la sabato kwa njia ya Imani (4:1-13).
C. Kama kuhani mkuu aliye mkamilifu, Kristo hutoa wale walio waaminifu wokovu wa milele (4:14—6:18)
    1. Ni lazima tudumu katika uaminifu (4:14-16)
    2. Kama kuhani mkuu, Kristo ni chanzo cha wokovu wetu (5:1-10)
    3. Ni lazima tuufikie ukomavu wa kiroho kwa juhudi (5:11—6:3)
    4. Kuanguka baada ya kuijua kweli na hatari (6:4-8)
    5. Tunashikilia tumaini lililowekwa mbele yetu kwa kuutunza uaminifu (6:9-18)
D. Kristo ni mdhamini wa tumaini letu kwa kuwa Yeye ni kuhani mkuu kwa mfano wa Melekizedeki (6:19—8:5)
    1Tuna matumaini kwa sababu Kristo ni kuhani kwa mfano wa Melekizedeki (6:19-20)
    2. Asili ya Melekizedeki na ukuhani wake (7:1-10)
    3. Tofauti kati ya ukuhani wa Lawi na ukuhani wa Kristo (7:11—8:5)

III. <u>Agano Jipya ni bora kuliko Agano la Kale kwa sababu ya dhabihu ya Yesu Kristo. (8:6—10:18)</u>

A. Kristo ni mpatanishi wa Agano Jipya (8:6)
B. Asili ya Agano Jipya (8:7-12)
C. Agano la Kale ni kuukuu (8:13)
D. Matokeo ya dhabihu ya Kristo (9:1—10:18)
    1. Tofauti kati ya Patakatifu pa Agano Jipya na Patakatifu pa Agano la Kale (9:1-14)
    2. Tofauti kati ya Agano Jipya na Agano la Kale (9:15-22)
    3. Tofauti kati ya dhabihu za Agano la Kale na dhabihu za Agano Jipya (9:23—10:18)

IV. <u>Tunadhihirisha Agano Jipya kwenye Maisha yetu kwa njia ya Imani (10:19—13:19)</u>

A. Kwa kuwa Kristo ni kuhani wetu mkuu, ni lazima tuvumilie kwa uaminifu (10:19-39)
    1. Kwa sababu ya Kristo, tunaweza kuwa na uhakika mkamilifu wa Imani (10:19-25)
    2. Kuendelea kutenda dhambi kwa makusudi kutasababisha hukumu kali (10:26-31)
    3. Kuvumilia kwa Imani kutasababisha thawabu kuu (10:32-39)
B. Asili na mifano ya Imani ya kweli (11:1-40)
    1. Asili ya Imani ya kweli (11:1-3)
    2. Mifano ya Imani ya kweli (11:4-40)
C. Jinsi ya kudhihirisha Imani yetu (12:1-29)
    1. Ni lazima tuweke kando kila kinachotuzinga na kukaza mwendo hata mwisho, tukimtazama Yesu (12:1-3)
    2. Ni lazima tukubali kurudiwa na Bwana (12:4-11)
    3. Ni lazima tuwasaidie kaka na dada zetu katika Kristo (12:12-17)
    4. Ni lazima tutambue kwamba tumekwisha kuufikia Mlima Sayuni na Yerusalemu ya Mbinguni (12:18-29)
D. Maelekezo ya mwisho ya vitendo (13:1-19)

1. Maelekezo kuhusu Maisha ya kijamii (13:1-3)
2. Maelekezo kuhusu Maisha binafsi (13:4-6)
3. Maelekezo kuhusu Maisha ya kidini (13:7-19)

V. <u>Hitimisho (13:20-25)</u>

A. Shukrani (13:20-21)
B. Faraja (13:22)
C. Salamu za kibinafsi (13:23-25)

II. ITIFAKI KATIKA KITABU CHA WAEBRANIA

I. Ukuu wa Kristo (1:1—2:18)

Kitabu cha Waebrania inaanza katika mst. wa **1** kwa kuongelea ukuu wa Kristo. Maudhui haya huendelea katika kitabu chote.

A. Kristo ni ufunguo wa Mungu (1:1-3)

[1]Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, [2] mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. [3]Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu,

Kitabu cha Waebrania kinaanza kwa kuelezea kwamba Mungu ni Mungu anayesema. Hii ilikuwa kweli huko nyuma na ni kweli sasa. Hata hivyo, katika mistari hii tunaona yote mawili yaani fundisho la ufunuo unaoendelea na pia ukuu wa Yesu Kristo usioweza kulinganishwa na chochote na kujifunua Yeye mwenyewe katika Kristo. Kama mstari wa **1** unavyoeleza kwa wazi, hapo mwanzo, Mungu kimsingi alinena kupitia manabii. Hata hivyo, mawasiliano yake na sisi hayakuwa tu kwa njia ya manabii. **Zab 19:1** inaonyesha kuwa uumbaji wenyewe hutangaza utukufu wa Mungu. Mungu pia alisema na watu wake kwa njia ya ndoto. (**Mwa 28:12-15**), maono (**Isa 6:1**), Urimu na thumimu kwenye ephodi (**Hes 27:21; 1 Sam 23:9-12**), kwenye kichaka kinachoungua moto (**Kut 3:4-6**), malaika (**Dan 9:20-22**), "amiri jeshi wa Jeshi la Bwana" (**Yos 5:13-15**), Melkizedeki (**Mwa 14:18-24**), na "Malaika wa Bwana" (**Mwa 22:15-18**).[2]

Mstari wa 2 inaonyesha tofauti kati ya Mungu ya Mungu akinena na mababa *"zamani sana"* kuongea kwake na sisi leo *"katika siku hizi za mwisho."* Sasa, amenena nasi *"katika mwanaye."* Hata matumizi ya msemo *"siku hizi za mwisho"* inaweka msisitizo katika umuhimu na ukuu wa Yesu Kristo. Hii ni kwa sababu katika AJ inaweka wazi kwamba ujio wa kwanza wa Kristo (au, kimahususi zaidi, kifo chake kisicho cha kawaida, kufufuka kwake, kupaa kwake, na umwagiko wa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste) vina umuhimu mkubwa kwa habari ya siku za mwisho. Hususan, kuja kwa Yes umara ya kwanza: (A) ni mwanzo wa nyakati za mpya za Historia ya Maisha ya mwanadamu amabyo inathibitishwa na ukweli kwamba kuja kwake kwa mara ya kwanza ni mwanzo wa "siku za mwisho" ambazo ndizo hizi na zitaendelea hata atakaporudi;[3] na (B) kumetimiza unabii wa siku za mwisho kuhusu "siku za mwisho"au "nyakati za mwisho'' Kwa hiyo, "Waandishi wa Agano Jipya wanafahamu kuwa tayari wanaishi katika siku za mwisho. Hili hususan limeelezwa na Pet katika mahubiri yake ya siku ya Pentekoste, aliponukuu unabii wa Yoeli kama ifuatavyo: 'Kwa kuwa watu hawa hawakulewa, kama mnavyodhani, kwa kuwa bado ni saa tatu asubuhi, lakini hiki ndicho alichosema nabii Yoeli "Na katika siku za mwisho, itakuwa, Asema Mungu, nitamimina Roho wangu juu ya wote wenye mwili. . ."' (Mtd 2:16-17). Maneno 'katika siku za mwisho' (*en tais eschatais hēmerais*) ni tafsiri ya maneno ya Kiebrania'*acharey khēn,* ikiwa na maana ya *baadaye.* Pet anaponukuu maneno haya kuhusu tukio ambalo tayari limetokea, kimsingi anasema: 'Tupo katika siku za mwisho sasa.'" (Hoekema 1979: 16) Matumizi mengine Zaidi ya usemi huu "siku za mwisho" katika AJ vile vile unaonyesha kuwa sisi tunaishi katika "siku za mwisho" sasa (ona **2 Tim 3:1-5; Ebr 1:1-2;**

---

[2] "Jemedari wa majeshi ya Bwana," Melekizedeki na "Malaika wa Bwana" inawezekana ni Yesu aliyetokea kama ya kufanyika mwili na kuonekana kama Yesu Kristo (tazama Menn 2025: 51-60).

[3] Kuja kwa Yes umara ya kwanza pia kulibadili nyakati kutoka KK (Kabla ya Kristo) hadi BK (Baada ya Kristo) ambayo kwa kilatini imefupishwa na kuwa AD (kirefu chake ni *"anno domini"*— "katika mwaka wa Bwana"). Hata wale wasiotumia KB na BK hizo herufi—lakini hutumia "Kipindi cha kawaida (Common Erra)" vifupisho vyake, "BCE" na "CE"—hata hivyo wanatambua kwa badiliko la nyakati kwa ajili asili ya Yesu kubadilisha ya ujio wake kwa mara ya kwanza. Tarehe zote ni sawa zinaandikwa kama KK na BK lakini wale wanaotumia vifupisho vya BCE na CE hawataki kukubali kwamba Yesu ni Bwana kwa hakika.

Yak 5:1-3; 2 Pet 3:1-4).[4]

Kutajwa kwa mara ya kwanza kwa "Mwana" kunatambulisha umuhimu wa usio na mfano wa Yesu Kristo. Katika huu mstari na mingine michache inayofuata tunaambiwa kwamba Yesu: ni *"mrithi wa yote"* (**mst. 2**); *"aliufanya ulimwengu,"* mbingu na dunia (**mst. 2, 10**); ni *"mng'ao wa [Mungu] utukufu wake"* (**mst. 3**); ni *"mwakilishi halisi wa asili Yake"* (**mst. 3**); *"huvishikilia vitu kwa neno la nguvu zake"* (**mst. 3**); *"alizitakasa dhambi"* (**mst. 3**); *"ameketi mkono wa kuume wa Ukuu mbinguni"* (**mst. 3**); ni *"bora zaidi kupita malaika"* (**mst. 4**); *"amerithi jina bora zaidi kuliko lao"* (**mst. 4**); ni Mwana wa Mungu (**mst. 5**); anaabudiwa na malaika (**mst. 6**); ni Mungu (**mst. 8**); ni Bwana (**mst. 10**); na ni wa milele (**mst. 11-12**).

Vipengele kadhaa vya maelelezo haya kuhusu Kristo ni nani na kile alichoafanya kina umuhimu wa kipekee. Katika **mst. 1**, mahali panaposema kwamba Mungu *"husema nasi kwa njia ya Mwanaye,"* katika lugha ya kiyunani hakuna neno "Yake." Kuhusu jambo hili, Leon Morris anaeleza, "Kimsingi mwandishi anasema kwamba Mungu alisema nasi 'kupitia yule ambaye ana sifa ya kuwa Mwana.' Ni sifa hiyo ya Uana iliyo na asili iliyo na nguvu." (Morris 1981: 13) Hii asili ya Mwana inapewa hadhi ya kuwa na mwili katika **mst. wa 3**, inayosema kwamba Kristo ni *"uwakilishi halisi wa utukufu [Mungu]asili Yake,"* hii inatuambia sisi kwamba, ingawa Kristo alikuwa mwanadamu kwa muda mfupi, alikuwa ndivyo alivyo, na asili iliyo sawa kwa utimilifu na pia maumbile na kusudi kama Mungu, hiyo ni kusema alikuwa Mungu kweli na mwanadamu kweli. Ingawa Kristo kwa muda alifanyika mwanadamu, wakati huo huo pia alikuwa na asili hiyo hiyo ya uwepo na katika nafasi ya Mungu, yaani, Yesu alikuwa yote mawili Mungu kamili na mwanadamu kamili. (tazama Menn 2025: 221-36). Wazo hilo linaendana na tamko la Paulo katika **Kol 2:9** ndani ya Kristo *"unakaa utimilifu wote wa Mungu katika umbile la mwili."* Ingawa **mst. 2** unatafsirika kwamba Kristo *"aliufanya ulimwengu,"* Kiyunani ina maana kwamba aliumba "nyakati" (Kiyunani = *aiōnas*) ambayo "ambayo inabeba mengi zaidi, ikihusisha wakati ule ambao vyote vinaonekana sasa viliumbwa" (Guthrie 1983: 65). Katika **mst. 3**, neno la Kiyunani "hushikilia" ni *pherō,* ambapo katika mstari ule maana nit endo linaloendelea. Kwa maneno mengine, ulimwengu unashikiliwa, kudumishwa, na kuendelezwa hadi mwisho wake ulioamriwa utakapofikia na Mungu huyo huyo wa utaratibu aliyeratibu mpangilio wa mbingu na kupangilia vitu vyote tangu milele iliyopita. (Isaya 46:10; Yer 31:35). Katika ulimwengu unaotawaliwa na huyo Mungu, mfanano wa asili unategemewa, na kutokana na matarajio haya, kanuni ya sayansi na ubunifu wa kisayansi yote mawili yanawezekana na ni ya thamani." (Laskaris 2018: 444; pia tazama Meyer 2021: 441-43). Hitimisho la **mst. 3**, kwamba *"ameketi kwenye kiti cha Ukuu Mbinguni,"* ni nukuu ya wazi ya **Zab 110:1**. Maudhui haya, **Zab 110:1**, na kwamba Kristo amefanya utakaso wa dhambi (**mst. 3**), vitaelezwa kwa mapana baadaye kwenye kitabu hiki.

B. Kristo ni mkuu kuliko malaika (1:4-14)

[4] amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao. [5] Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, "Mimi nitakuwa kwake baba, Na yeye atakuwa kwangu mwana"? [6] Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu."

[7] Na kwa habari za malaika asema, "Afanyaye malaika wake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa miali ya moto." [8] Lakini kwa habari za Mwana asema, "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. [9] "Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio." [10] Na tena, "Wewe, Bwana, hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako; [11] Hizo zitaharibika, bali wewe unadumu; Nazo zote zitachakaa kama nguo, [12] Na kama mavazi utazizinga, nazo zitabadilika; Lakini wewe u yeye yule, Na miaka yako haitakoma."

[13] Je! Yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, "Uketi mkono wangu wa kuume Hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako"? [14] Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?

Kwa kuwa, katika lugha ya Kiyunani, **mst. 1-4** unaunda sentensi moja ndefu, wachambuzi wengi wanahusisha **mst. 4** kama sehemu ya mjadala pamoja na **mst wa 1-3.** Hata hivyo, mst. 4 unafuatiwa na mkato unatambulisha wazo jipya-Ukuu wa Yesu kupita malaika-ambao unaelezewa Zaidi katika **mst. wa 5-14**. Matokeo yake, ni sahihi kuuhesabu **mst. 4** kama mwanzo wa kipengele kipya.

Hilo *"jina lililo bora zaidi"* Yesu inawezekana linahusiana na jina lenyewe kuitwa "Mwana" katika **mst. 2**. Kuna mambo matatu katika hili: (1) Wakati kitabu cha Waebrania kinaandikwa, malaika walikuwa wanaheshimika

[4] Kwa ajili ya mjadala wa kina juu ya "siku za mwisho," tazama Menn 2018: 45-49.

sana na kuinuliwa. (2) Kurejewa kwa hilo "jina" (Kiyunani = *onoma*) na, bila kukawia mapema katika mst. **3**, "Ukuu" (Kiyunani = *megalōsynē*) inarejea nyuma na kuhusisha na Agano la Daudi katika **2 Samweli 7**, ambapo Mungu aliahidi kuuinua uzao wake baada yake na *"kuimarisha kiti chake cha enzi hata milele."* Katika Septuagint, ambayo mwandishi wa Waebrania anaitumia neno *onoma* linaloonekana mara nne, katika **2 Sam 7:9, 13, 23, 26;** na *megalōsynē* inapatikana katika **2 Sam 7:21, 23** na muundo wa kitenzi cha neno unapatikana katika **2 Sam 7:22, 26** (mahali inatafsiriwa "kuu" au "ukuu"). (3) Kurejewa kwa Agano la Daudi kumethibitishwa katika **mst. 5** ambao hunukuu kipekee tamko muhimu katika Agano la Daudi, **2 Sam 7:14**, *"Nitakuwa Baba kwake naye atakuwa Mwana Kwangu Mimi,"* na kulitumia kwa Yesu. Nukuu hii na kuhusishwa huku vinatuweka wazi kwamba, pamoja na mambo mengine, kwamba Yesu ametimiza Agano la Daudi.[5]

Katika **mst. 5**, kitabu cha Waebrania kinanukuu **Zab 2:7**, *"Wewe ni Mwanangu, nimekuzaa leo."* **Zaburi ya 2** ni "ni zaburi ya kuweka wakfu wafalme wa Israeli – ni tangazo la hadhara la ufalme. Na wengi wa wafalme waliingia kwenye ufalme wakiwa watu wazima. **Hakuna** aliyepewa ufalme akiwa tumboni mwa mama yake. Hii inatumika vile vile kwa Yesu katika Agano Jipya, kwamba kufufuka kwake ni tangazo la hadhara alilotoa Mungu kuhusu utambulisho wa kweli na mamlaka yay a Yesu, Masiha, mfalme wa kweli wa Israeli, mwakilishi wa Mungu kati ya wanadamu." (Katz, "Wewe ni" n.d.: n.p.) Nukuu ya **Zab 2:7** katika **mst. 5** (na tena katika **Ebr 5:5**) inanena kuhusu "**ufufuo na kuinuliwa** kwake Kristo. Hii inadhirisha kitendo chake cha kushika ofisi ya mfalme na kuhani . . . ninafikiri Rum 1:4 inasema kwa wazi zaidi kwamba Yesu 'alitangaza kwa uweza ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu kwa kufufuka kwake kutoka kwa wafu: Yesu Kristo Bwana wetu.' Kufufuka kwake kulikuwa tangazo la hadhara la yote yaliyoendelea." (Katz, "Wewe ni" h.t.: n.p., msisitizo wenye nguvu. Katika asili.; pia tazama Guthrie 2007: 927-28). Nukuu hii pia katika **Zab 2:7** inatumika kwa wazi kuonyesha Kufufua kwa Kristo katika **Mtd 13:33**. Hii pia inaendana na **mst. 3**, inayoongelea kuhusu Kristo kuketi mkono wa kuume wa Mungu. Wote **2 Samweli 7** na **Zaburi 2** inaeleweka kuwa wanasema kuhusu ujio wa Masiha. Na usemi huu *"Mwana wa Mungu"* unakuwa, pamoja na mambo mengine, kama usemi wa kimasiha na pia unamwonyesha Yesu kama Mwana wa Mungu wa kiungu. Imetumika kwa Yesu katika **Ebr 4:14; 6:6; 7:3; 10:29**. Maelezo yaliyorudiwa kuhusu Uana wa Kristo yanadhihirisha kwamba, kwa kila njia, kwa hakika, *"ni bora zaidi kuliko malaika."*

Nukuu katika **mst. 6** kwa "mzaliwa wa kwanza" inaakisi **Zab 89:27**. **Zaburi 89** ni zaburi ya kimasiha. Kwa hiyo, **mstari wa 6** unaendeleza maudhui ya Yesu. Yesu pia anaitwa "mzaliwa wa kwanza" katika **Rum 8:29** (*"mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi"*), **Kol 1:15** (*"mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote"*), na **Kol 1:18** (*"mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu"*). Cheo "mzaliwa wa kwanza" haimaanishi kwamba Yesu ni kiumbe aliyeumbwa (kwa kuwa yeye ni wa milele, Mungu asiyeumbwa na Bwana, yeye mwenyewe, muumbaji) lakini inaonyesha hali yake ya ukuu unaowapita malaika na pia unaopita viumbe vyote. **Mstari wa 6** unanukuu **Zab 32:43** (LXX), na kuakisi **Zab 96:7** (LXX). Kwamba malaika "huabudu" Mwana tena hudhihirisha ya kwamba yeye ni Mungu.

Mstari wa 7 umenukuliwa kutoka **Zab 104:4** (**Zab 103:4,** LXX). Kinachosemwa hapa ni kwamba malaika ni roho zitumikazo tofauti na Mwana, ambaye ni Bwana. (pia tazama **mst. 14**). Malaika wanatofautishwa naye kwa Yeye Mwana anao ukuu mkamilifu, na ameinuliwa na ni Bwana atawalaye, katika **mistari ya 8-9**, amabayo ni nukuu kutoka **Zab 45:6-7** (**44:7-8**, LXX), zaburi nyingine inayomhusu masihi. Nukuu kutoka Zaburi ya **45** inathibitisha kwamba Yesu, kwa hakika ni Mungu. Nukuu *"Mungu, Mungu wako"* katika **mst. 9** ni "mtazamo wa wazi juu ya utatu unamthibitisha Mwana akiwa kama Baba lakini ikimtofautisha yeye na Baba" (Guthrie 2007: 939). **Mistari ya 10-12** inaendelea kuonyesha ukuu wa Mwana usio na mwisho kwa kunuu kwenye **Zab 102:25-27** (**Zab 101:26-28**, LXX). Mwana ni "Bwana," ni muumba wa mbingu na nchi habadiliki, na ni wa milele, wakati ambapo uumbaji wote unabadilika na utaharibika. Kama vile Mwana alivyoumba ulimwengu, hivyo vyote ataviharibu na kuumba mbingu mpya na nchi mpya (**Isa 66:22; Ufu 21:1**).

Mistari ya 13-14 inahitimisha mjadala wa ukuu wa Kristo kuzidi malaika kwa kuhusisha nukuu ya kwanza kutoka kwenye **Zab 110:1** (**109:1**, LXX). **Zab 110:1** pia inahusishwa na au kunukuliwa katika **Ebr 1:3; 8:1; 10:12;** and **12:2**. **Zab 110:1** imekuwa fungu la muhimu katika AJ (kuna nukuu 21 au kuhusianishwa kwenye mengi

[5] Hii inaonyeshwa pia katika mstari wa **3**, kuhusu Yesu kuketi mkono wa kuume wa ukuu wa Enzi Mbinguni. Kabla hajazaliwa, Malaika Gabrieli alimwahidi Mariamu kwamba Bwana Mungu alimpa Yesu *"kiti cha Baba yake Daudi; na yeye atatawala juu ya nyumba ya Yak milele, na ufalme wake hauta kuwa na mwisho''* (**Lk 1:32-33**). Siku ya Pentekoste Pet alieleza kwa jinsi Yesu alipotimiza Agano la Daudi kupitia ufufuo wake na kupaa kwake (**Mdo 2:22-36**). Pet alihusika na nukuu na kuhusisha **2 Sam 7** na **Zab 16:8-11; 110:1**, na **132:11** na husema kwamba wale wanaotoa unabii *"alitazama kwa mbali akaunena ufufuo wa Kristo''* (**Mdo 2:31**). Kwa kifupi, "*kuketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi imeunganika na kuketi mkono wa kuume wa Mungu.* Kwa maneno mengine, kufufuka kwake na kupaa kwenda mkono wa kuume wa Mungu kunatajwa na Pet kama kutimizwa kwa Agano la Daudi.'' (Bock 1992: 49, msisitizo. Kwa asili.) Kupata zaidi juu ya namna Yesu alivyotimiza Agano la Daudi, tazama Meen 2025: 142-46.

ya maandiko ya AJ). Yesu mwenyewe ananukuu **Zab 110:1** wakati anajadili Mafarisayo. Yesu aliwauliza Mafarisayo kuhusu wanachowaza kuhusu Kristo: *"Yeye ni mwana wa nani?"* Walijibu kwamba yeye ni *"mwana wa Daudi."* Kisha Kristo akanukuu **Zab 110:1** inayosema, *"Bwana alimwambia Bwana wangu."* Kisha yeye akauliza, *"Kama Daudi* [mwandishi wa Zaburi] *anamwita 'Bwana,' yeye atakuwaje Mwanaye?"* Yesu anajisema mwenyewe ya kwamba Yeye ni masihi, ''mwana mkuu'' wa Daudi, na kwamba yeye anao uungu. (tazama Goppelt 1982: 83 ["Neno 'Bwana' (*kurios*) inamfanya kuwa sawa na Mungu"]). Tofauti na Bwana Yesu aliyeinuliwa, **mst. 14** unaeleza kuwa malaika ni *"roho zitumikazo, zilizotumwa kutumika"* katika mwili wa Kristo (yaani, *"wale wataourithi wokovu"*). Malaika, toauti na Kristo, malaika hawajawahi kusemakana kuwa wameketi na kwamba wanatawala lakini wanaonekana wakiwa kwenye nafasi za utumishi kwa Kristo na wakitumika kwa niaba ya Kristo kwa wengine.

C. Yesu pekee hutoa wokovu (2:1-18)

Ukuu wa Yesu unaonekana katika kazi yake ya kipekee anayofanya: yeye peke yake ndiye anayetoa wokovu na uzima wa milele kwa wanadamu walioanguka dhambini.

1. Ni lazima tuujali wokovu wetu (**2:1-4**).

[1]Kwa hiyo, imetupasa kuwa waangalifu sana kuhusu kile tulichosikia, ili tusije tukakiacha. [2]Kwa kuwa kama ujumbe ulionenwa na malaika ulikuwa imara, na kila uasi na kutokutii kulipata adhabu ya haki, [3] je, sisi tutapaje kupona kama tusipojali wokovu mkuu namna hii? Wokovu huu, ambao mwanzo ulitangazwa na Bwana, ulithibitishwa kwetu na wale waliomsikia. [4]Pia Mungu aliushuhudia kwa ishara, maajabu na kwa miujiza mbalimbali, na karama za Roho Mtakatifu alizozigawa kulingana na mapenzi yake.

Sura ya 1 inaonyesha Ukuu mkamilifu wa Yesu juu ya kila mmoja na juu ya kila kitu katika ulimwengu wote. Mistari hii ni faraja na maonyo ya moja kwa moja kutoka kwa kile kilichosemwa kuhusu Kristo katika Sura ya 1. Wito katika **mst. 2-4** unatumia fikra zile zile za kumlinganisha Kristo na malaika katika Sura ya 1. Maneno*"neno lililonenwa na malaika"* inaenda sawa na kile alichosema Paulo katika **Gal 3:19**, kwamba Torati ilikuwa *"imenenwa na malaika."* Ikiwa hiyo haikutakiwa kuvunjwa, kweli za Kristo na Injili ni zaidi sana, kwa kuwa Injili ilinenwa kwanza na Bwana, siyo tu kupitia malaika, ilishuhudiwa na Mungu, na kuhusu Yesu ni nani nay ale aliyosema yanathibitishwa kwa ishara, maajabu na miujiza na kwa kupitia karama za Roho Mtakatifu. Neno la Kiyunani kama "karama" ya Roho Mtakatifu siyo neno la kawaida katika AJ (*charismata*) lakini ni neno la jumla zaidi kwa ajili ya "mgawanyo" (*merismoi*). Matokeo yake, msisitizo "unamwangukia mgawanyaji," mana yake, Roho Mtakatifu, anayegawanya karama *"kama atakavyo mwenyewe"* (**mst. 4**; pia tazama **1 Kor 12:11**; Guthrie 1983: 83). Zinagatia kwamba **mst. 3-4** nafsi zote tatu katika Utatu zinahusika katika kutangaza na kuthibitisha kweli za Injili. Matokeo yake, kutokuamini ni hatari.

Kwa sababu ya vile Kristo alivyo na jinsi neno lake limethibitika, kamwe hatuna kisingizio cha kukosa kuamini na kutomtii yeye. Hata hivyo, tunaweza *"kupinda mbali"* na yeye, polepole, na bila kukusudia. Shughuli za maisha, kupuuza yale aliyoyasema Yesu, kutaka urahisi na utulivu, tamaa za miili yetu, ushawishi wa kijamii na wa kitamaduni (mambo ambayo tunaweza hata tusiyatambue kirahisi), kukosa kuomba kwa bidii na kutojifunza kwa bidii, na kukosa kulitumia Neno katika Maisha yetu, yote hayo yanaweza kusababisha kupinda huo. Katika tafsiri ya **mst. 1**, *"kutoka kwenye hilo"* hayapo katika Kiyunani cha asili: wanafanya kupunguza ukubwa wa jambo hilo kuliko kulikuza. Tatizo linaweza kuelezwa kwa udogo sana. Kama ndege itakosa mwelekeo sahihi hata kwa nyuzi digrii moja tu, mtu anaweza asigundue mwanzoni, lakini baada ya kwenda umbali wa maelfu ya maili, ndege itakuwa imeenda mbali na mwelekeo kwa mamia ya maili. Hukumu ya Yesu kwa watu waliokuwa wakiishi katika kipindi cha Nuhu siyo kwamba wao walikuwa wakatili, bali ni kwamba wao walikosa ufahamu, kwa sababu maisha yao waliyaelekeza kwenye *"kula na kunywa, kuoa na kushughulika na mambo ya ndoa"* na mahangaiko mengine ya maisha ya ulimwengu huu (**Mt 24:37-39**). Kwa hiyo hapa, tatizo siyo uasi bali ilikuwa upuuzaji tu. Kupinda kiimani hudumaza hisia zetu juu ya hatari iliyopo.

Tatizo linakuwa kubwa zaidi pale ambapo hakuna ambaye amewahi *kupinda* kuelekea kwa Kristo. Kubakia mwaminifu na kukaa katika uhusiano na Kristo ni uamuzi na inahitaji juhudi za makusudi. Kuwa makini na *"yale tuliyoyasikia"* ambayo ni kweli za Injili, mambo ya kweli, yenye thamani, na maonyo yanayotufanya tujikite kiroho na kimaadili na tudumishe afya njema ya rohoni na kwenye maadili **Ebr 6:18-20** inatuonya sisi *"tushikilie tumaini lililowekwa mbele yetu. [19] Tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, [20] alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu."* Meli ambayo ameshikiliwa kwa hakika haiwezi kupinda. Ikiwa Kristo kweli ni ''nanga ya roho zetu,'' na ikiwa tutamshikilia kwa nguvu, kamwe hatutaweza kupindishwa.

2. Vitu vyote vipo chini ya utawala wa Kristo (**2:5-8**).

[5] Maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao tunaounena. [6] Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema "Mwanadamu ni nini hata umkumbuke? Ama mwana wa binadamu, hata umwangalie?[7] 7Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, Umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; [8] Umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake." Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hamjaona vitu vyote kutiwa chini yake.

Kitabu cha Waebrania kinarejea tena ukuu wa Kristo ukilinganishwa na ukuu wa malaika. Hapa mwandishi ananukuu **Zab 8:4-6** ili kuelezea kwamba kila kitu kilichopo kipo chini ya utawala wa Kristo. **Mstari wa 7** ni nukuu ya **Zab 8:5**. Katika Maandiko ya Kiyahudi (Kiebrania) kifungu cha mstari huo kinatumia neno *elohim* na linatafsiriwa kama *"Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu."* Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania hata hivyo alitumia Septuagint, ambayo hutafsiri kama "malaika."

Kusudi la Mungu la awali ni kumwumba mtu kwa mfano wake na kumpa utawala wa dunia yote (**Mwa 1:26-28; Zab 8:4-6**). Hii haihusishi tu kila kitu kilichopo sasa ulimwenguni sasa bali *"ulimwengu ujao"* pia (**mst. 5**). Kwa sababu ya dhambi zetu, hatuoni hayo yakitokea sasa (**mst. 8**). Muktadha wa zaburi haukuwa mahususi kwa ajili ya masiha lakini unahusika na wanadamu wote kwa ujumla. Hata hivyo, Kristo akiwa ndiye mfano mkamilifu wa Mungu (**Ebr 1:3**), Kristo alikuja duniani na kufanya kwa ajili yetu yale ambayo hatukuweza sisi kuyafanya wenyewe. Kama vile alivyofufuka na alivyoinuliwa juu hata kuwa mkono wa kuume wa Mungu, mahali ambalo kila kitu huwa chini ya utawala wake (**Efe 1:20-23; Flp 2:8-10**), kwa hiyo tumeinuliwa pamoja naye na yeye *"ametuketisha pamoja naye katika mbingu"* (**Flp 2:4-7**). Na **1 Kor 6:3** inaweka wazi kuwa siku moja *"sisi tutawahukumu malaika."* Kwa hiyo, Mpango wa Mungu umekuwa na utatimizwa na wanadamu kwa njia ya Kristo. Maneno *"Kwa maana hakuuweka ulimwengu ujao chini ya utawala wa malaika,"* yanayoanzia **mst. 5**, inadhihirisha kuwa yote haya yalikuwa ni mpango wa Mungu- dhambi zetu zilizoanzia kwenye bustani ya Edeni, hazikuweza kuharibu kabisa mpango wa Mungu.

3. Kristo hutoa wokovu kwa njia ya mateso na Kifo (**2:9-18**).

[9] Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu. [10] Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. [11] Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake, [12] akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; Katikati ya kanisa nitakuimbia sifa." [13] Na tena, ''Nitakuwa nimemtumaini yeye''. Na tena, ''Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu."

[14] Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, [15] awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa [16] Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu. [17] Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake. [18] Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

Sehemu hii hujenga juu ya yale yaliyotangulia kusemwa katika **mst. 5-8.** Inatumia lugha kama ile iliyotumika katika **Zab 8:5** (*"Umemfanya mdogo punde kuliko malaika"*) na inatumika kwa Yesu. Kipekee, hii ndiyo mara ya kwanza Kristo anatajwa kwa jina, na jina lililotumika katika Maisha ya kawaida duniani, jina la kibinadamu, "Yesu." Hili eneo linaonyesha ubinadamu wa Yesu na utambulisho wake mkamilifu katika ubinadamu wetu ikiwa ni pamoja na mateso na kifo chake (**mst. 9-10, 14, 18**); kwa vile anavyotuita sisi ndugu zake na Watoto wake (**mst. 11-14, 17**); kwa alivyoshiriki mwili na damu kama sisi (**mst. 14**); kwa vile alikuwa sawa na sisi katika mambo yote (**mst. 17**); kwa vile alivyojaribiwa kama sisi (**mst. 18**). Kwa hakika ni kupitia majaribu yake, mateso na kifo Yesu alifanyika *"mdogo kuliko malaika."*

Kwa upande mwingine, sehemu hii inakamilisha sura ya 1 ambayo inaongelea ukuu wa Yesu. Katika eneo hili tunaona, kwa mshangao, kwamba ni kwa mateso hayo hayo na kifo, Yesu *"alivikwa taji [yeye] ya utukufu na heshima"* (**mst. 9**). Mateso na kifo chake sit u vilimpatia taji ya utukufu na heshima lakini pia vilileta *"wana wengi*

kwenye utukufu" (**mst. 10**). Hii inafanana na maelezo yaliyopo katika **Ufunuo 5**. Hapo Yoh aliambiwa hilo tu *"simba aliye wa kabila la Yuda, shina la Daudi, ameshinda ilia pate kukifungua kitabu na muhuri zake saba"*. (**Ufu 5:5**). Hata hivyo, Yoh alipotazama hakumwona simba bali *"mwana kondoo amesimama, kana kwamba amechinjwa"* (**Ufu 5:6**). Ishara hizo mbili zinamwelezea Yesu. Yesu ni simba aliyeshinda hasa hasa kwa sababu alitolewa dhabihu na kuchinjwa kama *"mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu"* (**Yoh 1:29**). Hii ndiyo Injili. Wokovu ambao ni wetu sisi (**Ebr 2:3**) hatukuupata kwa chochote tulichofanya au ambacho tungeweza kufanya; kwa asilimia 100 unategemea Kristo alivyo na kile alichofanya kwa ajili yetu: alijifananisha na sisi kwa kila kitu; aliishi Maisha ambayo sisi tulitakiwa kuyaishi; na alikufa kifo ambacho sisi tulipaswa kufa; na alilipa gharama ya dhambi ambazo sisi tulitakiwa kulipa ingawa tusingeweza kamwe. Hakuna dini nyingine kama hii ulimwenguni mwote, kwa sababu hakuna mwingine aliye kama Yesu.

Katika **mst. 10**, misemo *"kwa ajili yake, amabaye kwa ajili yake vitu vyote, na kwa njia yake vitu vyote"* ingefaa isemwe kuhusu Mungu au Yesu Kristo. Labda pia ingesemwa kuhusu wa kwanza, kwa kuwa maelezo yanayofanana na hayo yametumika kwa ajili ya Mungu katika **Rum 11:36**, na **1 Kor 15:24** inasema kwamba hatimaye ufalme utarejeshwa kwa Mungu Baba. Kwa upande mwingine, tumekwisha ona katika Ebr. I:2 Yesu ndiye; *''amabaye kwa njia yake vitu vyote,"* na ni kwa njia ya kujidhabihu kwake msalabani aliweza *"kuwaleta wana wengi katika utukufu."* Wakati **mst. 10** unasema juu ya *"kumka[milisha] mwanzilishi wa wokovu wetu kupitia mateso,"* neno "kukamilisha" maana yake "kufikisha kwenye utimilifu," kwa kuwa, yeye ni nafsi ya pili katika Utatu, Yesu alikuwa mkamilifu tayari. Kwa maneno mengine kuteseka kwake hakukuwa muhimu kwa ajili yake, lakini ni muhimu sana kwa ajili ya kuleta wokovu kwa wengine. Pia, mateso yake halisi "vilimkamilisha" au vilimfanya Yesu awe sawa na sisi, akiteseka kwa ajili yake, kwa kuwa yeye aliyapitia yote kwa ajili yetu tangu mwanzo hadi mwisho, badala ya kule kuwa tayari tu kuteseka.

Maana halisi ya "takasa" (**mst. 11**) siyo kutenga kwa ajili ya kusudi takatifu. Yesu aliwekwa wakfu kama *"kuhani mkuu aliye mwaminifu"* kwa ajili yetu kwa kusudi takatifu la kufanya *"upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu"* (**mst. 17**). Wale watu ambao aliwafanyia upatanisho waliwekwa wakfu kwa ajili ya wokovu. Kinachoelezwa hapa ni **mst. 11** ni kwamba Mungu Baba ni chanzo cha wote wawili atakasaye na wenye kutakaswa, yaani, Mungu alimweka wakfu Mwana na kumtuma kwa ajili ya utume wa mateso kwa sababu ya upendo wake kwa wanadamu (**Yoh 3:16**).

Mistari ya 12-13 ina nukuu tatu za AK. Ya kwanza ni kutoka **Zab 22:22**, ya pili **Isa 8:17** (LXX), na ya tatu ni kutoka **Isa 8:18**. **Zab 22** ni ya kinabii na kimasihi, hasa tukiangalia kwa undani kuhusu kusulubiwa kwa Yesu katika hali zote mbili kisaikolojia na vinginevyo. Kwa hiyo, **Zab 22:14, 16b, 17a** hali hii, *"Nimemiminwa kama maji, na mifupa yangu yote imeteguka, moyo wangu umekuwa kama nta, umeyeyuka ndani yangu. . . . Wamenichoma mikono yangu na miguu yangu. Ninaweza kuhesabu mifupa yangu."* Hichi ndicho kilichotokea kama sehemu ya kusulubiwa na kile kilichomtokea Yesu. Alichomwa mkono na miguu yake (Davis 1982b: Golgota; **Yoh 20:25, 27**). **Zab 22:15** inaongeza, *"Nguvu zangu zimekauka kama kigae, na ulimi wangu waambatana na taya zangu."* Hiyo inaelezea wazi kukaza sana kwa misuli, kuishiwa nguvu sana, na kukosa maji mwilini kwa sababu kusulubiwa (Davis 1982a: 14, 17, 33, 35, 42). Maelezo ya Yesu katika **Yoh 19:28** (*"Nina kiu"*) yanafanana na **Zab 22:15** (*"ulimi wangu waambatana na taya zangu"*). Unabii katika **Zaburi 22** ni wa kushangaza, hasa hasa Zaburi iliandikwa miaka takribani 500–600 miaka kabla ya Waajemi kuanzisha adhabu ya kusulubisha watu.

Zaburi 22 inatabiri kwa usahihi mengine juu ya kusubiliwa kwa Kristo. **Zab 22:18** inasema, *"Waliyagawana mavazi yangu, na kupigia kura vazi langu."* Askari wa kirumi waliyafanyia hivyo mavazi ya Yesu na Yoh anaandika kuhusu hilo *"ilifanyika hivi ili kutimiza maandiko"* (**Yoh 19:24–25**; pia tazama **Mk 15:24; Lk 23:34**). Akiwa msalabani, Yesu ananukuu **Zab 22:1**, *"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeiacha?"* (**Mt 27:46; Mk 15:34**) kutimiza lilichotabiriwa katika **Zab 22:1**. Nukuu katika **Zab 22:7** kuhusu watu "kutikisa vichwa" ilitimizwa Yesu alipokuwa msalabani (**Mt 27:39; Marko 15:29**). **Mt 27:43** inatuarifu kuwa waliokuwa wakisimama Yesu akiwa msalabani waliyatamka maneno yaliyoandikwa katika **Zab 22:8**, *"Alimtumaini Mungu; Mungu na amwokoe sasa, kama anapendezwa Naye; kwa kuwa Yeye alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.'"*

Ebr 2:12 anahitimisha maneno ya **Zaburi 22** kwa kunukuu **Zab 22:22**, *"Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, Katikati ya kusanyiko nitakusifu."* Haya "maneno ya Kristo aliyefufuka katikati ya kusanyiko la watu wa Mungu. . .inaonyesha umoja wa Kristo na watu wake, na umoja wake hautokani tu na ukweli kwamba Kristo wa Zaburi ya 22 … anawaita ndugu zake lakini pia ni pamoja na ukweli kwamba ameunganika nao kwa njia ya mateso yake, kama sehemu ya Zaburi iliyosalia inavyoelezea." (Hays 1993: 126–27). Zaburi inaanza na kilio cha kutengwa na inaishia na wimbo wa sifa, ambao unaakisi kile kile anachosema mwandishi wa Webrania mahali hapa: kwa njia ya mateso na kifo chake, Kristo huwaleta ndugu zake kwenye utukufu na wokovu. Nukuu katika **mst. 13** inatoka katika kitabu cha **Isaya 8** haikazii tu tumaini la Yesu kwa Baba yake bali inafunua mahusiano ya karibu kati ya Kristo na watu wake.

Mahusiano ya karibu kati ya Kristo na watu wake yanaendelea kuwa ya kina Zaidi katika **mst. 14.** Kwamba Kristo, *"alishiriki sawasawa"* mwili na damu kama watu wake inarejea katika ubinadamu mkamilifu wa Kristo. Katika **Waebrania 1-2** hapo tunaona asili mbili za Kristo: Kristo ni Mungu kamili (mkuu kuliko malaika) mtu kamili (sawa na mwanadamu). Ukweli kwamba Kristo ni mtu kamili na ni Mungu kamili siyo kwamba ni muhimu tu lakini ni lazima kabisa kwa ajili ya wokovu. Gleason Archer aneleza, "Mungu kama Mungu asingeweza kutusamehe dhambi zetu ila pale ambapo itatokea fidia kamilifu; la sivyo Yeye angekuwa anakubaliana na kukingia kifua ukiukwaji wa sheria zake mwenyewe zilizo takatifu. Ni katika hali ya Mungu kuwa mtu katika Kristo angeweza kutimiza kikamilifu dai la dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu; kwa kuwa ni mtu pekee, mwanadamu wa kweli, angeweza kuwakilisha jamii ya wanadamu. Lakini mwokozi wetu ni lazima pia awe Mungu, kwa kuwa ni Mungu pekee angeweza kutoa dhabihu yenye thamani isiyo na mfano, kulipia kwa ajili adhabu ya milele jehanamu ambayo tulistahili kwa sababu ya dhambi zetu, kulingana na madai ya haki ya kiungu." (Archer 1982: 323)

Anselm wa Canterbury analisemea hivi: Kwa sababu mwanadamu *hawezi* kulipia kikamilifu deni tulilonalo kwa Mungu, "hakuna nje na Mungu *anayeweza* kufikia utoshelevu huu. Lakini pia hakuna nje ya mtu anayepaswa kufanya hili, vile vile mtu hawezi kufanya hilo kiasi kinachotosheleza. Kwa hiyo, kwa kuwa ni lazima, kama inavyoonekana, kwamba ufalme wa mbinguni umefanywa kwa ajili ya wanadamu, na kwamba hili haliwezi kutendeka pasipo huo utoshelevu kufikiwa, ambao hakuna awezaye kuufikia isipokuwa Mungu na pia anayepaswa kufanyika si mwingine ila mtu, ni lazima Mungu-mtu afanya hili. . . . Kwa hiyo ili kwamba Mungu mtu aweze kufanya hilo, ni lazima kiumbe hicho kiwe Mungu kamili na mtu kamili, ili kufanya upatanisho huu. . . . Kwa kuwa, ndivyo, ni lazima kwamba Mungu-mtu atunze utimilifu asili hizo mbili, na siyo lisilo na ulazima kwamba asili hizi zinapaswa kuungana katika nafsi moja, kama vile nafsi yenye kufikiri na mwili huishi pamoja kwa kila mwanadamu; vinginevyo haiwezekani nafsi moja iwe Mungu kweli na mtu kweli." (Anselm 1903: II:6-7) Yesu pekee anakidhi vigezo hivyo. Ni muunganiko huu tu ulio wa ajabu wa Mungu na mtu katika nafsi ya Kristo kulimfanya aweze kutoa adhabu na kuvumilia adhabu ya msalaba.

Maelezo katika **mst. 14** yanayoeleza kwamba *"ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi"* yanaturejesha nyuma kabisa hadi **Mwa 3:15** (pia tazama **1 Yoh 3:8**). Hapo, alimwambia nyoka (yaani, Shatani katika umbo la nyoka) kwenye bustani ya Edeni aliposababisha anguko la Adamu na Eva katika dhambi, *"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino."* Hili limepewa jina la "protoevangelium" ("injili ya kwanza"), kwa kuwa tangazo la kwanza la Mungu mwenyewe kuhusu mpango wake wa wokovu kwa ulimwengu. Ingawa unabii ulihusisha *"uzao wake na uzao wa mwanamke,"* mstari unaofuata umeeleza wazi kwamba ni mapambano ya moja kwa moja kati ya mmoja wa uzao wa mwanamke na ''wewe'' ina maana Shetani mwenyewe. Kulingana na unabii huu, kutoka katika uzao wa mwanamke utamponda kabisa Shetani kwa kipigo cha mauti—"Kumponda nyoka kichwa ni kipigo kitakacho sababisha kifo chake"—wakati shetani atamgonga mtu kisigino, au kumfanya ateseke na hata aweze kusababisha kifo (Lunn 2020: 43). Yesu alimshinda shetani kwa kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa kufanya hivyo, aliwaumba wanadamu wapya ambao kwao shetani hana nguvu tena juu ya wale walio katika Kristo (tazama **Yak 4:7**). Atakaporudi mara ya pili, hatimaye atamharibu kabisa shetani milele. (**Ufu 20:10**).

Mstari wa 15, unapoongelea kuhusu Kristo kuweka huru *"wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa,"* unaongelea kuhusu wanadamu kuwa watumwa wa dhambi. Neno *"kuwa chini ya"* linaashiria *aliye chini ya kifungo,* maana yake "amefungwa, ameshikiliwa, amebanwa, hayupo huru" (Zodhiates 1993: *aliye chini ya utumwa,* 592). Kwa sababu dhambi ni sehemu yetu inayotenda kazi ambayo ni ya asili na hiyo inatutenga na Mung una pia huharibu matendo yetu mema, Biblia inawaeleza watu kama walio ''watumwa wa dhambi'' (**Yoh 8:34; Rum 6:6, 16-17, 20; 7:14**). Au, tukiweka kwa maneno mengine, "kila aliyezaliwa katika ulimwengu huu ameharibiwa na Anguko lile la kwanza kiasi kwamba wanadamu wote kimaadili wameharibiwa, na watu hawana nguvu ya kurekebisha hali yao wenyewe wasipookolewa na Mungu" ("Dhambi ya Asili" n.d.: Utangulizi; tazama **Yoh 3:3, 5; 6:44, 65; 8:34; Rum 6:16-17, 20; 8:6-8; 1 Kor. 2:14; Efe 2:1-3, 8-9; Ebr 11:6**). Kinachoelezwa na sehemu hii ya kitabu cha Waebrani ni kutuonyesha jinsi ambavyo Yesu alishughulika na maadui watatu na kuwashinda wale ambao walituingiza sisi sote kwenye janga;: dhambi, Shetani, na mauti. Yeye pekee akiwa Mungu kamili na mwanadamu kamili, aliweza kufanya hili. **Mstari wa 16** unaturejesha kwenye maudhui ya malaika na tena inasisitiza uhusiano wa Kristo na watu wake kwa kuwapatia *"kuwapatia msaada uzao wa Ibrahimu."* Katika **Gal 3:29**, Paulo anaeleza kuwa *"ikiwa ninyi ni wa Ibrahimu, basi ninyi wa Kristo, kwa hiyo ninyi ni uzao wa Ibrahimu, warithi sawa sawa na ahadi."*

Mstari wa 17 unatoa utangulizi wa mada ambalo litaongelewa sana baadaye kwenye kitabu hiki, yaani Yesu ni kuhani wetu mkuu. Mstari unahitimisha kwa kurejea kwenye mada kuu ya kipengele hiki, kwamba Kristo hutupa wokovu kwa njia ya mateso na kifo chake, lakini anafanya hivyo kwa kuwa yeye pia ni kuhani wetu mkuu.

Kristo kama kuhani mkuu alifanya *"upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu."* Upatanisho ni lugha ya hekalu. (**Rum 3:25; Ebr 2:17**). Inaonyesha kwamba tulikuwa chini ya hasira ya Mungu lakini sasa hasira imeondolewa na kutulizwa. Neno la Kiyunani kuuelezea upatanisho ni *hilaskesthai.* Zodhiates anafafanua, "Yesu ni kuhani mkuu anayejitoa mwenyewe, anakuwa kwa wakati mmoja yote mawili mkosaji na kuhani, kwa hiyo akitimiza haki ya Mungu na wakati huo huo akitangaza msamaha wa dhambi ambapo mtu aliyepatanishwa anapewa nafasi ya kumfikia Mungu na kuwa na ushirika naye." (Zodhiates 1993: *hilaskomai,* 768). Lugha inayotumiwa na kitabu cha Waebrania hapa inaturudisha nyuma kwenye sanduku la agano/hekalu na Siku ya Upatanisho. Siku ya Upatanisho, kuhani mkuu ananyunyiza damu ya mnyama aliyetolewa dhabihu kwenye kiti cha rehema katika Patakatifu pa Patakatifu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu. "Kiti cha rehema" kilikuwa kifuniko cha sanduku la Agano kwenye madhabahu ba hekalu. Septuagint inatafsiri neno "kiti cha rehema" kama "*hilastērion,*" neno linalolingana na *hilaskesthai* (**Kut 25:17**, LXX). **Rum 3:25** inaitaja dhabihu ya Yesu msalabani kama *"upatanisho"* (au "dhabihu ya upatanisho"—NIV). Neno lililotumika hapa lenye maana ya "upatanisho" ni *hilastērion* (pia tazama **Ebr 9:5** ambalo linamaanisha kiti cha rehema kama *hilastērion*). Hivyo, tunachoona siyo tu kina cha kile alichofanya Yesu lakini pia jinsi Mungu alivyoweka katika mfumo wa matendo ya dhabihu za Israeli katika AK na maudhui yale ambayo Kristo angekuja kuyakamilisha miaka zaidi ya elfu ijayo.

Kipengele hiki kinahitimishwa na maelezo kwamba Kristo *"kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."* Kristo kujaribiwa kwake kama sisi ni matokeo ya Yeye kuwa kama sisi. **Ebr 4:15** inafafanua hili, na jambo la kujaribiwa kwa Yesu litajadiliwa kwa undani zaidi mahali hapo. Kwa sasa, yatosha kusema kwamba, kwa kuwa yeye *"alifananishwa na ndugu katika mambo yote"* (**mst. 17**), ikiwa pamoja na majaribu, yeye pekee angeweza kuhusiana na sisi kikamilifu na, kama ''*Mwana Kondoo wa Mungu"* angeweza kutoa dhabihu kamilifu kwa Baba na hivyo *"kuondoa dhambi za ulimwengu"* (**Yoh 1:29**). Yote haya yanafunua jambo la ajabu kuhusu asili ya Mungu. Kama Richard Bauckham anavyoeleza, "Yesu anafunua utambulisho wa kiungu—Mungu ni nani hasa—katika hali ya kushushwa na katika kuinuliwa pia, na katika muunganiko wa yote mawili. Utambulisho wa Mungu mwenyewe unafunuliwa katika Yesu, Maisha yake na msalaba wake, kama ilivyo kweli katika kuinuliwa kwake, kwa namna ambayo inaendana sawa na pasipo kubadilika katika AK na uelewa wa Wayahudi kuhusu Mungu, lakini pia ya ajabu na kushangaza." (Bauckham 1998: viii)

MASWALI YA MJADALA

1. Nini huonyesha kwamba ukuu wa Kristo upo juu ya uumbaji wote viumbe vyote?

2. Kwa namna gani tunaweza "kuujali wokovu wetu"?

3. Ni kwa jinsi gani tunaweza kupinda mbali na Kristo na katika uhusiano wetu na yeye? Tunawezaje kuepuka hilo au kuzuia lisitokee?

4. Waebrania 2:9-18 inaelezea kuhusu mateso ya Kristo

   - Ni kwa nini na kwa namna gani mateso ya Kristo yalikuwa ya muhimu, na yalitimiza nini?
   - Je mateso ya Kristo ni kielezo kwetu, na kama ndiyo kwa namna gani?
   - Kwa nini hudhani kuwa mateso yote siyo halali, kwamba Mungu hana sababu katika hayo, na kudhani yanatokana na dhambi, laana, au shetani? Je mtazamo huo ni sahihi, kama siyo, ni mtazamo gani ni wa kibiblia Zaidi kuhusu mateso, na tunajifunza nini tunapokuwa kwenye mateso?

5. Asili ya Mung inafananaje, na Waebrania 1-2 inafunuaje asili ya Mungu?

6. Kwa nini ni muhimu na lazima kwa Kristo kuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili?

7. Kitabu cha Waebrania kinanukuu au kuhusianishwa Zaidi na AK kuliko kitabu kingine chochote cha AJ isipokuwa, labda Ufunuo wa Yoh. Sura ya 1-2 inanukuu au inahusiana na vifungu vingi vya AK. Umejifunza nini kutokana na hili, na je umegundua kitu kinachokufurahisha au kilicho muhimu katika nukuu hizi au kufafana na AK?

II. <u>Kristo ni kuhani wetu mkuu sana (3:1—8:5)</u>

Kitabu cha Waebrania kinaendelea kuelezea ukuu wa Yesu Kristo kwa kuonyesha kwamba, kama kuhani mkuu wa kweli na wa milele, yeye hutupa wokovu wa milele ambao Agano la Kale halikuweza.

A. Kristo ni mkuu zaidi ya Musa (3:1-6)

[1]Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu, [2] aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyemweka, kama Musa naye alivyokuwa, katika nyumba yote ya Mungu. [3]Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba. [4]Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu; ila yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu. [5]Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi, awe ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye; [6]bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.

"Kwa hiyo," inayoanza katika **mst. 1**, inaturudisha nyuma kwenye kile kilichosemwa kuhusu Kristo, ikisema, Yeye alichukua asili yetu ili kwamba, kwa uaminifu wake katika mateso na kifo chake, awe kuhani mkuu na kwa hiyo aweze kumshinda shetani, dhambi, na kifo chenyewe. Katika sura ya **2:17** mwandishi alisema kwamba kwa njia ya mateso na kifo chake Kristo *"aweze kuwa kuhani mkuu mwaminifu na mwenye huruma."* Sasa, anatutaka kumtambua Yesu, ambaye ni *"mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu."* Huu ni wakati pekee katika Agano Jipya Yesu anaitwa "Mtume." Msemo huu unatoka kwenye ukweli ambao Yesu mwenyewe aliusema, *"Kama Wewe ulivyonituma Mimi ulimwenguni, Mimi nami nawatuma wao ulimwenguni''* (**Yoh 17:18**). Kama Donald Guthrie asemavyo, "Kwa maneno mengine walifanyika mitume kwa kuwa yeye alikuwa mtume. Yeye ni mkamilishaji mkamilifu wa ofisi hiyo ya kitume. Wengine wote wanamwakisi yeye katika hali iliyofifia." (Guthrie 1983: 98)

Tena, katika **mst. 2-6**, mwandishi anamlinganisha Yesu na Musa, kama alimlinganisha Yesu na malaika katika sura ya 1. Musa ni mtu wa muhimu sana katika Agano la Kale. Ameandikwa zaidi ya mara 750 katika AK, na maelezo yake na matokeo yake ni kiini kikuu. Ametajwa mara nyingi kama mtoa sheria, mpatanishi wa Agano, nabii, wakala wa wokovu wa Mungu kwa Israeli kutoka Misri, mchungaji wa Israeli walipokuwa jangwani, na ''Rafiki wa Mungu'' aliyeongea na Mungu uso kwa uso na kupokea amri kumi moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Pamoja na umhimu mkubwa wa Musa, Yesu Kristo anaonekana akiwa mkuu sana akilinganishwa naye. Kwa hiyo, Kristo anasemekana kuwa na *"utukufu zaidi ya Musa"* kama vile mjenzi wa nyumba alivyo na utukufu kuliko nyumba yenyewe (**mst. 2-4**) na kama vile Mwana alivyo na utukufu kuliko mtumwa (**mst. 5-6**). Na "nyumba" hapa ni watu wa Mungu: Yesu yupo "juu" ya nyumba kwa sababu yeye ni mjenzi, lakini ni mtumishi na sehemu ya hiyo nyumba.

Maneno yaliyotumika katika kumlinganisha Yesu na Musa—"Mwana," "nyumba," na "mjenzi"—ni muhimu. Matumizi ya "Mwana," kwa kweli, yanaturejesha kwenye sura ya 1, mahali nafasi ya Yesu kama "Mwana" imekaziwa sana. Lakini hilo neno pamoja na "nyumba" na "mjenzi," yanaleta maana zaidi. Maneno yote matatu yanatupeka hadi kwenye Agano la Daudi la **2 Sam 7:8-17**. Baada ya Daudi kuwa mfalme na sanduku la Agano lilipopelekwa Yerusalmu, Daudi alitaka kujenga nyumba (hekalu) kwa ajili ya Mungu, amabye mpaka wakati alikuwa akiishi kwenye madhabahu inahamishwa hamishwa (hema) (**2 Sam 7:1-7**). Majibu ya Mungu kwa Daudi, ni kwamba hawezi kuruhusiwa kujenga nyumba kwa ajili ya Mungu, kwa kuwa *"Bwana atajenga nyumba kwa ajili yako"* (**2 Sam 7:11**). Mungu aliendelea kusema Mwana wa Daudi ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya Bwana, kwamba *"Nitaimarisha pembe ya ufalme wake milele. Nitakuwa baba kwake naye atakuwa mwana Kwangu"* (**2 Sam 7:13-14**).

Kwa kuangalia **2 Sam 7:14,** maneno *"Mwana wa Mungu"* ulikuwa msemo wa kimasihi ukiashiria ahadi ya mfalme anayetokana na Daudi. Ingawaje utawala wa uzao wa Daudi ulidumu kwa mamia kidogo, haukudumu "milele," kama alivyosema Mungu katika Agano lake. Kwa hiyo, agano hilo lilikuwa linaenda Zaidi ya Daudi na mwanaye Sulemani. Ilikuwa inamlenga Yesu, ambaye amejadiliwa katika **Ebr 1:4-14**, ni utimilifu wa Agano la Daudi (tazama hasa **Ebr 1:5**, ambayo inanukuu **2 Sam 7:14** na kutumika kuhusu Yesu). Yesu mar azote anaitwa *"Mwana wa Mungu"* (**Mt 4:3, 6; 8:29; 26:63; 27:40, 54; Mk 1:1; 3:11; 15:39; Lk 1:35; 3:38; 4:3, 9, 41; Yoh 1:34, 49; 11:27; 20:31; Mdo 8:37; 9:20; Rum 1:4; 2 Kor 1:19; Gal 2:20; Ef 4:13; Ebr 4:14; 6:6; 7:3; 10:29; 1**

Yoh 3:8; 4:15; 5:5, 10, 12, 13, 20). Yesu pia anajitambulisha mwenyewe kama *"Mwana wa Mungu"* (**Mt 26:63-64; 27:43; Mk 14:61-62; Lk 22:70; Yoh 3:18; 5:25; 10:36; 11:4; 19:7; Ufu 2:18**).

Lugha ya "nyumba" na "mjenzi" pia inawalenga wale waliungana na Kristo kwa imani, yaani kanisa. Paulo anahusisha na **2 Sam 7:14** katika **2 Kor 6:18** na anahusisha pia Agano la Daudi na Kanisa. Akijua hilo, Paulo anabadili maneno ya ahadi alizotia Mungu kuhusu Sulemani mwana wa Daudi (*"Nitakuwa baba kwake na yeye atakuwa mwana Kwangu"*) kuwa *"Nitakuwa baba kwenu, nanyi mtakuwa wana wa kike na wa kiume Kwangu."* Hilo linaelezea kwamba Agano la Daudi linatimia kwa utimilifu wake katika Kristo na kanisa. Kwa kuongeza, katika **Efe 2:20-22**, Paulo analielezea kanisa kama *"[20]Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. [21]Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. [22]Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho."* Lugha hii inaambatana **Ebr 3:4**, inayoongelea juu ya "nyumba" ambayo "hujengwa" na Mungu, na **Ebr 3:6**, amabayo husema, *"lakini Kristo alikuwa mwaminifu kama Mwana juu ya nyumba yake yote-amabye nyumba yake ni sisi."* Onyo mwishoni mwa **mst. 6**, *"kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho,"* inalenga kuelezea uvumilivu katika Imani, ambao unahitajika kuwepo katika Imani ya kweli inayookoa, ambao umedokezwa katika kifungu kinachotupa maonyo katika sura 2:1-4, ambalo pia limedokezwa katika vifungu vya sura ya 3, 6, na mahali pengine.

Ile "nyumba" ambayo Sulemani aliijenga mwanzo ilikuwa, hekalu kimsingi. Agano jipya linafafanua wazi wazi kwamba kanisa ndiyo hekalu la kweli, ambalo hekalu la Yerusalemu lilikuwa linaashiria. Msemo halisi "hekalu la Mungu" imeandikwa mara kumi na moja kwenye AJ (**Mt 26:61; 1 Kor. 3:16, 17a, 17b; 2 Kor. 6:16a, 16b; 2 The. 2:4; Ufu 3:12; 7:15; 11:1, 19**; pia tazama **Efe 2:21; 1 Pet 2:5;** na **Ufu 13:6** ambapo kanisa linaitwa *"maskani yake"*). Msemo huu kila wakati unaelezea kanisa, hasa hasa katika **Mt 26:61**, mahali Yesu ananukuliwa akisema, *"Ninaweza kuharibu hekalu la Mungu na kulijenga kwa siku tatu."* G. K. Beale anafafanua, "Mathayo anaona hekalu linaloonekana kubomolewa na kujengwa kupitia kufufuka kwa Yesu kimwili . . . . Hekalu la kale la Israeli lilikuwa ni kivuli cha Kristo na kanisa lake kama hekalu. Kwa maana, kumbuka, kusudi la msingi la hekalu ni kwamba palikuwa mahali ambapo utukufu wa Mungu ulikuwa duniani kwa watu wake. Kwa hiyo sasa Yesu alikuja kama Mungu aliyefanyika mwili, yeye sasa ni mahali ambapo Mungu anajifunua duniani katika mwili." (Beale 2004: 275-76; tazama pia **Yoh 2:19-22**) Kwa wazi zaidi, katika **1-2 Kor,** "Paulo alikuwa anawaelezea waamini katika miaka ya 50 BK, *wakati hekalu la Yerusalemu lilikuwa bado halijabomolewa,* kama hekalu la Mungu ambalo Roho anaishi ndani yake'' (Sweeney 2003: 629).[6] Kwa hiyo, machoni pa Mungu hekalu la Yerusalemu lilikuwa tayari limeondolewa hata kabla halijabomolewa kimwili na Rum mwaka 70 BK. Katika **2 Kor 6:16-7:1**, baada ya kulinganisha kanisa na hekalu, Paulo anahitimisha kwa kusema, *"Kwa hiyo, tukiwa na ahadi hizi."* Ahadi ambazo ananukuu katika **2 Kor 6:16-18** zinahusisha **Law 26:11-12, 2 Sam 7:14,** and **Ezek 37:27**, mahali ambapo Mungu anaahidi kumjengea Daudi nyumba na kuuimarisha ufalme wake milele na kuwa Baba kwake na kuimarisha madhabahu na mahali pa Yeye kukaa pamoja na watu wake hata milele. Akirejea kwenye ahadi hizo katika muktadha wa kuliita kanisa *"hekalu la Mungu aliye hai"* (**2 Kor 6:16**) Paulo anasema, "Kukamilika kwa Agano la Mungu kwa utimilifu wake, uwepo wa ufalme wa Mungu wa milele, akiwaunganisha watu wake na Yeye mwenyewe na yeye mwenyewe akijiunganisha na watu wake hata milele: hizi ndizo ahadi zilizotimizwa katika kanisa—sisi *ni* hekalu la Mungu aliye hai" (Clowney 1972-73: 186).

Pia mistari hii inatoa muhutasari wa ulinganifu kati ya Musa na Yesu ambao tunauona kwenye Biblia nzima, ulinganifu ambao huonyesha ukuu wa Kristo dhidi ya Musa. Kwa mfano, Muujiza wa kwanza wa Musa ni kubadilisha maji kuwa damu, alama ya hukumu na mauti (**Kut 7:20–21**); Muujiza wa kwanza wa Yesu alioufanya hadharani ulikuwa kubadilisha maji kuwa divai, ishara ya furaha na uzima (**Yoh 2:1–11**).[7] Tunaona vitu vinavyofanana na vikielezea Ukuu wa Yesu katika mambo muhimu ya Maisha ya Musa na Yesu:

- *Musa ni mtangulizi wa Masihi.* Musa ni wa pekee miongoni mwa manabii, kwa mambo mawili ayofanya na ukweli kwamba hakuongea naye kwa njia ya maono na ndoto bali ''*uso kwa uso"* na ''*mdomo kwa mdomo"* (**Kut 33:11; Hes 12:6–8; Kum 34:10–**12) kama vile mtu anayeongea na rafiki yake. Hata hivyo, Yesu alikuwa ni mkuu sana ukimlinganisha na Musa.Yesu alifanya miujiza mikubwa zaidi kuliko Musa, ikiwa ni pamoja na kufufua wafu na kufufuka kutoka kwa wafu. Yesu anamzidi Musa kwa sababu yeye pekee ndiye aliyemwona Baba, kwa kuwa alitoka kwa Baba (**Yoh 6:46**) na yeye mwenyewe *"ni mwakilishi halisi"* wa Mungu (**Ebr 1:3**). Yesu hakunena tu Neno la Mungu kila wakati; badala yake hakufanya chochote yeye mwenyewe, lakini kila *alichofanya* na kusema ni kile tu ambacho alimwona Baba akifanya

[6] "Tarehe ya 1 Korintho katika muongo wa tano wa karne ya kwanza haijadiliwi sana'' (Sweeney 2003: 629n.116).

[7] Kinywaji, kimsingi, ni ishara ya damu ya Yesu Kristo, kumwagika kwa damu alianzisha Agano Jipya, ambayo kwa hiyo watu hupata msamaha kwa dhambi zao zote, moyo mpya, nia, Roho na uzima wa milele (**Luka 22:20; 1 Kor 11:25**).

(**Yoh 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Hii ni kwa sababu Yesu ni Neno halisi la Mungu lililokuja humu duniani kama mwanadamu (**Yoh 1:1, 14; Ufu 19:13**).

- *Uhuru toka utumwani.* Musa aliwaongoza watu watoke utumwani kule Misri kwenda kuanza Maisha mapya ya uhuru (**Kut 12:29–32**), ingawa hakuwahi kufanikiwa kuwafikisha watu kwenye nchi ya ahadi. Yesu aliwaongoza watu wake kutoka kwenye utumwa mbaya zaidi wa dhambi, shetani, mauti na kifungo cha torati, na kwamba alisema *"nanyi mkidumu katika Neno Langu, ndipo mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli; nanyi mtaifahamu kweli nayo kweli itawaweka huru''* (**Yoh 8:30–31**).
- *Mana.* Kama vile Bwana alivyotoa mana wakati Musa anawaongoza Israeli jangwani (**Kut 16:1–21**), hivyo Yesu akasema, *"Kweli, kweli, nawaambia ninyi, siyo Musa aliyewapa ule mkate kutoka mbinguni, lakini na Baba yangu ndiye ambaye huwapa mkate wa kweli kutoka mbinguni. . . . Mimi ni Mkate wa uzima."* (**Yoh 6:32, 35**) Mana ilikuwa ya muda mfupi na ya kimwili; ule mkate anaotoa Yesu (mwenyewe) hutoa uzima wa milele kwa kila alaye (**Yoh 6:48–58**).
- *Sheria za Mungu zilizotolewa mlimani.* Kama vile ambavyo Mungu alimpa Musa Sheria juu ya mlima (**Kut 19:20**), vivyo hivyo na Yesu alitoa sheria zake, "sheria ya Kristo," juu ya mlima (**Mt 5:1–48**; tazama **1 Kor. 9:21; Gal 6:2**). Hata hivyo, kwa kuwa Yesu ni mkuu sana, alikuwa na uwezo wa kubadili sheria ya Mungu kwa mamlaka yake Yeye mwenyewe (**Mt 5:21–22, 27–28, 31–34, 38–44; Mk 7:18–19**). Zaidi ya hayo, sheria ya Musa na sheria ya Kristo ni tofauti kwa ubora; mtume Yoh anasema, *"Torati ilikuja kwa mkono wa Musa; bali neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo"* (**Yoh 1:17**).
- *Dhabihu na Upatanisho. Ingawa Musa alitoa dhabihu ili kufanya upatanisho na kujitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi za watu wake* (**Kut 32:30–32**), Kwa hakika alijitoa Yeye Yesu alifanya upatanisho kwa kujitoa dhabihu yeye mwenyewe kwa ajili ya dhambi za watu wake (**Rum 3:23–25; 5:6–8; Ebr 9:26–28; 10:11–12; 1 Yoh 2:2**).
- *Wapatanishi.* Kama vile Musa alivyokuwa mpatanishi kati ya Mung una Israeli. (**Kut 20:19; Kum 5:5; Gal 3:19**), kwa hiyo Yesu ni *"mpatanishi pekee kati ya Mungu na watu"* (**1 Tim 2:5**).
- *Maagano.* Musa alilianzisha Agano la Kale (**Kut 24:8**). Kwenye karamu ya mwisho Yesu alilianzisha Agano Jipya (**Lk 22:20**; pia tzama **Mt 26:28; Mk 14:24**). Musa alirasimisha Agano la Kale kwa damu za Wanyama, lakini Yesu alimshida Musa kwa kuwa alirasimisha Agano Jipya kwa damu yake mwenyewe (**Mt 26:28; Mk 14:24; Lk 22:20**; tazama **1 Kor 11:25; Ebr 8:7–13; 9:11–14**), ambalo lilifanya Agano la Musa liwe kuukuu (**Ebr 8:13**). Agano La Musa hakikuweza kusamehe dhambi au kutoa uzima wa milele lakini Agano Jipya husamehe dhambi na kutoa uzima wa milele.
- *Wokovu kutoka mautini.* Yesu alilinganisha kifo chake na kifo cha Musa. Yesu alisema, *"Kama vile Musa alivyomwinua nyoka jangwani, hivyo imempasa mwana wa Adamu naye kuinuliwa"* (**Yoh 3:14**; tazama **Hes 21:9**). Kumtazama nyoka wa shaba jangwani kulimwokoa mtu kutoka mauti ya mwili; kumtazama Yesu humpa mtu uzima wa milele na kumwokoa mtu kutoka kwenye mauti ya pili.
- *Miili iliyokufa.* Miili iliyokufa yote ya Musa na ya Yesu haiwezi kupatikana. **Kum 34:6** inasema kwamba Musa alizikwa katika nchi ya Moabu. *"lakini hakuna mtu anayejua mahali alipozikwa."* Yesu pia alizikwa, lakini mwili pia haukupatikana kwa sababu alifufuka! (**Mt 28:6**)

B. Tofauti na Waisraeli walioasi, tukibakia waaminifu, tunaingia kwenye pumziko la sabato ya kweli. (3:7—4:13)

1. Msiwe wasioamini kama Wana wa Israeli (**3:7-19**).

[7]Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, ''Leo, kama mtaisikia sauti yake, [8]Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha, Siku ya kujaribiwa katika jangwa, [9]Hapo baba zenu waliponijaribu, wakanipima, Wakaona matendo yangu miaka arobaini. [10] ''Kwa hiyo nalichukizwa na kizazi hiki, Nikasema, Sikuzote ni watu waliopotoka mioyo hawa; Hawakuzijua njia zangu; [11]Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia rahani mwangu.'''

[12]Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. [13]Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo ''leo''; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. [14]Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho; [15]hapo inenwapo, ''Leo, kama mtaisikia sauti yake, Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha.'' [16]Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia? Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa? [17]Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa? [18]Tena ni akina nani aliowaapia ya kwamba

hawataingia katika raha yake, ila wale walioasi? [19]Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao.

Hii sehemu ni maonyo yanayotoka kwenye mstari wa **1-6**. Hususani mstari wa **6** ambao unasema *"tulishike tumaini la wito wetu kwa ujasiri mpaka mwisho,"* kwa sababu sasa sisi ni nyumba ya Kristo, siyo nyumba ya Musa. Haya ni maonyo ya kutokufuata mfano wa Israeli ambao uliomfanya Mungu akasirike kwa miaka 40 jangwani kwa ugumu wa mioyo yao, kutotii, na kutokuamini. **Mistari ya 7b-11** inanukuu **Zab 95:7c-11**. Kifungu cha Waebrania cha **Zab 95:8** inaelezea Meriba na Masa, wakati wana wa Israeli waligombana na Musa wakidai awape maji (**Kut 17:1-7; Hes 20:2-13**). "Moyo" (**mst. 8, 10, 15**) huzingatia umuhimu au kiini cha uhai wetu, kuhusu mawazo, hisia, na nia. Nukuu katika mistari ya **10** na **11** juu ya Mungu "hasira" na "hukumu" inaelezea kwamba Mungu hawezi kuvumilia dhambi. Hii inaonekana kwenye mstari wa **11** ukweli kwamba Mungu ameapa kwa hasira yake. Maonyo katika mstari wa **7-11** yanawekewa uzito na utangulizi katika **mst. 7a**, *"Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu."* Kwa maneno mengine, maonyo yanatoka kwa Mungu mwenyewe, siyo tu kwa mwandishi wa Kitabu cha Waebrania.

Mistari ya 12-19 unatoa ufafanuzi wa**,** na maneno ya kutia moyo, na maelezo yanayozingatia, **Zab 95:7c-11**, na tena nukuu katika **Zab 95:7c-8**. Maneno yanayohimiza kudumu katika uaminifu yanazingatia ukweli kwamba *"tumekuwa washirika wa Kristo"* (**mst. 14**).[8] Kushindwa kwa Waisraeli kuingia kwenye pumziko la Mungu ilikuwa ni *"kwa sababu ya kutokuamini"* (**mst. 19**). Kitendo cha kutokuamini kinahusisha. "Kutokuamini" siyo tu mashaka ya kiakili au kuamini jambo fulani lakini ni pamoja na, na sifa zake ni hizi: moyo mbovu, usioamini (**mst. 12**); kuanguka kutoka kwenye mikono ya Mungu aliye hai (**mst. 12**); kufanywa mkaidi kutokana na udanganyifu wa dhambi (**mst. 13**); ugumu wa moyo (**mst. 15**); kumchokoza Mungu Mungu (**mst. 16**); kumkasirisha Mungu (**mst. 17**); dhambi (**mst. 17**); kutotii (**mst. 18**); kushindwa kuingia katika raha ya Mungu (**mst. 18-19**); na, kifo cha mapema (**mst. 17**). Kwa maneno mengine, kutoamini ni jambo la moyoni, ni kuwa mwenye dhambi, na mara zote inatupelekea kwenye matokeo mabaya-kwa hakika, matokeo ambayo yanayosababisha kifo. Ubaya wa kutoamini umesisitizwa kwenye mstari wa **12** ambao unamwongelea mtu "anayeanguka mbali" kutoka kwa Mungu aliye hai. Neno la kiyunani lenye maana ya "kuanguka mbali" ni *apostēnai,* ni mzizi ambao umezaa neno "kijitenga". Kwa kuwa Yesu ameelezwa kama Mungu aliyekuja humu duniani, kumkataa Yesu—hata kwa kurejea kwenye dini ya Kiyahudi na kwa Mungu ya dini ya Uyahudi — inaonekana ni kujitenga na kumwacha Mungu mwenyewe.

Umuhimu wa kubaki kwenye uaminifu pia umesisitizwa kwa maneno ya kuhimiza katika mistari: *"Jihadharini, wapendwa"* (**mst. 12**); *"mkitiana moyo kila mtu na mwenzake siku kwa siku"* (**mst. 13**); ''*kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho"* mst**. 14**); *"Msifanye mioyo yenu kuwa migumu"* (**mst. 15**); na kitendo kujirudia kwa neno "Leo" katika **Zab 95:7b**, ni msisitizo kwamba kudumu katika Imani yetu sasa ni muhimu sana kwa ajili yetu (**mst. 15**). Maneno haya ya kutuhimiza siyo yanalenga kutufanya tuwe makini na kuwa na bidii kwa ajili ya Imani yetu tu au Imani yao tu, bali ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ndugu zetu na dada zetu wote katika Kristo hawajitengi mbali na Kristo au hawapotei.

2. Tunaingia kwenye pumziko letu la Sabato kwa imani (**4:1-13**).

[1]Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. [2]Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia. [3]Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyosema, ''Kama nilivyoapa kwa hasira yangu,'' Hawataingia rahani mwangu: ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. [4]Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, ''Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi zake zote;'' [5]na hapa napo, ''Hawataingia rahani mwangu.'' [6]Basi, kwa kuwa neno hili limebaki kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani walikosa kuingia kwa sababu ya kuasi kwao, [7]aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, ''Leo''; kama ilivyonenwa tangu zamani, ''Leo, kama mtaisikia sauti yake, Msifanye migumu mioyo yenu''.

[8]Maana kama Yoshua angaliwapa raha, asingaliinena siku nyingine baadaye. [9]Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. [10]Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi

[8] Lakini zingatia kwamba kuwa *"washirika wa Kristo"* sharti lake ni *"kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho."* John Piper kwa usahihi anatoa angalizo kuwa "ustahimilivu katika imani unathibitisha kuwa umekuwa mshirika wa Kristo. Hii ina maana kuwa kama huna ustahimilivu katika Imani, haionyeshi kwamba umejitenga na ushirika na Kristo, bali hujawahi kamwe kuwa mshirika wa Kristo." (Piper 1996: 3. Zinagatia pia Waebrania 3:14 (na 3:6))

yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake. [11]Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi. [12]Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. [13]Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.

Sehemu inapokea na kuendeleza mjadala umiofanyika katika **Ebr 3:7-19** na kuutumia kwa ajili yetu. **Mstari wa 2** unasema, *"Sisi nasi tumehubiriwa habari njema pia kama wao."* Hata hivyo, tumehubiriwa Injili (i.e., "habari njema") kwa njia bora zaidi. Kama **Ebr 1:1-2** inavyosema, *"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana."* Charles Fritsch anafafanua, "Lengo kuu la kusudi la ukombozi la Mungu ni kumpatia mwanadamu pumziko la kiungu ambalo linaashiriwa katika sabato ya duniani" (Fritsch 1947: 96; Jackson 2025b: aya ya (2)–(5)). **Ebr 3:7—4:11** inaweka wazi kuwa "pumziko" la kiungu linakamilika katika wokovu wa Agano Jipya, ambao ndio "pumziko la sababto'' la kweli. **Ebr 3:7–11, 15; 4:3, 7** yote hunukuu kutoka Zaburi **95:7–11** ikitoa mrejesho kuwa kile kizazi kilichokuwepo pale jangwani baada ya kutoka Misri walikosa "pumziko" lao kwa sababu ya uasi na kutokuamini (**Ebr 3:16–19**). Ingawaje Yoshua hatimaye aliwaongoza wana wa Israeli kuingia kwenye nchi ya Ahadi, hiyo haikuhusu the Sabbath "pumziko" la Sabato ambalo Mungu alikusudia, kwa sababu *"kama Joshua angewapa pumziko, Yeye asiongelea habari za siku nyingine baada ya ile*" (**Ebr 4:8**).[9] Badala yake, imebakia pumziko kwa ajili yetu "leo" (**Ebr 4:7**). Kila mmoja aliye na imani katika Kristo (**Ebr 4:2–3**) tayari *"amekwisha pumzika katika kazi zake,"* kama alivyofanya Mungu (**mst. 4**, akirejea **Mwa 2:2**), na *"na amekwisha ingia kwenye pumziko lake"* (**Ebr 4:10**), kama alivyoahidi Kristo (**Mat 11:28-30**). Kwa maneno mengine, "Sabato haina tena maana ya siku; . . . Kwa wale walio katika Kristo, kila siku kwao ni Sabato (ling. Rum 14:5)." (Wells and Zaspel 2002: 236) Kama A. T. Lincoln anavyohitimisha, kwa kuwa Sabato ya AK ni ishara iliyokuwa inatuonyesha Sabato ya kweli, ambayo ni pumziko letu la wokovu ndani ya Kristo, "Kristo analeta uhalisia wa kiroho; Kazi yake inatimiza lengo la Sabato, na kwa kwa njia ya Kristo huja kile ambacho kwa hicho Sabato ilikuwepo. Uhalisia wa pumziko la Sabato hushinda ile ishara." (Lincoln 1982: 215) Kwa kifupi, wakati Agano la Kale lilipoondolewa na Agano Jipya, na ishara za Agano la Kale nazo ziliondolewa; kwa hiyo, katika Agano Jipya Sabato na "siku maalumu" zingine za AK siyo lazima tena (**Rum 14:5; Gal 4:8–11; Kol 2:15–17**). Kama **Kol 2:16–17** inavyosema, *"Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika . . . au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato—mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo."*

Mjadala katika **Waebrania 3–4** ni sawa kabisa na maelezo ya Paulo kuhusu Imani na torati katika **Wagalatia 3–4**. Katika kitabu cha Wagalatia, Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani, na siyo kwa sheria (**Gal 3:6–11**), na ahadi ya baraka kupitia Ibrahimu inawahusu wale tu wanaomwamini Yesu Kristo (**Gal 3:14, 16, 18, 22, 29**). Sheria ilikuwa ni kwa matumizi kabla ya Kristo kuja (**Gal 3:23–25**). Vivyo hivyo, Kitabu cha Waebrania kinaeleza kwamba kwa sababu ya kutokuamini kwao, Wana wa Israeli wa AK hawakuweza kuingia katika ''pumziko'' la kweli ambalo Mungu aliahidi. (**Ebr 3:7–12, 16–19; 4:2, 5–6**). Ingawa Waisraeli hatimaye waliingia nchi ya ahadi, haijawahi kamwe kupata pumziko na amani bali waliendelea na vita, kuonewa na hata kuwa wakimbizi. Katika AK, kuacha kazi kwa siku moja kwa wiki (yaani, "kushika sabato") iliashiri pumziko lisilo kamili la waisraeli kutoka kwa maadui zao. Kwa upande mwingine, Yesu aliwashinda maadui wetu pekee wa kudumu—dhambi, Shetani na mauti. Kwa kuwa Kristo amekwisha fanya kazi yote inayohitajika kutupa wokovu wa milele, "pumziko" letu ni la kudumu. Matokeo yake, baba wa kanisa la kwanza Justin Martyr aliitambua hilo kwamba Ukristo hauhitaji kushika siku moja maalumu ya Sabato; badala yake, sisi kwenye "sabato ya kudumu" (Justin Martyr 1994a: 12; tazama pia *Waraka wa Barnaba* 1989: 15.8–9).

"Pumziko la Sabato" (**mst. 9**) ile inayozungumziwa hapa inaturejesha kwenye siku ya Siku ya Upatanisho, hususan, kwa Yesu kama kuhani wetu mkuu aliyefanya *"utakaso kwa ajili ya dhambi za watu wake"* (**2:17**). Lugha ya utakaso inaturejesha nyuma kwenye madhabahu/thekalu na Siku ya Upatanisho. Siku moja ya Upatanisho, kuhani mkuu hunyunyiza damu ya mnyama wa dhabihu kwenye kiti cha rehema ikilichopo mahali patakatifu pa patakatifu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu (tazama maelezo hapo juu katika **Ebr 2:17**). Siku ya Upatanisho inaitwa *"sabato ya pumziko la hakika"* (**Law 16:31**) na *"sabato ya pumziko kamili"* (**Law 23:32**). Lugha hii inatutazamisha kweye kile alichofanya Yesu, kwa kuwa ni dhabihu yake ya upatanisho pekee inatupa sisi "pumziko kamili." Kwa hakika, mambo makuu ya ibada yanayofanyika katika siku ya upatanisho yalikuwa

[9] Katika Waebrania, "Yoshua" ni "Yehoshua" au "Yeshua"; jina hilo hilo kwa kiingereza ni "Yesu." **Ebr 4:4, 8** tumia neno la Kiyunani, *Iēsous,* wote Yoshua na Yesu. Kwa huyu ''Yesu'' wa kwanza (Yoshua) hakuweza kuwaongoza watu wake kwenye pumziko la Mungu, lakini Yesu wa pili (Kristo) aliweza na alifanya.

“kivuli” kinachotutazamisha kwa Kristo: taratibu za ibada zilifanyika hekaluni (**Law 16:23, 20, 33**)—Kristo ni hekalu la kweli (**Yoh 1:14; 2:18–22**); kuhani mkuu alifanya desturi za ibada (**Law 16:2–3, 32–33**)—Kristo ni kuhani wetu mkuu (**Ebr 4:14–15; 5:5–10; 8:1–6; 9:11; 10:21**); ng’ombe dume na mbuzi aliotolewa kama dhabihu za dhambi na damu zao zilimwagika (**Law 16:8–9, 15**)—Kristo alitolewa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu na damu yake ilimwagika (**Ebr 7:27; 9:12, 14, 26, 28**); kuhani mkuu aliingia patakatifu pa patakatifu nyuma ya pazia (**Law 16:12–15**)—Mwili wa Kristo ndiye pazia la kweli **Ebr 10:19–20**) na aliingia pakatifu pa patakatifu (**Ebr 8:1–2; 9:11–12, 24**); damu ya mbuzi ilinyunyizwa juu ya kiti cha rehema (**Law 16:14–15**)—Kristo yupo kwenye kiti cha rehema (**Rum 3:25**; kulingana **Kut 25:17**, LXX); dhambi za taifa ziliwekwa juu ya mbuzi wa azazeli (**Law 16:20–21**)—Kristo alichukua dhambi zetu (**Isa 53:4–5; Ebr 9:28; 1 Pet 2:24**) na akawa dhambi kwa ajili yetu (**2 Kor 5:21**); mbuzi wa azazeli alifukuzwa jangwani (**Law 16:21–22**)—Kristo aliongozwa kwenda jangwani ametengwa mbali na Mungu (**Isa 53:8; Mt 27:46**); miili ya Wanyama walichomwa nje ya kambi (**Ebr 13:11**)—Kristo*“aliteswa nje ya kambi”* (**Ebr 13:12**).

Hitimisho la upatanisho wa Kristo “pumziko kamili” kwamba ambacho yeye tu huweza kutupa kinaonekana katika ulinganifu wa haya mawili ni siku ya upatanisho na dhabihu ya Yesu na upatanisho: Kwanza, siku ya Upatanisho ilikuwa kama “ukumbusho” kwa ajili ya dhambi kila mwaka. Kwa njia ya dhabihu ya Kristo, Baba *“hatakumbuka kamwe dhambi zao na makosa yao.”* (**Ebr 10:3, 16–18**). Pili, kwa kufufuka kwake na kupaa kwake, Yesu *“ameketi mkono wa kuume wa Mungu”* katika patakatifu pa patakatifu pa kweli mbinguni (**Ebr 1:3; 10:12, 14**; pia tazama **Zab 110:1; Mk 16:19; Lk 22:69; Rum 8:34; Efe 1:20–21; Kol 3:1; 1 Pet 3:21–22**). “Kwa kuwa utoaji wa dhabihu ulihusisha kitendo cha *kusimama* mbele za Mungu au mbele ya madhabahu ([**Ebr**] **10:11; Kum. 10:8; 18:7**), kitendo tofauti cha Yesu cha *kuketi chini* kinadhihirisha hitimisho la tendo la utoaji wa dhabihu ya Kristo ([**Ebr]** 10:12). Lakini, wakati huo huo, kuketi kwake kwenye kiti cha enzi mkono wa kuume wa Mungu kunampa Yeye kumfikia na hadhi inayoendelea, na maombezi yanayoleta matokeo.” (Nelson 2003: 257)

Wakristo wa mwanzo katika siku za awali walitambua umhimu wa mwisho wa Agano la Kale kwa kubadili mtazamo wao kuhusu Sabato na hawakuwa wakiendelea ‘‘kuheshimu siku ya saba’’ kama siku ya mapumziko na ya kuabudu. Katika baraza la Yerusalemu (**Mdo 15**) mjadala ulihusu ikiwa ni lazima muumini mpya ambaye si mwisraeli, kutahiriwa na kushika sheria ya Musa (**Mdo 15:5**). Jibu halikuwa na ubishi na lilikuwa ni “Hapana!” Kutunza Sabato (au hata sabato nyinginezo “Siku ya sabato” kwa mataifa wasio waisraeli) haikuwa lazima kwa waamini wa mataifa kwa agizo la mitume la **Mdo 15**. “Moja ya jambo la kiimani la kiyahudi ambalo lilikuwa likizingatiwa kwa umakini mkubwa ilikuwa ni kutunza Sabato, na pamoja na hayo Wakristo wa kiyahudi walihamisha siku yao ya ibada kutoka Jumamosi hadi Jumapili ambayo waliita ‘siku ya Bwana’ [**Ufu 1:10**]” (Maier 1973: 122; pia tazama *Didache* c.70-110: 14.1). Wakristo walianza kukusanyika siku za Jumapili kwa ajili ya heshima ya siku ya kufufuka kwake Kristo, na hilo lilitokea mwanzoni mwa (**Mdo 20:7; 1 Kor.16:2**). Hili linathibitishwa na mababa wa mwanzo wa Kanisa. Ignatius wa Antiokia alisema, “Kila Rafiki wa Kristo na aishike siku ya Bwana kama sherehe, siku ya ufufuo, malkia na kuu kuliko siku zote” (Ignatius 1989: 9). Justin Martyr yeye vile vile alisema, “Sote tunashika hili kusanyiko la pamoja siku ya Jumapili, kwa kuwa ilikuwa ni siku ya kwanza, ambayo katika hiyo nguvu ya Mungu igeuzayo giza na vitu vyote iliufanya ulimwengu, na Yesu Kristo mwokozi wetu alifufuka kutoka kwa wafu siku hiyo hiyo.’’ (Justin Martyr 1994b: 67). Ushahidi kutoka karne ya pili unatufunulia kwamba “hakuna fununu yoyote kuhusu ubishi kwamba ikiwa wakristo wanatakiwa kuabudu siku ya Jumapili, na hakuna kumbukumbu ya kikundi chochote cha ambacho hakikuwa kinaabudu siku ya Jumapili” (Bauckham 1982: 236).

Wakristo hawajapewa “agizo” la kuabudu siku za Jumapili. Wapo huru kuabudu siku yoyote ya wiki. Hata hivyo, wakristo huabudu siku ya Jumapili (“siku ya Bwana”) amabyo ina upendeleo kwa ibada ya Kikristo zaidi kuliko ibada siku ya Sabato ya Kiyahudi. Hii ni kwa sababu Ufufuo wa Yesu unatimiza ile ahadi ya pumziko lililokuwa linaashiriwa katika Sabato ya AK, na pia kuna mwunganiko kati ya siku ya saba (Sabato) na siku ya kwanza ya wiki ambayo Wakristo huabudu. Muunganiko huo haugeuzi siku ya kwanza ya wiki kuwa siku ya kupumzika kimwili bali kuifanya kuwa siku ya “sherehe ya pumziko la Sabato ya kweli ya wokovu ulioletwa na Kristo ambaye waamini humwabudu na kuwa na ushirika naye.” (Lincoln, 1982: 205, 215–16).[10] Hakuna sababu ya kutumia mahitaji ya Sabato ya Agano la Kale la kupumzika kimwili kwa ajili ya Siku ya Bwana ya AJ.

[10] Walter Martin 1985: 459–73 hutupa upinzani dhidi ya Biblia wa madai yenye maelezo ya kina ya Muumini wa Dhehebu la Wasabato kwama siku ya saba (Sabato) ndiyo siku wanayopaswa wakristo kuabudu (pia tazama Martin 1999 n.p.). Ni jambo ambalo wakristo huzingatia kidogo sana “wasabato” kwamba, yote mawili yaani wakati Mungu anapumzika na wakati Mungu anaitakasa siku ya saba **Mwa 2:1–3**, hakuna amri kuhusu kuabudu siku ya Sabato au kushika siku ya saba, “wala hakukuwa na umhimu wa kidini uliohusianishwa na hiyo siku, kuhusiana na majukumu ya mtu au tabia zake” (Wells and Zaspel 2002: 214n.292). Amri ya nne inayohusu siku ya Saba inasema tu kwamba Wana wa Israeli wanatakiwa ‘‘*kushika Siku ya Sabato*’’

Ukweli kwamba Siku ya Sabato ilikuwa ni "kivuli" ambacho hufikia kutimia kwake kwa uhalisia katika kule kutokuwa na mwisho kwa pumziko la Sabato yetu katika Kristo pia imedokezwa na Mungu pale alipotaja kwa mara ya kwanza pumziko la siku ya saba katika **Mwa 2:1–3**. William Dumbrell anafafanua kwamba ni "ni jambo lisilo la kawaida" kwamba "tofauti na siku sita, siku ya saba haikutajwa kuwa na mwisho wala mwanzo wake [linganisha **Mwa 1:5, 8, 13, 19, 23, 31** pamoja na **2:2–3**]. Kusudi la maelezo linaonekana kutilia mkazo wa kipekee na wa kimahususi wa nafasi ya siku ya saba isiyo na ukomo. . . . Siku ya Sabato isiyo na ukomo inatupa muktadha ambao ndani yake Maisha ya bustanini yanatakiwa yapatikane na kudumu katika jamii ya wanadamu**."** (Dumbrell 2001: 220–21) Moja ya tahadhari au sifa kwenye maelezo hapo juu ni kwamba kudhihirishwa kwa mwamini' pumziko, yale ''Maisha makamilifu,'' yatapatikana kwenye mbingu mpya na nchi mpya, ambapo *"watapumzika kutoka kwenye taabu zao"* (**Ufu 14:13**), tofauti na wasioamini, *"ambao hawana pumziko mchana wala usiku"* (**Ufu 14:11**). Hii inaonyesha kwamba ingawa kwa njia ya Imani tumeingia kwenye pumziko lisilo na ukomo sasa, kuna namna ambayo pumziko halijafikia ukamilifu wake katika kila eneo. Hili linakubaliana na ukweli kwamba kama walivyokuwa wana wa Israeli, kuna namna ambayo kanisa, ingawa limeingia kwenye pumziko la Mungu, hata hivyo bado lipo jangwani (tazama **Ufu 12:13-17**). Muambatano huu unaojulikana kama "tayari, lakini bado" upo ndani ya Ufalme huu. "Haijafahamika sana, kwa sehemu, kwa ama manabii wa AK au wanafunzi wa AJ, walikuwa na mchanganyiko wa kile kinachojulikana kama, tayari-lakini bado ya kipindi cha masihi." (Yarbrough 1996: 65): yaani, ufalme wa Mungu na utawala wa Kristo umesimikwa, unatambulika kikanuni, na upo sasa(kilicho ''tayari'' cha Ufalme wa Mungu); hata hivyo, bado hawajadhihirishwa kwa ukamilifu, lakini wanangoja kudhihirishwa katika utukufu wao wote baadaye (kilicho "bado" cha ufalme wa Mungu). Kwa sasa, mema na mabaya yapo kwa wakati mmoja, lakini utakuja wakati wa mavuno na kutenganishwa mema na mabaya. Baadhi ya mifano ya Yesu, kama vile mfano wa ngano na magugu (**Mt 13:24-30, 36-43**) na mfano wa nyavu (**Mt 13:47-50**), inaongea kuhusu hali hizi mbili katika ufalme. Waamini tayari wameufikia Yerusalemu ya Mbinguni (**Ebr 12:22**); lakini utukufu mkamilifu wa Yerusalemu mpya unakuja wakati ujao (**Ufu 21:10-11**).

Maneno ya kutia moyo yaliyopo katika **mst. 11** *"kujitahidi kuingia katika raha yake"* is based on God's revelation to us: *"Neno la Mungu"* (**mst. 12**). Neno la Mungu *"Neno la Mungu li hai n ani kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huchooma hata kugawanya nafsi na roho, viungo na mafuata yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kutambua mawazo na makusudi ya moyo* "hai," "lina nguvu," "linachoma," na *"li jepesi kuatambua,"* huko kote hata kufikia *"mawazo na makusudi ya moyo."* Hii inaenda sambamba na kile alichotuambia Yesu, *"maneno niliyowaambia ninyi ni roho ten ani uzima"* (**Yoh 6:63**), na *Yeye anayenikataa Mimi na asiyepokea maneno niyasemayo Mimi, anaye amhukumuye, Neno nisemalo ndilo litakalomhukumu siku ile ya mwisho.* (**Yoh 12:48**). Pia kulinganishwa kwa Neno na upanga tunapata katika **Efe 6:17** (pia tazama **Isa 49:2; Ufu 1:16; 19:15, 21**). Kuhusishwa kwa hali ya kuwa hai, ukali, kuchoma, uwezo wa kutambua wa Neno, hayo yanapatikana katika kuhuishwa kwa asili yetu ya Maisha kwamba Neno linapenya, huweza kutofautisha, hutambua: *"nafsi na roho,"* nayo ni, fahamu zetu, hisia, na Maisha ya kiroho; *"viungo na mafuta,"* nayo ni, Maisha yetu ya kimwili; na *"mawazo na makusudi ya moyo,"* i.e., mambo yaliyo ndani yetu hasa. Kile ambacho **mst. 12** hutuambia kinasisitizwa na **mst. 13**, unatuhimiza kwamba *"hakuna kiumbe kilichojificha machoni pake, lakini vitu vipo wazi na utupu machoni pake Yeye aliyetuumba."* Kwa kifupi, Mungu huchunguza na atamhukumu kila mmoja na kila kitu, ndani nan je; hakuna kitakachofichika au atakachofichwa. Kama Yesu mwenyewe alivyosema, ''Kama Yesu mwenyewe akivyosema, *"Hakuna jambo la siri ambalo halitawekwa wazi, na kilichofichika ambalo halitajulikana. Kwa sababu hiyo, kile usemacho gizani, kitasikiwa mwangani, na kile ulichonong'ona katika chumba cha ndani kitatangazwa kwenye dari ya nyumba."* (**Lk 12:2-3**; pia tazama **Mt 10:26-27; Mk 4:22; Lk 8:17**)

C. Kama kuhani mkuu mkamilifu, Yesu huwapa wale waaminifu wokovu wa milele (4:14—6:18)

1. Ni lazima tubaki katika uaminifu. (**4:14-16**).

[14]Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. [15]Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. [16]Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

Ingawa Yesu akiwa kama kuhani wetu mkuu ametajwa katika **2:17** na **3:1,** hapa maudhui yameshatajwa kwa namna rahisi Zaidi na itawekwa wazi zaidi kupitia **8:5**. Katika **mst. 14** tunajifunza mambo matatu kuhusu

"kuitakasa," na *"kutokufanya kazi yoyote"* katika siku hiyo. Hakuna maelezo mahususi kuhusu kuhudhuria ibada au mambo mengine.

kuhani wetu mkuu; (1) yeye ni "mkuu," inayomfanya yeye kuwa mkuu kuliko kuhani mkuu mwingine yeyote; (2) yeye *"amepita katika mbingu,"* kinachomtofautisha yeye na kumweka juu zaidi ya makuhani wakuu wote, yeye pekee, jambo kubwa zaidi, waliweza kuningia patakatifu pa patakatifu ndani ya hekalu; na (3) yeye ni *"Mwana wa Mungu."* Hili lilitajwa kwa mara ya kwanza katika sura ya **1:5** na likajadiliwa mwanzoni likihusishwa na Agano la Daudi na Yesu kama Mfalme Masihi. Sasa, hii inamtofautisha yeye na kuhani mkuu mwingine yeyote, ambao wote walikuwa watu wa kawaida. Ni wazi kabisa kwamba Yesu ni kuhani mkuu wa hadhi ambayo sisi ni lazima *"tushike sana ungamo letu,"* kusudi ambalo limeelezwa katika sura ya **2:1-18**, na ya **3:7—4:13** na litarejewa tena baadaye.

Sababu nyingine ya kushika ungamo la Imani yetu inatolewa kwenye mst. wa 15, ambayo ni, kwamba Yesu anaweza *"kuchukuliana na udhaifu wetu,"* kwa sababu *"amejaribiwa katika mambo yote kama sisi, pasipo kutenda dhambi."* Guthrie anafafanua kwamba neno n "kuchukuliana" inaelezea si tu kutuhurumia bali linaonyesha "kuteseka pamoja na sisi" (Guthrie 1983: 122). Yesu kujaribiwa, *"katika mambo yote"* ni muhimu. Hakuna jaribu ambalo tunaweza kukutana nalo—tamaa, jaribu la kusema uongo, kuiba, kutamani, kudanganya, Maisha yasiyo na utaratibu, au kitu chochote zaidi-ambacho Yesu hajawahi kukutana nacho. Tofauti ni kwamba katika majaribu yake yeye hakushindwa. Hiyo ni muhimu sana. Mara nyingi, tunaweza kushindana na majaribu yetu kwa muda fulani lakini mwishoni tunashindwa. Kristo hakufanya hivyo. Alishinda hadi mwisho. Tunaweza kusema tulishindwa kwa sababu jaribu lilikuwa kubwa sana. Hatuwezi kujua jaribu linaweza kuwa kubwa kwa namna gani, kwa sababu tunashindwa hata kabla jaribu halijamaliza kusudi lake. Kristo peke yake anajua jaribu linaweza kuwa kubwa kwa namna gani, kwa sababu kila wakati alishinda kila jaribu hadi mwisho.

Lile neno "Kwa hiyo" linaanza katika mstari wa **16** linasema hivyo kwa sababu Yesu alijaribiwa kwa kila namna kama sisi tulivyo, anajua tunachokabiliana nacho na kile tunachopitia; anajua udhaifu wetu, lakini anatujali sisi. Kwa hiyo tunaweza kumwendea yeye na *"kumkaribia"* yeye, siyo katika hali ya hofu au hata kusitasita, bali *"kwa ujasiri,"* tukijua kwamba kuhani wetu mkuu sana si kwamba anatuhurumia tu bali pia amejaa rehema na neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji. Hii inaelezwa kwa uzito Zaidi kwa Kiyunani *"kumkaribia"* ni *proserchomai.* Katika Septuagint, neno hilo linatumia wakati kuhani anamkaribia Mungu. Sasa, waamini wote ni makuhani machoni pa Mungu. (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6**), na si kwamba tunaingia kwenye hekalu la kidunia bali tunaingia katika uwepo wa Mungu mwenyewe ambaye, katika nafsi ya Roho Mtakatifu, kimsingi anakaa ndani yetu. Ni nini basi kinaweza kutupa uhakika kuliko hicho?

2. <u>Kama kuhani mkuu, Kristo ni chanzo caha wokovu wetu (**5:1-10**).</u>

[1]Maana kila kuhani mkuu aliyetwaliwa katika wanadamu amewekwa kwa ajili ya wanadamu katika mambo yamhusuyo Mungu, ili atoe matoleo na dhabihu kwa ajili ya dhambi; [2]awezaye kuwachukulia kwa upole wao wasiojua na wenye kupotea, kwa kuwa yeye mwenyewe yu katika hali ya udhaifu; [3]na kwa sababu hiyo imempasa, kama kwa ajili ya watu, vivyo hivyo kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi. [4]Na hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni.

[5]Vivyo hivyo Kristo naye hakujitukuza nafsi yake kufanywa kuhani mkuu, lakini yeye aliyemwambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa. [6]kama asemavyo mahali pengine, Ndiwe kuhani milele Kwa mfano wa Melkizedeki.

[7]Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu; [8]na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; [9]naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii; [10] kisha ametajwa na Mungu kuwa kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.

Mistari minne ya kwanza hujadili juu ya ukuhani wa Haruni. Neno la utangulizi ''Kwa ajili ya'' inahusiana na **4:14-16**, ambayo inamjadili Yesu kama kuhani mkuu sana. Kwa ujumla yanatuonyesha yanayohitajika ili mtu awe kuhani mkuu na kudhihirisha, hasa wakati yanapochukuliwa pamoja na mstari ya 5-10, kwamba Kristo siyo tu alitimiza mahitaji ya ukuhani mkuu lakini yeye ni mkuu zaidi kuliko ukuhani wa ukoo wa Haruni. Kulingana na mstari wa **1**, kila kuhani mkuu ni: (1) *"huchukuliwa miongoni mwa wanadamu"*; (2) *"anateuliwa kwa niaba ya watu"*; (3) anawajibika kwa *"mambo yamhusuyo Mungu"*; (4) ili aweze kutoa *"sadaka pamoja na dhabihu kwa ajili ya dhambi."* Yesu alitimiza masharti hayo yote kwa njia ambazo hakuna kuhani wa kidunia anayeweza. Kwanza, Yesu ni mtu kamili, lakini wakati huo huo ni Mungu kamili (tazama Menn 2025: 221-34). Pili, Yesu ni *"mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Yesu Kristo''* (**1 Tim 2:5**), ambaye aliitwa na kuteuliwa na Baba na kwa ukamilifu *"nimemaliza kazi uliyonipa niifanye"* (**Yoh 17:4**). Tatu, Yesu siyo kwamba alifanya tu *"mambo yamhusuyo Mungu,"* bali pia *"Mwana hawezi kufanya jambo lolote isipokuwa lile ambalo amwona Babab akifanya, kwa maana chochote afanyacho Baba, hayo Mwana huyafanya kwa namna hiyo hiyo."* (**Yoh 5:19**; pia

tazama **Yoh 8:28; 12:49**). Nne, Yesu *ni* "zawadi" kutoka kwa Mungu (**Yoh 3:16**) aliyefanya *"dhabihu moja kwa dhambi zote kwa nyakati zote"* (**Ebr 10:12**). Kwa kuzingatia **mst. 2**, Yesu aliweza na alifanya *"alitenda kwa upole"* kwa ajili ya watu kwa sababu yeye ni *"mpole na mnyenyekevu wa moyo"* (**Mt 11:29**). Zaidi sana *"kwa kuwa Yeye mwenyewe alijaribu kwa njia ya mateso aliyopata, Anaweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa."* (**Ebr 2:18**) na anaweza *"kuchukuliana na udhaifu wetu"* kwa kuwa yeye *"amejaribiwa katika mambo yote kama sisi, pasipo kutenda dhambi"* (**Ebr 4:15-16**). Pamoja na hayo, Yesu anawapita wale makuhani wengine wote, kwa hana haja ya kutoa dhabihu kwa ajili yake mwenyewe (**mst. 3**), kwa sababu yeye hakuwa na dhambi. Badala yake, *"alimfanya Yeye asiyejua dhambi awe dhambi kwa ajili yetu, ili tuwe wenye haki wa Mungu katika Yeye"* (**2 Kor 5:21**).

Mistari ya 5-10 unaendelea kumwonyesha Kristo, kuwa ana kiwango kikubwa zaidi cha ukuu kuliko ukuhani mkuu wa ukoo wa Haruni ambacho Mungu amempa kama kuhani mkuu zaidi ya makuhani wote wakuu—kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki (**mst. 5-6, 10**). **Mistari ya 5-6** inaonyesha kwamba, ni Mungu Baba ndiye aliyemteua Kristo kuwa kuhani wetu mkuu. **Mstari wa 5** unanukuu **Zab 2:7** na kwa hiyo (pia tazama **Zab 2:2**). Kama ilivyoelezwa kwenye mstari wa **5**, Kristo hakujitukuza mwenyewe bali alitukuzwa na Baba (**Yoh 8:54**). **Mstari wa 6** pia unaonyesha Kristo ateuliwa na Baba. Inanukuu **Zab 110:4** inaonyesha kwamba ukuhani wa Kristo ni mkuu pasipo mwisho kuliko kuhani wa kawaida wa kibinadamu kwa sababu ni wa "milele" na ni *"kuhani kwa mfano wa Melkizedeki."* Hii itaelezwa kwa ndani sana katika sura ya 7.

Mistari ya 7-10 pia inatueleza kuhusu asili ya kibinadamu ya Yesu kama kuhani wetu mkuu, kwa sababu alikuwa mtu kamili na Mungu kamili vile vile. Kama mwanadamu kamili, alifanya maombi na maombezi kwa Baba, kwa kulia machozi, na alisikiwa kwa sababu ya unyeyekevu wake. (**mst. 7**), alifanywa mkamilifu kwa njia ya majaribu yake (**mst. 8-9**), na akawa, tofauti na makuhani wakuu wa mkondo wa Haruni, *"kwa wale wote wanaomtii yeye chanzo caha wokovu wa milele''* (**mst. 9**). Wakati Rafiki wa Yesu, Lazaro alipofariki Yesu alilia (**Yoh 11:35**), na maombi kwa ajili ya Lazaro kuwa hai yalisikiwa (**Yoh 11:41-44**). Hata hivyo, **mst. 7** huhusika kimsingi na inamhusu maombi ya Yes una dua zake katiak Bustani ya Getsemane na pia msalabani. Hata kama maombi ya Yesu akiwa bustanini, kwamba *"kama inawezekana, kikombe hiki kiniepuke''* (**Mt 26:39**) hakujibiwa, lakini alisema, *"lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo wewe.''* Maombi yake yalisikiwa, Mungu alimtuma malaika ili amtie nguvu (**Lk 22:43**), na Yesu siyo kwamba alikubaliana tu na mapenzi ya Mungu bali pia aliyatimiza. Kwa sababu ya utii wake mkamilifu, kuanzia mwanzo hadi mwisho, kutoka kwake tunaweza, *"kupata rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji [yetu]''* (**4:16**). Yesu "alijifunza utii" na kukamilishwa kwake "kufanywa mkamilifu" (**mst. 9**) usifikiri kwamba mtu amekuwa na ukosefu wa utii na kutokuwa mkamilifu. Hiyo inaonyesha kuwa utii wake na ukamilifu wake vimejaribiwa, na kusafishwa, kuwa na kina katika mambo ya Mungu, na akadhihirishwa kwa yeye kuwa mtii na pia kukutana na mateso.

3. <u>Ni lazima tujitahidi kufikia ukomavu wa Kiroho. (**5:11—6:3**).</u>

[11]Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia. [12]Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. [13]Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. [14]Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.

6 [1] Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, [2] na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele. [3]Na hayo tutafanya Mungu akitujalia.

Huyo "yeye" anayeongelewa katika **mst. 11** kimsingi anahusiana na Melkizedeki, ambaye atazungumziwa katika sura ya 7. Haya maonyo dhidi ya kufubaa kiroho na kutiwa moyo kwa ajili ya kufikia ukomovu wa kiroho upo kwenye msingi wa muundo wa kitabu hiki. Kwa hiyo, katika sura ya 1 mwandishi ameeleza kuhusu ukuu wa Kristo; kisha anatutia moyo katika sura ya **2:1-4** kuwa*"kuzingatia zaidi yale tuliyosikia" na kuto "puuza wokovu mkuu."* Kisha anaelezea jinsi ambavyo vitu vipo chini ya Kristo (**2:5-8**), jinsi ambavyo Kristo hutupa wokovu kwa njia ya Kifo na mateso yake (**2:9-18**), na jinsi Kristo alivyo mkuu kuliko Musa (**3:1-6**); maelezo hayo yaliambatana na onyo la kutokuwa wasioamini kama walivyokuwa wana wa Israeli (**3:7-19**) bali tuingie kwenye raha ya sabato yetu kwa njia ya Imani (**4:1-13**) na, kwa hiyo akatutia moyo kubakia kuwa waaminifu (**4:14-16**). Sasa, baada ya kueleza jinsi alivyo, kama kuhani mkuu, Kristo ndiye chanzo cha wokovu wetu (**5:1-10**), anatutia moyo kukaza mwendo hadi kufikia ukomovu wa kiroho (**5:11—6:3**).

Anasema katika **mst. 12** kwamba *"kufikia wakati huu mlitakiwa kuwa waalimu."* Ingawa kuwa "mwalimu" ni ni karama ya kiroho (**1 Kor 12:29; Efe 4:11**), kila mwumini kila mara anatakiwa kuwa *"kutoa majibu kwa mtu yeyote anayeuliza kwa habari ya tumaini lililo ndani yake*" (**1 Pet 3:15**). Hii sehemu inatueleza kuwa sote tuna wajibu wa kukua katika kulijua Neno la Mungu. Waliokomaa kiroho wana wajibu wa kuwafundisha wale ambao ni wachanga kiroho. Kwa kuongezea, kama sura **5:14** unavyoeleza, ukomavu wa kiroho wa uelewa wetu wa Neno la Mungu siyo tu kwa habari ya kusoma na kujifunza. Bali, ukomavu wa kiroho na ufahamu hutokea *"kutokana na kutendea kazi."* Biblia ya tafsiri ya ESV inaeleza hivi: waamini waliokomaa ni *"ni wale ambao uwezo wa kupambanua umefunzwa kutokana na kuzoelea kupambanua mema na mabaya."* Wazo hili ni kama lile aliloeleza Paulo katika **1 Tim 4:7b**, *"jizoeze mwenyewe kwa ajili ya utauwa."* Nidhamu ya kiroho inahitaji siyo tu kujifunza kila wakati bali pia kuyaweka kwenye utendaji kila wakati. Kuna funguo nne za kufikia ukomavu wa kiroho ambazo zimejadiliwa katika **mst. 13-14**—na zote hizo vimeungana. Nazo ni: (1) "chakula kigumu"; (2) "kutendea kazi"au "kuendelea kutendea kazi"; (3) nguvu ya kupambanua; na (4) uwezo wa kutofautisha mema na mabaya.

(1) *Chakula kigumu.* **Mstari wa 13** inawafananisha wale wanaotumia maziwa peke yake na watu wasio na ujuzi wa neno la haki. **Mstari wa 14** unaanza na neno "Lakini," ambalo linaloonyesha tofauti, na kisha huongea kuhusu "chakula kigumu." Yote mawili "maziw" na "chakula kigumu" ni viwakilishi vinavyosimama kwa ajili ujuzi au kutokuwa na ujuzi wa kushika *"neno la haki"* linaongelewa kwenye **mst. 13**. Hilo *"neno la haki"* ndilo kusema Neno la Mungu—Biblia. Hilo limewekwa wazi **Zaburi 119** na **Isaya 45** amablo pia huunganisha neno la Mungu na haki. Kwa nini Biblia inaitwa "neno la *haki*"? Haki maana yake ni utakatifu; ukamilifu; kuwa sawa katika maeneo yote. Kwetu sisi kama wanadamu, "haki" inahusika na tabia na maadili. Kama tabia zetu zikiwa za "haki," ina maana matendo yetu ni yas haki; tunaishi maisha ambayo yanampendeza Mungu. Biblia inaitwa *"neno la haki"* kwa sababu Mungu mwenyewe haki mkamilifu. Inaitwa *"neno la haki"* kama njia ya kutusaidia sisi kuona kuwa neno la Mungu limekusudiwa kubadilisha Maisha yetu na kutufanya tutende matendo yanayotufanya wenye haki, wasio na upendeleo na watakatifu, kama Kristo alivyo mwenye haki. "Neno" (kile asemacho Mungu) na "haki" (jinsi tunavyoenenda) vinatakiwa kwenda pamoja. Kwa kuunganisha Neno la Mugu na kuishi maisha ya haki, na kuongelea ujuzi wa mtu juu ya matumizi ya Neno, mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatuambia kwamba Neno la Mungu linatakiwa liwe sehemu ya maisha yetu. Tunalihitaji neno la Mungu ndani yetu kimsingi ili litubadilishe, kubadilisha mitazamo yetu na kubadilisha matendo yetu. Neno la Mungu linamfunua Mungu, yaani, yeye ni nani na mapenzi yake kwa ajili yetu ni yapi. Kama tunampenda Mungu tutahitaji tutahitaji kumpendeza yeye na kufanana naye. Neno lake linapokuwa sehemu ya Maisha yetu, Roho Mtakatifu hulichukua neno na kulifanyia kazi ndani yetu ili tuweze kuanza kufikiri na kutenda kama Yesu mwenyewe (tazama **Flp 2:12-13**). Tofauti kati ya mtu mchanga kiroho na mtu mkomavu kiroho ipo katika uwezo wa mtu kulipokea, kulitafakari, kuliweka moyoni na kulitumia *"neno la haki."* Linapokuwa sehemu yetu linaanza kutuathiri na kubadilisha namna tunavyofikiri, tunavyohisi, tunavyotenda, na jinsi tunavyowatendea watu. Neno linakuwa maisha na uhalisia.

(2) *"Kutenda au "kudumu katika kutenda."* Misha ya Kikristo ni ya ukamilifu—yamekusudiwa kuathiri maeneo yote ya maisha. Katika **Yoh 3:36**, Yoh husema, *"Amwaminiye Mwana anao uzima wa milele; lakini yeye asiyemtii Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."* Yoh amefanya kitu kile kile kinachoendelea katika kitabu cha Waebrania. Katika kipengele cha kwanza cha **Yoh 3:36** anatumia neno la kawaida la "kuamini." Lakini kwenye sehemu ya pili ya mstari hasemi "bali yeye *asiyeamini* hataona uzima*."* Badala yake, anatumia neno "kutii," ambalo linaongelea juu ya kutoamini lakini likiwa linaeleza hali ya mtu kukosa utii kwa vile anavyoishi maisha yake. Kwa maneno mengine, Imani halisi kwa Yesu siyo jambo linalotokea kwenye ufahamu peke yake—ingawa ni muhimu. Bali, Imani ya kweli huathiri Maisha yetu, inaathiri tunavyotenda na inaathiri vile tunavyowatendea watu.

(3) *Nguvu ya kupambanua.* Hapa ni eneo ambalo kile tunachojua au tunachofahamu na kile tunachoamini vinaungana kwa undani na pasipo kupishana na vile tunavyoishi maisha yetu. **Mstari wa 14** unatuambia jambo la muhimu siyo tu kujua mambo mengi, bali "kupambanua" inahusisha *hekima*; maamuzi; ufahamu; uwezo wa kutoafautisha na kutumia tunachojua.

Upambanuzi, hekima, maamuzi, na ufahamu unaweza tu kupatikana tunapojifunza kile asemacho Mungu, kufikiria, kutafakari, na kutendea kazi.

(4) *Uwezo wa kutofautisha mema na mabaya.* Huu ni ufunguo wa nne. Hii ni zaidi ya vile tunavyofikiri. Ninachomaanisha ni yote mawili mema *kiutendaji* na mabaya na mazuri *kikanuni* na mabaya. Kwa kusema mema "kiutendaji" na mabaya ninamaanisha mambo yanaweza kuwa sahihi au yasiwe sahihi, mema au mabaya vile yanavyoonekana yenyewe. Kuua na kutoa mimba ni mabaya. Kwa nini? Kwa sababu kwa kufanya hivyo unatoa uhai wa mtu asiye na hatia kimakosa, uhai aliotoa Mungu, uhai wa mtu umeumbwa kwa mfano wa Mungu. Kuonyesha kuwapenda watu ni ni kitu chema. Kwa nini? Kwa sababu *"Mungu ni pendo"* (**1 Yoh 4:8**). Hiyo inaweza kuwaonekana kuwa jambo la msingi sana, lakini kupambanua lililo sahihi na lililo sahihi, jema na baya, tunatakiwa kumjua Mungu na kulijua Neno lake. Sababu ni kwamba ili kupambanua ikiwa kufanya kitu fulani ni

vibaya au vizuri kukifanya, ni sahihi au siyo sahihi, ni sawa na maadili au ni kinyume na maadili, ni lazima kuwe na vigezo vya kufanya maamuzi—na msingi unaotosha na wenye kiwango ni Mungu. Hata wanafalsafa wasio wakristo wanatambua hili. Mwanafalsafa asiye-Mkristo Richard Taylor husema, "Kizazi cha kisasa, hupinga sana au kidogo wazo la mtoaji wa sheria wa kiungu, pia wameacha sheria za haki za kimaadili za maana zinazoelezea mambo sahihi na yale yasiyo sahihi, bali ya kutambua kwamba, kwa kumweka Mungu mbali, wameacha sheria za maadili sahihi na yale yasiyo sahihi vile vile. . . . Wazo la wajibu wa kimaadili [ni] hauwezi kufahamuka nje na wazo la Mungu." (Taylor 1985: 2-3, 84) Kama usahihi na kutokuwa sahihi, mema na mabaya ni mambo yaliundwa kijamii tu, basi hakuna msingi wa kusema walichofanya Wanazi na wanachofanya wajahidina wa kiislamu ni jambo baya. Mnazi au Mwislamu angesema kirahisi, ,"Lakini hilo ni utamaduni wetu wanazi au waislamu—usituletee mawazo ya utamaduni wako kwetu." Pia kuna jambo ninaloliita jema au baya "kikanuni". Kwa mfano, **Flp 4:15** inasema tunatakiwa *"kusema kweli katika upendo."* "Ukweli" ni sehemu ya kiutendaji—mambo ni ama kweli au uwongo. Lakini "upendo" ni eneo la kikanuni. Tunavyofanya au tunavyosema jambo mara zote ni munimu kama tunachosema na tunachofanya.

Sura ya 6:1 inahusisha aina mbili za kutiana moyo: (A) Mambo ya kuacha kufanya, nayo ni, *"kuyaacha mafundisho ya awali kuhusu Kristo"* na *"tusiweke tena msingi"*; na (B) cha kufanya, i.e., *"kukazana kufikia ukomavu."* **Mstari wa 2** unaorodhesha "mafundisho ya awali" ambayo anayaongelea. Viti hivi vyote vinahitaji kujulikana na kufahamika. Vyote ni muhimu. Kwa upande mwingine, wakati ukristo unaanzia hapa, hauishii hapa. Badala yake, Ukristo unahusika na maeneo yote ya Maisha, na tunahitaji kujua na kuelewa Neno vema kwa kiwango cha kutosha ili kuweza kutumia Imani ya kikristo katika maeneo yote ya maisha. Matokeo yake yatakuwa kwamba mwili wote wa Kristo utajengwa kwa namna ambayo *"[13]hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; [14]ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. [15]Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. [16]Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"* (**Efe 4:13-16**). Huo ndio mwelekeo wa mwandishi.

Kipengele kingine muhimu katika haya "mafundisho ya awali" ni hiki: inawezekana kuwa haya mambo yote yalishafundishwa katika mafundisho ya Kiyahudi ya AK. (Guthrie 1983: 140; Morris 1981: 53; Rayburn 1989: 1137). Ikiwa, ndivyo inavyotarajiwa, Kitabu cha waebrania kimeandikwa kimsingi kwa waumini wa kiyahudi ambao walikuwa wanapitia majaribu ya kutaka kurejea kwenye dini yao ya kiyahudi, hapa tunaona msingi wa mwandisho kuchagua hayo mambo sita. Maelekezo au maonyo yake ya kuacha kuendelea kujifunza haya mambo na kusonga mbele kuelekea kwenye ukomavu wa kiroho yanaweza kuwa yanalenga mbali zaidi kuliko inavyoonekana kwa juu juu, na pia wasomaji wake wa karne wa kwanza inawezekana walikuwa hali ya hatari zaidi kuliko tunavyoweza kuona kwa juu juu. Haya ni maonyo kwamba, watu wakibakia katika hali waliyonayo—*"wavivu wa kusikia"* na kung'ang'ana tu na *"kanuni za awali"*—itaonyesha kwamba hawakuwa wameokoka kabisa. Sababu ni kwamba, katika **mstari. 12**, Neno la kiyunani lililotafsiriwa *"kanuni za awali"*ni *stoicheion.* Usemi huo umetumika mara nne zaidi katika AJ ukiwa na maana ya mafundisho kuhusu imani au mambo ya kiroho: **Gal 4:3** inasema kwamba *"sisi, tulipokuwa Watoto, tulifanywa watumwa wa <u>kawaida za kwanza</u> ya ulimwengu."* **Gal 4:9** inasema, *"Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena <u>mafundisho ya kwanza</u> yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena?"* **Kol 2:8** inatumia neno lile lile inaposema, *"Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya <u>mafundisho ya awali</u> ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo."* **Kol 2:20-21** inatumia neno lile lile inaposema, *"Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale <u>mafundisho ya awali</u> ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, Msishike, msionje, msiguse!"*"[11] Yote hayo yanatumia *stoicheion* yanaonyesha kwamba kushikilia hayo "mafundisho ya awali" au kanuni hakuonyesha kwamba mtu ameokoka au ataokoka, ingawa hayo mambo yanaweza kuonyesha kana kwamba mtu ameokoka, na pia ni mambo yaliyopo ndani ya wokovu, n ani ya msingi ndani katika Ukristo. Kama vile Paulo anavyosema katika **Kol 2:23**, *"Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili."* Kwa hiyo, wakati mwandisho wa kitabu cha Waebrania anawalinganisha wale wanaojiita wenyewe kuwa wakristo na watoto wachanga (*"wavivu wa kusikia . . . bado mnahitaji mtu mwingine awafundishe mafundisho ya awali ya neno la Mungu, nanyi mnahitaji maziwa na si chakula kigumu"*) anafanya ulinganisho kwa namna ya kuwashusha hadhi sana. Wakati mtoto anazaliwa, yeye bado ni mchanga sana, na

[11] Msemo huo huo unatumika katika **2 Pet 3:10, 12** unaongelea kuhusu mambo kimwili ambayo yataharibiwa wakati atakapokuja Yesu kwa mara ya pili.

anakuwa hajui chochote. Baadhi ya hao waebrania ambao anawaandikia inawezekana wamekuwa wakristo kwa miaka mitano, kumi au kumi na tano. Ikiwa mtu ana kimo kile kile, uzito ule ule na bado hajui chochote kama mtoto mchanga, wakati yeye ana miaka mitano, kumi au kumi na tanoSome of the people, that huyo mtu angekuwa wa ajabu sana. Ungeonekena kama ukuaji usio wa kawaida. Hii ndio maana kushindwa *"kuendelea mbele kuelekea ukomavu"* ni zaidi ya maneno ya kutia moyo—ni maonyo kwamba hali iliyoelezwa ya kiroho katika kipengele hicho cha kitabu cha waebrania ni hali mbaya Zaidi ya vile anavyoweza kuona msomaji, kwa kuwa kuendelea kuwa mchanga kwa muda mrefu kiasi hicho inaonyesha watu hao sio watu waaminio wanaomaanisha na waliozaliwa mara ya pili hata kidogo.

4. <u>Kuanguka baada ya kuijua kweli ni kifo (**6:4-8**).</u>

[4]Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, [5]na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, [6]wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri. [7]Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu; [8]bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.

Sehemu ni moja ya sehemu ngumu sana kuelewa katika kitabu cha Waebrania, ikiwa siyo katika AJ nzima. Monyo hapa ni dhidi ya ''kunguka'' ikiwa ni mwendelezo wa onyo dhidi ya kushindwa kusonga mbele katika Imani na matumizi ya neno *stoicheion*. Muunganiko kati ya sehemu na hii na ile iliyotangualia unaonekana kwenye neno la utangulizi "Kwa ajili ya." Kuna mitazamo minne kuhusu nani anaongelewa na nini kinaendelea:

Mtazamo wa Arminian[12]	<u>Watu wanaohusika</u> = Wakristo wa kweli	<u>Matokeo ya mwisho</u> = Wameokoka, lakini wamepotea	<u>Uhalisia</u> = Haiwezekani kwa wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili kupoteza wokovu wao.
Mtazamo wa malisho hafifu kiroho[13]	<u>Watu wanaohusika</u> = Wakristo wa kweli	<u>Matokeo ya mwisho</u> = Wameokoa lakini wanapitia umaskini wa kiroho katika Maisha hayo na kukosa thawabu katika ulimwengu ujao.	<u>Uhalisia</u> = Haiwezekani kwa wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili kupoteza wokovu wao.
Mtazamo wa kinadharia[14]	<u>Watu wanaohusika</u> = Wakristo wa kweli	<u>Matokeo ya mwisho =</u> Wameokoka, lakini wamepotea	<u>Uhalisia</u> = Mtazamo huu unasimamia kuwa Haiwezekani kwa wakristo

[12] Mtazamo unaoungwa mkono na McKnight 1992.

[13] Mtazamo huu unaungwa mkono pia na Hurtado 1999. Ingawa hauungwi mkono kwenye kitabu hiki, ''Mtazamo wa Kupungukiwa malisho ya Kiroho'' una faida ya kutupatia fursa ya maonyo ya kila wakati kukagua Maisha yetu kuhakikisha kuwa tunaishi Maisha ya kweli ya toba ya kweli na imani.

[14] "Mtazamo wa kinadharia" una amini kwamba uasi "ni jambo linaloweza kutokea, lakini kwa wateule haliweza kutokea. Kwa hiyo ni uwezekano wa kinadharia usioweza kuwa halisi." (DeWaay 1998: Msimamo wa Tatu) Mtazamo huu unaonekana umeanzia kwenye Biblia ya KJV kuanzia **mst. 6**, *"Ikiwa watajitenga."* Tafsiri siyo sahihi. Maneno halisi *"wameanguka,"* ambayo inadokeza kuwa watu hao wanaweza au waliweza kuanguka. Mtazamo huu unakubaliwa na Guthrie 1983: 145-47 na Johnson 2006: 160-64. Bob De Waay anatoa maelezo kwamba "Ikiwa tunauhakika wa wokovu na uthibitisho ni wa Maisha yetu ya kweli ya wana wa Mungu, kwa hakika ni kweli hatuwezi kupotea. Lakini ikiwa tunaweza basi tutakuwa tunakabiliwa na kuangamia milele na bila tumaini la kutubu. Ni haki kutambulisha uwezekano wa jambo kutokutokea na kuhimiza mojawapo ili kulizuia. Mara zote tunawaonya Watoto kuhusu vitu ambavyo kwa hakika hawatavifanya. Tunawaambia wakicheza kwenye barabara ambayo inapita magari mengi watakufa. Ikiwa hili halitokei, maonyo bado ni ya muhimu. Kwa kuwa hatari ni jambo ambalo linawezekana katika ulimwengu kuwapata wanadamu kama tujuavyo, maonyo yana nguvu ya ushawishi." (DeWaay 1998: Position Three) Mwandishi mmoja anajadili mtazamo huu kama ifuatavyo, "Kwanza, haina sababu kuwa na maonyo ambayo yamejengwa juu ya mawazo ya mtu ambayo siyo sahihi. Pili, tendo ambalo limekamilika ''ikiwa watajitenga'' (*parapesontas*) siyo lazima itokee. Imeunganishwa na maelezo yanayofuata na 'na.' Kiuandishi kwa kanuni ya lugha, inaenda sambamba na kanuni ya matumizi ya aoristi ya dhidi ya na tano ni kama ''halisi'' kama yalivyo. Tatu, sauti yenye udharura hapa inaifanya iwe isiyo ya kawaida kwamba mwandishi alikuwa anashughulika na nadharia tu na hali ambazo haziwezi kuwa halisi. Marudio ya maonyo kama hayo katika Waebrania 10:26-31 inaonekana kupingana na jaribio la kutafsiri kifungu kama la kinadharia tu (Taylor 2020: Dhambi ya ''kuanguka na kujitenga'' Art Hurtado vile vile anasema kwamba si rahisi msemo kwa ajili *"wamejitenga au wameanguka"* katika mstari wa **6** kwamba ni "ni kitenzi

			halisi waliozaliwa mara ya pili kupoteza wokovu wao, bali unatoa angalizo muhimu dhidi ya udanganyifu.
Mtazamo wa kiagano wa Jamii[15]	Watu wanaohusika = Siyo mtu binafsi bali ni Jamii ya wakristo kwa ujumla	Matokeo ya mwisho = Jamii yote kwa ujmla itakataliwa na Mungu, lakini inawezekana kuna wachache wao walio waaminifu ambao hawatakataliwa.	Uhalisia = Mtazamo huu unasema kwamba, mkristo halisi anaweza kupoteza wokovu wake kwa namna moja au nyingine.
Mtazamo wa Matengenezo[16]	Watu wanaohusika = Wanaokiri, lakini siyo wakristo halisi.	Matokeo ya mwisho= Hawajaokoka, lakini pia wamepotea.	Uhalisia = Haiwezekani kwa wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili kupoteza wokovu wao.

Kati ya hii mitazamo tofauti, huu wa mwisho unaonekana kuwa sahihi kabisa kibiblia.[17] Ili kuona kwa nini, tunahitaji kujadili Imani ya kweli inayookoa ni ipi na inahusisha nini, na muktadha mpana na ule wa karibu na mstari wa **4-8**. Msingi huo unatuwezesha kuona kwa nini mtazamo wa Matengenezo ni mtazamo wa kweli Zaidi kibiblia wa mstari wa **4-8**.

- **Sifa za Imani ya kweli, inayookoa**

Imani ya kweli iokoayo inahusisha mambo yafuatayo. Kwanza uteuzi wa Mungu. Uteuzi wa Mungu ni Mungu mwenyewe anachagua watu baadhi kwa kusudi lake mwenyewe na mapenzi yake ili kuonyesha neema kwa wenye dhambi wasiostahili (tazama **Mdo 13:48; Rum 8:29-30; Efe 1:4-5, 11**). Wale aliochagua kuwaokoa wanaitwa "wateule" (tazama **Mk 13:20**). Pili ni kuzaliwa tena. Kuzaliwa tena au kuzaliwa upya ni kazi ya Roho Mtakatifu, mara zote huitwa "kuzaliwa mara ya pili" (**Yoh 3:3-8**), ambapo Mungu hubadilisha moyo wa mtu, akimpa Maisha mapya ya kiroho na asili ya kiungu (tazama **Ezek 36:26; Yoh 1:12-13; 2 Kor 5:17; Tit 3:5**). Kuzaliwa mara ya pili siyo mwanadamu kujiboresha yeye mwenyewe lakini ni tendo la kimamlaka linalofanya wokovu uwezekane, kuruhusu roho iliyokufa kutubu na kuamini. Tatu ni kubadilishwa. Kubadilishwa ni mwitikio wa kuzaliwa upya; inahusisha mtu kutubu dhambi zake, kuamini injili, kugeuka kutoka kwenye dhambi zake, kugeukia Imani, na kuamini katika, Yesu kama Bwana na Mwokozi wake (tazama **Mk 1:14-15; Mdo 3:19; 11:21; Efe 2:8-9; 1 Thes 1:9; 1 Pet 1:5**). Nne ni kuhesabiwa haki. Kuhesabiwa haki, tendo la ghafla la kisheria la Mungu kumtangaza mwenye dhambi kuwa mwenye haki kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo, na si kwa matendo ya mtu (tazama **Rum 3:24-26; 5:1; 2 Kor.5:21**). Tano ni kupigwa muhuri na Roho Mtakatifu (2 Kor 1:22; 5:5; Ef 1:13-14; 4:30). Kupigwa muhuri kwa Roho Mtakatifu ni utibitisho kwamba sisi ni mali ya Mungu na ni ''malipo ya awali'' au ''kulipia kabla'' ili kuhakikisha kwamba tutapokea urithi wetu kamili kama wana wa Mungu. Sita. ni kufanywa wana. Kufanywa wana ni neema ya Mungu katika kuwakaribisha waamini katika familia kama wanaye na warithi pamoja na Kristo (tazama **Rum 8:15-17; Gal 4:4-7, Efe 1:5**). Saba ni utakaso. Utakaso ni kutengwa na Mungu kwa ajili ya kusudi lake na kubadilishwa na kufanana na Yesu Kristo. Inahusisha mchakato wenye hatua tatu: (A) utakatifu unaopatikana mara tu pale mtu anapoingia katika wokovu; (B) ukuaji wa kivitendo katika neema unaondelea; na (C) kukamilishwa baadaye (kutukuzwa) (tazama **Yoh 17:17-19; Mdo 13:39; Rum 8:29-30; 1 Kor. 1:2, 30; 1 Thes 5:23; Ebr 12:14**). Utakaso ni kazi ya Mungu kupitia Roho; jambo la pili katika utakaso linahitaji kuhusika kikamilifu kwa muumini kuwa mtiifu na mwenye haki.

Zingatia kuwa yale yote yaliyotajwa kuanzia namba 1, 2, 4, 5, 6, 7(A) and 7(C) yote ni kazi ya Mungu pekee. Ila lile la 3 ni kazi ya mtu peke yake. Jambo la 7(B) ni kazi ya Mungu ambayo mtu anapaswa kuonyesha ushirikiano. Mambo yote saba huenda pamoja kana kwamba ni tukio moja tu lililo na vipengele kadhaa. Mtu hawezi kuwa na mojawapo na kukosa mengine.

---

kilichopo katika wakati mtimilifu ambalo huelezea tukio ambalo ni nadharia isiyofikiwa kwa uhalisia" (Hurtado 1999: Na Wamejitenga/Wameanguka). Hata hivyo, mtazamo huu una una faida kama maonyo ya kuwa na tahmini ya mara kwa mara kwa ajili yetu wenyewe ili kuhakikisha tunaishi Maisha ya toba ya kweli na imani.

[15] Usemi huu unaungwa mkono na Verbrugge 1980.

[16] Mtazamo huu unaungwa mkono na Grudem 2000.

[17] Ingawa watu waliorejewa hasa hasa katika **mst. 4-8** ni wale wanaokiri tu lakini siyo waamini halisi, wakristo waliozaliwa mara ya pili, kifungu hiki hata hivyo inahitaji kutumika kama maonyo makali kwa wakristo wa kweli, wakristo waliozaliwa mara ya pili ili wakae sawasawa katika njia iliyonyooka ya uaminifu na *''kukaza mwendo kufikia ukomavu''* (**6:1**).

- **<u>Asili ya Imani ya kweli, iokoayo: 1—Uvumilivu</u>**

Ebr 6:4-8 (kama vifungu vingine vyote) haviwezi kusoma pasipo kuangalia muktadha mpana na ule wa karibu wa Maandiko. Kwa kuzingatia muktadha mpana wa Maandiko, moja ya fundisho lililothibitishwa sana kuhusu asili ya Imani ya kweli, inayookoa ni uhakika wa uvumilivu wa Mungu kwa watakatifu, nayo ni, Mungu hufanya kazi ili kuhakikisha kwamba waamini halisi waliozaliwa mara ya pili hatimaye watavulia katika Imani yao na hawatapotea. Hapa kuna maandiko machache ambayo ni baadhi ya vifungu hivyo:

- **Yoh 6:39, 44—***[39] Na mapenzi yake aliyenipeleka ni haya, ya kwamba katika wote alionipa nisimpoteze hata mmoja, bali nimfufue siku ya mwisho . . .[44] Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho.*
- **Yoh 10:27-29—***[27] Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata; [28] Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. [29]Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.*[18]
- **Mdo 13:48**— *Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana, nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini.*
- **Rum 8:29-30—***[29]Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. [30]Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza.*
- **1 Kor 1:7-8—***[7] … hata hamkupungukiwa na karama yo yote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; [8]ambaye atawathibitisha hata mwisho, ili msilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo..*
- **Efe 2:4-7—***[4] Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; [5]hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. [6]Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; [7]ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu.*
- **Efe 1:13-14; 4:30—***[13] Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. [14]Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.. [30] Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi.*
- **Flp 1:6—** *Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.*
- **1 Thes 5:23-24**—*[23] Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. [24]Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya*.
- **Ebr 7:24-25**—*[24] bali yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. [25]Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.*
- **Ebr 10:14—***Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*
- **Ebr 13:20-21—***[20] Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, [21]awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una yeye milele na milele. Amina.*
- **1 Pet 1:3-5—***[3] Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; [4]tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. [5]Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.*
- **1 Yoh 5:18-20—***[18] Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi. [19]Twajua ya kuwa sisi tu wa Mungu; na dunia yote pia hukaa katika yule mwovu. [20]Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili*

[18] Charles Finney anatoa maoni katika kifungu anasema, "Hii ina maana kuwa, wangeweza au wanaweza kuasi na kupotea, lakini ukweli ni kwamba, kamwe hawawezi. Kitu gani kingeweza kusema kuhusu yale yote aliyoyasema yeye kama mchungaji katika kifungu hiki, kama, baada ya yote, angepoteza baadhi ya kondoo zake?" (Finney 1878: 570-71)

kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele.

Kwa upande mwingine, pia kuna vifungu kadhaa ambavyo vinaonekana kuwa na masharti. Hivyo vifungu ni pamoja na vifuatavyo:

- **Mk 13:13—** *Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka.*
- **Yoh 8:31**— *Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli."*
- **Rum 11:22**— *Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa katika wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali.*
- **1 Kor 9:26-27—***[26] Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; [27]bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*
- **1 Kor 10:12—** *Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.*
- **1 Kor 15:1-2**—*[1] Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, [2]na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure.*
- **Kol 1:21-23**—*[21] Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; [22]katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama … [23]mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake.*
- **Ebr 3:6--***… bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.*
- **Ebr 3:14—** [14]*Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho?*
- **Ebr 10:36**— *Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.*

Hivi vifungu vinavyoitwa "vilivyo na masharti" si hivyo, kwa ukweli, havipingani na vifungu vya "uhakika". Sababu ni kwamba, wakati vifungu vyenye "masharti" vinatoa mkazo ya kwamba mkristo wa kweli anahitajika kuvumilia, kuendelea mbele, na kuzidi kuendelea, na kusimama katika Imani kwa uvumilivu ili kuwa na uhakika wa wokovu wao, hapa kinachosemwa ni kwamba wale *wasio wa* kweli, wakristo waliozaliwa mara ya pili, *hawata*vumila hivyo, hawataendelea na kusimama imara. Au, ili kuweka kwa namna nyingine, wokovu wa kweli ni wa uhakika na una masharti, ni wa masharti kwa kuwa mtu ni lazima avumilie hata mwisho ili aokoke; ni wa uhakika kwa kuwa, kwa neema ya Mungu yenye mamlaka ambayo hufanya kazi ndani ya Maisha ya mtu, Mungu atahakikisha huyo mtu anavumilia hata mwisho na kuokoka. Kwa hiyo, katika kitabu cha Waebrania, waamini wa kweli waliozaliwa mara ya pili wanaelezwa kwa namna inayoelezea hadhi yao ya kudumu. Waelezwa kama *"wale watakaourithi wokovu"* (**1:14**), Wana wa Mungu (**2:10; 12:5**), Wapendwao na Kristo (**2:12, 17**), watoto*"ambao Mungu amenipa Mimi"* (**2:13**), *"uzao wa Ibrahimu"* (**2:16**),[19] *"watakatifu wapendwao"* (**3:1**), Myumba ya Kristo (**3:6**), *"washirika wa wito wa mbinguni"* (**3:11**), *"washirika wa Kristo"* (**3:14**), wale walioingia kwenye raha ya Mungu (**4:3, 9**), *"watu wa Mungu"* (**4:9; 8:10**), wale walio na *"wokovu wa milele"* (**5:9**),*"warithi wa ahadi"* (**6:17**), wale ambao tumaini lao ni *"ni la hakika na imara"* (**6:18-19**), wale walio *"waliopokea ukombozi wa milele"* (**9:12**), wale watakao *"pokea ahadi ya urithi wa milele"* (**9:15**), wale waliotakaswa na *"kukamilishwa kwa nyakati zote"* (**10:10, 14**), na wale *"walioandikwa mbinguni"* (**12:23**). Kwa kuzingatia hayo, Mungu katika Kristo anaelezwa kama mwenye mamlaka juu ya yote (**1:2-3**) na anatenda kazi katika kutimiza mapenzi yake (**2:4**). Yeye *"huwaleta wana wengi kwenye utukufu"* (**2:10**), humfanya shetani asiwe na nguvu kabisa (**2:14**), anawaweka huru wale waliokuwa chini ya utumwa, i.e., *"uzao wa Ibrahimu"* wa kweli (**2:15-16**), ni *"kuhani mkuu aliye mwaminifu"* ambaye hufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu wake (**2:17**), ni "hakikisho" la *"agano lililo bora zaidi"* (**7:22**), anaweza *"huweza kuwaokoa milele wale wamjiao Mungu kwa njia Yake, kwani Yeye yupo siku zote akiwaombea"* (**7:25**), kwa dhabihu yake moja *"amewakamilifu kwa nyakati zote wale waliotakaswa"* (**10:14**),ni*"mwanzilishi na mkamilishaji wa Imani"* (**12:2**), na ni mchungaji wa kondoo wake, yeye ambaye *"atawawezesha ninyi kwa kila kitu kilicho chema ili kufanya mapenzi yake, akifanya ndani yetu kile kinachopendeza machoni pake kwa njia ya Yesu Kristo"* (**13:20-21**). Kwa maneno mengine, ni Kristo ndiye aliye kazini ndani ya watakatifu wake kuwafanya watakatifu wake waweze kuvumilia katika imani yao.

[19] Ingawa neno lnalotafsiriwa kama "wana," neno halisi "uzao."

Kwa kifupi, *sharti* au *namna* ya kuufikia wokovu wetu ni Imani yetu, na Imani ya kweli inayookoa huvumilia na *hudhihirishwa kwa jinsi tunavyoishi*. Charles Finney hueleza kwamba "kama mwisho ni wa uhakika, hivyo na namna ya kufika pia ni ya uhakika; na kama moja ya hizo itafunuliwa kuwa ni ya uhakika, kwa hiyo na hiyo nyingine pia ni ya uhakika; na kwamba kwa hiyo ni ujinga, na inaonyesha kutoamini, kuwa na hofu kupuuza namna yaa kufika, au kwamba hatima au namna ya kuifikia itashindikana" (Finney 1878: 602). Uhakika wa wokovu wetu ni kama "uhakika wa mkulima kwamba atapata mazao kwa masharti ya bidi yake, kufanya kwa wakati, na uvumilivu wa kutimiza masharti ya kufikia malengo, huo ungemhimiza mkulima asipuuze hayo masharti. Mkulima angekuwa na maarifa kuhusu uhakika wa kupata mazao pamoja na masharti yake, kusingekuwa na majaribu ya kupuuza hayo masharti; lakini kwa upande mwingine, maarifa haya yangefanya kazi kama motisha yenye nguvu kufanya yale wanayotakiwa kuyafanya. Kwa hiyo kamwe maarifa ya hakikisho la wokovu kwa watatifu, na masharti yake, hayatakuwa kwao jaribu la kuwafanya waishi kwenye dhambi, lakini, kinyume chake maarifa haya ni lazima yafanye kazi kama motisha yenye nguvu na kuwafanya jasiri kwa Mungu, na katika kuvumilia katika utakatifu mpaka mwisho." (Finney 1878: 551-52) Hali hii inafanana na kuvunjika kwa meli ya Paulo katika kitabu cha **Matendo ya Mitume 17.** Malaika alimwambia Paulo kwamba meli aliyopanda itaharibika, lakini hakutakuwa na mtu atakayepoteza Maisha (**Mdo 27:22-25**). Hata hivyo, baadhi ya mabaharia walitaka kutoka kwenye meli. Kisha Paulo akasema, *"Ikiwa hawa watu hawatasalia kwenye meli, hata ninyi hamtaokolewa"* (**Mdo 27:31**). Kwa maneno mengine, malaika alikuwa ameahidi kwamba hakutakuwa na maisha yatakayopotea, lakini ahadi ilikuja na sharti, nalo ni, yeyote asitoke kwenye meli. Masharti yalipotimizwa, *"wote walifika salama nchi kavu"* (**Mdo 27:44**).

Vile vile, sisi tuishi Maisha yetu katika hali ya kuwa watendaji. Hata hivyo, Biblia imejaa vifungu vya maonyo yanayotuweka kwenye njia ''nyembamba na iliyonyooka'' (**Mt 7:13-14**). Ndio maana kitabu cha Waebrania kinatoa maonyo kwa watakatifu *"tuzingatie sana yale tuliyosikia, ili kwamba tusikengeuke"* (**2:1**), na *"kufanya bidi ili kuingia kwenye ile raha"* (**3:11**),na *"kushika sana ungamo letu"* (**4:14**), na *"kukaribia kwa ujasiri kwenye kiti cha neema"* (**4:16**) na ku *"kukaza mwendo kufikia ukomavu"* (**6:1**).Kwa hakika, **6:4-8** imebeba maonyo makali sana kwa watakatifu wa kweli ili *wasi*we *"wavivu katika kusikia"* (**5:11**) na kudhihirisha kwa vitendo ya kwamba wao *si* miongoni mwa hao *"walioanguka"* na ambao *"haiwezekani kuwafanya upya"* (**6:6**). Kwa kutimiza vigezo vya Imani yenye uvumilivu, ambayo huthibitishwa kwa Maisha ya uaminifu, mwishoni (wokovu wetu) ni wa uhakika.[20] Lakini pia tunapaswa kukumuka kwamba, kama tulivyoona hapo juu sisi hatupo peke yetu. Mungu katika Kristo yupo pamoja nasi ili kutuwezesha sisi kuvumilia. "Kwa hiyo hakuna mkristo anayejitunza mwenyewe, isipokuwa kwa namna ambavyo anatunzwa na neema, na Roho, na nguvu za Mungu…. Hakuna misngi ya kutokuwa na uhakika, kwamba moja wao ataokolewa, labda fundisho liwe na kasoro [yaani, juu ya umvumilivu wa watakatifu] kusema kweli, ni kwamba, isipokuwa neema na uaminifu wa Mungu katika Kristo huenda mbele, na hatua kwa hatua kuwahakikishia uvumilivu wao." (Finney 1878: 555, 587) Kuna mawasiliano endelevu kati ya Mungu na wakristo ambayo hutufanya sisi siyo kuamini katika Kristo kwa mara ya kwanza bali pia kuvumilia katika hiyo Imani. Kama **Flp 2:12-13** inavyosema *"utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka."*

- **<u>Asili ya Imani ya kweli, iokoayo: 2—Mihimili mitatu ya imani</u>**

Watu wengi hutumia misemo kama "usalama wa milele" na "ukiokoka mara moja, umeokoka mara zote" bila kujua misemo hiyo ina maana gani hasa na inaashiria nini. Semi hizo, ingawa ni kweli, siyo semi za "kimazingaumbwe". Hapo swali ni ikiwa waamini wa kweli waliozaliwa mara ya pili—yaani, wale wenye hizo sifa sita za Imani ya kweli inayookoa (iliyoelezwa hapo juu)—wanaweza kupoteza wokovu wao. Jibu ni kwamba hawezi. Kutokuelewa na matumizi mabaya wa semi hizi inatokana na ukweli kwamba baadhi ya watu husema au humaanisha kwamba, mtu akitoka mbele kwenye mkutano wa injili na kukiri Imani yake katika Kristo, basi yeye anasemekana ameokoka milele, bila kujali kile anachofanya au anachoamini baada ya hapo. Hiyo siyo sahihi. Siyo sahihi kwa sababu haiendi sawa sawa na Injili; haipatani na asili ya Imani yenyewe ya kweli na inayokoa. Hicho ndicho kiini chenyewe.

[20] Hapa tena tunaona jinsi vifungu vya "uhakika" na vya "masharti" vinagongana. Kustahimili ni "uhakika" katika mtazamo wa Mungu lakini "unategemea masharti" kwa mtazamo wa mwanadamu. Finney anaeleza, "Kwa Mungu hakuna masharti kamwe, kwa habari ya kutokuwa na uhakika, kwa habari ya hatima ya mwisho ya kiumbe chochote. Lakini kwa wanadamu karibu kila kitu kina masharti. Mungu anajua kabisa lini mtu ataokoka ikiwa mtu ataokoka au ataasi. Mtu anaweza akajua kuwa yeye ameokoka na anaweza kuamini kuwa kwa nguvu za Mungu ataweza kuvumilia. . . . Lakini kujua kwake hivyo hakuwezi timamu kila mara na kuendana na mazingira yote ya majaribu hata kufikia kifo chake, ikiwa tu uvumilivu wake unategemea hali yake ya uhiari na pia kwa sababu kustahimili ni sharti la wokovu wake wa mwisho." (Finney 1878: 470)

Kwa kuwa injili—na wokovu wa watu—ni kwa msingi wa kile alichofanya Yesu, wokovu hauwezi ‘‘kupatikana’’ kwa kufanya ‘‘matendo mema” Bali, wakovu *unatolewa* na Mungu kwa watu kama *zawadi* ya *neema* yake; *unapokelewa* na watu kwa *imani* pekee katika Kristo. **Efe 2:8–9** inasema, *“[8]Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; [9]wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.* Kuokolewa ina maana kutubu dhambi zetu, kukubali kwa Imani kile alichofanya Yesu kwa ajili yetu, na kumgeukia Kristo kama Bwana wa Maisha yetu (**Mt 11:28; Mk 1:14–15; Yoh 1:12; 3:16; 17:3; Mdo 26:20; 1 Yoh 1:8–9**). Ndani ya Kristo, sisi tunakuwa huru kutoka kwenye hatia na adhabu ya dhambi zetu kana kwamba sisi wenyewe tumelipia gharama yote kwa ajili ya dhambi zetu (**Rum 6:3–7; Gal 2:20**). Kwa kweli, tunapomgeukia Kristo kwa Imani, yeye hachukui tu dhambi zetu juu yake mwenyewe na kulipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu ambazo tungepaswa sisi wenyewe kulipia, bali yeye pia anatupatia haki yake ili tuweze kusimama mbele za Mungu (**Isa 53:5–6, 10–11; Rum 10:4; 2 Kor 5:21; Ebr 2:17–18; 1 Pet 2:4; 3:18**).

Imani ya kweli, iokoayo siyo tu kusema kirahisi “maneno fulani yanafanya maajabu” kama vile “Ninakupokea Yesu moyoni mwangu kama mwokozi wangu binafsi.” Ingawa tunaokolewa kwa neema ya Mungu pekee (**Efe 2:8-9**), Imani iokoayo siyo peke yake. Maana yake ni hii hapa: Kutoka kwenye *mtazamo wa kibinadamu*, kuna, mtu mmoja anaweza kusema, “mihimili” mitatu ya Imani ya kweli, inayookoa. Hiyo yote inahusiana; yote lazima iwepo kwa mtu ili awe na Imani ya kweli inayookoa. Mmoja anaweza kufikiri juu ya hiyo mihimili kama ifuatavyo: mhimili X ni wa kiakili, kifundisho, kuamini katika vipengele vya Imani ya Kikristo (tazama, k.mf., **Mdo 2:22-24, 32-36; Rum 1:1-4; 10:9; 1 Kor.15:1-8**)—tunaweza kusema kwa muhutasari muhimili huu kwa maelezo haya, “Yesu ni Bwana juu ya yote, na alithibitisha hilo kwa kufufuka kwake kutoka kwa wafu’’; muhimuli Y ni wa kipengele cha tabia (tazama, k.mf., **Mt 28:18-20; Yoh 14:23-24; Efe 2:8-10; Yak 2:14-20**)— tunaweza kusema kwa muhutasari muhimili huu kwa maelezo haya, “Tunavyoishi huthibitisha tunachoamini”; mhimili Z unahusu kipengele cha ibada ya Imani ya Kikristo (tazama, k.mf., **Yoh 15:4-15; 17:3; 21:15-17**)— tunaweza kusema kwa muhutasari muhimili huu kwa maelezo haya, “Upendo na kujitoa kwa Kristo ni kiini cha Imani inayookoa.” Wakati sisi hatuwezi kujitafutia njia yetu ya kwenda mbinguni na tunaokoka kwa neema ya Mungu kwa njia ya Imani katika Kristo (**Yoh 3:16–18; 6:28–29; Rum 2:16–17; 10:8–13; Gal 3:1–14; Efe 2:8–9**), tumeokolewa kwa *kusudi*: *“Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.* (**Efe 2:10**) Kwa kifupi, kazi tunayofanya baada ya kumpokea Kristo kwa Imani “ni kielelezo cha hali ya kiroho ya moyo wa mtu. . . .Hukumu haiangalii siyo uwiano wa uzito kati ya mema na mabaya. Bali, matendo yanaonekana kama uthibitisho wa kweli ya utii wa moyo; yanaelezea Imani au kutokuamini, uaminifu au kutokuwa mwaminifu. Hukumu itaonyesha ikiwa utii wao ulikuwa kwa Mungu na Mwanakondoo au kwa adui wa Mungu.” (Ngundu 2006: 1576; tazama, k.mf., **Mt 24:45–51; 25:31–46; Yoh 3:19–21; 1 Tim 6:18–19**).

Kuwa na muhimili moja au miwili kati ya tatu hiyo ina maana kwamba huyo mtu hana Imani inayookoa na kwa hiyo hajokoka na siyo muumini aliyezaliwa mara ya pili. Kwa mfano, Yak anasema, *“Mapepo pia yanaamini na kutetemeka”* (**Yak 2:19**). Kwa maneno mengine, pepo wanaamini na wanaweza maneno kwamba, “Yesu ni Mwana wa Mungu,” lakini hayana muhimili wa imani wa tabia na wa ibada; kwa hiyo hawana Imani ya kweli inayookoa. Vivyo hivyo, Yesu alisema, *“Mtu akinipenda Mimi, atalishika Neno langu”* (**Yoh 14:23**). Kwa maneno mengine, alikuwa anaunganisha muhimili wa ibada na wa tabia. Mtu anaweza kusema yeye anampenda Yesu lakini hafanyi asemayo Yesu basi huyo mtu hampendi Yesu na kwa hiyo hana Imani ya kweli inayookoa (pia tazama **Mt 7:21-23; 25:31-46; Mdo 8:13, 18-23; 1 Kor 13:1-3; 1 Yoh 4:20** kwa muunganiko unaofanana wa imani na imani isiyookoa).[21]

Tunapoiamini Injili na kumgeukia Kristo kama Bwana kwa Imani ya kweli inayookoa, sehemu zote za Maisha yetu zinaathirika: (1) Wote walioungana na Kristo wana uhakika wa wokovu wao. Ikiwa wokovu unategemea hata kidogo sehemu ya bidi yetu, tusingeweza kamwe kupata uhakika kwamba ‘‘tumefanya vya kutosha’’ ili kustahili kupokea wokovu. Hata hivyo, kwa sababu Mungu katika Kristo alifanya kwa ajili yetu kile ambacho sisi tusingeweza, Wakristo wanaweza na wanao uhakika kwamba wameokoka na milele watabakia wameokoka (**Yoh 3:36; 6:37, 47; 11:25; 1 Yoh 5:11–12**). (2) Kuokoka na kuungana na Kristo kunabadilisha hadhi ya kisheria ya mwamini. “Msalaba unatuokoa kutoka kwenye nguvu ya dhambi, unaondoa hasira ya Mungu, unaondoa hatia na madoa ya dhambi, humpatanisha mwamini na Mungu, na kupata ushindi unaozidi dhidi maadui wa wanaoua kiroho” (Demarest 1997: 196). (3) kuokoka na kuungana na Kristo huwabadilisha kutoka ndani kwenda nje. Mtu anapokuja kwa Kristo, yeye anapokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), ufahamu wa Kristo (**1 Kor 2:16**), na Roho kutoka kwa Kristo (**Ezek 36:26; Yoh 14:17**). (4) Kuokolewa na kuungana na Kristo humpatia mkristo ushirika wa ndani kabisa na Mungu kwa njia ya Kristo. Mkristo anaweza *“kukikaribia kwa*

[21] Tazama mfululizo wa jumbe S “Mihimmili mitatu ya imani” na Jonathan Menn kwenye https://www.eclea.net/sermons.html#topical.

ujasiri kiti cha neema" (**Ebr 4:16**; pia tazama **Ebr 7:19**) kwa kuwa Kristo yupo ''ndani'' ya waaminio (k.mf., **Gal 2:20; Flp 3:17; Kol. 1:27; 1 Yoh 3:24**) na waamini wapo "ndani ya Kristo" (k.mf., **Rum 8:1; 1 Kor 1:30; 2 Kor 1:21; 5:17; 1 Pet 5:14**). (5) Kuokoka na kuungana na Kristo huumba ubinadamu mpya (**Yoh 3:3; Rum 6:4; 2 Kor 5:17; Gal 6:15**); waamini wanafanyika wana katika familia ya Mungu (**Yoh 1:12; Rum 8:14–17, 23; 9:4; Gal 3:26; 4:5–7; Efe 1:5; 2:19; 1 Yoh 3:1**) na kuwa na mahusiano ya kina kama kaka na dada (mf., **Mt 12:50; Mdo 1:16; Rum 14:10; 1 Tim 5:1–2**).

- **<u>Asili ya Imani ya kweli iokoayo: 3—"Ya mpito" au Imani ya uongo</u>**

Kama tulivyosema, tumeokolewa kwa neema ya Mung utu kwa njia ya Imani; kwamba kubadilishwa kutoka kwenye hali ya kubadilishwa kutoka kwenye hali ya mtu ambaye hajaokoka hutokea katika kipindi fulani cha wakati. Pia tumeona ya kwamba, imani ya kweli, inayookoa siyo tu kukubaliana na mawazo fulani yanayotokana na akili za kibinadamu, bali ina mihimili mitatu ambayo huathiri maeneo yote ya maisha ya mtu, na hiyo, imani inayookoa, kwa kweli, imani hiyo itadumu hata mwisho wa maisha ya mtu. Kipengele kingine cha Imani inaoneshwa katika mfano wa Yesu unaohusu mpanzi na udongo (**Mt 13:1-23; Mk 4;1-20; Lk 8:4-15**). Mbegu hiyo hiyo ya injili ilipandwa kwa watu tofauti tofauti na mapokezi yao yalikuwa tofauti. Ya kwanza ilianguka njiani; Yesu anaeleza, *"Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia."* (**Mt 13:19**). Ya pili ilianguka kwenye mwamba; Yesu akasema, *"Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha; 21lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa."* (**Mt 13:20-21**) Katika maelezo ya Luka, Yesu anaongeza kwamba *"waliamini kwa muda"* lakini baadaye walijitenga (**Lk 8:13**). Ya tatu ilinguka kwenye miiba; Yesu akasema, *"Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno; likawa halizai."* (**Mt 13:22**). Ni moja iliyoanguka kwenye *"udongo mzuri";* Yesu alisema, *"Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyo ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo; yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu sitini, na huyu thelathini."* (**Mt 13:23**).

Katika maelezo ya mifano hii, D. A. Carson anaelezea kuhusu Imani mambo ambayo mara nyingi hayasemwi. Carson anafafanua kwamba "kama ilivyo kwenye vitabu vingine vya AJ waraka kwa Waebrania unaruhusu aina fulani ya imani ya mpito, muundo wa wokovu ambao, kama ile mbegu iliyopandwa kwenye mwamba, iliyokuwa na ishara zote za kuwa na uhai, lakini haikuweza kudumu. Mwz Roho huleta maarifa kwa mtu; mtu analifurahia neno la Mungu (kama yule mtu . . . anayelisikia neno na mara analipokea kwa furaha), na kuonja nguvu ya zamani zijazo: labda tabia za kale huondoka kwake, na upendo mpya kwa utakatifu na kwa Mung una utawala wake kutokea. Lakini kulingana na tafsiri ya ukristo wa kweli ambao umejadiliwa kwenye kitabu hiki, bado hili halitoshelezi: ni lazima uwepo uvumilivu pia." (Carson 2000: 267) Hivyo, mfano unatueleza kwamba watu wanaweza kusikia na kupokea injili, kupata furaha ya injili, na kuonyesha dalili zote za kuwa wamebadilishwa na Yesu. Hata hivyo, wakakosa uvumilivu, na matokeo yake, wakati Fulani hujitenga na Imani waliyokuwa wameikumbatia. Siyo kwamba walikuwa na Imani inayookoa na ya kweli, lakini baadaye wakapoteza hiyo Imani, bali—pamoja na mwonekano wao—kamwe hawakuwahi kuokolewa kabisa.

Kuna mifano mingine ya kibiblia wa aina hii ya muda ya imani isiyookoa. Katika **Mdo 8,** Simoni mchawi aliona Filipo akihubiri akaona miujiza ikiwa inafanyika. Matokeo yake akaamini na kubatizwa, na *"akaungana na Filipo"* (**Mdo 8:13**). Hata hivyo, "imani" yake kwa hakika haikuwa ya Imani ya kweli, inayookoa, kwa kuwa baadaye alitaka kutoa fedha ili ajaribu kupata mamlaka ya kuwapatia watu ujazo wa Roho Mtakatifu (**Mdo 8:17-19**). Pet akamwambia, *"Lakini Pet akamwambia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. 21*Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. 22Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako. 23*Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu.."* (**Mdo 8:20-23**) Yesu anaelezea aina zingine za visa vya Imani ya muda mfupi, ya uongo. **Yoh 2:23-25** anasema, *"[23] Hata alipokuwapo Yerusalemu kwenye sikukuu wakati wa Pasaka, watu wengi waliamini jina lake, walipoziona ishara zake alizozifanya. [24]Lakini Yesu hakujiaminisha kwao; kwa kuwa yeye aliwajua wote; [25]na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu. Basi watu wengi miongoni mwa wanafunzi wake waliposikia, walisema, Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia?* (**Yoh 6:60**), na *"Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena"* (**Yoh 6:66**). Vile vile, **1 Yoh 2:18-19** inaeleza kuwa wapotoshaji ambao wana kila dalili ya kuwa wakweli, watu waliozaliwa mara ya pili hata wanaweza kuwa waalimu ndani ya kanisa, ingawa hata hivyo *si* kweli kuwa wao ni watu waliozaliwa mara ya pili ambao wamepoteza

wokovu wao, bali kamwe hawakuwahi kuwa waamini wa kweli, waliozaliwa mara ya pili hata kidogo. Hiyo mistari inaeleza, *"[18]Watoto, ni wakati wa mwisho; na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo. Kwa sababu hiyo twajua ya kuwa ni wakati wa mwisho. [19]Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu."*

Hii ndiyo sababu kwanini, AJ lote lina vifungu vyenye maonyo mengi. Kwam mfano, kwenye kitabu cha Waebrania zimtolewa tahadhari dhidi "kujitenga" (**2:1**), "kutojali wokovu" (**2:3**), "kuanguka" kwa sababu "moyo mbovu, usioamini" (**3:12**), uliofanywa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi (**3:13**), kutotii (**3:18; 4:6, 11**), "kupungukia" wa kuingia kwenye raha yake (**4:1; 12:15**), "kuchoka na kukata tamaa" (**12:3**), kuwa "na shina la uchungu" (**12:15**), "kukataa na kumwacha Kristo (**12:25**). Hata hivyo maonyo have na maelekezo hayamaanishi kwamba wale wanaojitenga, walio na mioyo migumu, wasiotii, wenye mapungufu, wanaochoka na kukata tamaa, wenye shina la uchungu, au wanaokataa na kumwacha Yesu kwamba walishawahi kuwa waamini wa kweli, waliozaliwa mara ya pili. Kwa kweli, baadhi ya mifano hii inawazungumzia Waisraeli wasiotii (**3:16-19; 12:25**) na Esau (**12:16-17**), ambao kwa wazi *hawakuwa* waumini wa kweli, waliozaliwa mara ya pili.[22]

- **<u>Uchambuzi wa Waebrania 6:4-8</u>**

Huu mjadala wa kina uliozingatia muktadha ni wa muhimu ili kuelewa vema **Ebr 6:4-8**. **Mistari ya 4-6** inatamka mambo sita kwa wale wanaozungumziwa: (1) Wao *"wamewahi kutiwa nuru"* (**mst. 4**); (2) Wao *"wameonja kipawa cha Mbinguni"* (**mst. 4**); (3) Wao *"wamefanyika washirika wa Roho Mtakatifu"* (**mst. 4**); (4) Wao *"wameonja kazi njema za Mungu"* (**mst. 5**); (5) Wao *"wameonja . . . nguvu za zamani zijazo"* (**mst. 5**); lakini pamoja na haya yote (6) *"Wamejitenga, [kiasi kwamba] ni vigumu kuwafanya upya tena na kuwafanya watubu tena, kwa kuwa wanamsulubisha tena Mwana wa Mungu na kumdhihaki kwa dhahiri"* (**mst. 6**).

Moja ya sababu inayofanya kifungu hiki kuwa na ngumu kukitafsiri ni kwamba maelezo kuhusu wale watu wanaoongelewa *yanaweza* kutumiwa hata kwa wakristo wa kweli waliozaliwa mara ya pili. Kwa umuhimu, hata hivyo, watu wanaojadiliwa katika **Ebr 6:4-6** hawakuwa na sifa zile saba za Imani ya kweli inayookoa, zilizojadiliwa hapo juu. Kwa kweli, kuna badiliko muhimu kutoka kwa mtu "kibinafsi" (wa kwanza na wa pili) kwenye matamshi yanayokuja mara tu baada ya Sura ya **5:11—6:3** ("wewe," "yetu," "sisi") na kile kinachofuata mara katika sura ya **6:9-12** ("sisi," "wewe," "yenu") kwa "ubinafsi" (mtu wa tatu) katika **mst. 4-8** ("wale," "yao," "wao," "yake"). A. W. Pink anaelezea, "Inayo umihimu wa kwanza kujua kwamba mtume hasemi kuwa, '*sisi* ambao tulikuwa tumetiwa nuru', au hata pia 'ninyi', badala yake, anasema 'wale'. Kwa kujitofautisha moja kwa moja na wao, anasema kwa Waebrania, 'Wapendwa, tumeshawishiwa kwa habari mambo mazuri ya kwenu." (Pink n.d.: sura ya 24) Ingawa kama tulivyoona hapo juu, hawa walipokea faida faida kubwa tano, Pink anaeleza "Lakini bado hawakuwa Wakristo wa kweli. Hii inathibitishwa na kile *kisicho*semwa. Tambua, hawakutajwa kama wateule wa Mungu, kama ambao Kristo alikufa kwa ajili yao, kama wale waliozaliwa kwa Roho. Hawakutajwa kuwa wamehesabiwa haki, wamesahewa, wamekubaliwa miongoni mwa Wapendwao. Wala kwa chochote kilichotajwa kuhusu Imani yao, upendo au utii. Na wakati haya ndiyo yanayomtafoutisha mwana halisi wa Mungu. (Pink n.d.: ch. 24)

Kwa kuongezea, kila maelezo katika mistari ya **4-5**, au moja moja au yote kwa pamoja, siyo lazima yawe yanawahusu waamini wa kweli, waliozaliwa mara ya pili (tazama Grudem 2000: 139-48). Kwa mfano, ingawa neno linalomaanisha "kutiwa nuru" mara nyingine hutumika kwenye muktadha wa wokovu (k.mf., **2 Kor 4:6; Efe 1:18; 5:8**), visa vingine vinaeleza kuhusu watu ambao wameona nuru lakini hawajafikia kuipata Imani ya kweli iokoayo (**Yoh 1:9-11; 3:19; 9:39-41;** pia tazama **Mt 4:16-17; 2 Kor 4:4; 2 Pet 2:19-21**). Katika vifungu vinavyoendana na kifungu cha **Ebr 10:26**, watu hao wanasemekana *"[wame]pokea maarifa ya kweli"* (pia tazama **2 Pet 2:20-21**). Kwenye Septuagint msemo unaotumika kwa Jehoash kupewa ''maelekezo'' na kuhani Yehoyada (**2 Fal 12:2** [**2 Fal 12:3**, LXX]) na neno la Mungu lililofunuliwa kuwapa maarifa wajinga (**Zab 119:130** [**118:130**, LXX]). A. W. Pink anaeleza, "Kwa hiyo, "kutiwa nuru" hapa ina maaana kufundishwa fundisho la injili, ili kuondoa hali ya kutokufahamu. . . . [Lakini huko 'kutiwa nuru'] inapishana kwa mbali na kutiwa nuru ambako *kunabadilisha* (2 Kor. 3:18)." (Pink n.d.: Sura ya 24). *"Kipawa cha Mbinguni"* ya **mst. 4** imedhaniwa kuwa ni ya Kristo, Roho Mtakatifu, au baraka zinazohusianishwa na wokovu. Siyo lazima kufumbua kisa hicho na tuona kwamba neno linalotumika hapa ni kwamba *"wameonja." "neno zuri la Mungu"na "nguvu za zamani zijazo''katika* mstari wa **5**. Kuonja mara nyingine maana yake ni kumeza yote (k.mf., **Ebr 2:9**, Yesu alikuja

[22] Hata hivyo, mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili ni lazima azingatie vifungu vyote vya maonyo kwa sababu kwa kadiri wanavyo *"zidi kuwa makini kwa kile tulichosikia, ili tusichepuke na kwenda mbali"* (**Ebr 2:1**) ana *"kushikilia ungamo letu kwa nguvu"* (**Ebr 4:14**).

"kuonja kwa ajili ya kila mmoja"). Kwenye mazingira mengine, ina maana kutumia sehemu kidogo ya kitu fulani ili kuona kama ni kitamu (**Mt 27:34; Yoh 2:9**). Katika **mst. 5**, *"kuonja neno zuri la Mungu"* inaendana sana na kupatiwa neno lakini si kulipatana neno lote la Mungu. Vile vile, wao *"wameonja . . . nguvu za zamani zijazo."* Hizo *"nguvu za zamani zijazo"* inawezekana ni nguvu zinazoongelewa kwenye **Ebr 2:4**. Ingawa "kuonja" nguvu hizo ingekuwa inazungumzia watu waliopokea uzima wa milele, usemi huo ni kama unaelezea "watu waliopokea nguvu isiyo ya kawaida ya injili (cf. Mat 11:20; Marko 9:1; Luka 17:21), au baadhi ambao wametenda miujiza (*maajabu*) katika jina la Yesu bila ya kujitoa kwake kikamilifu (Mt 7:22,23)" (Nicole 1975: 361). Hali hii inafanana na wale ambao *"waliofanywa washirika wa Roho Mtakatifu"* (**mst. 4**). Neno la kiyunani linaloelezea "washirika" ni *metochoi.* Wakati mwingine inaonesha uhusiano wa karibu kama vile "kushiriki" maziwa (**Ebr 5:13**) au Kristo kuuchukua mwili wa mwanadamu katika umwilisho (**Ebr 2:14**). Kwa upande mwingine, inaweza ikawa inahusu ushirika wa nje tu, bila ya kuwa na wokovu wa kweli (**1 Kor 10:21** [*"Huwezi ukashiriki meza Takatifu ya Bwana na meza ya mashetani"*]; **Ebr 12:8** [*"ikiwa wewe huna nidhamu, ya kila ambacho wote mmekuwa washirika, kwa hiyo ninyi mmekuwa watoto wa haramu na siyo wana"*]).[23] Kwa njia moja au nyingine, vipengele vitano vya maelezo vinaonyesha kwamba watu wanaojadiliwa wanaonekana kuwa ni watu wazoefu wa mafundisho ya Kikristo, Roho Mtakatifu na karama zake. Hata hivyo, kwa kuwa kila kinachoelezwa kinaweza kutumika kwa wale waliozaliwa au wale wasiozaliwa upya, kutambua walengwa katika maelezo hayo ni lazima kuzingatia muktadha mpana na ule wa karibu wa Maandiko. Kama tulivyojadili kwa kina katika maelezo hapo juu, kwa kuwa wenye Imani ya kweli inayookoa (hao ni., wa kweli, waliozaliwa mara ya pili) watavumilia katika imani na hawawezi kupotoka, watu wanaojadiliwa kwenye mstari wa **4-5** lazima walikuwa ni watu ambao wamesikia kweli, inawezekana walihudhuria kanisani, inawezekana pia walikuwa walimu (kama katika **1 Yoh 2:19**), lakini hawakuwahi kubadilishwa na Kristo.

Katika **mst. 6**, neno la Kiyunani lenye maana *"waliojitenga"*ni *parapesontas.* Huo msemo pia unafungua kwamba wale ambao *"wamejitenga"* ni wazi hawakuwa Wakristo wa kweli, waliozaliwa mara ya pili. Hili ni eneo pekee ambalo hili kitenzi hiki kinatumika katika AJ. Hata hivyo, inapatikana katika Septuagint. Hapa kila wakati kilipotumika, kilimaanisha kumwacha Mungu kwa makusudi (**Ezek 15:8; 18:24; 20:27; 22:4**). Huo usemi unaonekana kuwa sawa na *apostenai,* kama ilivyotumika katika **Ebr 3:12**, amabyo huongea kuhusu *"moyo mbovu usioamini ambao unajitenga mbali na Mungu aliye hai."* Watu wanaoelezewa **6:4-8** wanafanana na wale waliozungumziwa katika kifungu cha **10:26-29**, *"[26]Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; [27]bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. [28]Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. [29]Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?* Hapa suala siyo kutenda baadhi ya dhambi, au dhambi kubwa kama vile uzinzi au kuua. Kama DeWaay anavyoeleza, "Tunahitaji kuelewa hii haihusu kurudi nyuma. Kama ingekuwa hivyo, wengi wa Waebrania wangevunjika moyo. Kinachoelezwa, ni kuikataa Imani kwa makusudi, siyo mkristo mwenye madhaifu, asiye makini au tofauti ya muda mfupi na kuanguka kwenye dhambi mbaya." (DeWaay 1998: Kujitenga) Kinachoongelewa hapa kukataa kwa makusudi na kufuata udanganyifu na kumkataa Mungu. Hilo si jambo ambalo linamruhusu mtu mwenye Imani ya kweli inayookoa kuweza kudai kwamba amezaliwa mara ya pili'' Hilo ndilo ambalo mtu mwenye Imani ya kweli, inayookoa anaweza kufanya; ''mtu anaweza kudai kuwa amezaliwa mara ya pili''na anaweza kuonyesha ishara nyingi kwamba yeye yupo sawa, lakini kwa makusudi kumkataa na kumwacha Mungu hufunua mtu kuwa hakuwahi kuokoka kabisa.

Neno "haiwezekani" (**mst. 6**) inaweza kuwa na baadhi ya matokeo, kwa kutugemea muktadha. Kuna mambo "hayawezekani" kulingana na asili ya Mungu, k.mf., ''*ni vigumu kwa Mungu kudanganya''* (**Ebr 6:18**). Kwa upande mwingine, vitu vingine vinawezekana kwa sababu ya vinawezekana kwa asili ya Mung una bado vinaweza visiweze kufanyika kwa sababu ya utaratibu aliouweka Mungu, k.mf. ni vigumu kuamini pasipo kusikia Neno la Kristo (**Rum 10:13-17**), ni vigumu kuokoka pasipo kutubu (**Lk 13:3**), ni vigumu kumpendeza Mungu pasipo imani (**Ebr 11:6**). "Kutowezekana" katika **mst. 6** ni sawa na matumizi ya Neno yaliyoongelewa awali. Kwa sababu watu wanaojadiliwa hapa wamemkana Kristo na amekataa injili, swali ni: Kwa kuwa ni nani ambaye kwake

[23] **Ebr 6:4** hivyo hutofautisha kwa udogo kwenye muktadha, kuwa "mshirika wa Roho Mtakatifu" kutoka kwenye kuzaliwa mara ya pili katika kweli. Tofauti hii inaonyeshwa na **Ebr 3:14**, inayosema, *"Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho."* Kwa maneno mengine **Ebr 3:14** inasema kwamba tunaweza ''washirika wa Kristo'' *ikiwa tu* tutastahimili hadi mwisho; hata hivyo **Ebr 6:4** inasema kuwa mtu anaweza kuwa "mshirika wa Roho Mtakatifu" hata kama yeye *hata* stahimili hata mwisho, lakini akijitenga.

ni vigumu *"kufanywa upya kama akitubu"*?[24] Kufanywa upya ili kutubu ni tofauti na tabia za Mungu (tazama **Mt 19:26; Mk 10:27; Lk 8:27**). Matokeo yake, William Mounce anaeleza kuwa "ni lazima tuseme ni vigumu *kwa maana kwa wanadamu* ili kuwaleta watu kwenye imani'' (Mounce 2006: 354). Ingawa sababu kwa nini ni "ni vigumu" haikutolewa, A. W. Pink anaelezea, ni vigumu "kwa maana *watumishi* wa Mungu 'kuwafanya upya *tena* hata watubu', kwa sababu zote zinazotosha hawakuwa na ujumbe mwingine wa kuwapatia. Hawakuwa na Injili nyingine ya akiba, na hakuna mguso mwingine wa kuwapatia. Kristo aliyesulubiwa alitolewa mbele yao. Yeye ambaye sasa wanamkana kama mwongo. . . . Kumkana kwao Kristo hadharani kulifanya tumani lao lisiwepo na hata watumishi wa Mungu walilijua hilo. 'Tukiachana na wao' (**Mt 15:14**) sasa ilikuwa ndio hali yao: . . . Ikiwa ilikuwa inawezekana au haiwezekani kwa Mungu, akiwa mtakatifu daima, kuwaibisha wao, kifungu chetu hiki hakiweki wazi." (Pink h.n: sura 24)

Hii inakaziwa zaidi na ukweli kwamba wale watu *"humsulubisha mwana wa Mungu kwa mara ya pili na kumdhihaki kwa Dhahiri"* (**mst. 6**). Neno "humsulubisha" lipo katika wakati uliopo, unaoendelea, nayo ni., *"wanamsulubisha tena."* Inafanana na neno "humweka"; lipo katika wakati uliopo unaendelea, nayo ni., *"humweka kwenye dhihaki kwa Dhahiri."* Piper anaelezea hivi, "Ni Jambo moja kwa mgeni katika Imani kumpinga Kristo. Lakini ni jambo lingine kwa mtu aliyekuwa kanisani ambaye amepewa nuru na kuonja kipawa cha mbinguni na kuwa mshirika wa Roho Mtakatifu na ameonja Neno zuri la Mungu na nguvu za zamani zijazo— ni jambo jingine kwa huyo mtu kusema baada ya matendo hayo yote na baraka hizo zote, 'Ninadhani gunia inatoa kilicho bora kuliko Kristo.' Huko ni kumsulubisha Yes umara ya pili na kumweka kwenye aibu kwa Dhahiri ambayo ni mbaya Zaidi kuliko angefanya mtu wa nje na Yesu, ambaye hajawahi kuonja kweli." (Piper 1996: (Kwa nini inaitwa Kumsulubisha mara ya pili) Hakuna mtu aliyepo katika hali hiyo inayoendelea ya kumchukia na kumkana Kristo anayeweza kuokolewa, kwa sababu, wapo katika hali ya kutoamini inayoendelea, kutotubu, na wanaendelea kumwaibisha Kristo. Kwa hali hiyo hawatafuti kutubu na wanapingana na namna pekee ambayo kwa hiyo toba ingewafikia. Kama asemavyo Grudem, ni vigumu kuwarejesha hao watu kwenye toba labda kwa sababu mioyo yao "mioyo yao ni migumu na dhamiri zao zimekuwa sugu" (Grudem 2000: 154). Hali hii inafanana na ile ya 1 Tim. Katika **1 Tim 1:5** lengo la mafundisho ya Kikristo ni (na kweli, Imani iokoayo) ni *"upendo katika moyo safi na dhamiri njema na Imani isiyo na unafiki''* **1 Tim 4:1-2** inasema kuhusu wa aina hiyo "kujitenga," ambayo husababisha ndani yao *"wakichomwa moto dhamiri zao kama kwa chuma cha moto cha kuwekea alama."* Neno la kiyunani linalosimama kwa ajili "kujitenga" katika **1 Tim 4:1** na neno "kujitenga" katika **Ebr 6:6**, lakini matokeo yanafanana. Zodhiates anaeleza hivi, wale wanaojitenga katika **1 Tim 4:1** "haisemi kuhusu wale ambao waliamini wakati fulani, bali wale waliokataa kuamini, waliosimama mbali" (Zodhiates 1993, *aphistēme,* 301). Hao watu hawana "dhaminiri njema" ya kweli, Imani inayookoa, bali wana "dhamiri zilizochomwa," kwa hiyo huwafanya iwe vigumu kwao kutubu na kuiamini injili. Hii pia inaonyesha Zaidi katika **Ebr 9:14** na **10:22**, vifungu hivyo viwili huonyesha kwamba wale walio na Imani ya kweli inayookoa dhamiri zao zimesafishwa na Kristo na sasa wana dhamiri safi.

Ingawa Kristo aliwaombea wale ambao walikuwa wanamsulubisha yeye, *"Baba, uwasamehe; kwa kuwa hawajui watendalo"* (**Lk 23:34**), kukosekana kwa toba ya kweli na Imani, ilikuwa vigumu kwa Baba kuwasamehe kama ilivyo vigumu kuwafanya upya wale waliojitenga katika **mst. 6**. Kama Pet O'Brien anavyoeleza, "Kwa kutowarejesha wale wanaopinga, Mungu anaruhusu maamuzi ambayo ni msimamo wao kusimama." (O'Brien 2010: 226). Kwa nyongeza, wale waliomsulubisha Yesu walifanya hayo kwa ujinga (**1 Kor 2:8**); Wale wanaohusika na **mst. 4-8** siyo wajinga bali walikuwa wamepokea ufahamu sahihi, na kujihusisha nao, na kuuweka kwenye utendaji, katika kanisa na katika injili. Hali hii inaendana na hali ya mtu anayeelezwa kwenye **Ebr 10:29**, ambaye alikuwa *"aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo."* Watu wanaoelezwa katika **mst. 4-8** wanafanana na wale ambao ni *"[16]kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. [17]Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa (maana hakuona nafasi ya kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi."* (**Ebr 12:16-17**)

---

[24] Kwa sababu mstari wa **6** unaongea juu ya kufanywa upya na kutubu, hii inatupa kujua kuwa wahusika wa vifungu hivi huko nyuma ni kama walishawahi ''kutubu'' Biblia hutofautisha toba ya kweli na ya uongo. Toba ya uongo ni ya kujifanya, ya kihisia, au kujihurumia na majuto ambayo lengo lake ni kuepuka madhara ya dhambi wala si majuto ya kweli kwa ajili ya kutenda kosa au moyo uliobadilika, kuchukia na kuiweka dhambi mbali. Kwenya toba ya uongo, mtu anakuwa anasikitika kwa kua amekamatwa, au anasikitika kwa kuwa ataadhibiwa, lakini si kwa tendo alilofanya. Toba ya kweli ni badiliko la ndani la ufahamu inayosababisha badiliko la Maisha, yaani kugeuka kutoka kwenye Maisha ya dhambi na kumgeukia Mungu. Kwa hiyo, **2 Kor 7:10** inasema *"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti."* **Mt 3:8** inaonya watu *"Basi zaeni matunda yapasayo toba [ya kweli]."* Waliojadiliwa katika **Ebr 6:6** kwa hakika walifanya toba ya uongo amabayo kwa sababu ya maamuzi ya makusudi ya kumwacha Mungu, ilifanya iwe vigumu kwao kufanywa upya na kufanya toba ya kweli (tazama Grudem 2000: 148-50).

Ni kama Yuda Iskariote, aliyekuwa pamoja na Yesu kwa miaka mitatu alipata baraka zote zilizotajwa kwenye **mst. 4-5**, na bado alimsaliti Yesu. Baada ya kufanya hivyo, *"Akavitupa vile vipande vya fedha katika hekalu, akaondoka; akaenda, akajinyonga."* (**Mt 27:3, 5**), lakini hakuwahi kutubu kweli na kumgeukia Bwana.

Mistari ya 7-8 inafafanua yale yaliyokwisha kuelezwa na kuelezea uhusiano uliopo kwenye mstari unaofuata kwa kutumia neno "Kwa kuwa." Hii mistari miwili haielezei "shamba ambalo lilikuwa hai na lenye mimea ambalo sasa limepoteza mimea yake. Picha inayoonyeshwa hapa ni ya mashamba mawili tofauti—moja ni yenye kutoa mazao na iliyobarikiwa; nyingine ni kame na imelaaniwa. Ninafikiri hapa kinachosemwa ni: ikiwa tupo kanisani pamoja na nuru na Roho Mtakatifu na neno na kazi ya Mungu inayokuja kwetu kutubariki na kutujenga kwa kiwango fulani, na baadaye tukageuzia mgongo hayo, sisi tunakuwa kama shamba lisilo na mazao na tutaingia kwenye hukumu. Mvua tuliyopata (nuru, Roho, neno, nguvu) havijasababisha uhai kwenye shamba." (Piper 1996: 1. Angalia mstari wa 7-8) Kulinganisha mavuno ya mashamba yote mawili. William Lane anaeleza, "Kwenye mfano [**mst. 7-8**] shauku yote ipo kwenye mavuno, na wala siyo dalili za awali za ukuaji. ''Kinachoamua ni kinachozalishwa." (Lane 1991: 143) Na tena, hii inaelezea juu ya jambo la uzalishaji na uvumilivu. Hiki kifungu chote kinafanana na mfano wa Yesu wa mpazi na mbegu. (**Mt 13:1-23; Mk 4;1-20; Lk 8:4-15**). Mbegu za aina moja zilipokelewa kwa njia tofauti na watu tofauti. Moja tu ilianguka juu ya *"udongo mzuri";* hiyo tu ilizaa na kuvumilia. Nyingine "hazikuwa na thamani" kwa mpanzi, kama ilivyo katika **mst. 8** ambao husema juu ya watu wale wanaojadiliwa katika **mst. 4-6**.

Tulipotazma kwenye muktadha wa karibu Zaidi kabla ya fungu la, **5:11—6:3**, tuliona kwamba msemo *stoicheion* (*"kanuni za awali"*) umetumika katika **5:12**. Kama tulivyojadili hapo juu, matumizi mengine yote ya *stoicheion* kwenye AJ inaonyesha kwamba kushikilia haya mafundisho ya awali haionyeshi kuwa mtu ameokoka au ataokolewa, hata ingawa mafundisho hayo yanapatikana kwenye ukristo na ni ya msingi katika Ukristo. Hiyo ndio maana labda kifungu cha **mst. 4-8** ikifuatiwa na **5:11—6:3**: wale ambao hushikilia tu those "kanuni za awali" wanaweza kuonekana wakristo lakini siyo. Kwa upande mwingine, muktadha wa karibu Zaidi baada ya kuanza kwa kifungu chetu katika **6:9**. Huo mstari unaotofautisha "wewe" kutoka kwa wale watu waliojadiliwa kwenye **mst. 4-8**. **6:9** ambao husema, *"Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na yaliyo na wokovu."* **Mistari ya 10-20** kisha inaendelea kuongelea juu ya nguvu za Mungu zinazotuokoa katika Imani yetu. **10:39** Inaongeza, *"Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye."* Kwa hiyo mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaonyesha kuwa mwumini wa kweli, aliyezaliwa mara ya pili, hawezi, kwa hakika kujitenga na Kristo mwandishi wa Waebrania anaonesha kuwa mtu ambaye kwa hakika amezaliwa mara ya pili haweza kwa hakika kujitenga na *"kumsulubisha Mwana wa Mungu kwa mara ya pili na kumdhihaki wa dhahiri"* (yaani., kufanywa mgumu, kutotii, kupungukia, kuchoka na kukata tamaa, kuwa na shina la uchungu, au kukataa na kwenda mbali na Kristo) na kwa sababu hiyo hawezi *"kushindikana kufanywa upya tena na kutubu"* (**mst. 6**).[25] Kwa ujumla watu wanaoelezewa kwenye **Ebr 6:4-8** walikuwa na baraka nyingi za kiroho lakini hawajawahi kuokolewa kamwe.

5. <u>Tunashikilia tumaini liliwekwa mbele yetu kwa uaminifu unaovumilia (**6:9-18**).</u>

[9]Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na yaliyo na wokovu. [10]Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia. [11]Nasi twataka sana kila mmoja wenu aidhihirishe bidii ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho; [12]ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu. Uhakika wa Ahadi ya Mungu [13]Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sababu alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapa, aliapa kwa nafsi yake, [14]akisema, "Hakika yangu kubariki nitakubariki, na kuongeza nitakuongeza." [15]Na hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi. [16]Maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao; na kwao ukomo wa mashindano yote ya maneno ni kiapo, kwa kuyathibitisha. [17]Katika neno hilo Mungu, akitaka kuwaonyesha

[25] Mambo haya yote ya kimuktadha inaondoa mtazamo wa Arminian na kuufanya siyo mtazamo ulio na uwezekano. Shida nyingine ya mtazamo huo ni kwamba, kwa kufahamu mstari huu **6:6**, inaweza kusababisha uwezekano wa "ukipotea mara moja, umepotea siku zote." Na hilo si sawa katika mtazamo wa fundisho la Arminian. Vile vile, Mtazamo wa Kukosa lishe bora kiroho nao hauna maelezo ya picha inayojitokeza katika mstari wa 7-8, ambao unasema kuhusu kulaaniwa na kuchomwa ikiwa ni tofauti na kukosa baadhi ya faida. Pia hauonekani ukisimamia kwa nguvu ''kutowezekana'' kufanywa upya na kutubu (**mst. 6**), ambao tena huenda Zaidi ya kukosa ya kukosa tu faida kadhaa za kiroho. Mtazamo wa Kinadharia unaonekana hauendani na sauti ya maonyo ya mstari wa 6 na wa 8, ambayo inaonekana kuwa na ukali sana kama ambavyo ingekuwa kama hicho kitu hakiwezi kutokea kamwe. Hatimaye, Jamii ya Agano mtazamo wao unaonekana unaenda sawa lugha ya kibinafsi ya **Waebrania 6** na msisitizo wa wahusika katika maeneo kama **Waebrania 11**.

zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati; [18]ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu;

Mistari hii inatofautiana na hadhira ya mwandishi na wale aliokuwa anawaongelea katika **mst. 4-8**. Mistari hii pia inaeleza tofauti kati ya Imani ya kweli inayookoa na imani ya muda mfupi isiyookoa. Kwa hiyo, **mst. 9** inawaita wale ambao wanapewa ujumbe sasa "wapendwa," na pia anasema *"katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi,."* Maelezo katika **mst. 9** ni kuhusu *"yale mambo yahusuyo wokovu,"* **mst. 10** unahusu *"kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu,"* **mst. 11** kuhusu kuonyesha "bidii", na **mst. 12** kuhusu kutokuwa "wavivu" na kuwa *"wafuasi wa wale ambao kwa njia ya Imani na uvumilivu wanekuwa warithi wa ahadi"* yote hayo yanadhihirisha asili ya imani ya kweli na hai, inayokoa, kama ilivyojadiliwa mapema katika ile "mihimili mitatu" ya Imani. Kipekee, **mst. 10** unaonyesha huduma na kuwatumikia wengine (*"kuwahudumia watakatifu"*) inatokana na kujitoa kwa Mungu (*"upendo ambao umeonesha kwa jina lake"*). Hii inaonyesha kwamba Imani ya kweli inayookoa inajidhihirisha yenyewe katika kutimiza kile ambacho Yesu amesema ni amri mbili zilizo kuu, *"'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako"* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Mt 22:37-39**). Upendo ndiyo udhihirisho mkuu wa uhalisia wa wokovu, na sio maarifa(kuangaziwa), nguvu za miujiza (nguvu za zamani zijazo), au uzoefu wa kiroho (kuonja kipawa cha mbinguni, neno zuri la Mungu, na kuwa mshirika wa Roho Mtakatifu). Upendo wa Mungu kwa wengine (**mst. 10**) unabeba *"mambo yaliyo mazuri zaidi . . . mambo yahusuyo wokovu,"* (**mst. 9**). Hii ina maana wale watu katika **mst. 4-5** *hawaja*okoka. Vipengele katika **mst. 11** kuhusu kutambua uhakika mkamilifu wa tumanini *"hadi mwisho"* na **mst. 12** na **15** kuhusu "uvumilivu" inaonesha huo uvumilivu ni sehemu ya ile Imani ya kweli inayookoa.

Maneno ya kutia moyo katika mstari wa **12** kwamba*"msiwe wavivu, bali iweni wafuasi wa wale ambao kwa njia ya Imani na uvumilivu wamerithi ahadi"* inarejea nyuma kwenye maonyo na kutia moyo katika **5:11—6:3**. Neno "uvivu" ni neno lile la kiyunani linalotafsiriwa kama "butu" katika sura ya **5:11**. Maneno ya kutia moyo ya kuwa ''wafuasi'' wa wale ambao *"kwa njia ya Imani na uvumilivu wamezirithi baraka"* ni njia kuu ambayo kwayo wasonaji wa kitabu cha Waebrania wataweza *"kfanya bidi hata kufikia ukomavu"* (**6:1**). Kuwa wafuasi wa watu waliotembea sawa na Mungu inashauriwa mara kwa mara katika AJ (**Yoh 13:15; 1 Kor 4:16; 11:1; 1 Thes 1:6; 2:14**). Kuwa wafuasi kuna thamani kubwa ya kiutendaji, na tena, inaonyesha asili ya Imani ya kweli inayookoa.

Mistari ya 13-18 inasisitiza umakini wa ahadi za Mungu, makusudi yasiyobadilika, na kwa hiyo, uhakika wa neno lake. Hii ni lazima iwe motisha kuu kwetu na hamasa ya kubakia kwenye uaminifu n akutorudi nyuma, kwa sababu, kwa kubakia waaminifu, tutakuwa na *''uhakika mkamilifu wa tumaini mpaka mwisho''* (mstari wa **11**), *"kuzirithi zile baraka"* (**mst. 12**), na *wata "lishika lile tumaini lililowekwa mbele yao"* (**mst. 18**). **Mstari wa 14** unanukuu **Mwa 22:17**. Rejea ya viapo kwenye **mstari wa 16** inaakisi hitaji la asili la watu kuhakikishiwa na kutumanishwa kwa njia ya kiapo. Viapo mara kwa mara huwa vinatumika katika nyeti ya Maisha, kama vile kutoa Ushahidi mahakamani, kuingia kwenye ndoa, au kuingia kwenye nafasi katika ofisi. Mungu hahitaji kuapa, kwa kuwa *"haiwezekani kwake kusema uongo''* (**mst. 18**). Hata hivyo, aliapa kwa Ibrahimu ili kumpa uhakika juu ya Agano aliloingia naye. Melezo kwenye **mst. 13** kwamba*"kwa kuwa hana aliye mkubwa wa kuapia kwake, Aliapa kwa nafsi yake mwenyewe"* na rejea hii ipo kwenye **mst. 17** Mungu anaweka agano rejea nyuma kwenye **Mwa 22:16-18**, mahali Mungu anamwambia Ibrahimu *"[16]Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee, [17]katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; [18]na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu."* (tazama **Gal 3:7, 13-14, 16, 29**). Vile *"vitu viwili ambavyo havibadiliki na kwa hayo Mungu hawezi kusema uongo"* (**mst. 18**)—kutobadilika kwa kusudi lake (yaani ahadi yake) na kiapo chake—vinatuhakikishia kwamba, ikiwa tutavumilia katikaImanii, kile ambacho Mungu ametuahidi, kwa kuwa *"tumemkimbilia"* Kristo.

D. Kristo ndiye mdhamini wa tumaini letu kwa sababu yeye ni kuhani mkuu kwa mfano wa Melekizedeki (6:19—8:5)

1. <u>Tunalo tumaini kwa sbabu Kristo ni kuhani kwa mafano wa Melekizedeki (**6:19-20**)</u>.

[19] Tumaini tulilonalo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, [20]alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.

Ingawa wachambuzi wengi wanahusisha mistari miwili kwenye hitimisho la sehemu ya mwisho, lakini kiukweli kiunganishi na yanatambulisha sehemu inayofuata kuhusu Melekizedeki. **Mstari wa 19** unasema kuhusu "tumaini" ambalo limerejewa kwenye **mst. 18**; **mst. 20** unasema kuhusu Yesu aliyeingia kwenye patakatifu pa patakatifu pa kweli kama mtangulizi wetu ambaye amefanyika *"kuhani mkuu kwa mfano wa Melekizedeki."* Maudhui hayo yataelezwa kwenye sura ya **7:1—8:5**.

Tumaini letu siyo shauku tu ya kutaka kitu kiwe kweli au kitokee. Ni Zaidi ya hivyo. Tumaini la Kikristo ni ni shauku yenye ujasiri wa matarajio kutimia. Tunaweza kuwa na ujasiri wa kutimia kwa matarajio yetu kwa sababu yapo kwenye misingi ya kusudi la Mungu lisilobadilika. (yaani, ahadi yake) na kiapo cha Mungu. Matokeo yake **mst. 19** unaeleza tumaini letu kama *"nanga ya roho."* Nanga hubakia imara chini ya bahari, bila kujali mawimbi yakoje wala bahari yenyewe. Nanga ya tumanini letu lazima lifanye kazi ya kuimarisha Maisha yetu yote, pasipo kujali hali tunazopitia. Ndio maana, hasa hasa katika nyakati ngumu na zinazobadilika, ni muhimu kujua na kukumbuka kwamba kusudi la Mungu ''halibadiliki'' (**mst. 17**). Kwa hiyo, tumaini katika ukamilifu wake ni *"hakika na imara."*

Sehemu ya mwisho ya **mst. 19** na **20** inafanya zaidi. Inaelezea tumaini letu kama *"lile linaloingia kwenye pazia, alipoingia Kristo kama mtangulizi wetu, aliyefanyika kuhani wetu mkuu kwa mfano wa Melekizedeki."* Haya si maelezo tu kuhusu Melekizedeki bali pia inalifungamanisha tumaini letu na Yesu Kristo. **Ebr 9:24** inatuambia kwamba *"Kristo hakuingia kwenye patakatifu palipotengenezwa kwa mikono, nakala tu ya ile ya kweli, bali aliingia mbingu yenyewe, sasa aonekane mbele za Mungu kwa ajili yetu."* Zaidi ya hilo, kuhani wetu mkuu sana *"aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee"* (**Ebr 7:25**). Kwa sababu Yesu ni "mtangulizi," wetu na tuna uhakikisho wa kumfuata yeye nyuma ya pazia na kuingia patakatifu pa patakatifu. Matokeo yake, mpaka siku ambayo *"tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, [20]njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake; [21]na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; [22]na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi. [23]Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu."* (**Ebr 10:19-23**) Matokeo yake ni kwamba, kwa hakika tumaini ni *"lenye uhakika na imara,"* kwa sababu haitutegemei sisi, au mazingira yetu, bali Yesu Kristo, ambaye ni *"yeye yule jana leo n ahata milele"* **(Ebr 13:8**).

2. <u>Asili ya Melekizedeki na ukuhani wake (**7:1-10**).</u>

[1]Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki; [2]ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, mfalme wa amani; [3]hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.

[4]Basi, angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu, ambaye Ibrahimu, baba yetu mkuu, alimpa sehemu ya kumi ya nyara. [5]Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani, ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu. [6]Bali yeye, ambaye uzazi wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, akambariki yeye aliye na ile ahadi. 7Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa. [8]Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai. [9]Tena yaweza kusemwa ya kuwa, kwa njia ya Ibrahimu, hata Lawi apokeaye sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi; [10]kwa maana alikuwa katika viuno vya baba yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye.

Wasomi kadhaa wanamtambua Melekizedeki kama "kivuli" cha Kristo, wakipingana na wazo linalosema yeye ni Yesu aliyeonekana kabla ya kuzaliwa kwake kama mwanadamu. (tazama, k.mf., Duncan 2013; Jackson 2025a; "Alikuwa Melekizedeki" n.d.; "Yesu ni bora" 1993-1994; Hanson 1965: 66–68; Carson 2013: 162–72). Hata hivyo, kwa ajili ya sababu zifuatazo, Ninafikiri ni vizuri kumtazama Melekizedeki kama kuonekana kwa Kristo kabla ya kufanyika mwili, kuliko kuwa tu kivuli cha Kristo. Melekizedeki anaoekana mara moja, katika **Mwa 14**, baada ya Ibrahimu kuwashinda wafalme wanne kwenye vita. **Ebr 7:1-3** inamwelezea yeye kwa misemo yenye kumwinua sana, kama vile *"mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki; [2]ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, mfalme wa amani; [3]hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.*

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania hamwiti Melekizedeki "kivuli" cha Kristo kama vile Kristo au Kristo aliye "ambaye si kivuli" ya Melekizedeki, ingawa alitumia neno la kiyunani *tupon* ("kivuli") katika **Ebr 8:5**, mahali inatafsiriwa kama "mfumo," kuhusu mfano wa hema ya kukutania. Yeye pia alitumia neno *antitupa* ("iliyo halisi") katika **Ebr 9:24**, mahali inapotafsiriwa kama "nakala," ikiwa inahusu mahali patakatifu hekaluni. Yeye pia aliziita sadaka zitolewazo na makuhani kwa kufuata sheria *"nakala na kivuli cha mambo ya mbinguni"* (**Ebr 8:5**; *hupodeigma* ikiwa na maana ya *"nakala"* na *skia* ikiwa na maana ya "kivuli") na sheria yenyewe aliita *"kivuli cha mambo mazuri yanayokuja"* (**Ebr 10:1**, *skia* kwa ajili ya "kivuli"). Na katika **Ebr 9:23** anarejea kwenye *"nakala* [*hupodeigmata*] *ya mambo ya mbinguni"* ikiwa na kinyume *"mambo ya mbinguni yenyewe."* Alitumia neno la kiyunani *parabolē* (kielelezo, kiwakilishi, au mfanano) katika **Ebr 9:9** kwa ajili ya hema ya kukutania au hekalu kama ''alama'' kwa wakati uliopo na katika **Ebr 11:19** kwa ajili ya Isaka, ambaye Ibrahimu alimpokea tena kama "kivuli" cha ufufuo. Kwa kuwa mwandishi ametumia lugha hii katika matukio kadhaa, yeye kutokufanya hivi kwa ajili ya Melekizedeki ni muhimu na inaonesha kwamba hamtazami Melekezedeki kikawaida yaani kama kivuli, bali ni uhalisia wa kweli ambao ni Yesu Kristo mwenyewe katika mwonekano wake kabla ya kufanyika mwili.

Pili, kulingana na **Mwa 14:18**, Melekizedeki *"alitoa mkate na divai."* Hiyo humweleza kwa wazi Yesu aliyeasisi ushirika wa mkate na divai (karama ya Bwana) kwenye "Kwenye karamu ya mwisho" (**Mt 26:26–28; Mk 14:22–24; Lk 22:14–20; 1 Kor 11:23–26**). Maelezo mengine kuhusu Melekizedeki katika Ebr **7:1–3** vile vile inamhusu Yesu. Kwa mfano Melekizedeki ni *''mfalme wa Salemu, ambaye ni ''mfalme wa amani''* (**Ebr 7:2)** *''Salemu'' maana yake ni ''amani''* Yesu ni *''mfalme wa amani''* (Isaya **9:6**), yeye atoaye *"Amani yangu . . . si kama ulimwengu unavyotoa na si kama"* (**Yoh 14:27**). **Efe 2:14** anaongeza *"Yeye mwenyewe ni amani yetu.''* Namna ambavyo "Salemu" na "amani" zimeungana katika mstari wa 2 inatupa kujua kuwa "Salemu" siyo eneo la kijiografia la mji, bali imetumika kama ishara, na inatoa ujumbe kwamba "Salemu" ni "amani" yaani amani ya Kristo. Salemu siku zote inafahamika kama Yerusalemu (tazama **Zab 76:2**). Yesu alikuwa, kwa hakika, "mfalme wa Wayahudi" (k.mf., **Mt 2:2; 27:11, 29, 37**), ambao makao yao makuu ni mji mkuu wa Yerusalemu[26]. Kwa kuongezea, Yesu ni masihi aliyetabiriwa, moja ya jukumu ambalo lilikuwa ni kuwa mfalme—mfalme wa mwisho wa ulimwengu—na kutawala kutoka Sayuni (**Zab 110:1–2; Yer 23:5–6**). Melekizedeki yeye pia anatambulishwa kama *"mfalme wa haki."* Yesu ni mwenye haki mkuu (**Rum 3:25; 10:4; Flp 3:9; 1 Yoh 2:1**); **Ebr 1:9** ni mahususi kwa ajili ya Yesu, *"Umependa haki."* Tesfaye Kassa anaeleza kwamba jina la Melekizedeki "*maana yake ni 'mfalme wa amani'* na cheo chake cha *'mfalme wa Salemu' ina maana 'mfalme wa amani'* (7:2). Vyeo hivi vyote viwili vinahusiana na masiha, na kimahususi vinahusiana na Yesu (Isaya 9:6-7; 2 Tim 4:8)." (Kassa 2006: 1498) A. M. Stibbs anaongeza, "Tunafahamu kuwa maandiko humweleza yeye kama *mfalme* pia kama *kuhani*. Muunganiko wa haya mawili ulikiwa ni sifa inayomtofautisha Masiha *Ling.* [**Ebr**] 8:1 and Zc. 6:13." (Stibbs 1970: 1203) Hilo pia linazidi kutilia mkazo mfanano kati ya Melekizedeki na Yesu.

Ebr 7:3 inamweleza Melekizedeki kama mtu *"asiye na baba wala mama."* D. A. Carson anaeleza, "Wakati Yesu anaitwa mwana wa Maria, yeye ni uzao wa Mungu wa milele: pasipo baba, na pasipo mama" (Carson 2013: 170). Kwa kuwa **Ebr 7:3** pia inamfafanua Melekizedeki kama asiye *"na mwanzo wa siku zake wala mwisho wa Maisha,"* yeye "unaweza kushindwa kusema kwamba Kristo alikuwepo kabla yake kwa muda kidogo kuliko yeye" (Hanson 1965: 66). Akielezwa kama asiye na mwanzo wala mwisho ina maana Melekizedeki hakuumbwa, hafi, na wa milele. Hii inakuwa siyo sifa ya kiumbe kilichoumbwa, hata malaika. Matokeo yake, Melekizedeki lazima atakuwa ni Yesu Kristo aliyeonekana kabla katika mwili, ambaye pekee, kama Mwana wa Mungu, hakuumbwa, hafi, na ni wa milele. **Ebr 7:3** inasema yeye *"alifanyika Mwana wa Mungu."* Ingawa yale maneno hayaelezi kwa wazi kwamba yeye *alikuwa* Mwana wa Mungu, haizuii Melekizedeki kama Kristo, kwa kuwa katika **Dan 3:25** mtu wa nne kwenye tanuru la moto anaelezwa kama *"mwana wa miungu."* Mtu wa nne kwenye tanuru la moto anayesemwa na Danieli siyo tu "kama" mwana wa miungu wa kawaida, bali mwana wa miungu halisi, nayo ni, malaika, kama anavyoelezwa kwenye **Dan 3:28**, au mwonekana wa Yesu Kristo kabla ya kufanyika mwili. Kwa namna hiyo hiyo, **Flp 2:6-8** inasema huyo Yesu *"alikuwa na namna ya Mungu . . . lakini . . .*

[26] Wakati wa matukio ya ufunuo 14, Yerusalemu ilikuwa inakaliwa na kabila la Wakanani linaloitwa Wayebusi ambao waliuita mji "Yebusi" (Amu 19:10) (Eames 2020: Ngome ya Wakanani). Ilikuwa haikubaliki kabisa alikuwa au angeweza kuwa ''*kuhani wa Mungu aliye juu sana''* kama angekuwa mfalme wa kabila lisilo la Mungu katika mji wa kipagani. Hilo tena linatujulisha kwamba Melkizedeki alikuwa Kristo aliyeonekena katika mwili kabla ya kufanyika mwili akiwa si mfalme halisi wa kidunia na wa kihistoria. Pia hakuna maelezo ya ziada ya kibiblia au chochote kinachomtaja Melkizedeki kama mfalme aliyekuwepo katika historoa au kuhani au kinachoonesha kuwa kwamba alikuwepo mtu wa aina hiyo (Yeyote asiye katika Biblia wakati wowote). Kwa nyongeza, kwa muktadha mwonekano wa Kristo wowote ni wa kimatukio (tazama Menn 2025:48-60). Hilo lisingekuwa tatizo kama Melkizedeki angekuwa mfalme halisi, mwanadamu, kwa kuwa angekuwa ameishi kwa miaka mingi tofauti kabisa na mwonekano wa Kristo katika mwili kulingana na muktadha.

alijishusha mwenyewe akachukua namna ya mtumwa, akawa na mfano wa mtu. Alipoonekana ana mfano wa mtu." Yesu kwa hakika alikuwa Mungu na si tu kwamba alionekana kama mtu, kwa hakika alikuwa mtu kamili.

Hii imetajwa katika **Ebr 7:15-16**, inayoongelea "*mfano wa Melekzedeki ambaye hakufanyika kwa sheria ya kimwili, bali kwa nguvu ya uzima usioweza kuharibiwa*." Huyu ni lazima awe ni Kristo tu ambaye pekee hawezi kuharibiwa.

Katika **Ebr 7:3**, maelezo kuhusu Melekizedeki inahitimisha kwa kusema kwamba *"ni kuhani milele."* Ukweli unamfunua Melekizedeki kama Yesu kwani **Zab 110:4** inasema kuhusu Yesu, *"BWANA ameapa, Wala hataghairi, Ndiwe kuhani hata milele, Kwa mfano wa Melkizedeki.'"* (pia tazama **Ebr 5:6, 10; 6:20; 7:11, 15, 17**). Yesu alimtokea Ibrahamu katika nafsi ya Melekizedeki "akionyesha ukuu wa ukuhani wa masihi anayekuja dhidi ya ukuhani wa Lawi anayekuja" (Hanson 1965: 72). Hili linakaziwa katika **Ebr 7:8**, amabyo inarejea kwenye fungu la kumi alilotoa Ibrahimu kwa Melekizedeki, akisema, *"Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai."* Hii ni kusema kwamba Melekizedeki ni mkuu kuliko Lawi, kwa sababu ukuhani wa Lawi upo kwa watu ambao hufa lakini ukuhani wa Melekizedeki unaishi milele. Anthony Hanson anaeleza kuwa "tunajua ya kwamba Melekizedeki anaishi milele kwa sababu tu ya Zaburi 110.4, mahali Mungu anamwahidi Kristo ukuhani wa milele. Kwa hiyo Melekizedeki anafanana na Kristo." (Hanson 1965: 70) Hii inathibitishwa katika **Ebr 7:25**, ambayo huelezea moja ya sifa za ukuhani mkamilifu ambao ni uwezo wa milele wa kuhani kuomba kwa ajili ya watu wake. "Melekizedeki anasemekana anao huo ukuhani endelevu milele kwa ukuhani wake kwa hakika una hiyo sifa ya ukamilifu; lakini, ni Mungu pekee anayo nguvu ya kuishi milele na kwa hiyo, Mungu tu ndiye anayekidhi kigezo hiki" ("13 Sababu" 2014: 7, Ukuhani wa Melekizedeki). Vile vile, **Ebr 7:27–28** inasema kwamba kuhani mkuu kwa mfumo wa Lawi kwanza hutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake, hata hivyo kwa kuwa Yesu hakuwahi kwa na dhambi na hana, hakuwa na haja ya kutoa kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake bali mwenyewe bali ni *"mkamilifu milele."* Kwa kuwa ni kuhani milele kwa *"kwa mfano wa Melekizedeki,"* Melekizedeki yeye mwenyewe ni lazima asiwe na dhambi. Kwa hiyo, Kristo na Melekizedeki lazima ni moja na wanafanana.

Kwa kuongezea, alimbariki Ibrahimu inayoonyesha ukuu wake kwa Ibrahimu, kwa sababu *"mdogo hubarikiwa na mkubwa"* (**Ebr 7:7**). Nje na baraka alizotoa Melekizedeki, mtu pekee kwenye Biblia aliyembariki Ibrahimu ni Mungu, ambayo huonyesha mfanano wa Melekizedeki na Mungu. Ibrahimu alitoa zaka kwa Melekizedeki. Hiyo haionyeshi tu ukuu wa Melekizedeki bali pia inaonyesha hadhi ya Melekezedeki, kwa kuwa *"zaka yote ya nchi, ya mbegu ya nchi au matunda ya miti, ni ya Bwana, na ni takatifu kwa Bwana"* (**Law 27:30**).

Hatimaye, "moja ya nakala za Bahari ya Shamu (11QMelch) inamwelezea Melekizedeki kama kiumbe cha Mbinguni ambacho kitaleta wokovu (ili kutimiza Isaya 52.7–10 na 61.1–3) na hukumu (kutimiza Zaburi. 7.7–8; 82.1–2) kwenye hitimisho la Jubilei ya mwisho (Lawi. 25)" (Nelson 1993: 511). Wokovu na hukumu ni kazi za Kristo pekee. Yesu pia alimnukuu **Isa 61:1–2** akijisemea yeye mwenyewe (**Lk 4:18–19**). Yote haya yanafunua ya kuwa Melekizedeki ni Yesu Kristo aliyeonekana kabla hajafanyika mwili.

Yote haya yanaenda sawa na kile tulichoona katika **1:1—2:18**, ambayo hujadili na kuonyesha ukuu wa Kristo: Yesu ni ufunuo wa Mungu (**1:1-3**); Kristo ni mkuu kupita malaika (**1:4-14**); Kristo pekee hutoa wokovu (**2:1-18**).

3. Makuhani wa Lawi wakilinganishwa na ukuhani wa Kristo (**7:11—8:5**).

[11] Basi, kama ukamilifu ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena ya kuhani mwingine ainuke, kwa mfano wa Melkizedeki, wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni? [12] Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike. [13] Maana yeye aliyenenwa hayo alikuwa mshirika wa kabila nyingine, ambayo hapana mtu wa kabila hiyo aliyeihudumia madhabahu. [14] Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani. [15] Tena hayo tusemayo ni dhahiri sana zaidi, ikiwa ametokea kuhani mwingine mithili ya Melkizedeki; [16] asiyekuwa kuhani kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili, bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo; [17] maana ameshuhudiwa kwamba, "Wewe u kuhani milele Kwa mfano wa Melkizedeki."

[18] Maana, kuna kubatiliwa kwa ile amri iliyotangulia, kwa sababu ya udhaifu wake, na kutokufaa kwake; [19] (kwa maana ile sheria haikukamilisha neno); na pamoja na hayo kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri zaidi, ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu. [20] Na kwa kuwa haikuwa pasipo kiapo, [21] (maana wale walifanywa makuhani pasipo kiapo; bali yeye, pamoja na kiapo, kwa yeye aliyemwambia, ''Bwana ameapa wala hataghairi, Wewe u kuhani milele") [22] basi kwa kadiri hii Yesu amekuwa mdhamini wa agano lililo bora zaidi.

[23]Tena wale walifanywa makuhani wengi, kwa sababu wazuiliwa na mauti wasikae; [24]bali yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. [25]Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.

[26] Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu; [27] ambaye hana haja kila siku, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yeye alifanya hivi mara moja, alipojitoa nafsi yake. [28]Maana torati yawaweka wanadamu walio na unyonge kuwa makuhani wakuu; bali hilo neno la kiapo kilichokuja baada ya torati limemweka Mwana, aliyekamilika hata milele.

8 [1]Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, [2]mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. [3]Maana kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe vipawa na dhabihu; kwa hiyo lazima huyu naye awe na kitu cha kutoa. [4]Kama angekuwa juu ya nchi, asingekuwa kuhani; maana wako watoao sadaka kama iagizavyo sheria; [5]watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima."

Ebr 7:11 inaanza na kiwango cha "ukamilifu." Kisha inalinganisha ukuhani wa Lawi wa AK na ukuhani wa Kristo, *"kwa mfano wa Melekizedeki"* (**mst. 15-17**). Ingawa Yesu hakuwa kuhani Although *"moja ya sheria za msingi za kimwili zinazohitajika"* (nayo ni, ni kwamba awe ametoka kwenye kabila la Lawi), kulikuwa na ''hitaji la kutimiza la kimwili'' muhimu kwa ajili ya ukuhani wa, nalo ni kufanyika mwili, ambalo kwa hilo Yesu *"ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake."* (**Ebr 2:17**). Sehemu hii na sehemu zingine za kitabu cha Waebrania, huonyesha kwamba Kristo ana kiwango cha ukamilifu kilichotajwa kwenye **mst. 11**: Alitimiza misingi yote wa kutoa dhabihu na kutimiza na kuzidi ukuhani wote wa AK, kwa sababu yeye pekee alikuwa na uwezo wa dhabihu kwa niaba yetu kwa sababu yeye pekee hakuwa na dhambi (**7:26**; pia tazama **Ebr 4:15**). Hii sehemu inaishia na **8:5** ikinukuu **Kut 25:40**. Nukuu hii inasisitiza kwamba mfumo wote wa AK, na ukuhani wake, hema, na sadaka, ni wa kidunia na una hadhi ya chini kwa kuwa ni,*"nakala na kivuli"* cha, mfumo wa AJ wa Kristo, ambao ni wa mbinguni. Kristo, kuhani wa kweli na wa milele, alijitoa mwenyewe kwenye hema ya kweli ya mbinguni. (**Ebr 9:11, 23-24**), ambayo hema ya dunia ilifanywa kwa mfano wake, iliyo nakala tu na kivuli.

Dhabihu ya Kristo msalabani, na kufufuka kwake na kupaa kwake, inazidi kwa mbali yote ambayo waliyatumaini kuyapata kupitia dhabihu za Waisraeli na makuhani, pamoja na kuhani mkuu katika Siku ya Upatanisho:

- Kwa sababu ya dhambi za wanadamu, pamoja na zake mwenyewe, kuhani mkuu katika siku ya Upatanisho alikuwa ni lazima kwanza atoe dhabihu kwa ajili ya dhambi zake na kisha kwa ajili ya watu wake (**Law 9:7; 16:6, 11, 15–16, 19–22, 24**). Kwa upande mwingine, ''*Yeye [Mungu]asiyejua dhambi alimfanya [Kristo] kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.''* (**2 Kor 5:21**).
- Kwa sababu ya Ukuhani wa Haruni kukosa ukamilifu, **Ebr 7:1—8:5** hii hutuambia kulikuwa na haja ya kuwa na ukuu mkuu kwa mfano wa Melekizedeki. Kwa hiyo, **Ebr 7:21** inanukuu **Zab 110:4**, *"BWANA ameapa, Wala hataghairi, Ndiwe kuhani hata milele, Kwa mfano wa Melkizedeki,"* na **Ebr 7:28** husema, *"Maana torati yawaweka wanadamu walio na unyonge kuwa makuhani wakuu; bali hilo neno la kiapo kilichokuja baada ya torati limemweka Mwana, aliyekamilika hata milele,"* ukuhani "dhaifu" wa AK ulizidiwa milele. *''Yesu ni kuhani kwa mfano wa Melekizedeki, na si…. Kwa mfano wa Haruni''* (**Zab 110:4; Ebr 5:6; 7:11**). Ingawa Mungu alimwapia Ibrahimu miaka zaidi ya 400 iliyopita kabla ya Lawi (tazama maelezo kwenye **6:3-18**, hapo juu), *"neno la kiapo, lililokuja baada ya sheria"* (**7:28**) inahusu uteuzi wa Kristo kama kuhani mkuu ukiwa umeungana na kufanywa kwake mwili, kulikorekodiwa kwenye **Zab 110:4**, kulikofuata na tangazo la kisheria.
- **Ebr 7:12** inasema kwamba, kwa kuwa kuja kwa Kristo kulifanya ukuhani mpya, *"ukuhani ukibadilika, kuna ulazima wa sheria pia kubadilika.''* T. D. Alexander anaeleza kwa muhutasari kwamba "kwa kurejea kwenye hili hapa 'badiliko katika sheria' inaonyesha kuwa taratibu zinazohusiana na ukuhani wa Lawi, hazitumiki tena kwa kuwa kanisa limekuwa hekalu jipya la Mungu'' (Alexander 2008: 150). Ukweli kuwa Kristo anitwa yote mawili "kuhani" na "kuhani mkuu" (**Ebr 2:17; 3:1; 4:14–15; 7:11, 15–17, 24, 26, 28; 8:1–2; 9:11**) inaonesha kuwa mifumo yote ya ukuhani wa AK imeondolewa kwa sababu, kulingana na sheria za AK, Yesu asingeweza kuwa kuhani kwa kuwa si wa uzao wa Haruni na wa ukoo wa Lawi bali ni

wa kabila la Yuda (**Ebr 8:4**; tazama **Mt 1:2–3; Lk 3:33–34**). Badala ya ukuhani wote kufanya kazi kama wapatanishi kati ya Mungu na wanadamu, sasa kuna *"Mungu moja, mpatanishi moja kati ya Mungu na watu, mwanadamu Yesu Kristo"* (**1 Tim 2:5**). Tofauti na ukuhani wa AK kuwa wa kabila la Lawi peke yao (**Hes 18:1–24; Yer 33:19–22**), kama matokeo ya dhabihu ya Kristo, waamini wote katika Yesu Kristo sasa ni makuhani mbele ya macho ya Mungu (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6; 5:10**).

- Kristo siyo tu alizidi ukuhani wa zamani na kuleta badiliko la sheria, kutoka sheria ya Musa na kuwa Sheria ya Kristo (**1 Kor 9:21; Gal 6:2**), pia alitupa *"tumaini bora, ambalo kwa hilo tunamkaribia Mungu"* (**Ebr 7:19**); hili *"tumaini bora"* hatimaye kwa sababu *"Yesu amekuwa mdhamini wa agano lililo bora"* (**Ebr 7:22**). *"Tumaini letu bora"* limejadiliwa kwenye **Ebr 6:19-20**. Agano Jipya ni mada ya sehemu inayofuata, **Ebr 8:6—10:18**. Tofauti ya kushangaza kati ya Agano la Kale na Agano Jipya inaweza kuandikwa kwa muhutasari kama ifuatavyo:

Agano la Kale	**Agano Jipya**
1. Katika Agano la Kale, watu walihitajika kutoa sadaka za dhambi daima (**Law 4:1-5:13; 5:14-6:7; 6:24-30; 7:1-8; 8:14-17; 16:3-22; Hes 5:5-10; Ebr 7:27**).	1. Katika Agano Jipya, alifanyika dhabihu ya kutosha kwa ajili ya dhambi zote za watu wake milele. (**Yoh 1:29; Ebr 7:26-28; 9:11-12, 28; 10:1-18**).
2. Katika Agano la Kale, dhambi za baadhi ya wana wa Israeli zilifunikwa, na ni kwa mwaka mmoja tu (**Hes 15:30-31; Ebr 9:7; 10:1-3**).	2. Kwenye Agano jipya dhambi zetu zote—zilizopita, za sasa, na zinazokuja na baadaye zimesamehewa milele—(Y**er 31:34; Mdo 10:43; 13:38-39; Ebr 10:1-18**).
3. AK halijatupatia uzima wa milele (**Rum 3:21; Gal 3:11, 21**).	3. Katika Agano Jipya, tumepewa uzima wa milele. (**Yoh 3:14-16, 36; 17:2-3; Ebr 5:9**).
4. Katika AK, Uwepo wa Mungu ulikuwepo ndani ya hekalu tu, na watu walitakiwa kwenda huko hekaluni ili kuwa karibu na uwepo wa Mungu (**1 Fal 8:10-11; 2 Nya 5:11-14; 7:1-2**).	4. Katika AJ, sisi *ni* hekalu, na ameingia ndani yetu (**1 Kor 3:9, 16-17; 2 Kor 6:16-7:1; Efe 2:21; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12**).
5. Katika AK, ni makuhani tu wanatakiwa kuingia hekaluni (**Hes 18: 22-23; Ebr 9:6**).	5. Katika AJ, Wakristo wote *ni* makuhani (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6; 5:10**).
6. Katika AK, Kuhani mkuu tu aliweza kuingia patakatifu pa patakatifu ili awe katika uwepo wa Mungu (**Law 16:2-34**).	6. Katika AJ, Kristo ni kuhani wetu mkuu (**Ebr 4:14-5:10; 7:1-10:25**).
7. Katika AK, kuhani mkuu angeweza kuingia pakatifu pa patakatifu siku moja kila mwaka (**Law 16:34; Ebr 9:7**).	7. Katika AJ, Kristo yupo katika uwepo wa Mungu akituombea (**Ebr 7:25; 9:24**).
8. Katika AK, Roho aliondoka hekaluni na hakurudi tena (**Ezek 9:3; 10:1-19; 11:22-23**).	8. Katika AJ, Yesu aliahidi kwamba yeye hataweza "kutuacha kamwe wala hatatusahau" (**Ebr 13:5**).
9. Katika AK, Roho Mtakatifu hakuwahi kuwa ndani ya watu ili alikuja juu ya baadhi ya wat una kisha huondoka (**Kut 31:3;** Hesabu **11:16-29; Amu 3:10; 6:34; 14: 6, 19; 1 Sam 10:1-11; 16:13-14; 19:20-24**).	9. Katika AJ, Roho Mtakatifu amekuja kuishi ndani ya waamini na hatawaacha wala hatawasahau (**Ezek 36:27; Yoh 14:16-17; 16:7; Mdo 2:14-18, 38-39; Rum 8:9; 1 Kor 3:16; 6:19**).
10. Katika AK, watu walikuwa watumwa wa sheria ambazo kamwe hawakuwezi kuzishika (**Mdo 15:10; Rum 7:6, 23; 8:2-3; Gal 3:23; 5:1**).	10. Katika AJ, Kristo alitimiza sheria kwa ajili yetu na kuandika sheria zake (sheria ya Kristo) kwenye mioyo yetu (**Yer 31:33; Mt 5:17; Rum 10:4; Kol 2: 13-15; Ebr 8:10; 10:16**).
11. Katika AK, watu walikuwa na mioyo ya jiwe (**Zek 7:12**).	11. Katika AJ, Mungu ameondoa mioyo yetu na kutupa mioyo ya nyama (**Ezek 11:19; 36:26; 2 Kor 3:3**).

Katika AJ tuna uhusiano wa moja kwa moja na wa kibinafsi na Mungu ambao hawakuwa nao waamini wa AK (**Yer 31:34; Ebr 4:16; 7:19**). Tunaweza kumfikia Mungu Baba yetu pasipo kikwazo, kwa njia ya Yesu Kristo, kitu ambacho ni ndoto tu kwa waamini wa AK (**Mt 27:51; Ebr 10:19-22**). Mungu pia ametufanya moja wa familia yake mwenyewe (**Rum 8:14-17; Gal 3:26; 4:6-7; Efe 1:5**). Yote haya yamefanywa, na anayeweza kufanya na Kristo tu.

- Mfumo wa zamani wa utoaji wa dhabihu ulihitaji dhabihu nyingi na makuhani (**Ebr 7:23; 9:25; 10:1, 11**). Makuhani zamani walikuwa na idadi kubwa *"kwa sababu kifo kiliwafanya wasidumu"* (**Ebr 7:23**). Lakini *"kwa kuwa [Yesu] anadumu milele, [yeye] anabaki na ukuhani wake siku zote"* (**Ebr 7:24**), na anahitajika kutoa dhabihu moja tu kwa ajili ya watu wote kwa nyakati zote (**Ebr 7:24, 27; 9:12, 25–28; 10:10–14**).
- **Ebr 8:3** inaeleza, *"Kwa kuwa kuhani anateuliwa ilia toe sadaka na dhabihu; kwa hiyo ni lazima pia kwa huyu kuhani kuwa na kitu cha kutoa."* Na hii, tena, inatuonesha tofauti kubwa ya thamani kwa kile alichofanya Yesu ikilinganishwa na kile na makuhani wa kidunia. **Law 16-17** inaeleza ulazima wa damu ya dhabihu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi. Kumwagika kwa damu ya mnyama anayetolewa kuwa

dhabihu ni muhimu ili kuhani mkuu apate damu ya kupeleka patakatifu pa patakatifu na kuinyunyiza kwenye kiti cha rehema. Dhabihu ya Yesu msalabani ilikuwa ni kitu ambacho Siku ya Upatanisho ilikuwa inatutazamisha siku zote. "Msalaba ulikuwa na maana kwamba ilikuwa lazima kuwe na 'kitu cha kutoa' ili kwamba Kristo awe na kitu cha kutoa kama kuhani (8:3). . . . Asili isiyo ya kawaida ya dhabihu ya Yesu ilikuwa ni Yeye kuwa na jukumu la ukuhani na la mkosaji kwa wakati mmoja, akijitoa mwenyewe kuwa dhabihu iliyowanufaisha wafuasi wake (7:27; 9:14, 26)." (Nelson 2003: 254, 257).

- Mfumo wa kale wa utoaji wa dhabihu haukuweza kuwabadilisha watu kutoka ndani au kuwafanya wakamilifu. Kwa dhabihu yake, Kristo hufanya hilo (**Ebr 7:11; 9:9–10; 10:1–2, 14–16**).
- Siku ya Upatanisho ilitumika kama ''ukumbusho'' wa dhambi kila mwaka. Kwa njia ya dhabihu ya Kristo, Baba *"hatakumbuka tena dhambi zao na uasi wao"* (**Ebr 10:3, 16–18**).
- Kristo alichofanya asichoweza kufanya kuhani wa kidunia. Kuhani wa kidunia alitumika tu kweye hema na hekalu na *"alitumikia nakala na kivuli cha mambo ya mbinguni"* (**Ebr 8:5**). Kristo alipaa mbinguni yeye mwenyewe, ambako hudumu akiwaombea watu wake mbele za Baba (**Ebr 7:24–25**). Hili linasisitizwa katika **Ebr 8:1-2**, inayosema kwamba Kristo *"ameketi mkono wa kuume kwenye kiti cha enzi cha ukuu katika mbingu, muhudumu wa madhabahu ndani ya hema ya kweli, ambayo Bwana ameitengeneza na siyo mtu."*
- **Ebr 7:25** pia inasema kwamba *"Yeye aweza kuwaokoa milele wale wamkaribiao Mungu kwa njia yake."* Neno lililotafsiriwa "milele" hapa, kwa hakika ni usemi wa kiyunani *eis to pantelēs,* wenye maana ya "kwa ukamilifu, utimilifu, kwa ujumla, ikihusu muda, siku zote, milele" (Zodhiates 1993: *pantelēs,* 1093). Kwa maneno mengine wokovu anaotoa Kristo ni mkamilifu kwa kila njia.
- Kwa kifo chake, ufufuo, na kupaa kwake, sasa Kristo anamwezesha kila mwamini kufanya kile ambacho kile ambacho makuhani wa AK peke yao wanaweza kufanya. Katika AK, makuhani peke yao waliweza kuingia mahali patakatifu pa hekalu. Yesu amewawezesha watu wake kwa kuwapa wote *"ujasiri wa kuingia mahali patakatifu kwa damu ya Yesu"* nyakati zote (**Ebr 10:19–22; 4:16**).

Kwa muhutasari, tofauti kati ya Ukuhani wa Lawi wa AK na Ukuhani wa Kristo ipo wazi katika maelezo yaliyotolewa: Ukuhani wa Lawi wa AK unatajwa kwamba ulikuwa na "udhaifu" (**7:18**), "usiofaa" (**7:18**), "haukuweza kuleta ukamilifu" (**7:19**), makuhani walikuwa "pasipo kiapo" (**7:21**), "walishindwa kuendelea kwa sababu ya kifo" (**7:23**), walikuwa na dhabihu kwa ajili ya dhambi zao" (**7:27**), "makuhani wakuu walio dhaifu" (**7:28**), wao "walitumika nakala na kivuli cha mambo ya mbinguni" (**8:5**); ukuhani wa Kristo unaelewa kwamba ulikuwa "ukamilifu'' (**7:11**), "kutokana na nguvu ya uhai usio haribiwa" (**7:16**), ni "kuhani milele" (**7:17, 21, 24**), huleta "tumaini bora" (**7:19**), "wenye kiapo" (**7:21**), "hakikisho la agano bora" (**7:22**), "aweza kuokoa milele" (**7:25**), "hudumu siku zote akiwaombea" (**7:25**), "takatifu" (**7:26**), "usio na hatia" (**7:26**), "usio na uchafu" (**7:26**), "uliotengwa mbali na wenye dhambi" (**7:26**), "ulioinuliwa katika mbingu" (**7:26**), "uliofanywa mkamilifu milele" (**7:28**), "kiti chake kipo mkono wa kuume wa Enzi mbinguni" (**8:1**), "Muhudumu wa madhabahu katika hema ya kweli, amabyo Bwana ameijenga na siyo mtu'' (**8:2**).

MASWALI YA MJADALA

1. Kristo ni mkuu kwa Musa kwa namna gani?

2. Kwa nini ilimpasa Yesu Kristo achukue asili yetu na kufanyika mwanadamu?

3. Eleza ukweli kwamba kanisa ni hekalu la kweli, au kile ambalo hekalu ilikuwa inaashiria siku zote. Kwa nini hiyo ni muhimu?

4. Asili ya ''kutokuamini'' ni nini na inahusisha nini? Kwa nini ni jambo linalohitaji kuwa makini sana?
5. ''Pumziko la sabato'' kwetu sisi ni nini? Hii ina matokeo gani kwa namna tunavyochukulia siku ya Jumapili *na siku zingine za wiki?*

6. Siku ya Upatanisho ilimwashiria Yesu kwa namna gani, na aliitimiza kwa namna gani?

7. Kwa nini ni muhimu kwamba Yesu ''*alijaribiwa katika mabo yote kama sisi, lakini hakutenda dhambi''* (Ebr 4:15)?

8. Eleza umuhimu wa Yesu kama kuhani mkuu. Hii inahusisha nini?

9. **Ebr 5:11—6:3** inaongelea umhimu wa "kukazana hata kufikia ukomavu," tofauti na kubakia tu kwenye "kanuni za awali." Kwa nini ni muhimu sana *"kukazana kufikia ukomavu"* na siyo kubakia kwenye "kanuni za awali? Tunawezaje *"kukazana ili kufikia ukomavu"?*

10. Ni nini asili ya Imani ya kweli inayookoa? Inahusisha nini? Inaonekanaje? "Mihimi mitatu ya Imani" ni ipi?

11. Imani ya mpito au Imani ya uongo ni nini? Tunawezaje kuitofautisha na Imani ya kweli inayookoa?

12. Tutafanya nini ili kuwasaidia watu kuwa wakristo wa kweli, waliozaliwa mara ya pili wenye Imani ya kweli inayookoa, tofauti na wakristo "wanaokiri" walio na Imani ya mpito au Imani ya uongo?

13. **Ebr 6:4-8** ni moja ya kifungu chenye ugumu katika kitabu cha Waebrania na AJ. Elezea kifungu hiki. Je unafikiri inaongelea nini na kwa nini?

14. Eleza kuhusu Melekezedeki. Kitabu kinaweka msimamo kuwa yeye alikuwa Yesu Kristo aliyejidhihirisha kabla ya kufanyika mwili. Wewe wanamwona kama "kivuli" cha Kristo. Je wewe una msimamo gani kuhusu hili na kwa nini?

15. Je ukuhani wa Kristo na Kristo ni mkuu kwa namna gani dhidi ya mfumo wa utoaji wa dhabihu wa Walawi wa AK na ukuhani wao?

16. Je ni kwa namna gani Agano Jipya ni kuu kupita Agano la Kale la Musa?

III. <u>Agano Jipya ni kuu kuliko Agano la Kale kwa sababu ya Dhabihu ya Kristo (8:6—10:18)</u>

Katika AK, Mungu aliahidi kufanya "Agano Jipya" na watu wake (**Yer 31:31-34**). Kwenye karamu ya Mwisho, Yesu alichukua kikombe, akasema, *"Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu."* (**Lk 22:20**). Agano Jipya ni kitu ambacho AK ilikuwa inalenga kukifikia. Sehemu hii inaelezea jinsi ambavyo na kwa nini Agano Jipya ni kuu kuliko yote yaliyotangulia kabla.

A. Yesu ni mpatanishi wa Agano Jipya (8:6)

Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora.

Wachambuzi wengi wanahusisha **mst. 6** kama hitimisho la sehemu iliyotangulia. Hata hivyo, mstari huu ni mwendelezo. Msemo wa utangulizi *"Lakini sasa"* inatofautisha Agano la zamani la Musa na ukuhani akirejea mst. wa 5 kile anachofanya Kristo kwa kuwa na *"huma bora Zaidi"*; pia inatambulisha Agano Jipya, ambayo *"imejengwa kwenye ahadi zilizo bora."* Huu utakuwa mwelekeo wa sehemu hii yote ambayo inaishia kwenye sura ya **10:18**. Kutokana na hilo, ni sahihi kuanza na mstari kama mwanzo wa sehemu hii kuhusu matokeo ya dhabihu ya Kristo na ukuu wa Agano Jipya dhidi ya Agano la Kale.

"Huduma bora zaidi" ya Yesu na Agano Jipya ambalo *"limejengwa juu ya ahadi zilizo bora"* inaonesha kwa mara nyingine tena ukuu wa Kristo na kile alichofanya juu ya kila kiumbe au mfumo. Kristo akiwa ndiye ''mpatanishi'' wa Agano Jipya inaakisi kile alichosema Paulo katika **1 Tim 2:5**, *"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu;"* Umuhimu wa Agano Jipya umeoneshwa katika **2 Kor 3:5-6**, ambayo inasema *"Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu. Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya."*

B. Asili ya Agano Jipya (8:7-12)

[7]Maana kama "lile la kwanza" lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili. [8]Maana, awalaumupo, asema Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya; [9]Halitakuwa kama agano lile nililoagana na baba zao, Katika siku ile nilipowashika mikono yao niwatoe katika nchi ya Misri. Kwa sababu hawakudumu katika agano langu, Mimi

nami sikuwajali asema Bwana. [10] ***"Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli Baada ya siku zile, asema Bwana; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika; Nami nitakuwa Mungu kwao, Nao watakuwa watu wangu.*** [11] ***Nao hawatafundishana kila mtu na jirani yake, Na kila mtu na ndugu yake, akisema, 'Mjue Bwana;' Kwa maana wote watanijua, Tangu mdogo wao hata mkubwa wao.*** [12]***Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena"***

Katika **mst. 7**, "agano la kwanza" ni Agano la Kale au Agano la Musa. "La pili" ni Agano Jipya. **Mistari ya 8-12** unanukuu **Yer 31:31-34** (**Yer 38:31-34**, LXX) kama ilivyo. Hii ni nukuu ndefu kuliko yote ya AK katika AJ. **Mstari wa 8-9** unanukuu **Yer 31:31-32**. Wanarudia historia ya wana wa Israeli kukosa uaminifu kwa Mungu, na hivyo kujenga msingi wa ulazima wa Agano Jipya. Umuhimu wa Agano unaelezwa kwenye mstari wa **10-12** (**Yer 31:33-34**). Agano Jipya ni agano la milele ambapo Mungu huandika sheria zake ndani ya mioyo ya watu wake; Watu wa Mungu watamjua Bwana sawa sawa; na Mungu atawasamehe dhambi na hatazikumbuka kamwe (pia tazama **Yer 32:38-40; 50:4-5; Ezek 11:14-20; 36:24-32; 37:15-28**). Kwenye karamu ya Mwisho Yesu alilisema hilo kwa wazi akizindua rasmi Agano Jipya katika damu yake (**Lk 22:20;** tazama **1 Kor 11:25**). "Kutajwa kwa yote mawili msamaha unaotabiriwa na Yeremia (Mat. 26:28; Yer. 31:34) na damu inayohusishwa na uanzishwaji wa agano la asili la Musa (Luka 22:20; Kutoka 24:7) inazidi kupigia mstari kwamba Yesu alielewa kifo chake kama uanzishwaji wa rasmi wa agano jipya" (Williamson 2007: 184). Kwa hakika, "katika mengi ya nukuu za [mwandishi wa Waebrania] kuhusu 'mpya' au 'bora' agano, ni damu ya Yesu inayosisitizwa na mwandishi wetu (10:29, 12:24, 13:20). Anatafsiri maneno ya Yeremia kwa kutumia maneno ya kikuhani na kidhabihu kwa sababu anatazama Agano la Kale kwa misingi hiyo na anaiona kazi ya Kristo kama *uhalisia kile kinachonyooshewa kidole na matukio na unabii."* (Peterson 1979: 77) Agano litimizwa msalabani (**Ebr 9:12-17**). Ilikamilishwa pale Kristo alipofufuka kwa wafu, kisha akapaa mbinguni na kuketi kwenye kitu pamoja na Baba (**Ebr 10:11-18**). Kwa hiyo, "Yeye siyo tu ni mpatanishi wa Agano Jipya la Mungu; yeye ni umwilisho wake'' (Goppelt 1982: 116).

Ingawa katika **mst. 8** (**Yer 31:31**) husema kwamba katika *muundo* wake Agano Jipya ni *"ni kati ya nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda,"* AJ linathibitishwa kuwa kwa hakika lilitimizwa katika Kristo na Kanisa, siyo na mataifa ya kimwili ya Israeli na Yuda. Kwa hiyo, sehemu iliyobali ya kitabu cha **Waebrania 8-10** hutumia Agano Jipya kwa kanisa. Inanukuliwa tena katika **10:15-18** na inatumika "kwetu" [yaani, wakristo, kanisa]. **Ebr 8:6**, **9:15,** na **12:24** yote inaeleza kuwa ni mpatanishi wa Agano Jipya. Ukweli kwamba yeye "ni" (wakati uliopo) mpatanishi inaonesha kwamba Agano Jipya linaendelea sasa. **Ebr 9:12-17** inaeleza kwamba damu ya Yesu inahitimiza na kuthibitisha Agano Jipya. **Ebr 10:9** vile vile husema kwamba *"huliondoa la kwanza ili kuanzisha la pili."* "Pointi hii inaungwa mkono na ukweli kwamba Agano Jipya linaitwa agano la milele. **Isaya 55:3; 61:8; Yer 32:40; 50:5; Ezek 16:60; 37:26**] ambapo usemi 'isiyo na mwisho' haukuwahi kutumika kwa ajili ya Agano la Sinai [la Musa]" (Gentry 2010: 38; see also at 43n.33 ["Hakuna mahali ambapo Agano la Sinai limeitwa 'agano la kudumu"]). Mjadala wote wa **Waebrania 8-10** ni kwamba Agano la Musa, hekalu, ukuhani, sheria, mfumo wote wa utoaji wa sadaka wa wana wa Israeli, vilikuwa "ishara" (Ebr **9:9**), au "nakala" (**Ebr 9:23-24**), au "kivuli" (**Ebr 10:1**; pia tazama **Kol 2:16-17**) za *"agano lililo bora"* ambalo lilizingatia *"ahadi bora"* (**Ebr 8:6**): yaani, uhalisia wa kweli na wa kudumu unapatikana katika Kristo na Agano Jipya.

Paulo pia analitumia Agano Jipya kwa ajili ya Kanisa. Katika **2 Kor 3:5-6** (iliandikwa kwa ukubwa kwa kanisa la mataifa la Korintho) Paulo anasema kwamba *"Mungu . . . ametufanya sisi . . . kuwa watumishi wa agano jipya."* Maelezo yote ya **2 Kor 3** yanatofautisha Agano la Musa na Agano Jipya: (1) Ni tofauti kati ya andiko na Roho (**2 Kor 3:3, 6, 17-18**). (2) Ya kwanza ni huduma y amauti na hukumu; ya pili ni ni uzima, tumaini na uhuru na Roho (**2 Kor 3:6-9, 12, 17**). (3) Ni toafuti kati ya kitu kilichoandikwa kwenye vibao vya mawe na kilichoandikwa kwenye mioyo ya watu (**2 Kor 3:2-3, 7**). (4) Yote yana utukufu, lakini la pili lina utukufu unaozidi sana (**2 Kor 3:7-11, 18**). (5) Ya kwanza linachakaa na kwisha, lakini la pili linadumu milele (**2 Kor 3:7, 11, 13**). (6) La kwanza lina pazia, la pili pazia limeondolewa (**2 Kor 3:13-16, 18**). Matokeo yake, Agano Jipya pekee hutupa sisi ujasiri na kutubadilisha na kutufanye tufanane na Kristo (**2 Kor 3:2-3, 12, 18**). Vile vile, katika **2 Kor 4:3-6** Paulo "Anaita 'agano jipya' injili ya Yesu Kristo (2 Kor. 4:3-6), na jamii ya Wakristo kama wale ambao kwao baraka za agano jipya zimekuwa halisi. (2 Kor. 3:3; cf. Yer. 31:32-33; Ezek. 11:19; 36:26-27). . . . Kwa wazi, mistari hii inafunua huduma ya Roho inayohuisha, inayoweka na yenye utukufu' (2 Kor. 3:8) tukijumuishwa na wahudumu wa Agano Jipya' (2 Kor. 3:6)." (Williamson 2007: 192, 192n.33) Katika **Gal 4:21-31** "Wake za Ibrahimu Hajiri na Sara, wanatafsiriwa kama wawakilishi wa maagano mawili tofauti. Ya kwanza katika haya (ikiwakilishwa na Hajiri) hiyo inawakilishwa Agano la Musa ('kutoka mlima Sinai . . . uliopo Arabia' Gal. 4:24-25 ESV). Agano la pili (linawakilishwa na Sara), likiwa halijaelezwa vema, kwa wazi linahusishwa na Mlima Sayuni na ahadi za agano jipya (Gal. 4:26-27; cf. Isaya 54:1). Kwa hiyo Hajiri anawakilishi agano la kufanywa watumwa (wa sheria), ikilinganishwa na 'Yerusalemu ya sasa' (Gal. 4:25 ESV), wakati Sara anawakilisha agano la uhuru na

ahadi zilizounganishwa na 'Yerusalemu iliyo juu' (Gal. 4:26 ESV)." (Ibid.: 199)

Agano jipya huwabadilisha kutoka ndani kwenda nje. Kwa sababu Agano Jipya inategemea kile alichofanya Yesu kwa ajili yetu, na siyo kile ambacho sisi tunachotakiwa kufanya, inatufanyia sisi kile tusichoweza kufanya wenyewe kwa ajili yetu. Wakati chini ya Agano la Kale tulikuwa na dhamiri chafu, katika Agano Jipya *"damu ya Kristo. . . hutusafisha dhamiri zetu kuondokana na kazi mfu ili tumtumikie Mungu aliye hai"* (**Ebr 9:14**) na *"imewakamilisha kwa nyakati zote wale waliotakaswa"* (**Ebr 10:14**). "Kwa kule kututakasa dhamiri zetu anawaweka wakfu watu wake kwa Mungu katika uhusiano wa utii wa moyoni ulioelezwa na Yeremia (9:4, 10:10, 22). Kwa kushughulikia dhambi ipasavyo Kristo alifanya iwezekane kwa wale walioitwa kupokea uzima wa milele ulioahadiwa (9:15)." (Peterson 1979: 81) Sasa sisi tunaweza kumfikia Mungu pasipo kizuizi na tunaweza kumkaribia kwa ujasiri (**Ebr 4:16**), kwa sababu Kristo *"ameingia kwenye hema iliyo bora na kamili zaidi"* (**Ebr 9:11**), yupo kwenye uwepo wa Mungu mwenyewe (**Ebr 9:24; 10:12**), na *"siku yu hai akituombea always [sisi]"* (**Ebr 7:25**). Kwenye Agano Jipya Mungu anaondoa mioyo yetu ya jiwe na kutupa mioyo ya nyama (tazama **Ebr 10:22,** ambayo inaendana na **Ezek 36:25-26**).

C. Agano la Kale ni kuukuu (8:13)

Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka.

Wakati Kristo anazindua Agano Jipya kwa Damu yake, **Efe 2:15** anataja ile sheria ya Musa (yaani., Agano la Kale) kwa hiyo ikawa "kusitishwa." Vifungu kadhaa katika kitabu cha Waebrania vinaeleza kwamba Agano la Kale na sheria za Musa zote zimesitishwa kutokana na kile alichofanya Kristo. Wayne Jackson anatupa mifano minne:

1. "Sasa kwa kuwa ukamilifu *umeweza* [wakati ambao haujakamilika — ilikuwa ikitenda kazi hapo nyuma] kufikiwa kwa njia ya ukuhani wa Lawi. . . " (Ebr. 7:11).
2. Kiapo ambacho kilimfanya Kristo afanyike kuhani mkuu kilitolewa "baada ya sheria" nayo ni, kabla ya kipindi cha Sheria ya Musa (Ebr. 7:28).
3. "Kama Agano la kwanza [sheria ya Musa] *lilikuwa pasipo* kosa, kusingekuwa na sababu ya kutafuta lignin la pili" (Ebr. 8:7).
4. Agano la kwanza lilikuwa na *"lilikuwa* na sheria zake" (Ebr. 9:1) na kadhalika. Misema hii inaonekana wazi inatazama kipindi cha sheria za Musa kama mfumo uliokwisha kupita— *kutoka kwenye mtazamo wa kiungu."* (Jackson 2002: Pasipo Mgongano)

Kwa upande mwingine, maelezo katika **Ebr 8:13**, *"Aliposema, 'Agano jipya,' alilifanya la kwanza kuwa kuukuu na inayochakaa na iliyo tayari kupotea"* ni wakati uliopo. Kwa nini? Kuna sababu zinawezekana kama mbili kwa maelezo haya:

Kwanza, matumizi ya wakati uliopo, inawezekana inadhihirisha kwamba hekalu na taratibu zake za ibada zilikuwa bado zinatumika wakati kitabu cha Waebrania kimeandikwa. Hii ina maana kwamba kitabu cha Waebrania kiliandikwa kabla yam mwaka wa 70 BK, wakati hekalu limebomolewa. Ingawa tarehe ya uandishi wa kitabu haina uhakika wa kutosha kuna Ushahidi mwingi unaounga mkono kipindi cha kabla ya mwaka wa 70BK (O'Brien 2010: 15-20). **Mstari wa 13** unamaana kwamba ibada za hekaluni "imepitwa na wakati na haina maana na kwa hiyo haitadumu kwa muda mrefu. Kama mwandishi alikuwa ameandika kwenye miaka mapema ya sitini hivi, anaweza kuwa anawaza kuhusu unabii wa Yesu juu ya anguko la Yerusalemu (Marko 13:2). Katika tukio lolote, angekuwa ameandika baada ya kuharibiwa kwa hekalu mwaka 70 BK, asingeweza kujizuia kurejea kwa uwazi uthibitisho wa kihistoria wa hoja zake za kitheolojia." (Hagner 1990: 124) Maelezo ya mwisho ya mstari wa **13** (*"tayari kupotea"*) kwa kiyunani ni *eggus aphanismou.* "Ingawa neno *aphanismos* limetokea hapa tu katika Agano Jipya, imetumika mara nyingi kwenye LXX (56x) kuelezea kuharibiwa kimwili na Israeli (Yer. 12:11; Ezekieli 6:14; Mika. 7:13; Yoeli 2:13), Yerusalemu (Yer. 19:8) na Hekalu (Dn. 9:26; Jdt. 4:12). Haitatumika tena kuonyesha kupotea polepole kama ilivyoelezwa na matamshi ya kiingereza ya Waebrania 8:13 (k.mf. 'tayari kupotea' NASB). Kwa upande mwingine, mara zote tunaona watu kufa na vitu kupotea kutokana na vita ni hukumu ya Mungu. Maelezo ya mwandishi ni kwamba ukuu wa Agano Jipya utatiwa muhuri kuharibiwa kabisa kwa Agano la kale ikiwa ni pamoja na makuhani wake, dhabihu zake na hekalu." (Gleason 2002: 108-09)

Pili, matumizi ya wakati uliopo katika uandishi ni kuthibitisha kwa ujumla, ukweli usiopitwa na wakati. Jackson anaeleza, "Waebrania 3:4 ni mfano mzuri kutoka kwenye waraka huu. 'Kila nyumba ina mjenzi wake.' Wakati uliopo katika uandishi, 'imejengwa,' hairejei moja kwa moja kwenye nyumba fulani iliyojengwa wakati fulani kwa muda ule, badala yake, inaelezea kirahisi ukweli uliotamkwa—ujenzi wa nyumba siku zote huhitaji mjenzi wa nyumba." (Jackson 2002: Ukweli uiopitwa na Wakati) As R. C. H. Lenski anasema kwa muhutasari,

"'karibu na kupotea,' kama maelezo yaliyo katika wakati uliokamilika uliopo, hairejea hivi hivi tu wakati uliopo bali kwa chochote kwamba muda ni kitu kinachofafanua hali ya udhaifu" (Lenski 1966: 272).

D. Matokeo ya dhabihu ya Kristo (9:1—10:18)

Katika eneo hili, unafanyika ulinganisho wa Agano la Kale na Agano Jipya, na Agano Jipya linaonekana lina ukuu kwa kila hali, kwa kuwa ina na misingi yake ni katika hema iliyo bora, asili iliyo bora, na dhabihu iliyo bora.

1. Hema ya kale na mpya zinalinganishwa (**9:1-14**).

[1]Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia. [2]Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya Wonyesho; ndipo palipoitwa, Patakatifu. [3]Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo Patakatifu pa patakatifu, [4]yenye chetezo cha dhahabu, na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; [5]na juu yake makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli kiti cha rehema; basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari za vitu hivi kimoja kimoja.

[6]Basi, vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani huingia katika hema hiyo ya kwanza daima, wakiyatimiza mambo ya ibada. [7]Lakini katika hema hiyo ya pili kuhani mkuu huingia peke yake, mara moja kila mwaka; wala si pasipo damu, atoayo kwa ajili ya nafsi yake na kwa dhambi za kutokujua za hao watu. [8]Roho Mtakatifu akionyesha neno hili, ya kwamba njia ya kupaingia patakatifu ilikuwa haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimama; [9]ambayo ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa, zisizoweza kwa jinsi ya dhambi kumkamilisha mtu aabuduye, [10]kwa kuwa ni sheria za jinsi ya mwili tu, vyakula na vinywaji na kutawadha kwingine kwingine, zilizoamriwa hata wakati wa matengenezo mapya.

[11] Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu, [12]wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. [13]Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili; [14]basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?

Mstari wa 1 unaanza kwa kuongelea juu ya *"sheria za ibada ya kiungu na hema ya kidunia."* Sheria zimeelezwa kwenye **mst. 2-10**. Tangu hapo sheria za Agano la Kale zilianzishwa na Mungu, na Agano jipya pia imeanzishwa na Mungu, Agano jipya halipingani na Agano la Kale, bali ni utimilifu wake. Vern Poythress anaeleza kwa, "Hema ya duniani ni nakala au kivuli cha makazi ya Mungu mbinguni (Waebrania 8:5; 9:24). Ili kuonyesha Mungu yukoje na ni nini kilihitajika ili kushughulikia dhambi. Kwa namna hii inatoa maelezo masiha ni nani na ahusikaje na wokovu wetu? . . . Kivuli siku zote kina hadhi ya chini kuliko uhalisia. Hema ya duniani imetengenezwa kwa vitu vya duniani, na kamwe haitafanana na uzuri au utakatifu wa Mungu uliopo Mbinguni. Dhabihu za kidunia za ng'ombe na mbuzi haziwezi kuwa sawa na damu ya Yesu iliyotusafisha na dhambi milele. . . . . Kwa hakika, hema ilikuwa kivuli cha ukweli kwamba Kristo Yesu angeuvaa mwili na kuishi kati yetu. 'Neno lilifanyika mwili na akakaa nasi kwa muda [alifanywa hema] [Yoh 1:14]. . . . [Kuhusu Jengo la Sulemani, hekalu la kudumu lililopo Yerusalemu] Sulemani alionyesha kivuli cha nini? Kwa nini, Kwa kweli ni kazi ya Yesu. Sulemani alikuwa mwana wa ukoo wa Daudi, huo mlolongo ulienda hadi kwa Masiha. Alijenga mahali pa Mungu kukaa, akimwashiria Kristo atakayejenga kanisa lake. (Mat 16:18) na yeye mwenyewe akiwa ndiye jiwe kuu la pembeni (Ef 2:20) au msingi (1 Kor 3:11). Kristo hajengi katika mlima Sayuni wa kidunia bali katika kao la mbinguni: 'Bali ninyi [Wakristo] mmeufikia mlima Sayuni, Yerusalemu ya Mbinguni, mji wa Mungu aliye hai' (Waebrania 12:22)." (Poythress 1991: 12-14)

Ingawa **mst. 4**, unaonekana ukionesha kwamba *"madhabahu ya dhahabu ya uvumba"* ilikuwa nyuma ya pazia mahali Patakatifu , kwa kweli ilikuwa halisi Mahali Patakatifu, na ipo nje tu ya patakatifu pa Patakatifu. Hii ilikuwa muhimu kwa sababu ilikuwa ikitumiwa na makuhani kila siku, ambao hawakuwa na ruhusa ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu (tazama **Kut 30:6-8**). Lugha iliyotumika katika **mst. 4** labda inaakisi ukaribu uliopo kati ya madhabahu na Patakatifu pa Patakatifu (tazama **1 Fal 6:22**). Hilo limeoneshwa na ukweli kwamba **mst. 4**

unaongelea Patakatifu pa Patakatifu pakiwa na madhabahu, pamoja na hayo madhabahu yallikuwa "ndani" ya Patakatifu pa Patakatifu. Ukaribu wa Patakatifu pa Patakatifu na madhabahu unaoneshwa na ukweli kwamba katika siku ya Upatanisho, kuhani mkuu alipaswa kutoa uvumba, akitumia kaa la moto kutoka kwenya madhabahu (**Law 16:12-13**).

Katika **mst. 5**, "kiti cha rehema" kilikuwa kifuniko cha sanduku la Agano kwenye hema na hekalu. Neno lililotafsiriwa "kiti cha rehema" ni *hilastērion,* lenye maana patanisha au lipia. "Upatanisho" naonyesha tulikuwa chini ya hasira ya Mungu lakini sasa hasira imetulizwa. Hili ni neno sahihi kwa kiti cha rehema, kwa sababu Siku ya Upatanisho, kuhani Mkuu ya dume wa ng'ombe mdogo (kwa ajili dhambi za kuhani mkuu) na mbuzi wa sadaka (kwa dhambi za watu) kwenye kiti cha rehema kwa ajili upatanisho kwa ajili ya dhambi (tazama **mst. 7**). **Rum 3:25** anaita dhabihu ya Yesu msalabani *"upatanisho."* Neno lililotumika pale linalomaanisha "upatanisho" vile vile ni *hilastērion.* Hii inaonesha, kama Poythress anavyoeleza hapo juu, kwamba hema/hekalu, na sehemu zake zote, ilikuwa na "kiwakilishi" au "kivuli" cha uhalisia wa mbinguni na Agano Jipya, kwa umahususi kwamba Kristo ni kiti cha rehema cha kweli.

Katika mstari wa **6**, mwelekeo unahama kwenye taratibu za ibada zinazofanyika kwenye hekalu/hema, tofauti na vilivyomo ndani ya hekalu/hema yenyewe. Maudhui ya **mst. 6-10** ni kwamba ibada za Agano la Kale zilikuwa zinafanywa kwa nje na ilikuwa ni mifano tu na hazikuwa katika uhalisia wa kwenye na wenye matokeo. Ukweli halisi wa upatanisho wenye matokeo ulikuja kupitia Yesu Kristo na Agano Jipya tu (**mst. 11-14**). Hatimaye, Agano la Kale ambalo si la kudumu na, ambalo halina matokeo linalinganishwa na upatanisho wa Yesu ambao ni wa kudumu na wenye matokeo. Kwa hiyo, mstari wa 9-10 unasema *"sadaka na dhabihu . . . zilihusu chakula na vinywaji na kunawa kwingi, sheria zilizowekwa za kimwili hadi wakati wa matengenezo.''* Kwamba *"wakati wa matengenezo"* ulianza kwa Yesu Kristo kuja. **Mstari wa 12** unalinganisha*"damu za mbuzi na ng'ombe"* na *"damu yake"* Kristo. Zaidi ya hayo, Agano la Kale ambalo linahusika na mambo ya mwilini na hivyo lisilo na uwezo wa kuleta matokeo limeelezwa kwenye mstari wa 9, unaoeleza kuwa Agano la Kale, *"sadaka na dhabihu zake . . . haziwezi kukamilisha dhamiri ya mtu aabuduye."* **Mstari wa 14** inalinganisha hii na matokeo ya ndani ambayo Kristo ameyaleta, kwa kusema *"basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu."* Huo mstari unaongeza kwamba kile kilichokuja kabla ya Kristo hatimaye kilikuwa hakijaleta matokeo, kwa sababu yote yaliyokuja kabla ya Kristo vileleta*"kazi zilizokufa."* Kilele na matokeo ya kile alichofanya Kristo imeoneshwa kwenye tofauti kati ya kuhani wa Agano la Kale ambao *"huingia mara kwa mara kwenye hema ya nje wakifanya ibada"* (**mst. 6**) na Yesu Kristo ambaye *"aliingia mara moja kwa ajili ya wote, akiwa ametupatia ukombozo wa milele''* (**mst. 12**).

Kwa umuhimu, **Waebrania** kamwe hakijaelezea kamwe juu ya "hekalu" bali kuhusu "hema" John Walker anaeleza ni kwa nini: "Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania, ingawa hakutaka kusema kuhusu hekalu lililokuwa likitumiwa wakati huo, bali akielezea mambo ya msingi zaidi kuhusu umuhimu hasa wa hekalu. Kwa kujielekeza kwenye 'hema' la jangwani, alikuwa anaweza kutuhakikishia kwamba mfumo wa ibada wa kwenye hema, hata ulipozingatiwa kwa utimilifu na katika usafi chini ya Musa (kabla ya dhambi ya mwanadamu kubadili nia ya kiungu), umetangazwa na Mungu kuwa haufai kwa njia ya Yesu. Maelezo yake kuhusu hekalu la sasa hayakuwa yanahusu mambo ya kisiasa au kutoridhika kibinafsi, bali yalihusu makusudi ya Mungu ya milele." (Walker 1996: 207-8) Yesu ni uhalisi wa kiroho wa mwisho. Mfumo wote wa hema/hekalu la hauna thamani tena. Kwa hiyo, **Ebr 9:11** inasema kwamba Kristo *"aliingia kwenye hema bora na iliyo kamilifu, isiyofanywa kwa mikono, hii ni kusema, siyo ya uumbaji huu."* **Ebr 9:12** inaongeza kwamba aliingia mahali Patakatifu *"kwa njia ya damu yake."* *"Hema"* ya kweli, ya mbinguni inalinganishwa na Yesu mwenywe (yaani, kwa *"damu yake"*).

2. <u>Asili ya AK na AJ inalinganishwa (**9:15-22**).</u>

[15]Na kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele. [16]Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. [17]Kwa maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya. [18]Kwa hiyo hata lile la kwanza halikuanzwa pasipo damu. [19]Maana kila amri ilipokwisha kunenwa na Musa kwa hao watu wote, kama ilivyoamuru sheria, aliitwaa damu ya ndama na ya mbuzi, pamoja na maji na sufu nyekundu na hisopo, akakinyunyizia kitabu chenyewe, na watu wote, [20]akisema, ''Hii ni damu ya agano mliloamriwa na Mungu.'' [21]Na ile hema nayo na vyombo vyote vya ibada alivinyunyizia damu vivyo hivyo. [22]Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.

Msemo *"Kwa sababu hii"* inayoanza katika **mst. 15** inaonesha kwamba sehemu hii ni mwendelezo na inategemea kile kilichosema hivi punde kuhusu Agano la Kale na Agano Jipya kwenye sehemu iliyopita.

Kimahususi inaanzia kwenye reja ya *"damu ya Kristo"* **mst. 14**. Hii sehemu inaelezea kwa upana umuhimu wa damu kama kitu cha lazima katika kuweka agano na la lazima ili msamaha upatikane. Damu ya Kristo ina thamani kuu kupita maelezo kuliko *"damu ya ng'ombe na ya mbuzi"* (**mst. 19**). Kristo kwa kumwaga damu yake anapata uhalali wa kuwa *"mpatanishi wa agano jipya"* (**mst. 15**), unatuhakikishia ukombozi wetu (**mst. 5**) na msamaha (**mst. 22**), na unatuhakikishia ya kwamba tuta *"tutapokea ahadi ya urithi wa milele"* (**mst. 15**). Mstari wa **16**, ingawa neno "agano" limetumika, maana inaonekana ni ile "urithi," kwa kuwa urithi unafanya kazi pale anapokuwa amekufa yule anayerithiwa. **Mstari wa 20** unanukuu **Kutoka 24:8** Kusisitiza kwamba maagano yanaanzishwa kwa njia ya kumwaga damu ya dhabihu. Hilo limeelezwa wazi katika **mst. 21-22**.

3. Dhabihu za Agano la Kale na Agano Jipya zinalinganishwa (**9:23—10:18**).

[23] Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo. [24]Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu; [25]wala si kwamba ajitoe mara nyingi, kama vile kuhani mkuu aingiavyo katika patakatifu kila mwaka kwa damu isiyo yake; [26]kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake. [27]Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; [28]kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.

10 [1]Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. [2]Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? [3]Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. [4]Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi. [5]Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema, "Dhabihu na toleo hukutaka, Lakini mwili uliniwekea tayari; [6]Sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi hukupendezwa nazo; [7] "Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu."

[8]Hapo juu asemapo, "Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa na hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo" (zitolewazo kama ilivyoamuru torati), 9ndipo aliposema, "Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako." Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili. [10]Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.

[11]Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. [12]Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; [13]tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake. [14]Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa. [15]Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema, [16] "Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, Na katika nia zao nitaziandika; ndipo anenapo," [17] "Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa." [18]Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapana toleo tena kwa ajili ya dhambi.

Kuna maswali hapa kuhusu *"vitu vya mbinguni vyenyewe"* vina maana gani hasa katika **mst. 9:23**. Vitu vya mbinguni vinaweza kuwa ni vitu vya mbinguni ambavyo mfano wake upo kwenye madhabahu ya duniani au watu wa Kristo wanaosemekana wapo mbinguni (**Efu 2:6; Ufu 20:4**) na ambao *"wenyeji wao upo mbinguni"* (**Flp 3:20**). Wengine wanasema kwamba kinachoelezwa kinarejea *"majeshi ya uovu katika ulimwengu wa roho"* (**Efe 6:12**; pia tazama **Kol 1:20; 2:15**). Kwa tukio lolote, rejea ya *"vitu vya mbinguni vyenyewe"* na sehemu hii yote inaelezea kwamba Agano la Kale na dhabihu zake zilikuwa za muda tu na na 'nakala'' zisizo kamili (**9:23**) na "kivuli" (**10:1**) cha the permanent and eternally effective *"dhabihu moja ya dhambi kwa nyakati zote"* inayodumu na inayotenda kazi milele (**10:11**) ambayo Kristo aliitoa. Kwa hiyo, Kristo hakuingia kwenye nakala ya kitu halisi bali aliingia mbingu yenyewe (**9:24**). Sasa yeye daima yupo kwenye *"uwepo wa Mungu kwa ajili yetu"* (**9:24**). Hahitaji kutoa dhabihu kwa kurudiarudia kama katika Agano la Kale, *"lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake."* (**9:26**). Dhabihu yake *"Aondoa la kwanza, [Agano nah ema] ili kusudi alisimamishe la pili. [Agano na hema ya kweli]"* (**10:9**). Hii inamaana kwamba Agano la Kale limezidiwa na kuondolewa na kile alichofanya Yesu alipoasisi Agano Jipya. Wakati

dhabihu za Agano la Kale hazikuweza kuondoa dhambi au kumkamilisha au kuwatakasa watu, dhabihu ya Kristo mwenyewe imefanya yote hayo (**10:11-18**).

Hii sehemu inaonyesha kwamba alichofanya Kristo kinazidi na ni kutimizwa kilichokuwa kinaashiriwa na siku takatifu sana ya Mwaka kwa Waisraeli—Siku ya Upatanisho.[27] Kwanza, Dhabihu za AK zilitolewa kwenye hema ya duniani; Kristo aliingia Mbingu yenyewe (**9:23-24**). Pili, **Law 16–17** inakazia umuhimu wa damu ya dhabihu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi. Kumwagika kwa damu ya mnyama wa dhabihu ilikuwa ni lazima ili kupata damu aliyoihitaji ili kuipeleka Patakatifu pa Pakatifu na kuinyunyiza kwenye kiti cha rehema. **Waebrania 7–10** inaonyesha kwamba dhabihu ya Kristo akiwa msalabani ndicho kilichokuwa kinaashiriwa siku zote na ile Siku ya Upatanisho. Damu ya Kristo ilizidi pasipo kipimo thamani ya damu za wanyama. (**10:4-10**). Tatu, ibada ya AK, kwa kutumia damu ya mnyama, ilikuwa ni lazima iwe inarudiwa pasipo mwisho (**Ebr 10:1–4**); Dhabihu ya Kristo ilihusisha damu yake na hufanyika mara moja (**Ebr 7:27; 9:25–26; 10:5-14**). Zaidi ya hayo, damu yake ni "ina tofauti kubwa sana ukilinganisha na chochote cha kimwili au cha muda tu ([Ebr] 9:12). Kazi ya damu yaani kukomboa na kutakasa ni tendo la ndani na la milele na siyo kwa nje na isiyodumu ([Ebr 9:12–14; cf. 10:1–4)." (Nelson 2003: 256)

Kipengele cha muhimunkwenye siku ya Upatanisho nit endo la kuhani mkuu kuingia kwenye uwepo wa Mungu mahali Patakatifu pa Patakatifu, nyuma ya hema, akitumia damu aya dhabihu kwenye kiti cha rehema ili kuvitakasa vitu vitakatifu na taifa kutokana na uchafu na dhambi (**Law 16:2–19**). Kinyume chake, kwa njia ya ufufuo wake na kupaa Kristo aliingia *"mbingu yenyewe"* (**Ebr 9:24**; pia tazama **Ebr 4:14; 8:1–2**), ndani ya *"sehemu ya ndani nyuma ya pazia"* (**Ebr 6:19–20**, RSV). Kwa hiyo, Kristo anatenda yote mawili, kama muhanga na kama kuhani mkuu: kama muhanga damu yake ilikuwa safi kwani aliishi Maisha pasipo kutenda dhambi (**Ebr 9:12–14; 10:4–10**); kama kuhani mkuu pia aliye mkamilifu kwa sababu hakuhitaji kujipatanisha mwenyewe. (**Ebr 7:26–27; 9:7**). Kuhani mkuu alinyunyuzi damu Patakatifu pa Patakatifu nyuma ya hema; Yesu mbele ya macho ya watu, na hata wakati wa Kifo chake *"pazia la hekalu lilipasuka mara mbili kutoka juu hadi chini"* (**Mt 27:51**). Hizi kweli mbili zinaonyesha kwamba Yesu amekamilisha upatanisho kwa ajili ya dhambi kwa kila mmoja aliye na imani katika yeye, badala ya kufunika dhambi za taifa kwa mwaka mmoja tu. Kwa nyongeza wakati mst. 24 unasema Kristo aliingia *"kwenye mbingu yenyewe, ili aweze kuwa kwenye uwepo wa Mungu kwa ajili yetu,''* inatuonyesha kwamba kile alichofanya Kristo kinazidi sana chochote ambacho kuhani mkuu wa AJ anaweza kufanya au ambacho ukuhani wote wa AK ungeweza kufanya. Kuhani angeweza kuingia Patakatifu pa Patakatifu siku moja kwa mwaka. Sasa Kristo na milele yote yupo kwenye mbingu yenyewe, katika uwepo halisi wa Mungu (siyo ''nakala'' tu), na yupo pale akitenda "*kwa ajili yetu."* Hatungeweza kupata hakikisho kuu na wakili kuliko huyu.

Katika sura ya **9:26**, inasema ile dhabihu moja ya Kristo imesababisha, it says that Christ's one sacrifice has occurred *"ukamilifu wa nyakati."* Ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza na kile alichofanya kinaanzisha nyakati mpya katika historia ya mwanadamu. Katika AJ lote, waandishi husema kuhusu *"nyakati mbili": "nyakati hizi/kizazi hiki," na "nyakati zijazo/kizazi kijacho"* "Nyakati hizi/kizazi hiki" sifa zake kuona na mambo ya kupita (k.mf., **Mk 10:30; Lk 20:34; Rum 12:2**), evil (**Gal 1:4; Ef 2:2**), na hekima ya kidunia (**1 Kor 1:20; 2:6-8**). Kwa upande mwingine, "wakati ujao/nyakati zijazo" sifa yake ni ufufuo na kutokufa (k.mf., **Mk 10:30; 1 Kor 15:50**), hakuna kuoa wala kuolewa (**Lk 20:35**), na hakuna uovu (**1 Kor 6:9-10; Gal 5:21; Efe 5:5**) (Riddlebarger 2003: 82-83). Nyakati hizi mbili zinahusiana na uanzishwaji na ukamilishaji wa Ufalme wa Masiha. Ingawa Ufalme wa Mungu ujao unatazamiwa baadaye na unamsubiri Kristo atakapokuja katika utukufu wake, Ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza ulianzisha huo huo ufalme wa Mungu unaokuja. Hii inajulikana kama "nyakati za masiha zilizotayari na bado" (Yarbrough 1996: 65): yaani ufalme wa Mungu na utawala wa Kristo umeanza na

[27] Siku ya Upatanisho ni kielelezo cha kifo cha Kristo na msalaba. Shughuli kuu za ibada ya Upatanisho inayofanyika Siku ya Upatanisho ni kielelezo kinachotuelekeza kwa Kristo: hayo yote yalifanyika ndani ya hekalu (**Law 16:23, 20, 33**)—Kristo ni hekalu la kweli (**Yoh 1:14; 2:18-22**); kuhani mkuu ndiye aliyeendesha hizo shughuli (**Law 16:2-3, 32-33**)—Kristo ni kuhani wetu mkuu (**Ebr 4:14-15; 5:5-10; 8:1-6; 9:11; 10:21**); ng'ombe dume, na mbuzi walitolewa kama dhabihu na damu zao zilimwagwa (**Law 16:8-9, 15**)—Kristo alijitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zrtu na damu yake ilimwagwa (**Ebr 7:27; 9:12, 14, 26, 28**); kuhani aliingia patakatifu pa patakatifu nyuma ya pazia (**Law 16:12-15**)—Mwili wa Kristo ulikuwa kama pazia ya kweli (**Ebr 10:19-20**) naye aliingia patakatifu pa patakatifu pa kweli (**Ebr 8:1-2; 9:11-12, 24**); damu ya mbuzi ilinyunyizwa kwenye kiti cha rehema (**Law 16:14-15**)—Kristo ni kiti cha rehema (**Rum 3:25**, cp. **Kut 25:17** LXX); dhambi ya taifa ziliwekwa juu ya mbuzi wa azezali (**Law 16:20-21**)—Kristo alichukua dhambi zetu (**Isa 53:4-5; Ebr 9:28; 1 Pet 2:24**) na kuwa dhambi kwa ajili yetu (**2 Kor 5:21**); mbuzi wa azazeli alifukuzwa jangwani (**Lawi 16:21-22**)—Kristo aliongozwa na Roho kwenda kwenye jangwa la kutengwa mbali na Mungu (**Isa 53:8; Mt 27:46**); miili ya Wanyama wa dhabihu ilichomwa nje ya kambi (**Ebr 13:11**; tazama Edersheim 1988: 324)—"*Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango."* (**Ebr 13:12**).

kutambuliwa kikanuni, na kwamba upo sasa hivi (ufalme ulio "tayari"); hata hivyo, ufalme huo haujadhihirishwa kwa ukamilifu bado, bali unangoja ukamilifu wake katika utukufu wake wote (ufalme ulio "ambao bado"). Kuja kwa Yesu mara ya kwanza ulianzisha nyakati za Masiha—nyakati zijazo—katika Kristo na kati ya wale walio wake. Matokeo yake, nyakati mbili sasa zote zipo kwa pamoja. Kwa kuwa utawala wa Kristo umeshaanza tayari (**Ebr 2:9; Efe 1:21**), kwa namna Fulani nyakati zijazo nazo pia zimeanza. Kwa kuwa nyakati hizi ni nyakati za uumbaji ule wa kale, na nyakati zijazo ni nyakati za uumbaji mpya, umeshazinduliwa/umeanzishwa (**2 Kor. 5:17; Gal 6:15).** "Nyakati hizi" zitafika mwisho na "nyakati zijazo" zitakuwa katika katika utimilifu wa utukufu wake Kristo atakaporudi mara ya pili (**Ebr 9:28**; ona **Mt 24:3; Tito 2:12-13**). Athari ya kihistoria ya ujio wa Yesu wa mara ya kwanza katika kubali nyakati unathibitishwa na ukweli kwamba kuja kwake kwa mara ya kwanza ni mwanzo wa *"siku za mwisho"* ambazo tupo ndani yak e sasa na ambazo zitaendelea hadi atakaporudi (tazama **Mdo 2:16-17; Ebr 1:2; Yak 5:1-3; 1 Pet 1:20; 1 Yoh 2:18**).

Kwa mujibu wa kuja kwake Kristo mara ya pili, **9:28** inasema kwamba wakati Kristo alipokuaja mara ya kwanza *"kuchukua dhambi za wengi,"* ata *"onekana mara ya pili kwa wokovu ambao si kwa habari ya dhambi."* Kwa maneno mengine, alishughulika na dhambi kikamilifu katika ujio wake wa kwanza. Hana cha ziada anatakiwa kufanya kwa habari ya dhambi. Atakarudi, atakuja na ''wokovu.'' Bila shaka, kuna namna ambayo katika hiyo ameshaleta wokovu kwa wale waliomwamini na kutubu, kama matokeo ya ujio wake wa kwanza. Hata hivyo, wokovu utakuwa katika ukamilifu wake atakapokuja mara ya pili, kama vile ambavyo nyakati zijazo zitakamilika katika ujio wa mara ya pili. Ndio wakati ambao tutapokea miili yetu mipya yenye utukufu (**1 Kor 15:52-54**); "mbingu mpya na nchi mpaya" tutasimikwa rasmi (**Ufu 21:1-2**), Mungu atakaa pamoja na watu wake (**Ufu 21:3**), tutamwona kama alivyo (**1 Yoh 3:2; Ufu 22:4),** na *"hakutakuwa na mauti kamwe; hakutakuwa na maombolezo kamwe, wala kilio, wala maumivu"* wala laana (**Ufu 21:4; 22:3**).

Ebr 10:1-4 inakazia upungufu wa ibada ya upatanisho wa AK. **Ebr 10:3**, husema kwamba *"katika dhabihu hizo kuna kumbukumbu ya dhambi mwaka kwa mwaka"* na kwa hiyo inaweka wazi upungufu huo. **Ebr 10:5-9** inanukuu kutoka **Zab 40:6-8a** (**Zab 39:7-9a**, LXX). Zaburi "inawakilisha hali ya utii na nia ya dhati ya kufa msalabani, aliyokumbatia Kristo katika kufanyika kwake mwili. Kutimia huku, zaidi ya hayo, unatakiwa uonekane kama kutimia kwa unabii wa kitaipolojia usio wa moja kwa moja, uzoefu wa Mfalme Daudi [mwandishi wa Zaburi] unaeleweka kama uzoefu unaotupa picha ya uzoefu wa Kristo." (Guthrie 2007: 977) Matumizi ya Zaburi inasisitiza kutoendelea kwa Agano la Kati pamoja na Agano Jipya, upungufu wa dhabihu za AK, na namna Kristo alivyojitoa kikamilifu yeye mwenyewe katika kutimiza mapenzi ya Baba, hivyo akifanya kwa ukamilifu wajibu wake kama kuhani mkuu na ule wa kuwa dhabihu. **Ebr 10:12-13** inanukuu kutoka **Zab 110:1**. Kristo kuketi mkono wa Mungu (**10:12**) inaonyesho hitimisho la dhabihu ya upatanisho na ukweli kwamba haihitaji kurudiwa, kuketi *"mkono wa kuume wa Mungu"* ni mahali pa heshima kuu. Wakati Yesu alipodai mahali hapo kwa ajili yake mwenyewe akiwa barazani mbele ya kuhani mkuu, kuhani mkuu akararua joho lake la kikuhani, kwa sababu alisema hii ni kufuru, yaani, Yesu alikuwa anadai kuwa yeye ni Mungu (**Mk 14:62-64**). Craig Blomberg anaelezea jambo hili, "Kujidai au kujiita masihi halikuwa kosa kubwa; vinginevyo, basi Wayahudi wasingeweza kamwe kumpokea masihi! Lakini kuwa umetukuka, Mwana wa Mtu wa kimbingu, yeye ambaye ni Bwana aliyeketi karibu kabisa na Mungu mbinguni, kulivuka mipaka ya kile ambacho viongozi wengi wa kiyahudi wangeona kinaruhusiwa kwa wanadamu wa kawaida wanaokufa." (Blomberg 2007: 93)

Sasa, Kristo yupo enzini, mkono wa kuume wa Mungu *"mpaka adui zake wawekwe chini ya miguu yake"* (**Zab 110:1; Ebr 10:13**). Kristo ameinuliwa na anatawala kutoka mbinguni sasa katika ule ufalme "ulio tayari". Kulingana na **Zab 110:1**, Kristo ataendelea kutawala *mpaka* adui zake watakapowekwa chini yake. Ni katika *parousia* (Kuja kwa Kristo mara ya pili) tunadhihirishiwa ukamilifu wa ushindi wa mwisho wa Kristo (yaani., inatufikisha kwenye ukamilifu au mwisho wa sehemu ya ufalme wa milele—ule "ulio bado,"). Nukuu katika **Zab 8:6** (*"Ameviweka vitu vyote chini ya miguu yake"*) ikatika **1 Kor 15:27** vile vile inaonyesha kwamba Kristo "utawala wake" ni kitu kilichopo sasa. Kitenzi "ameweka" (*hupotasso*) katika ile sentensi inaonyesha ipo katika wakati uliopita (kilichofanyika tayari) wakati (*hupetaksen*). Waldron anatoa maoni, "Taswira isiyoweza kuepukika ambayo mtu hubaki nayo ni kwamba Paulo alihisi kuwa mwanzo wa utawala wa ushindi wa Kristo ulikuwa jambo la kihistoria la zamani. "Kwa hakika namna Paulo anavyoleta nukuu hii ni ya kupotosha ikiwa hii siyo maana inayokusudiwa." (Waldron 2000: sec. II.B.2; pia tazama **Mdo 2:29-36**) George Eldon Ladd anatoa kwa muhutasari asili ya utawala wa Kristo, "Agano Jipya halifanyi utawala wa Kristo kuwa jambo linaloishia kwa Israeli peke yako katika kipindi cha milenia [akinukuu **1 Kor 15:24-26**]. Ni utawala wa kiroho ambao lengo lake ni kuharibu adui zake Kristo wa kiroho, wa mwisho akiwa ni mauti. . . . Ubwana na ufalme ni maneno yanyotumika kwa kubadilishana. . . . Wakati hili litakapofanyika na akiwa ameshaharibu 'kila utawala na kila mamlaka na nguvu,' Yesu aliye Bwana ataukabidhi *ufalme* kwa Mungu Baba (1 Kor. 15:24)." (Ladd 1977: 30) Hii yote ni katika kuhakikisha kuwa Yesu anabaki kuwa mkuu juu ya malaika na wote walio duniani pamoja na vyote, kama ilivyojadiliwa katika sura ya 1 na ya 2.

Ebr 10:9 na **14** inaongelea kuhusu kutakaswa kwetu. **Mstari wa 9** unasema kwamba *"tumetakaswa kwa njia ya dhabihu ya mwili wa Yesu Kristo mara moja kwa ajili ya wote."* **Mstari wa 14** unaongeza, *"Kwa maana kwa dhabihu moja, amewakamilisha kwa nyakati zote wale waliotakaswa."* Kutakaswa ni "kutengwa" na Mungu kwa ajili ya kusudi lake na kubadilishwa na kufanana na Kristo. Msalabani, Kristo alibeba dhambi zetu na adhabu tunayostahili juu yake mwenyewe. Matokeo ya kile alichokifanya, anatupatia pia haki yake na mema anayostahili (**2 Kor 5:21**; Pia tazama **Rum 3:22; 1 Kor 1:30**). Kumbuka, mjadala wetu wa **Ebr 6:4-8**, Utakaso ni mojawapo ya vipengele vya imani ya kweli inayookoa. Unahusisha mchakato wa hatua tatu: (A) immediate positional holiness at salvation, i.e., the imputation of Christ's righteousness to us; Utakatifu mara tu tunaopokea kwa kuwepo ndani ya Kristo katika wokovu, yaani, sisi kuhesabiwa haki ya Kristo (B) kukua katika neema kunakoendela; na (C) Ukamilifu wa baadaye (kutukuzwa) (tazama **Yoh 17:17-19; Mdo 13:39; Rum 8:29-30; 1 Kor 1:2, 30; 1 Thes5:23; Ebr 12:14**). Utakaso ni kazi ya Mungu kwa njia ya Roho, ambao msingi wake ni kile alichofanya Kristo. Sehemu ya pili ya utakaso inahitaji muumini kushiriki kwa vitendo katika kuishi Maisha ya utii na haki.

Mwandishi anahitimisha sehemu hii **10:16-17** kwa kunuu tena kifungu cha Agano la Kale **Yer 31:33-34**. Pamoja na mambo mengine hii inahitimisha sehemu hii yote (**8:6—10:18**) kuhusu ukuu wa Agano Jipya kwa kuwa alianza sehemu hii kwa kunukuu **Yer 31:31-34**. Nukuu katika **10:17** na maelezo yake ya kuhitimisha katika **10:18** husisitiza msamaha wa dhambi na hitimisho la dhabihu ya Kristo, yaani, kwa kuwa *"ni vigumu kwa damu za ng'ombe na mbuzi kuondoa dhambi"* (**10:4**), lakini dhabihu ya Kristo *"dhabihu moja kwa ajili ya dhabi kwa nyakati zote"* (**10:12**) ambayo *"imewakamilisha nyakati zote wale waliotakaswa"* (**10:14**), *"hakuna tena dhabihu kwa ajili ya dhambi"* (**10:18**) hiyo ni ya muhimu au kwamba ingekuwa na matokeo.

MASWALI YA MJADALA

1. Maana yake ni nini tunaposema kwamba Kristo ni "mpatanishi" wa Agano Jipya (8:6)?

2. Waebrania 8-12 hunukuu Yer 31:31-34, ambayo ni nukuu ndefu sana ya AK katika AJ. Kwa nini Yer 31:31-34 ni muhimu sana, na inatuambia nini sisi?

3. Vipengele vikuu vya Agano Jipya ni vipi, n ani kwa namna gani vinatofautiana na Agano la Kale (La Musa)?

- Ni nini ambacho Agano Jipya lilifanya, ambacho Agano la Kale halikufanya na haliwezi kufanya?

4. Agano la Musa, hekalu, ukuhani, sheria, na mfumo wote wa dhabihu za Israeli, ulikuwa ni "ishara" tu (Ebr 9:9), au "nakala" (Ebr 9:23-24), au "kivuli" (Ebr 10:1; pia tazama Kol 2:16-17) ya Agano Jipya; hii ina maana gani?

5. Jadili mfanano na tofauti kati ya dhabihu chini ya Agano la Kale na dhabihu ya Kristo ikiwa inaenda sambamba na Agano Jipya.

6. "Kiti cha rehema" ni nini na pia "upatanisho" ni nini?

7. Kwa namna gani Kristo alitimiza na kuzidi ibada za Waisraeli zinazofanyika katika siku takatifu sana, ambayo ni siku ya Upatanisho?

8. Jadili huhusiano uliopo kati ya "nyakati mbili" (nyakati hizi na nyakati zijazo zijazo) na asili ua ufalme wa Kimasihi "ulio tayari/lakini bado".

9. Ebr 10:12-13 (pia tazama Zab 110:1) unaonesha kwamba Kristo anatawala sasa. Jadili asili ya utawala wake.

10. Nini maana ya "utakaso," na unaohusianaje na kile alichofanya Yesu, na anachofanya, kwa ajili yetu?

IV. Kwa Imani tunafiki Agano Jipya katika Maisha yetu (10:19—13:19)

Mpaka sasa, tumekwisha ona kuhusu ukuu wa Yesu juu kila mmoja na kila kitu ulimwenguni, Kristo ni kuhani wetu mkuu, na msamaha na uzima wa milele ambao Kristo anatupa sisi kupitia Agano Jipya, ambalo yeye alilianzisha kwa njia ya dhabihu yake. Sasa, tunajielekeza kwenye namna ya kaufiki Agano Jipya katika Maisha yetu. Tunafanya hivyo kwa Imani. Sehemu yote hii inaelezea namna ya kuishi kwa Imani na kutupa mifano ya wale waliovumilia wakingojea kutimia kwa ahadi ya Mungu.

A. Kwa kuwa Kristo ni kuhani wetu mkuu ni lazima tuvumilie katika uaminifu (10:19-39)

1. Kwa ajili ya Kristo, tunaweza kuwa na uhakika mkamilifu wa Imani (**10:19-25**).

[19] Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, [20]njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake; [21]na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; [22]na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi. [23]Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu; [24]tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; [25]wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.

Kuna mfuatano kati ya kutiwa moyo katika kushika sana Imani yetu hapa na kutiwa kunakopatikana katika **Ebr 4:14-16**. Mawili hayo msingi wake ni ukuhani mkuu wa Yesu Kristo, lakini maelezo kuhusu jambo hilo umeweka wazi yotr aliyofanya Kristo kwa ajili yetu kama kuhani wetu mkuu. Matokeo yake, tunatiwa moyo kukaribia kwenye alizotupa sisi, kwa ajili yetu na kuwatia moyo ndugu zetu.

Sehemu zilizopita za waraka huu zimetueleza kuhusu Dhabihu ya Kristo na ukuu wa damu yake usio na mfano ikilinganishwa na damu ya dhabihu za Wanyama. Sasa, tumeoneshwa kwamba kukaribia kwa damu yake na dhabihu yake kibinafsi na kwa vitendo. Ni *"njia mpya na iliyo hai"* kwa watu wa Kristo *"kuingia mahali patakatifu"* kwa "ujasiri" na "uhahika mkamilifu." Njia ni mpya na inaishi kwa sababu Yesu ni njia (**Yoh 14:6**). Tofauti na dhabihu za AK za wanyama, Yesu anaishi, ameketi mkono wa kuume wa Baba (**Ebr 10:12**), na anatuombea (**Rum 8:34; Ebr 7:25**). **Mstari wa 20** unaweka wazi kwamba *"njia mpya na yenye uhai" "kuingia mahali patakatifu"* ime *anzishwa kwa ajili yetu kupitia kwenye pazia, ambayo ni mwili."* "Pazia" inaongelea kuhusu pazia kubwa iliyokuwa imetenganisha mahali patakatifu na mahali patakatifu pa patakatifu katika ile hema/hekalu. Kwa kusema pazia kwa hakika anasema kuhusu mwili wa Kristo, **mst. 20** tena, unatuambia kwamba hema/hekalu na vyote vinavyohusika ndani yake vilikuwa ni "ishara" na "vivuli" vikituelekeza kwenye ukweli halisi, ambao ni, Yesu Kristo.

Taipolojia inaenda mbali kuzidi hapo. Taipoloji Kati ya pazia na Kristo inarudi nyuma mpaka kwa Ibrahimu, nyuma sana kabla ya Musa kupatiwa na Mungu mpango ujenzi wa hema. Mungu aliingia Agano la Ibrahimu. Agano la Ibrahimu limeeleza masharti tofauti katika **Mwa 12, 13, 15, 17,** na **22**. Ukiyaweka pamoja, tunaona kwamba kuna ahadi kuu tatu ambazo Mungu alizitoa: (1) ahadi inayohusu "uzao" atakaowazaa; (2) ahadi kuhusu "ardhi"; na (3) ahadi inayohusu kubariki watu wa ulimwengu mzima kupitia uzao wa Ibrahimu. Agano la Ibrahimu linajifunua ndani ya Biblia nzima. Kwa hali zote, Agano la Ibrahimu ni uti wa mgongo wa kitheolojia ya Biblia nzima. Katika **Mwa 15**, Agano lilirasimishwa. Katika **Mwa 15:7** Ibrahimu aliahidiwa ardhi, na katika **Mwa 15:8** Ibrahimu alijibu, *"Ee Bwana Mungu, nitajuaje ikiwa nitamiliki?''* Katika kujibu, Mungu akamwambia Ibrahimu, "*Nilitee mimi ndama wa miaka mitatu, na mbuzi jike wa miaka mitatu, na beruberu wa miaka mitatu, hua na mwana njiwa" Kisha akamletea vyote hivi, na kuvikata vipande viwili, na akweka kila kipande kiangaliane na mwezake yaani nusu hii inaangalie nusu ile; lakini ndege hakuwapasua."* (**Mwa 15:9-10**) Kwa kawaida, katika Mashariki ya Kati hapo kale, hivyo ndivyo ulivyokuwa ukiwekwa. Wanyama mbalimbali wakichinjwa na kukatwa vipande viwili na kisha sehemu zinahusika na Agano wangepita kati ya vipande vya Wanyama waliokufa, kiishara nikisema, "Ikiwa nitavunja hili agano, na niwe kama hawa Wanyama waliokufa"

Kwa habari ya Agano la Ibrahimu, hata hivyo, Mungu peke yake, katika lugha ya ishara, alitemebea kati ya vipande vya Wanyama. Hakumfanya Ibrahimu apite juu ya hivyo vipande. Mungu alikuwa anasema, "Ibrahimu, Mimi nikivunja mashrati ya Agano hili, mimi niwe kama mmoja wa hawa Wanyama waliokufa" Kwa kuwa Mungu alipita mwenyewe kati ya vile vipande, pia alikuwa akipita kwa ajili ya Ibrahimu. Kwa maneno mengine, alikuwa pia akisema, Ibrahimu, wewe ukikiuka masharti ya agano hili, kwa kutokuniamini, au kutonifuata, mimi na ni, siyo wewe, niwe kama wanayama waliokufa." Historia ya Ibrahimu na uzao wake, taifa la Israeli, imeonyesha kuwa, kwa muda mwingi, Maisha yao yalikuwa na sifa ya kukosa uaminifu kwa Mungu. Ingawa alishughulika na laana ya agano yeye mwenyewe wakati alipotembea katikati ya vile vipande vya Wanyama, kama miaka 2000 baadaye, juu ya mlima uitwao Kalvari, katika nafsi ya Yesu Kristo, Mungu alifanya kwa hakika. Kama vile ambavyo Wanyama walikatwa vipande viwili, **Mt 27:51** inatuambia kwamba Yesu alipokuwa amekata roho, *"pazia la hekalu lilipasuka mara mbili kuanzia juu kuelekea chini."* **Ebr 10:19-20** inatueleza maana ya tendo hilo. Inatuambia kwamba *"tunaweza kuingia mahali patakatifu kwa damu ya Yesu, kwa njia mpya na iliyo hai ambayo aliianzisha kwa ajili yetu kupitia kwenye pazia, amabayo ni mwili wake."* Kwa kuwa pazia ilikuwa ni "ishara" inayoonyesha

mwili Yesu, kupasuka kwa pazia wakati Yesu anakata roho pale msalabani, Yesu Kristo alitimiza Agano la Ibrahimu.

Yote aliyoyafanya Yesu ni lazima yatupe ufahamu na kutubadilisha. Matokeo yake, **mst. 22, 23**, na **24** unatutia moyo kwa mambo matatu: *"na tukaribie," "tushikamane,"* and *"na tuangalie."* Tunatiwa moyo, *"kumkaribia"* Mungu *"kwa moyo wa kweli kwa uhakika kamili unaotokana na imani."* Tunaweza kufanya hili na tunaweza kuwa na *"uhakika kamili unaotokana na imani,"* kwa sababu imani yetu, hatimaye haitutegemei sisi; Kristo amefanya kwa ajili yetu kile ambacho sisi wenyewe hatuwezi kufanya. Imani yetu ni karama ya Mungu (**Efe 2:8-9**) na kwa kuwa *"ni Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Flp 2:13**), tumehakikishiwa kwamba imani yetu itavumilia. Tunaweza *"kumkaribia"* kwa *"kwa moyo mweupe,"* kwa sababu Mungu alituhakikishia hilo, kama sehemu ya Agano Jipya, *"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama."* (**Ezek 36:26**). Zaidi ya hayo, **Ebr 10:22** inatukumbusha kwamba *"hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi."* Hiyo inarejea lugha ya Agano Jipya kutoka kwenye **Ezek 36:25**, ambapo Mungu anasema *"Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi."* Pia inarejea kwamba, tofauti na dhabihu ya Agano la Kale, ambayo *"zisizoweza kwa jinsi ya dhambi kumkamilisha mtu aabuduye"* (**Ebr 9:9**), *"basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"* (**Ebr 9:14**) Kwa kifupi, ndani ya Kristo kuna kila tunachohitaji na zaidi.

"Hakikisho kamili la imani" yetu haliishia hapa na sasa. Bali, tunatakiwa Instead, *"kushikilia ungamo la tumaini letu bila kukata tamaa."* Tumaini linahusika na wakati ujao. Tunaweza kushikilia ungamo la tumaini letu pasipo kukata tamaa, kwa sababu *"yeye aliyeahidi ni mwaminifu."* Kwa kuwa imani yetu, tumaini letu hatimaye haitutegemei sisi, bali katika Mungu kwa njia ya Kristo. Hii ina umuhimu mkubwa, kwa sababu inaweka msingi kwa ajili sehemu ya mwisho wa sura ya 10 na mifano ya sura ya 11, yote hayo yanalenga kwenye imani iliyo na uvumilivu ikimngojea Mungu atomize ahadi yake. Wengi katika sura ya 10 walivumilia *"mashindano makubwa ya maumivu, . . . mashutumu na mateso na . . . kupoteza mali"* (**Ebr 10:32-34**). Wengi katika sura ya 11 *"alikufa angali akiamin, pasipo kupokea ahadi"* (**Ebr 11:13**; pia tazama **mst. 39**). Hata hivyo, waliweza *"shikeni tumanini la wito wetu pasipo kukata tamaa,"* tukijua ya kwamba *"yeye aliyeahidi ni mwaminifu."* Walijua ya kuwa wanayo kwa ajili yao wenyewe pia *"urithi bora na unaodumu"* (**Ebr 10:34**). Hatimaye, Mungu atawatetea watu wake. Utetezi huo utadumu milele. Ikilinganishwa na umilele, hakuna ambacho Maisha haya yanaweza kutoa hata yaliyo mabaya zaidi. Kwa hiyo, kwa kulikaribia Neno la Mungu, moyo wetu mpya, akili, Roho, na ndugu zetu katika Kristo, sisi tulio ndani ya Kristo tunaweza *shikeni tumanini la wito wetu pasipo kukata tamaa* Hata sisi tunaweza kushikilia tumaini la wito wetu, siyo kwa kung'ata meno, lakini kwa ujasiri na hata furaha, na *"na zaidi ya kwa vile mwonavyo siku ile inakaribia"* (**Ebr 10:25**).

Hii inatufikisha kwenye kutiwa moyo/himizo kubwa la tatu, ku *"tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri, wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane"* (**Ebr 10:24-25**). Himizo hili/kutiwa moyo huku linatupeleke nje yetu wenyewe na kututazamisha kwa ndugu zetu kaka na dada kati Kristo. Sisi sote tunakutana na nyakati ngumu. Tunahitajiana. Tunahitajiana sisi kwa kwa sisi kwa ajili ya kutiana moyo, kusaidiana, na kuwa vielelezo kwa kila mmoja wetu. Ndio maana Kristo alianzisha kanisa lake—mwili wa Kristo hapa duniani. Huku kutiwa moyo au kuhimizwa aina tatu kazi yake ni kama ufafanuzi **1 Kor 13:13**: *"Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo."* Himizo la kwanza, ku *"kukaribia,"* linalenga imani; himizo la tatu, ku*"kushikilia,"* linalenga tumaini; na himizo la tatu,ku "kutazama/kuangalia," linalenga upendo. Ni kuhimizwa au kutiwa moyo ambako upo kwa ajili ya kuwekwa kwenye matendo. Kutajwa kwa *"matendo mema"* mwishoni mwa **mst. 24** ni kwa ajili ya kutukumbusha kwamba, ingawa hatuwezi kujipatia njia yetu ya kwenda mbinguni kwa njia ya matendo yetu mema, matendo tunayotenda baada ya kumwendea Kristo ni udhihirisho wa nje wa hali yetu ya ndani nay a rohoni. Yanadhihirisha ikiwa imani tunayokiri ni ya kweli au ya uongo. Moja ya sababu ni kwamba, ingawa hatujaokolewa kwa matendo, bali tumeokolewa kwa neema ya Mungu tu kwa njia ya imani, *"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo"* (**Efe 2:10**). Kwa kifupi, imani ya kweli, inayookoa inatufikisha tulipo, lakini haituachi pale tulipo. **Mstari wa 25** inaongeza kitu kinachotukumbusho cha muhimu kwamba hatujaachwa *"kusanyiko letu kwa pamoja."* Ibada ya pamoja ni muhimu. Kwa kweli, kusanyiko rasmi na lisiyo rasmi kati ya wale walio katika Kristo ni muhimu kwa ajili kuleta uwajibikaji, undugu, ujamii, ushirika, na urafiki. Sifa hizo zote, na zaidi ya hizo, ni muhimu ili kutusaidia sisi kutambua kanisa ni zaidi shirika: ni familia. Tunahitaji kufahamu kwamba kwa kila familia nzuri yenye kupendana, wanafamilia wanatunzana wao kwa wao.

2. <u>Kuendelea kutenda dhambi makusudi matokeo ni adhabu kali (**10:26-31**).</u>

[26]Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; [27]bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. [28]Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. [29]Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema? [30]Maana twamjua yeye aliyesema, "Kupatiliza kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa." Na tena, "Bwana atawahukumu watu wake." [31]Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.

Ebr 9:23—10:18 imetujulisha kuwa dhabihu moja ya Yesu Kristo ni njia pekee inayotenda kazi nay a mwisho ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. **Ebr 10:19-25** ikatuonyesha jinsi Kristo alivyo "njia iliyo hai" ya kutufikisha kwa Mungu, kwamba alikuwa mpango wa Mungu tangu zamani, na tena akatuonyesha matokeo ya kile alichofanya Kristo kwa ajili yetu, ambayo ni, tunahimizwa kuwa na imani, tumaini na upendo. Sehemu hii inafanana na **Ebr 6:4-8**, kuhusu waamini wa uongo ambao wanajitenga baada ya kutiwa nuru, kuonja kipawa cha mbinguni, neno la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, na ambao wamekuwa washirika wa Roho Mtakatifu. Kuzidi *"kuendelea kutenda dhambi kwa makusudi"* (**10:26**) ni sawa na "kujtenga" (**6:6**). Hilo linafuata ukweli kwamba, kama tulivyoona katika **10:24**, kwamba matendo yetu ni ishara ya nje ya hali yetu ya kiroho ya ndani. "Kumkanyaga Mwana wa Mungu, kuihesabu damu ya agano kama kitu kisichofaa ambayo kwa hiyo tumetakaswa, na kumdhihaki Roho wa neema'' (**10:29**) ni sawa na "kumsulubisha Mwana wa Mungu kwa nafsi zao na kumdhihaki kwa Dhahiri.'' (**6:6**). Sehemu ile, kama hii hapa, imefuata majadiliano yaliyohusu jinsi Kristo kama kuhani Mkuu, ni chanzo cha wokovu wetu na himizo la kuzidi kukaza mwendo hata kufikia ukomavu (**Ebr 5:1—6:3**).

Hukumu iliyozungumziwa katika mstari wa **27** inatoka kwenye, au ni sehemu ya, kile kilichosemwa katika **mst. 24-25** kuhusu *"kuhimi[zana] mmoja kwa mwingine kupendana na kutenda mema, . . . na kuzidi kutenda hayo kwa kadiri mwonavyo siku ile inakaribia."* Kwa maneno mengine, Kristo anarudi tena, na hukumu atakayofanya itakuwa ni wakati wa thawabu kwa walio waaminifu, bali moto mkuu kwa walisio waaminifu. **Mstari wa 27** unaendana na **Isa 26:11**. **Mstari wa 28-29** mabishano "kati ya mkubwa na mdogo." Inarejea kwenye **Kum 17:2-7** na **Kum 13:8**. Zinaonyesha matokeo ya kile kilichojadiliwa tayari, kwamba Kristo ni mkuu kuliko Musa (**Ebr 3:1-6**) na Agano Jipya ni kuu kuliko AK kwa sababu ya dhabihu ya Kristo (**Ebr 8:6—10:18**). **Mstari wa 30** hunukuu **Kum 32:35-36**. Kwa kuwa dhabihu ya Kristo imeshinda dhabihu zingine zote, kujitenga naye hakumwachia mtu tumaini lingine la kupata msamaha bali uhakika wa kuhukumiwa.

3. <u>Kuvumilia katika imani kutasababisha thawabu kubwa (**10:32-39**).</u>

[32]Lakini zikumbukeni siku za kwanza, ambazo, mlipokwisha kutiwa nuru, mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu; [33]pindi mlipotwezwa kwa mashutumu na dhiki, na pindi mliposhirikiana na wale waliotendewa hayo. [34]Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo. [35]Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. [36]Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. [37]Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. [38]Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye. [39]Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.

Neno "Lakini" linaanza katika sehemu hii inaonesha kutofautiana na sehemu iliyotangulia, kama ilivyo kweli kwenye tofauti kati ya **6:9-18** na **6:4-8**. Neno linalotafsiriwa "mashindano" katika **mst. 32** kwa kweli ni *athlēsis,* kutokana na neno hilo tunapata "riadha." Inaonesha mashindano au mazoezi na ''humaanisha tendo la kutana na hali ngumu inayolazimu kupambana na ktumia nguvu'' (Zodhiates 1993, *athlēsis,* 90). Msemo huu *"kushindana na mateso"* inatuambia kwamba, ingawa hawa waamini walitiwa nuru kwa nuru waliyopewa na Mungu, hawakuwa wameepusha na mateso waliyosababishiwa na mtu mwingine. Hayo mateso yanaelezwa kwenye **mst. 33-34.** Hayo mateso ni pamoja na kutukanwa, majaribu, kupoteza mali, na kushiriki mateso yanayofanana na ya wengine. Kuonyesha upendo kwa wafungwa ni kukumbuka yale aliyosema Yesu katika **Mt 25:36** (*"Nilikuwa kifungoni mkaja kuniona"*). Katika **mst. 34**, usemi kuwa waamini *"tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo."* unatabiri kile kilichosemwa kuhusu Musa katika **11:25-26** kwamba alichagua *"akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na*

watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo."

"Kwa hiyo" (**mst. 35**) unaunganishi himizo la kile kinachotakiwa kifanyike kwa kuvumilia magumu ambayo yametajwa hivi punde. Kwa maneno mengine, "Kwa mwangaza wa kuvumilia kwa uaminifu, kuendelea katika imani na, kwa kufanya hivyo, utapokea thawabu kuu, ambayo imetajwa katika **mst. 35-36**. **Mistari ya 37-38** inahusisha nukuu katika **Isa 26:20** (*"kitambo kidogo sana"*) na **Hab 2:3-4** (*"ajaye atakuja na hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani"*). Nukuu hizi zinalinganisha waaminifu na wasio waaminifu na huweka himizo la kuvumilia na siyo *"kutupa ujasiri wenu''* na si *"kurejea nyuma"* kwa muktadha wa ujio wa Yesu kwa mara ya pili. "Thawabu kuu" (**mst. 35**) na "kupokea kile kilichoahidiwa" (**mst. 36**) itakuwa wakati Kristo atakapokuja mara ya pili. Kwa hiyo, ni lazima kuvumilia na kuendelea kuishi kwa imani, lakini kama anavyoeleza mwandishi, katika ujumla wa mambo yote, uvumilivu huo ni kwa in *"ni wa kitambo kidogo sana"* na*"na hautachukua muda mrefu"* (**mst. 37**). **Mistari ya 38-39** unaeleza kuwa wale*"wanaorudi nyuma"* hawamfurahishi Mung una wanafanya hivyo kwa ajili ya uharibifu wao wenyewe. Kwa maneno, wanajidhihirisha wenyewe kama wale wanaokiri kwa uongo wa sura ya **6:4-8** na watendao dhambi kwa makusudi **10:26-31**. Ulinganifu kati ya waaminifu na wasio waaminifu unaonekana katika muktadha wa **Isa 26:20**, ambao ni ujio wa Bwana kwa ajili ya kuwaadhibu waovu kulingana na muktadha wa **Hab 2:3-4**, ambao unamtaka mwenye haki aishi kwa imani.

B. Asili na vielelezo vya imani ya kweli (11:1-40)

Sehemu imepewa jina la "ukumbi wa imani." Inatoka kwenye maneno ya kuhimiza na kutia yaliyopo kwenye sura ya **10:32-39** yaani kubakia waaminifu na kuto "rudi nyuma." **Ebr 10:38-39** inahitimisha, *"Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu."* Sura ya 11 inaonyesha wale ambao *"wanaishi kwa imani"* na*"wale wenye imani"* huonekanaa jinsi walivyo na hutoa vielelezo vingi cya watu waliobaki katika uaminifu na hawakurudi nyuma, hata kama walipitia kwa uvumilivu mateso makuu na taabu, ingawa hawakuona ile ahadi. Kwa ujumla, sura ina sehemu tano: (1) **mst. 1-3**—maana na maelezo ya asili ya imani ya kweli; (2) **mst. 4-12**—vielelezo kadhaa vya imani ya kweli; (3) **mst. 13-16**—muhutasari wa majadiliano katika **mst. 4-12**; (4) **mst. 17-38**—mifano ya imani ya kweli; (5) **mst. 39-40**—muhutasari kuhusu mjadala uliopo katika **mst. 17-38**.

1. Asili ya imani ya kweli (**11:1-3**).

[1]Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. [2]Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa. [3]Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.

Mistari hii inatoa maana na kuelezea asili ya imani ya kweli. Maana ya imani inatolewa katika mstari wa **1** na kuelezwa kwenye **mst. 2-3**. Katika maelezo ya kimwili, huwa tunafananisha tunachoona na kile tunachojua (tazama **2 Kor 4:18; 5:7**); tunachosikia ndicho tunachoamini (**Rum 10:14**). Kama **mst. 1** unavyotuambia, *"imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana,"* Kwa hiyo, tunatakiwa *"kutembea kwa imani"* (**2 Kor 5:7**). Hata hivyo, kuna uhusiano kati kuona, kusikia, na imani. **Rum 10:17** inasema, *"Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani."* Nuhu alisikia kutoka kwa Mungu na kuchukua hatua kwa imani *"kwa mambo yasiyoonekana"* (**mst. 7**). Mungu alinena na Ibrahimu (**Mwa 12:1**) na akamtokea (**Mwa 15:1**), lakini bado *"Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia"* (**mst. 13**). Musa aliongea na Mungu "uso kwa uso" (**Kut 33:11**), lakini alikuwa bado *"alitarajia thawabu"* (**mst. 26**), ambayo hakuweza kuishi hadi aipate, *"alivumilia, akimwona yule asiyeonekana"* (**mst. 27**). Kwa maneno mengine, ni kule kusikia neno la Bwana, na kuliamini, kunakotuwezesha kutembea kwa imani katika *"hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana."*

Kitabu kiitwacho *Ufafanuzi wa Biblia ya Afrika* kinafafanua kwenye kifungu hiki cha imani, **Waebrania 11,** kwa kuchunguza, "Mwandishi anaanaza kwa kutoa maana ya imani kama uwezo wa kuwa na uhakika wa yale tuyatarajiayo na bayana ya mambo yasiyoonekana. (**11:1**) na baadaye anataja mifano mingi ya AK ya ymambo yaliyowezekana kwa imani (**11:2**)" (Kassa 2006: 1504). Mifano ya imani katika Kitabu cha Waebrania sura ya inaonesha yafuatayo: (Kassa 2006: 1504-5):

(1) Imani huona yale wasiyoyaona wengine (**11:3-4**).
(2) Imani huwezezesha waamini kuwa karibu na Mungu (**11:5-6**).
(3) Imani huwezesha kuona hatari na uharibufu kabla (**11:7**).

(4) Imani huwezesha waamini kumtii Mungu wakati hawajui mwelekeo wao wenyewe (**11:8-10**).
(5) Imani huwezesha waamini kupokea ahadi za Mungu katika hali zisizo na uwezekano (**11:11-12**).
(6) Imani huwezesha waamini kuvumilia hata kama ahadi haitatimia haraka (**11:13-16**).
(7) Imani huwezesha waamini kutoa ahadi dhabihu (**11:17-19**).
(8) Imani huwezesha waamini kutambua na kupita kwenye baraka za Mungu (**11:20-22**).
(9) Imani huwezesha waamini kujitoa muhanga (**11:23**).
(10) Imani huwezesha waamini kukataa anasa za Maisha haya (**11:24-28**).
(11) Imani huwezesha waamini kushida hofu na vikwazo vingine (**11:29-31**).
(12) Imani huwezesha waamini kuvumilia magumu mengine mengi (**11:32-39a**).

2. Mifano mahususi ya imani ya kweli (**11:4-12**).

[4]Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena. [5]Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu. [6]Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. [7]Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.

[8]Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. [9]Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. [10]Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu. [11]Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba; alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu. [12]Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.

Abeli ni mfano wa kwanza wa imani: *"Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena."* (**mst. 4**). Sadaka ya Abeli ni *"kwa Mungu,"* na kwa njia yake yeye *"alishuhudiwa kuwa mwenye haki."* John Cross anaeleza kwanza tofauti ya muhimu ni kwamba sadaka ya Abeli ni ilikuwa ni dhabihu ya damu kwa ajili ya dhambi na ya Kaini haikuwa hivyo, na kuwa **Ebr 9:22** husema kwamba *"pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi"* (Cross 2014: n.p.) Hata hivyo hata kama hiyo ilikuwa ni sababu, ufunguo kwamba sadaka ya Abeli ilitolewa *"kwa imani"*; Ya Kaini haikuwa hivyo. Kwa hiyo, kwa vyovyote, Sadaka ya Kaini itakuwa ilitolewa kwa "matendo," yaani, jaribio la kujiinua yeye mwenyewe na kumrubuni Mungu. Sadaka ya Abeli ilikuwa ni limbuko, kuonyesha anatambua mazao yake yote ya mifugo yanatoka kwa Bwana na kwamba yote ni mali ya Bwana; Sadaka Abeli pia ile sehemu iliyo bora ya mifugo yake (yaani "sehemu iliyonona,") (**Mwa 4:4**). Kwa hiyo, ingawa haikutajwa wazi, Sadaka ya Kaini haikuwa limbuko, ilikuwa tu sehemu ya *"mazao ya nchi"*—Kwa wazi, tofauti na sadaka ya Abeli, sadaka isiyofikiriwa kabisa, iliyotolewa pasipo imani, na kwa nia isiyo njema (**Mwa 4:3**). Hivyo, **1 Yoh 3:12** inaita matendo ya Kaini (kwa kuzingatia muktadha wa sadaka) "maovu" na ya Abeli "ya haki." Sadaka ya Abeli *"kwa imani"* inaonyesha kwamba amekwisha ongea kuhusu asili ya sadaka, na Abeli alitii kile alichosema Mungu, ambapo Kaini hakuwa mtii (Bullinger 1979: 34-35).

Kwa namna ya kushangaza, kisa hili cha Kaini na Habili, kuna mambo ya muhimu kadhaa yanayofanana kati ya Habili na Kristo. Habili alikuwa mchungaji (**Mwa 4:2**); Yesu ni *"mchungaji mwema"* (**Yoh 10:11**). Habili alimtolea Mungu sadaka *"ya malimbuko ya kundi lake na sehemu zilizonona"* (**Mwa 4:4**). Yesu ni *"mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu"* (**Yoh 1:29**); alikuwa *"kama kondoo apelekwaye machinjoni"* (**Isa 53:7**). *"Mungu alimkubali Habili pamoja na dhabihu yake"* (**Mwa 4:4**). Baba alikubali dhabihu ya Yesu kwa kumfufua kutoka kwa wafu, na kumketisha mkono wa kuume wa Baba, na kumfanya yeye Bwana na Kristo (**Mdo 2:22–36; Ebr 10:12**). Kama ilivyokuwa sadaka ya Habili ilikuwa *"Kwa Mungu . . . ambayo kwa hiyo alishihudiwa ya kwamba alikuwa mwenye haki,"* Dhabihu ya Yesu msalabani ilikuwa *"Kwa Mungu"* (**Efe 5:2**), na *"Yule akida alipoona yaliyotukia, alimtukuza Mungu, akisema, 'Hakika yake, mtu huyu alikuwa mwenye haki. [neno la kiyunani ni kwa uhaisia "mwenye haki"]'"* (**Lk 23:47**; pia tazama **Rum 5:18; 2 Kor 5:21**). Habili alikataliwa na ndugu yake (**Mwa 4:8**); Yesu *"alikuja kwa walio wake, na walio wake hawakumpokea"* (**Yoh 1:11**; pia tazama **Isa 53:3; Mt 13:53–58; Mk 6:1–6; Yoh 7:5**). Habili aliuawa kikatili na damu yake ilimwagika (**Mwa 4:8–10**); Yesu aliuawa kikatili na damu yake ilimwagika (**Mt 27:27–54; Lk 22:20; 1 Pet 1:18–19**). Kuhusu Habili, **mst. 4**

unasema kwamba *"kwa imani, ingawa amekufa, angali akinena."* Mungu alimwambia Kaini, *"Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka ardhini"* (**Mwa 4:10**). **Ebr 12:24** inasema kuhusu hili ikiwazungumzia wale waliomwendea *"Yesu, mdhamini wa Agano Jipya, na kwa damu ya kunyunyiza, inenayo mema kuliko damu ya Habili."* Timothy Keller anahitimisha, "Yesu ni Habili bora na wa kweli, ambaye kwa kupitia kifo chake kisicho cha hatia, ana damu ambayo hulia kwa ajili ya uhuru wetu na siyo kwa ajili ya hukumu yetu" (Keller 2015: 77).

Mfano wa pili wa imani ni Heneko, ambaye *"kwa imani . . . alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu"* (**mst. 5**). **Mwa 5:22, 24** inasema kwamba *"Heneko alitembea pamoja na Mungu"* and *",Mungu alimchukua."* Msemo *"Mungu alimchukua"* imerudiwa kwenye **mst. 5**. Watu wengine pengine pekee ambalo wamesemewa hilo *"alitembea pamoja na Mungu"* ni Nuhu (**Mwa 6:9**) na Daudi (**1 Fal 8:25; 2 Nya 6:16**). Henoko pia alitabiri hukumu ya Mungu juu ya watu wasio na Mungu (**Yuda 14-15**). Kwa kuwa Heneko alitabiri, Ni lazima Mungu alimwambia aseme nini. Kwa kweli, Heneko alitabiri *"pia kuhusu watu watu hawa,"* yaani, watu waovu wa kipindi cha Yuda *"walienda njia ya Kaini"* (**Yuda 11**). Kwa maneno mengine, Heneko alitabiri hukumu ijayo. Kwa namna ya kushangaza, Heneko alikuwa Baba wa Methusela ambaye baadaye alikuja kuwa baba wa Nuhu. Methusela maana yake ni "kifo chake kitasababisha,"yaani, hukumu ijayo. Unabii wa Henoko kuhusu ilikuwa kwa ajili ya wakati wake, katika siku za Yuda (maelfu ya miaka baada ya Henoko kutwaliwa), na katika siku zetu. Nukuu ya Yuda kuhusu unabii wa Henoko akitabiri kuhusu wale *"walioenda njia ya Kaini"* anamwunganisha na Habili. Bwana *"aliikubali"* Habili na sadaka yake (**Mwa 4:4**) na, kwa njia hiyo, Habili *"alishuhudiwa kuwa mwenye haki"* (**Ebr 11:4**); Henoko *"alitembea pamoja na Mungu"* (**Mwa 5:22, 24**) na, kwa njia ya uaminifu wake na kutabiri, Henoko *"alishuhudiwa kuwa . . . anampendeza Mungu"* (**Ebr 11:5**). Vilevile, sisi *"tukienenda kwa imani na si kwa kuona''* tutakuwa *"tunampendeza"* (**2 Kor 5:7. 9**). Kwa kuwa *"kwa imani Nuhu alitwaliwa ili asione mauti mauti"* (**mst. 5**), tunatakiwa kuhitimisha kwamba Mungu aliahidi "kumtwaa" Henoko ili kwamba asione mauti, na Henoko aliamini ahadi hiyo, sawa na vile Mungu alivyomwahidi Nuhu kwamba yeye na familia yake wataokoolewa kutoka kwenye gharika wakiwa ndani ya Safina na jinsi Mungu alivyotuahidi sisi hivi Yesu atakaporudi mara ya pili, *"sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana"* (**1 Thes 4:17**). Hatimaye, **mst. 6** unahitimisha kwa kueleza kwamba, kama ilivyokuwa kweli kwa Habili na Heneko, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."* Watu wengi wanachukulia usemi huu *"yeye amwendeaye Mungu ni lazima aamini kwamba yeye yupo"* kama imani ya msingi kwamba Mungu yupo. Kwa upande mwingine, Donald Hartley anaelezea msemo huu kwamba *"yeye yupo"* ni maelezo yenye maana ya kisifa "mwaminifu" au "tumainiwa," yaani, *maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao,"* kama katika **Ebr 3:6; 10:23;** na **11:11** (Hartley 2006: 289-307).[28] Anatambua kwamba **Ebr 11:1** "inatoa maana ya imani ikiwa na neno uhakika na ni bayana kwa ajili mambo yatarajiwayo yasiyoonekana'' (Hartley 2006: 306). Hata hivyo, **11:1** haijibu swali kwa nini tunaweza kuwa na uhakika wa yatarajiwayo na ujasiri kwa vitu visivyoonekana. Tunaweza kuwa na uhakika huo na ujasiri hasa hasa kwa sababu ya uaminifu na tabia ya Mungu ya kwamba ni wa kutegemewa, ambayo ni We can have that assurance and confidence precisely because of the trustworthy, faithful character of God, which is the "dhamira kuu, msingi, na kichocheo cha aina hii ya imani ya wanadamu na uaminifu'' (Hartley 2006: 306). Kimuktadha, kwa hiyo tafsiri ya Hartley ya **mst. 6** itakuwa na maana. Kwa kifupi, imani ya Henoko ilikuwa zaidi ya kuamini kwamba Mungu yupo. Badala yake imani yake ilimpendeza Mungu kwa sababu Henoko *"alitembea pamoja na Mungu."* Imani yake ilikuwa ina "mihimili mitatu ya imani," iliyojadiliwa hapo juu. His faith was akin to the "three axes of faith," discussed earlier.

Mfano au kielelezo cha tatu cha imani ni Nuhu, ambaye *"Kwa imani . . . akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani"* (**mst. 7**). Kama ilivyo kwa habili na kwa Henoko, Mungu alinena na Nuhu, na kwa uaminifu akatenda kile alichoambiwa na Mungu. Kama vile ilivyokuwa sadaka ya Habili *"kwa Mungu"* na *"kwa imani,"* Nuhu aliatengeneza safina *"kwa utii."* Uaminifu wake katika kutengeneza safina *"alihukumu ulimwengu,"* ambayo ni sawa na Henoko kutoa unabii kwamba Bwana anakuja *"kuwahukumu watu wote."* Kama ilivyokuwa kwa Habili *"alishuhudiwa ya kuwa ni mwenye haki"* na Henoko *"alishuhudiwa kabla hajachukuliwa mbinguni ya kuwa alimpendeza Mungu,"* hivyo Nuhu anaitwa *"muhubiri wa haki"* (**2 Pet 2:5**) na*"akawa mrithi wa haki itokanayo na imani''* Neno "muhubiri" ni neno la Kiyunani *kēruka,* yenye maana ya "mtangazaji." Kama E. W. Bullinger anavyosema, Nuhu, kama Heneko, "hakuwa muhubiri wa neema ya Mungu iliyopo sasa, lakini mtangazaji wa hukumu ya Mungu inayokuja''

[28] **Ebr 3:6** inaaza *"bali Kristo alikuwa mwaminifu kama mwana juu ya nyumba yake."* Maneno *"alikuwa mwaminifu"* siyo kwa lugha ya kiyunani lakini yametumika katika **Ebr 10:23** na **11:11**, uaminifu wa Mungu umeelezwa kwa wazi.

(Bullinger 1979: 120). Sehemu moja muhimu ya mahubiri ya Nuhu ni kwamba, kwa yote yanayoonekana kwa nje, mahubiri yake yalikuwa kushindwa. Tofauti na Yona wa Ninawi, hakuna hata moja aliyetubu. Hii inatukumbusha tumeitwa kuwa mashahidi waaminifu, ni Mungu anayeamua matokeo ya yale tunayosema na kuyafanya. (tazama **1 Kor 3:6**).

Kwa kuzingatia Safina, tunaona mfano mmoja wa taipolojia unaoashiria kuhusu Yesu. Wazo na mpango kwa ajili ya Safina ilikuwa njia ya kumwokoa Nuhu na familia yake kutoka kwa Mungu, siyo Nuhu. Vile vile, Yesu kama njia ya wokovu kupitia kusulubiwa kwake na kufufuka kwake ilikuwa kusudi la Mungu la awali (**Mdo 2:22–24; 4:27–28; 1 Pet 1:20**). Kulikuwa na safina moja tu, siyo kutoka kwenye mlolongo wa Safina ambazo Nuhu angechagua mojawapo. Vivyo hivyo, ipo njia moja ya wokovu; Yesu alisema, *"Mimi ndimi njia, na kweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya Mimi''* (**Yoh 14:6**). Safina ilikuwa na mlango mmoja (**Mwa 6:16**). Yesu alisema, *"Mimi ni mlango, mtu akiingia kwa Mimi, ataokoka"* (**Yoh 10:9**). **Ebr 11:7** inasema Nuhu alitengeneza Safina *"kwa imani."* Vivyo hivyo, tunahesabiwa haki bure kwa neema ya Mungu *"kwa njia ya imani"* (**Efe 2:8**). Safina ilifunikwa ndani nanje kwa lami, kuipa uzito (**Mwa 6:14**); kwa hiyo, maji ya hukumu ya Mungu yaangukie kwenye Safina lakini hayakuweza kuingia ndani ya Safina. Vivyo hivyo, Kristo alichukua hukumu tuliyostahili, ilikwamba sisi tulio ''ndani ya Kristo'' hatuhukumiwi kamwe. Kwa hakika neno la Kiebrania yaliyotafsiriwa kama "kifuniko" au "lami" kama tendo na "eneo" kama jina siyo maneno ya kawaida kwa ajili ya eneo au lami. Bali, maana ya msingi ya lami ni "upatanisho," ambayo ndio inavyotafsiriwa kila mara, na lami kama jina, kwa kawaida inatafsiriwa "fidia" au "ukombozi" (Koehler and Baumgartner 2001: *kaphar, kopher,* 493–94). Kristo ni mpatanishi au dhabihu ya upatanisho (**Isa 53:4–12; Mt 26:26–28; Rum 3:25; 5:6–11; 1 Kor 15:3; Ebr 9:12–14; 1 Yoh 2:2; Ufu 5:9**). Alitoa uhai *"fidia kwa ajili ya wengi"* (**Mt 20:28; Mk 10:45**); kwa yeye tunao "ukombozi" (**Lk 1:68; Rum 3:24; 1 Kor 1:30; Efe 1:7; Kol 1:14; Ebr 9:12, 15**). Nuhu na familia yake walipaswa kuwa kwenye Safina kuepuka maji ya gharika (**Mwz 7:7**); vile vile, tunaokolewa kama tupo *"ndani ya Kristo"* (**Rum 8:1**). Mungu alifunga mlango wa Safina baada ya watu wanane na wanyama kuingia (**Mwa 7:16**); kwa hiyo, wale wote waliokuwa ndani ya Safina walikuwa salama. Ndivyo ilivyo pia kwa wote walio ndani ya Kristo: tumekwisha *"kutiwa muhuri kwa ajili ya siku ya ukombozi"* (**Efe 4:30**; pia tazama **Efe 1:13–14**) na *"wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."* (**Rum 8:38–39**). Baada ya Gharika, safina *"itulia juu ya mlima Ararati"* (**Mwa 8:4**). Huu ni mfano wa Yesu, ufufuo na kupaa, kwa kuwa Yesu, baada ya kuchukua hukumu yetu: *"alipaa juu"* (**Efe 4:8**). Yesu pia anaendeleza taipolojia ya Nuhu na Gharika katika ujio wake wa mara ya pili: *"Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, asitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."* (**Mt 24:37–39**; pia tazama **Lk 17:26–27**)

Mfano wan ne wa imani ni Ibrahimu ambaye anapongezwa. Moja, *"[8]Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. [9]Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yak, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. [10]Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu."* (**mst. 8-10**) Pili, *"[17]Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; [18]naam, yeye aliyeambiwa, Katika Isaka uzao wako utaitwa, [19]akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano. [20]Kwa imani Isaka akawabariki Yak na Esau, hata katika habari ya mambo yatakayokuwa baadaye."* (**mst. 17-19**)

Ibrahimu ni *"baba wa wote wanaoamini . . . wale walio wa imani ya Ibrahimu, ambaye ni baba yetu sote"* (**Rum 4:11, 16**; tazama **Rum 4:1–5, 9–25; Gal 3:1–18, 29**). Tunaona kwamba uaminifu wake na utii kwa wito wa kuondoka nyumbani kwake na kwenda kwenye nchi ambayo Mungu angemwonyesha (**Mwa 12:1; Ebr 11:8–10**). Mungu alimwita Ibrahimu alipokuwa anaishi Mesopotamia, akiwa bado anaabudu sanamu (**Mdo 7:2; Yos 24:2**). Kwa maneno mengine, Mungu hakumchagua Ibrahimu kwa kuwa anastahili kwa chochote yeye kama yeye, bali ni kwa sababu ilikuwa ni mapenzi yake kufanya hivyo (tazama **Neh 9:7**). **Yos 24:3** inasema kwamba Mungu *"alimchukua . . . na kumwongoza . . . na kumpa"* Ibrahimu. Mungu alitenda kwa neema yake, na Ibrahimu alitii wito na uongozi wa Mungu kwa kuondoka nyumbani kwake katika nchi ya Wakaldayo na hatimaye kwenda Israeli. Utii wake ni wa kipekee sana kwa kuwa Mungu alimwita yeye *"toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende hata nchi nitakayokuonyesha . . . . Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka mguu; akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, na ya uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto"* (**Mdo 7:3, 5**) Matokeo yake, wakati Ibrahimi alipofika kwenye nchi ambayo Mungu alimwambia atampa, Ibrahimu, pamoja na Isaka na Yak, *"kwa imani . . . waliishi kama wageni katika nchi ya ahadi, kama katika nchi ya watu wengine,"* kwa sababu ilikuwa nchi ya Kanani inayokaliwa na Wakanani (**Mwa 12:5-6**). Pia alijifunza kutoka kwa Mungu kwamba uzao

wake utakuwa wageni na watumwa tena katika nchi nyingine kwa miaka 400 kabla hawajaingia katika nchi ambayo Mungu amemwahidi Ibrahimu (**Mwa 15:7, 13-16**). Ibrahimu alikuwa anatembea kwa imani, siyo kwa kuona. Uaminifu katika kuondoka nyumbani kwake, kusafiri kwenda nchi ya ugeni, na kisha kungojea akiwa huko ni kwa sababu *"alikuwa anautazamia mji wenye misingi, ambayo mbunifu na mjenzi wake ni Mungu."* Uaminifu wa Ibrahimu ni mfano wa mtu mwaminifu kuzidi wote, Yesu, amabao kama Ibrahimu, "aliitikia wito wa Mungu aliacha mahali pazuri na alipopajua na kwenda mahali patupu 'asijue aendako' kuumba watu wapya wa Mungu" (Keller 2015: 77), ambaye hatimaye alijitoa dhabihu yeye mwenyewe kwa kumtii Mungu.

Nukuu katika **mst. 9** kwa Isaka na Yak *"warithi pamoja wa ahadi ileile"* anaweka wazi ukweli kwamba Isaka alikuwa hamtegemei Ibrahimu kwa ajili ya Ahadi, wala Yak alikuwa hamtegemei Isaka wote wawili Isaka na Yak walipokea ahadi moja kwa moja kutoka kwa Mungu. (**Mwa 26:3-4; 28:13-14; 35:12**). Isaka mwenyewe alikuwa mwana wa ahadi, ambaye kuzaliwa kwake kulitabiriwa na zaidi ya asili (**Mwa 17:19; 18:10–15; 21:1–2**; cp. **Mt 1:20–21**). Kwa hiyo, **mst. 11-12** unasema, *"Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba; alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu. Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu [k] watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika."* Wakati Sara alijulishwa kabla kuhusu kuzaliwa kwa Isaka, alidhani itakuwa vigumu kupata ujauzito (**Mwa 18:11–12**). Wakati Mungu alimwambia Ibrahimu kwamba atakuwa na mwana katika umri wake wa uzeeni, alicheka (**Mwa 17:17**). Wakati Sara aliposikia Mungu anasema yeye atapata ujauzito na kuzaa mwana katika umri wake mkubwa, akachekeka (**Mwa 18:10-15**). Wakati mtoto wake alipozaliwa, aliitwa Isaka. Jina Isaka asili yake ni Kiebrania (*Yitzchak*) na ina maana "hucheka" au "kicheko." Kwa hakika, baada ya Isaka kuzaliwa, Sara alisema, *"Sara akasema, Mungu amenifanyia kicheko; kila asikiaye atacheka pamoja nami."* (**Mwa 21:6**). Kwa kuwa **Ebr 11:11** inasema kuwa Sara alipokea uwezo wa kupata ujauzito *"kwa imani,"* inatupasa kuhitimisha kwamba, ingawa kicheko chake cha asili inawezekana ni kwa sababu kutokuamini na furaha, kutokuamini kwake iligeuka kuwa kuamini, kipekee tangu Mungu amwambie Ibrahimu kwa wakati ule, *"Je kuna lolote lililo gumu kwa Bwana?* (**Mwa 18:14**) Haishangazi, kwa hiyo, kwamba Sara anatajwa kama mfano wa *"mwanamke mtakafu"* wa zamani (**1 Pet 3:5-6**). Kwa kufuata mfano wake, Wake za wakristo pia wanaitwa, *"washirika wenza wa neema ya uzima"* (**1 Pet 3:7**). Kuzaliwa kwa Yesu, kama vile Isaka, kulitabiriwa na ni kwa nguvu isiyo ya kawaida; wakati wa kuzaliwa kwa Yesu kwa Mariamu, yeye kama Sara, alidhani ilikuwa ni vigumu kupata ujauzito (**Lk 1:26–38**).

Katika kuhitimisha mjadala wa kuzaliwa kwa Isakani muhimu ijulikane kuwa Isaka alikuwa ni wa 'pekee'' (yaani, wa kipekee) na mwana apendwayo (**Mwa 22:2, 12, 16**). Kwa namna ambayo alikuwa ''mfano'' wa Kristo. Rejea katika **Yoh 1:14, 18; 3:16, 18; 1 Yoh 4:9** kwa Yesu kama Mungu *"Mwana pekee wa Mungu"* na katika **Rum 8:32** (yeye *"hakumzuilia Mwanaye wa pekee"*) Ni mfano wa wazi kwa Isaka katika **Mwa 22:2, 12,** na **16**. Isaka "uzao" wa mwili alioahidiwa na Ibrahimu. Hata hivyo, hiyo ahadi aliyotoa kwa Ibrahimu kwa hakika iliendelea hadi kwa Isaka na kwa halisi ilikuwa inarejea kwa Kristo, kama Paulo anavyosema katika **Gal 3:16**, *"Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo."* **Ebr 11:12**, kwa hiyo nukuu, kutoka **Mwa 15:5; 13:16;** na **32:12** kwa kulinganisha uzao wa Ibrahimu *"kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika."* Hii inaweza kuwa na ishara ya uzao wa Ibrahimu: baadhi ni waamini, lakini wengi ni wasioamini. Bullinger anaeleza "wale ambao ni kama mchanga na vumbi ya dunia walitembea kwa imani, wale walio kama mchanga na vumbi na dunia walitembea kwa kuona, macho yakiwa yanatazama dunia na hawakumwamini Mungu kwa kile alichowaandalia wafurahie katika uzima wa milele. . . . Bali wale walio kama 'nyota' walikuwa washirika wa mwito wa mbinguni (Ebr. iii. 1). Walimwamini Mungu—na wakadhihirisha 'utii kwa imani.'" (Bullinger 1979: 153)

3. Muhutasari unaohusu mjadala katika **mst. 4-12** (**11:13-16**)

[13]Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi. [14]Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. [15]Na kama wangaliikumbuka nchi ile waliyotoka, wangalipata nafasi ya kurejea. [16]Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji.

Mistari ya 13-16 inaeleza kwa muhutasari uamininfu wa watu wote na matukio yaliyojadiliwa kwenye **mst. 4-12**. Kwa kila kisa, watu *"walikufa katika imani, pasipo kupoea ahadi, lakini wakiwa wameziona tokea mabali na kuzishangilia, wakikiri ya kwamba walikuwa wageni na wapitaji duniani…lakini kama ilivyo, walitamani nchi iliyo bora, nayo ni nchi ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; kwa kuwa*

amewaandaa mji kwa ajili yao." Kwamba "nchi ya mbinguni" itakuwa ni "Yerusalemu ya mbinguni" inayorejewa katika **Ebr 12:22** na **Ufu 21-22**. Ni wazi kutokana na ukweli kwamba **Ebr 11:39-40** inasema kwamba watakatifu wa AK aliojadiliwa kwenye sura ya 11 *"Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; 40 kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."* Hata hivyo katika Kristo, sisi ''*tumeufikilia mlima Sayuni na katika mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu ya Mbingun''* (**Ebr 12:22**; pia tazama **Gal 4:21-31**).

4. Mifano mahususi ya imani ya kweli (**mst. 17-38**).

[17]Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; [18]naam, yeye aliyeambiwa, Katika Isaka uzao wako utaitwa, [19]akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano. [20]Kwa imani Isaka akawabariki Yak na Esau, hata katika habari ya mambo yatakayokuwa baadaye. [21]Kwa imani Yakobo, alipokuwa katika kufa, akambariki kila mmoja wa wana wa Yusufu, akaabudu akiegemea kichwa cha fimbo yake. [22]Kwa imani Yusufu, alipokuwa amekaribia mwisho wake, alitaja habari za kutoka kwao wana wa Israeli, akaagiza kwa habari ya mifupa yake.

[23]Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri; wala hawakuiogopa amri ya mfalme. [24]Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; [25]akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; [26]akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo. [27]Kwa imani akatoka Misri, asiogope ghadhabu ya mfalme; maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyeonekana. [28]Kwa imani akaifanya Pasaka, na kule kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wao. [29]Kwa imani wakapita kati ya Bahari ya Shamu, kama katika nchi kavu; Wamisri walipojaribu kufanya vivyo [s]wakatoswa.

[30]Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba. [31]Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani. [32]Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yeftha na Daudi na Samweli na za manabii; [33]ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, [34]walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni. [35]Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora; [36]wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; [37]walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya; [38](watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.

Kwa kuzingatia utayari wa Ibrahimu kumtoa mwanawe kama dhabihu kwa Mungu (**Mwa 22:1-14; Ebr 11:17-19**), wakati **mst. 17** unasema kwamba Ibrahimu *"alimtoa Isaka,"* neno "alimtoa" lipo katika wakati mkamilifu. Hii "huomyesha kwamba Mungu alitambua imani kama tendo lake; na akampatia matokeo kana kwamba amekwisha kutimiza kwa uhalisia" (Bullinger 1979: 162). Tunaona kitu hicho hicho kwenye tukio la **Mwa 22:16**, ambapo husema *"Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee…"* Tena, Mungu anamchukulia Ibrahimu kama aliyekwisha kufanya tendo la kutoa sadaka. Kwa kuwa mstari wa **17** unasema kwamba Ibrahimu alimtoa Isaka *"kwa imani,"* hii ina maana utii unadhihirisha imani; au, kuliweka kwa maneno maneno mengine, kushindwa kutii inadhihirisha kukosekana kwa imani. Hii pia inaonekana katika **Mwa 22:5**, ambapo, Mungu baada ya kumwambia Ibrahimu aende kwenye mlima Moria amtoe Isaka, Ibrahimu aliwambia vijana waliokuwa pamoja naye *"Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena.* Hatimaye, utii wetu nit endo la ibada kwa Mungu. Sehemu ya pili ya **mst. 17** inatumia wakati usio kamilika (*"alipokuwa akimtoa"*) kuonyesha kwamba tendo la kutoa halijakamilika, kwa Mungu alizuia lisikamilike.

Tukio lote la Ibrahimu na Isaka lilikuwa ni ishara iliyoonekan mapema ya kusulubiwa kwa Kristo. Hiyo bila shaka ni sababu nyingine kwa nini litumike neno lililo katika wakati uliopita katika **Mwa 22:16** na mwanzo wa

Ebr 11:17. Kwa, Ibrahimu aliambiwa amtoe Ibrahimu katika Mlima Moria (**Mwa 22:2**). Hapo ndipo mahali ilipo Yerusalemu na hekalu, na ni mahali Yesu alisulubiwa (**2 Nya 3:1**). Kama vile Ibrahimu alivyoonyesha upendo wake kwa Mungu kwa utayari wake wa kumtoa mwanawe, hivyo ndivyo na Mungu alivyoonyesha upendo wake kwa ulimwengu kwa kumtoa mwanaye kwa ajili ya dhambi zetu. Kama kuni zilivyowekwa juu ya Isaka (**Mwa 22:6, 9**), ndivyo na Yesu alivyoubeba msalaba aliosulubiwa juu yake (**Yoh 19:17; 20:25–27**). Kama alivyosema Ibrahimu ya kwamba *"Mungu atajipatia mwanakondoo"* (**Mwa 22:8**) kwa ajili ya dhabihu, ndvyo Mungu alimtoa Yesu, *"mwanakondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu"* (**Yoh 1:29**; pia tazama **Ufu 5:6**). Kama Isaka alivyokuwa mtii kwa ajili ya mapenzi ya baba yakee hata kwa suala linalogharimu kifo, ndivyo Yesu alivyokuwa mtii kwa ajili ya mapenzi ya Baba yake hata (**Mt 26:39; Flp 2:8**). Kwa maneno mengine, utimilifu wakati wote ni mkuu kuliko kivuli: Isaka alikuwa mtii hata kwa kuhatarisha uhai wake; Kristo alikuwa mtii kwa gharama ya uhai wake. Kama ambavyo Ibrahimu laimhesabu mwanaye kuwa amekufa kwa siku tatu za safari yao, kwa kuwa Ibrahimu alishakuwa tayari kukamilisha dhabihu ya kumtoa uhai wa (**Mwa 22:4, 9–10**), ndivyo Yesu alivyokaa kaburini kwa siku tatu (**Mt 12:40; Lk 24:21; Mdo 10:39–40**). Mwisho, kama vile Ibrahimu alivyomwamini Mungu ya kuwa atamfufua Isaka kutoka kwa wafu, *"yeye alimpokea tena kama ishara"* (**Ebr 11:19**), ndivyo Yesu alivyofufuliwa kihalisia kutoka kwa wafu (**Mt 28:1–6; Mk 16:1–13; Lk 24:1–6; Yoh 20:1–28**).[29]

Mistari ya 20-22 inatoa maelezo mafupi ya jinsi ambavyo, *"kwa imani,"* Isaka alivyombariki Yak na Esau, Yakobo alivyombariki Efraimu na Manase na jinsi alivyoabudu, na Yusufu kutaja kutoka kwa wana wa Israeli kutoka Misri na kutoa maagizo kuhusu mifupa yake. Kwa kila kisa imani yao ilitazama Zaidi ya kifo, kila mmoja alikuwa na ujasiri kwamba Mungu atatimiza mapenzi yake, hata baada ya wao wenyewe kufa, lakini kutimia kwa mapenzi ya Mungu kulijulikana tu kwa njia ya imani. Mwanzoni inaweza kuonekana kama kitu cha ajabu kwamba matendo yale yameorodheshwa kwenye orodha ya matendo ya uaminifu pamoja na watu wanaotajwa katika sura ya 11. Maelezo ya Isaka kuwabariki Yakobo na Esau yapo katika **Mwa 27.** Yakobo alikula njama na mama yake na akajifanya Esau, akitafuta upendelea kwa matendo ya mwili. Ukweli Isaka alimbariki Yakobo *"kwa imani"* inaonyesha kwamba, pamoja na uongo wa Yakobo, Isaka ni lazima awe anatambua utambulisho wake halisi kabla ya kutoa baraka. Yeye kumbariki Yakobo ulikuwa ni mango wa Mungu, kwa kuwa Bwana alishatamka mapema kwamba wote wawili Yakobo na Esau hawajazaliwa kwamba *"mkubwa [Esau] atamtumikia mdogo [Yakobo]"* (**Mwa 25:23**). Wakati Esau alipotambua Isaka amembariki Yakobo, ingawa alilia kwa uchungu sana, hakuweza kubadilisha akili ya Isaka au zile baraka alizotoa. Isaka alimbariki Esau, lakini kwa kufuata vile Mungu alivyotamka kabla ya hao wawili kuzalwa (**Mwa 27:34-40**). Kama anavyohitimisha Bullinger, "Katika shughuli hii ya huzuni, 'mapenzi ya mwili' yaliwashinda Rebeka na Esau na Yakobo, lakini hayakumshinda Isaka, ingawa alikuwa na mgogoro mkubwa katika hilo. Imani ikayashinda hayo yote, akaendelea na 'mapenzi ya Mungu.'" (Bullinger 1979: 196)

Yakobo kumbariki Efraim una Manase na kuabudu, inaelezwa katika **mst. 21.** Baraka zinapatikana katika **Mwa 48**, na maelezo ya Yakobo akiwa anaabudu yapo katika **Mwa 47:31**. Katika Mashariki ya mabali, mtoto mkubwa kwa kawaida alikuwa anapendelewa Zaidi kuliko mdogo. Ndio maana wakati Yak anabariki wana wa Yusufu, Yusufu alitaka Yakobo ambariki Manase (mtoto mkubwa) na kwa mkono wake wa kulia na Efraimu(mtoto mdogo) kwa mkono wa kushoto. Yakobo akafanya tofauti sawa sawa na mapenzi ya Mungu (**Mwa 48:17-20**). Ingawa baraka za Yakobo/Esau na ya Efraimu/Manase ilikuwa ni baraka kwa mdogo zaidi ya mkubwa, misingi ya baraka hizo ilikuwa tofauti. Ya kwanza ilikuwa ni nia ya mwili ilitumika kupata kitu ambacho Yakobo hakustahili, ambacho kwa hakika ilikuwa ni mapenzi ya Mungu. Na ya pili ilikuwa dhidi ya mapenzi ya mwanadamu, yaani, mfumo wa upendeleo wa uliotengenezwa na wanadamu, ambao Mungu aliukiuka. Sababu ya kuwa tendo la Yakobo kumwabudu Mungu kinatajwa kwa kuunganishwa na tendo la yeye kuwabariki wana wa Yusufu, hata kama alichukua muda kabla ya kuwabariki, hii inaleta baraka chini ya mwavuli wa ibada. Katika **Mwa 47:31**, Ibada ya Yakobo ilikuwa kwenye muktadha wa Yusufu kukubali kutomzika Yakobo katika nchi ya Misri (mahali walipokuwepo wakati hayo yanatokea) lakini waliuchukua mwili wake kutoka Misri baada ya kifo chake. Mara tu baada ya kuwabariki vijana, Yakobo tena anaongea na Yusufu habari za kifo chake (**Mwa 48:21**). Kwa hiyo, imani ya Yakobo na ibada ilitawala tukio lote la Yakobo, Yusufu, Efraimu, na Manase.

---

[29] Wengi pia wamechukulia kondoo kama kiashiria cha Kristo (tazama Greidanus 1999: 310). Augustine anaeleza, "Kwa kuwa hakuchinjwa . . . ambaye alikuwa ndiye kondoo wa sadaka iliyokuwa ikamilike kwa damu halisi? Kwa kuwa wakati Ibrahimu alipomwona, alikuwa amekamatwa pembe zake kwenye kichaka. Inawakilisha nini kama si Yesu ambaye kabla hajatolewa kama dhabihu alikuwa amevikwa taji ya miiba na Wayahudi?'' (Augustine 1950: XVI, 32) Kondoo alikuwa ni dhabihu isiyo na hatia, alitolewa ili Isaka awe na uzima *katika mwili*. Kristo alikuwa dhabihu isiyo na mawaa iliyolewa ili watu wawe na uzima *wa milele*. Kwa mifano na vivuli, AK, ni mfano wa kanisa. **Gal 4:28-29** inasema, *"Basi, ndugu zangu, kama Isaka sisi tu watoto wa ahadi. Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomwudhi yule aliyezaliwa kwa Roho, ndivyo ilivyo na sasa."*

Ebr 11:22 inasema, *"Kwa imani Yusufu, alipokuwa amekaribia mwisho wake, alitaja habari za kutoka kwao wana wa Israeli, akaagiza kwa habari ya mifupa yake."* Unabii wa Yusuf una maagizo kuhusu mifupa yake inapatikana katika **Mwa 50:24-25**. Mwanzoni Mungu aliahidi kuhusu utumwa wa Wana wa Israeli na kutoka kwao utumwani katika **Mwa 15:13-14**, labda Yusufu alijua kuhusu hili. Inashangaza kwamba, pamoja na Maisha ya Yusufu kujaa matukio—Mungu kumpa ndoto akiwa kijana, kuuzwa kwake kama mtumwa, kutabiri ndoto, kuinuliwa kwake kwenye mamlaka huko Misri na kuwaokoa watu kutoka kwenye njaa, na Mungu kwa wazi akiyanyoosha njia zake—hata moja halikutajwa. Jambo moja linalotajwa ni kwamba Mugu alinena na Yusufu kuhusu utumwa wa katika Misri na hatimaye kutoka kwao. Kwa maneno mengine, Mungu alisema akasikia, na kwa imani akasema kile ambacho Mungu alimwambia. Imani ya Yusufu msingi wake ni maarifa na imani yake kwa kile anachosema Mungu. Katika **Mwa 50:24**, aliwaambia ndugu zake, *"Yusufu akawaambia nduguze, Mimi ninakufa, lakini Mungu atawajia ninyi bila shaka, atawapandisha toka nchi hii, mpaka nchi aliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yak."* Kwa maneno mengine, alikuwa hasemi tu mawazo yake; maneno yake, *''Hakika Mungu''* inaakisi imani yake halisi na tumaini lake kwa Mungu, kwa msingi wa ukweli kwamba hiki ndicho ambacho *"Aliahidi kwa kiapo kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo."* Hakuna uhakika ulio mkuu kuliko huo. Ndio maana kwa kuwa Waebrania sura ya 11inahusu imani na mifano ya imani inayovumilia, huu ni mfano bora kutoka kwa Yusufu ambao umewekwa kumbukumbu. Hii ni lazima iwe faraja kwetu na tuweke imani yetu isiyokufa kwenye neno la Mungu.

Mfano unaofuata ni mfano wa wazazi wa Musa na Musa mwenyewe. Farao wa Misri alitoa amri kwamba wana wote wa kiume walio wachanga watupwe mto Nile na wauawe. (**Kut 1:16, 22**). **Ebr 11:23** Inaeleza, *"Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri; wala hawakuiogopa amri ya mfalme."* Huu ni mfano wa imani inayoshinda hofu ya mwanadamu. Kwa kuwa *"imani huja kwa kusikia na kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo*" (**Rum 10:17**), Mungu pasipo shaka alisema na wazazi wa Musa na kuwaambia wamfiche mtoto. Kama wazazi wa Musa wangekuwa wamemficha Musa kwa ajili ya uzuri wake na upendo wao na kwa ajili ya huruma waliyonayo kwake, hofu ingeozeka kwao. Hata hivyo ilikuwa ni kwa ajili ya imani yao na tumaini walilonalo kwa Mungu kwamba, *"wala hawakuiogopa amri ya mfalme."* Kama tulivyoona, imani inatusaidia sisi kushinda mapenzi ya mwili, mapenzi ya mwanadamu na hofu ya mwanadamu.

Imani ya Musa mwenyewe inasifiwa kwa matukio mawili: (1) matukio kabla ya wito wake wa kuwaweka huru watu wa Mungu; na (2) matukio baada ya wito wa Mungu wa kuwaweka watu wa Mungu huru. Kuhusu seti ya kwanza ya matukio **Ebr 11:24-26** tell us, *"[24] Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; [25]akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; [26]akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo."* Matukio yaliyoorodheshwa hapa yanapatikana katika **Kutoka 2**. Kama ambavyo imani inashinda hofu ya mtu, mistari hii inatuonyesha imani inaweza kushinda hali ya kusifa na watu na anasa, mamlaka, cheo, na utajiri ambao mtu anaweza kuutoa. Kwa kukataa anasa, mamlaka, cheo na utajiri wa Misri kwa ajili ya kuteswa pamoja na watu wa Mungu, Musa alikuwa hachagui "kati ya mabaya mawili ili achague ubaya ulio mdogo" Badala yake, alithamini uaminifu kwa Mungu na kule kujitambulisha pamoja na watu wa Mungu, *"akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri."*

Kuhusu matukio baada ya wito wa Mungu kwa Musa ili awaweke watu wa Mungu huru, **Ebr 11:27-29** inasema, *"[27]Kwa imani akatoka Misri, asiogope ghadhabu ya mfalme; maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyeonekana. [28]Kwa imani akaifanya Pasaka, na kule kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wao. [29]Kwa imani wakapita kati ya Bahari ya Shamu, kama katika nchi kavu; Wamisri walipojaribu kufanya vivyo wakatoswa."* Kama ilivyokuwa kweli kwa wazazi wa Musa, imani ilimsaidia Musa kushinda hofu ya hasira ya mfalme. Wengi wanadhani Musa kutoka kwa mfalme ilikuwa ni wakati ule alipomwua Mmisri ambaye alikuwa akimpiga Mwebrania (**Kut 2:12-15**). Hata hivyo, **Kut 2:14** inasema, *"Musa akaogopa, akasema, Kumbe! Jambo lile limejulikana,'"* na **Kut 2:15** inaongeza kuwa Musa "alikimbia" kutoka mbele ya Fara aliyetaka kumwua. Kwa upande mwingine **Ebr 11:27** inasema, *"[27]Kwa imani akatoka Misri, asiogope ghadhabu ya mfalme."* Ingawa inawezekana kuwa Mungu alisema na Musa wakati Fulani baada ya kumwua yule Mmisri kabla ya kuondoka Misri, kuondoka kwake Misri, kuondoka kwake Misri ni mfano wa vile Musa na watu walipoondoka Misri katika **Kut 13:17—14:31**).[30] Kwa hiyo, Musa kuondoka kwake kwa awamu ya kwanza ni kwa sababu ya hofu na kukimbia, wakati katika safari yake ya pili ya kuondoka Misri ilikuwa na imani na iliyomfanya aondoke. Ilikuwa ni wakati wa Kutoka, Israeli walipopiga kambi mbele ya bahari ya Shamu na Farao akiwa anawafuatia waisraeli, ndipo akawaambia watu, *"Msiogope!"* (**Kut 14:13**) Ikiwa hii imerejewa katika **mstari wa 27**, kiufundi haijafuata mtiririko mzuri wenye mpangilio, kwa kuwa **mst. 28** kutunza Pasaka, Iliyotokea ghafla baada ya Waisraeli kuondoka Misri. Watu walioorodheshwa kwenye mstari wa 32 pia hawajapangiliwa vizuri,

[30] Leon Morris anatoa maelezo kwa pande zote za kisa hiki (Morris 1981: 126-27).

jambo ambalo linaonyesha mwandishi alikuwa na sababu ya kuwapanga hivyo. Sababu hapa inaweza kuwa Pasaka, kutoka Misri, na kuvuka bahari ya Shamu ni matukio yaliyo na uhusiano wa karibu na kule Musa kuwaambia watu ''*Msiogope!"* Kwa kuongezea, matendo yote yanayoelezwa kuwa yalifanyika ''*kwa imani"* ni mistari hii—kutoka Misri, kushika Pasaka, na kuvuka Bahari ya Shamu—hayakuwa ya Musa kibinafsi lakini yalihusu taifa zima.

Ingawa mstari wa **28** unaelezwa kwamba *"Musa alitunza Pasaka,"* neno lenye maana ya "kutunza Pasaka" ni *poieō,* kwa uhalisia linalomaanisha kufanya au fanya, hapa kwa maana ya ''kuianzisha'' Pasaka (Zodhiates 1993, *poieō,* 1187-88). Kuifanya Pasaka kuadhimishwa na wote ilionyesha imani kuu ya Musa, kwa sababu ilikuwa ni usiku ule ule wa Pasaka wana wa Israeli walitoka Misri (**Kutoka 11-12**). Imani ya Musa inadhihirishwa na jinsi alivyofafanua kwa wana wa Israeli mambo yote yaliyohitajika kuhusu jinsi Pasaka ilitakiwa kufanyika, hata kama yale mambo yanaweza kuwa hayaeleweki kwa watu na hata kama watu hawakuwa na haja sana ya kujiandaa kwa ajili ya kuondoka achilia mbali kufanya desturi za ibada (**Kut 12:3-32**). Imani pia inaonekana katika kufanya kile kisichoweza kufikirika yaani kwa nini kuweka damu kwenye miimo ya milango iwe sababu ya malaika w amauti kupita juu na wakati watu wapo kwenye Bahari ya Shamu, wazo kwamba wangeweza kukwepa jeshi la Farao ilikuwa kinyume na kile walichokuwa wanaona kwa macho yao. Katika mambo haya yote, Musa na watu walikuwa wakitembea kwa imani, na siyo kwa kuona.

Mfano unaofuata wa imani unahusu ukuta wa Yeriko na Rahaba. **Ebr 11:30-31** inaeleza, *"[30] Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba. [31]Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani."* Mpango wa Yoshua kwa ajili ya kuzunguka mji wa Yeriko na ukuta wake kuanguka chini siku ya saba inaonekana katika **Yos 6:1-21**. Mpango huu ulitaka imani kubwa kwa upande wa Yoshua na jeshi la Waisraeli, kwa kuwa ilikuwa jambo la ajabu na kinyume na mkakati dhidi ya mji wowote na jeshi lolote, kwa Waisraeli au wowote wengine. Zaidi ya hilo, kuliko hakuna sababu iliyo dhahiri kwa nini kwa nini kwa kuzunguka mji kwa siku saba na baadaye kupiga tarumbeta na kupiga kelele, ukuta wa uanguke chini. Msingi pekee kwa nini mpango huu ulifanya kazi ni kwa sababu Mungu ndiye alioutoa kwa Yoshua na kwamba Yoshua na jeshi lake walimwamini Bwana.

Maelezo ya Rahabu kuwaficha wapelelezi wa Waisraeli unapatikana katika **Yos 2:1-21**. Katika **Yos 2:11**, alishuhudia *"BWANA, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini.''* Mtd yake ya kuwatetea wapelelezi wa israeli yalifanyika ''kwa imani'' (**Ebr 11:31**). Kuhusishwa kwa Rahabu katika "ukumbi wa imani" ni muhimu kwa kuwa yeye hakuwa ametokea kwa Waisraeli na wala hakuwa Mwisraeli, bali yeye alikuwa mmtaifa kutoka Yeriko na alikuwa kahaba. Watu wanaotoka katika hali zozote wanaweza kuwa na imani. Kitambaa alichofunga kwenye dirisha lake ili kuweka alama kwenye nyumba yake kwa ajili ya kuwaonyesha wana wa Israeli (**Yos 2:18-21**) ilikuwa na uhusiano na Pasaka ya asili katika Misri. Ambapo, damu ilipakwa kwenye kizingiti cha juu na kwenye miimo ya milango ya nyumba zao, na wote waliokuwa ndani walilindwa dhidi ya malaika w amauti. Hapa Kamba nyekundu kwenye dirisha ilifanya kazi kama kitu kilichowaokoa wote waliokuwa ndani. Mfanano huu unalenga kwenye wokovu wa wote wawili Wayahudi (Waebrania kule Misri) na Mataifa (Rahabu na familia yake katika Yeriko) kwa damu ya Kristo (tazama Lunn 2020: 127). Ingawa siyo "ishara," halisi, Rahabu mwenyewe ni ishara ya Kristo, injili na kanisa. Akiwa mkanani kutoka Yeriko (**Yos 2:1–2**), yeye ni kivuli cha kanisa lenye watu "kutoka *kila kabila na lugha na taifa*" (**Ufu 5:9**). Kama vile Mataifa walivyokuwa sehemu ya Kanisa mapema kabisa (tazama **Mdo 10**), vivyo Rahabu alikuwa mwenyeji wa Yeriko, mji wa kwanza kutwaliwa na wana wa Israeli baada ya kuvuka Mto Yordani. Zaidi ya hayo, **Mt 1:4–5** inasema yeye alikuwa mama wa Boazi kupitia Salmon na kwa hiyo ni sehemu ya ukoo wa Yesu Kristo. Kwa hiyo, damu ya mkanani ilikuwa ndani ya mishipa ya Mwana wa Mungu.

Sehemu inayofuata inawataja watu sita na inarejea *"manabii"* Kisha inataja makundi ya watu yasiyopewa jina, ambao wote walidhihirisha imani, mara zote wakiwa wanakabiliana na mambo magumu. **Mstari wa 32-38** unaeleza, *"[32] Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yeftha na Daudi na Samweli na za manabii; [33]ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, [34]walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni. [35]Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora; [36]wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; [37]walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya; [38](watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi."* Gideoni, Baraka, Samsoni, na Yefta wote walikuwa waamuzi au, kwa habari ya Baraka, alishirikiana na mwamuzi (Debora). Gideoni na Yefta kila mmoja anatambulishwa kama *"askari shujaa"* (**Waamuzi 6:12; 11:1**). Kwa visa hivi viwili, uhusiano wa karibu unasisitizwa: Gideoni alikuwa kijana mdogo kupita wote katika familia *"ambaye alikuwa mdogo katika Manase"* (**Waamuzi 6:15**); Yefta alikuwa ni

mtoto wa mwanamke kahaba na alifukuzwa na hakupewa urithi, kutoka kwenye nyumba ya baba yake (**Waamuzi 11:1-2**). Pamoja na hayo, Mungu aliwatumia wote hawa wawili kuokoa wana wa Israeli kutoka kwenye mkono wa adui zao.[31] Hiyo ni moja ya alama za imani: haijaweka misingi kwenye utajiri wa kidunia au mamlaka. Badala yake "[27]*bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu;* [28]*tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko;* [29]*mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu."* (**1 Kor 1:27-29**)

Baraka na Samsoni wametajwa katika mpangilio usio sawa na vipindi vyao katika historian a wamewekwa pamoja. Sababau ni kwamba hao wote wanahusiana na wanawake. Baraka alikuwa anashirikiana na Debora, aliyeanzisha utume wake wa kupambana na Wakanani, na pamoja Yaeli ambaye alimaliza utume wake (**Waamuzi 4-5**). Wanawake ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa sababu wakanani walikuwa wakiwanyonya wanawake wakati wanawatesa wana wa Israeli (**Amu 5:30**). Samsoni alisalitiwa na mke wake na Delila, wote wawili wakiwa ni Wafilisti. Huku kusalitiwa mara mbili ulikuwa ni mpango wa Mungu ili amtumie Samsoni kuwashinda Wafilisti, amabo walikuwa wanawatesa Waisraeli (**Waamuzi 13-16**).

Kundi linalofuata limetajwa kwenye **Ebr 11:32** ambalo ni la akina Daudi, Samweli, na manabii wengine. Wanaungana kwa mantiki kwamba wote ni wafalme na manabii: Daudi alikuwa mtu wa mwisho kupakwa mafuta na Samweli kabla ya kufa kwake, alipompaka mafuta Daudi kama Mfalme (**1 Sam 16:12-13**). Samueli alipofanya hivyo, *"roho ya Bwana ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile na kuendelea"* (**1 Sam 16:13**). Hiyo ni ishara ya Roho Mtakatifu kuja na kubakia juu ya Yesu wakati anabatizwa (**Yoh 1:31-34**). Kwa kweli, Daudi alikuwa na "ishara" ya Kristo. Yesu alitambua hivyo. Wakati wanafunzi wa Yesu walipokuwa wanapura nafaka siku ya Sabato (**Mt 12:1–8; Mk 2:23–28; Lk 6:1–5**), walikuwa wakilalamikiwa na Mafarisayo ya kwanza wanavunja Sabato, Yesu alinukuu **1 Sam 21:1–6**, ambapo Daudi alikula ''*mikate ya wonyesho''* iliyowekwa wakfu madhabahuni. Yesu alitambua kosa alilofanya Daudi (siyo *"sahihi kwa yeyote kula isipokuwa makuhani peke yao"*). Yesu alikuwa anaweka dai la Kimasihi: ahadi yake isiyoelezwa kwamba "aliye mkuu kuliko Daudi yupo hapa" (France 1971: 46). R. T. France anahitimisha, "Majadala kuhusu mamlaka ya Daudi kwa kuhusianisha na mamlaka kuu ya Yesu inaelezwa vema kwa taipolojia iliyojificha, ikiwa Daudi, aliye mfano, ana mamlaka ya kutafsiri sheria, Yesu aliye mkuu halisi, ni lazima ana mamlaka kuu Zaidi." (France 1971: 47) Matamko kadhaa ya AJ, yananena kuhusu Mungu kumwinua Daudi tena kama masihi aliyeahidiwa na Mfalme (**Yer 30:8–9; Ezek 34:23–24; 37:24; Hos 3:5**). Walter Kaiser anaeleza, "Hii haimaanishi kwamba atapata mwili tena kama mfalme kwa mara nyingine. Badala yake, Masihi atatokea kwenye ukoo wa Daudi na atatimiza kila kitu alichoahidiwa." (Kaiser 1995: 189) AJ inaonyesha kwa wazi kwamba Yesu Kristo inatimza matarajio ya Waisraeli kwamba atatimiza mataraji ya Waisraeli kupata mfalme atokaye kwa Mungu (tazama k.mf., **Mt 2:4–11; 16:16, 20; 22:42–45; 26:63–64; Mk 8:29; 12:35–37; 14:61–62; Lk 4:41; 20:41–44; 22:67–70; 23:2–3, 39; 24:26, 46; Yoh 4:25–26; 11:25–27; 20:30–31; Mdo 2:30–36; 9:22; 17:3; 18:5, 28; 1 Yoh 2:22; 5:1**). Hili limetabiriwa kwa Mariamu na malaika Gabrieli, kabla Yesu hajazaliwa, "[32]*Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake.* [33]*Ataimiliki nyumba ya Yak hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho"* (**Lk 1:32–33**). Hii ilitambuliwa katika mwanzo wa huduma ya Yesu (**Yoh 1:49**, *"Mwalimun wewe ni Mwana wa Mungu; wewe Mfalme wa Israeli"*). Wakati Yesu ameingia Yerusalemu mara ya mwisho, injili nne zilikuwa zinatafsirika kwamba kama ilivyo kwa kuja kwa Ufalme wa Daudi ulivyotabiriwa (**Zek 9:9; Mt 21:1–11; Mk 11:1–11; Lk 19:28–40; Yoh 12:12–16**). Daudi kinabii aliongea kuhusu ufufuo wa Yesu, ufalme wa Kristo, na

[31] Kuhusu nadhiri ya (**Amu 11:29-40**), wachambuzi wengi wanafikiri kwamba hii imetokana na sadaka ya Yefta kumtoa binti yake kama sadaka ya kuteketezwa. Hii haikuwa sababu **Amu 11:30-31** anaooan, *"Naye Yeftha akamwekea BWANA nadhiri, akasema, Kwamba wewe utawatia wana wa Amoni mkononi mwangu kweli, ndipo itakuwa ya kwamba, kile kitakachotoka katika milango ya nyumba yangu kunilaki, hapo nitakaporudi na amani kutoka kwa hao wana wa Amoni, kitu hicho kitakuwa ni cha BWANA, nami nitakisongeza kiwe sadaka ya kuteketezwa."* Kwanza, hakuna mahali Mungu anakosoa nadhiri ya Yefta, na kwa hakika haiwezekani kuamini kwamba Mungu anaweza asimwadhibu Yefta kama asingemtoa dhabihu binti yake mwenyewe. Pili, neno "na" katika sehemu ya mwisho wa nadhiri kimaandishi inawezekana ikatafsiriwa kama "au" 'Tatu, **Amu 11:37-39** inasema, *"*[37]*Kisha akamwambia baba yake, Basi na nifanyiwe neno hili; niache peke yangu muda wa miezi miwili, ili nipate kwenenda milimani, na kuombolea uanawali wangu, mimi na wenzangu.* [38]*Akamwambia, Haya, enda. Akampeleka mbali muda wa miezi miwili; naye akaenda zake, yeye na wenziwe, akauombolea uanawali wake huko milimani.* [39]*Basi ikawa mwisho wa hiyo miezi miwili, akarudi kwa babaye, aliyemtenda sawasawa na ile nadhiri yake aliyokuwa ameiweka; naye alikuwa hajamjua mtu mume."* Yote hii haihusiki na sadaka za binadamu. Badala yake, inahusika na sehemu ya kwanza ya nadhiri kuweka wakfu chochote kitakachokuja cha kwanza kutoka nyumba ya Yefta kwenda kwa Bwana. Kwa maneno mengine, Yefta alimweka wakfu binti kwa ajili ya Bwana, na ambaye inahusu Maisha yake ya ubikira binafsi (tazama Bullinger 1979: 325-30).

kuketi kwake kwenye "kiti cha Daudi" Siku ya Pentekoste, Pet alitangazwa ya kwamba imetimizwa kwa Yesu kwa njia ya kufufuka kwake na kupaa kwake. (**Mdo 2:29–36**).

Kwa kutokana na hili, mambo kumi chanya, yenye ushindi, na yanatupa kushinda ambayo ni sifa ya imani yameorodheshwa katika **mst. 33-35**: *"[33]ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, [34]walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni. [35]Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora;* Mifano ya imani haiishii kwa Daudi, Samweli, na manabii bali ilidhihirishwa na wengi waliokuwa watu wa imani. Jambo la msingi la surah ii yote ni kuhusu imani yenye kuvumilia. Matokeo yake, wakati mstari wa 33 unaema *"kwa imani walishinda milki za falme"* ingawa wengi wanafikiri katika mrengo wa kijeshi, neno linahusu "kushinda" "si neno la kupigana vita kwa silaha, kama askari, vitani; lakini ni neno linalotumika kwenye mieleka, kama wanamichezo walioko jukwaani. . . . Ina maana kuingia kwenye mapambano (kwa mafaniko) na falme ; si kwa silaha ili kupata mali, bali kwa silaha za maadili ili kushikilia maisha ya kiroho yenye kweli." (Bullinger 1979: 334-35) Vivyo hivyo, *"waliokuwa dhaifu wametiwa nguvu"* (**mst. 34**) ni kwa ajili ya mambo ya rohoni siyo nguvu ya kimwili (tazama **Mdo 9:22; Rum 4:20; Efe 6:10; Flo 4:13; 1 Tim 1:12; 2 Tim 2:1; 4:17**). Msemo katika **mst. 34**, *"walio dhaifu wamefanywa wenye nguvu,"* anaakisi Paulo alichoambiwa na Mungu katika **2 Kor 12:9**, *"Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu."* Ukweli kwamba *"wengine waliepuka upanga"* (**mst. 34**) haionyeshi ukuu wa imani yao dhidi ya wapendwa ambao *"waliuawa kwa upanga"* (**mst. 37**) kwa sababu ya imani yao. Bali inaonyesha neema ya Mungu.

Baada ya mifano ya imani inayoshinda, ipo mifano mingi ya imani iliyosababisha kuteswa na kuumizwa na kifo: *" [35b]Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora; [36]wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; [37]walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya; [38](watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi."* Ingawa **mst. 35b** unatafsiriwa *"na wengine,"* kwa kiyunani kwa kweli unasomeka *"bali wengine,"* yaani, inatofautisha wale walioshinda na kustawi kwa sababu ya imani yao na wale walioteseka na kushindwa, lakini bado wakabakia waaminifu pamoja na mateso yao. Hakika waliteseka kwa ajili ya imani yao, kama vile wanafunzi walivyoteseka wote kwa ajili ya imani yao. Inweza kuonekana ni ajabu kwamba, katika **mst. 37**, inahusisha *"walijaribiwa"* baada ya kuongea kuhusu watu walibakia waaminifu pamoja na kupigwa mawe na kuchanwa vipande viwili. Neno "walijaribiwa" ni *peirazō*, ambayo ipo katika muundo wa matamshi wa neno "kupimwa" (*peirasmos*). Mungu hutumia majaribu, mateso, na taabu kupima imani yetu na ujasiri wetu kwake. Jaribu linaweza kuwa kipimo kikali. Jaribu linaweza kuwa kuvutwa kutenda dhambi, lakini lengo likiwa ni ikiwezekana ni jaribu la kumfanya mtu aikane imani na akose kumwamini Mungu na neno la Mungu. Majaribu kama hayo wakati mwingine yanaweza kuwa makali sana, mtu akiwa ameahidiwa hilo, ukiikana imani yako, hutateseka na unaweza pia ukapewa thawabu. Thamani kuu ambayo Mungu huweka kwenye mateso na maumivu imeonyeshwa mwanzoni mwa **mst. 38** unaosema wale waliobakia kwenye uamininifu kwenye mateso na maumivu wana kwamba wao ni *"watu ambao dunia haikustahimili kuwa nao."* Sifa hizo hazitolewi kwa mtakatifu awaye yote aliyekutana na mafanikio na baraka kama matokeo ya imani. Hii itafanye sisi kutathmini mitazamo yetu wenyewe kuhusu mateso na imani.

Muhutasari unaohusu mjadala katika **mst. 17-38** (**11:39-40**)

[39]Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; [40]kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

Waebrania 11 inahitimsha kwa kusema. *"[39]Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; [40]kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."* **Mstari wa 39** unaanza kama muhutasari wa mwanzo (**mst. 13-16**) unaanza, kwa kujua kwamba watu inamaanisha wale waliobaki kuwa waaminifu pasipo kujali ukweli kwamba *"hawakupokea ahadi."* Kwamba *"kilicho bora"* ni *"milki bora"* (**10:34**), *"nchi bora"* (**mst. 16**), "*ufufuo ulio bora"* (**mst. 35**). Haya yote yanapatikana tu kwa Yesu Kristo. Ahadi kuu ya Mungu, ambayo haikuwahi kutolewa kwenye AK, ilikuwa ni kuja kwake duniani katika nafsi ya Kristo na kufanya kwa ajili yetu kile ambacho sisi kamwe tusingeweza kufanya. Watakatifu wa AK walimtazamia Kristo, lakini hawakuweza kumpata na hawakuweza kumfahamu kibinafsi kama sisi tulivyo. Matokeo yake, hawakuweza *"kukamilishwa."* Katika **mst. 40**, ambao husema Mungu "alitoa" kitu chema kwa ajili yetu, neno lililotafsiriwa "alitoa" ni *problepromai,* ambalo lina maana

Commented [jm1]: Either translate this if you can or eliminate the word "the" since you do not have it in Swahili

ya "kuona kabla." **Mstari wa 40** unatuambia kwamba, hata wakati Mungu anaanza mpango wake mkuu wa ukombozi, akianzia na Ibrahimu, anatuwazia mema. Hata hivyo, hatujapata kupokea ukamilifu wa yote yaliyopo katika Kristo. Vivyo hivyo kwa watakatifu wa AK, ni lazima sisi tubakie waaminifu na kumtazamia Kristo kwa ajili ya kurudi kwake mara ya pili ndipo kukamilishwa kutakapotokea. Hili linaturudisha nyuma kwenye **Ebr 10:37**, *"Kwa maana bado kitambo kidogo, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia."* In Christ, *"Mungu ametoa kilicho bora kwa ajili yetu"* Sisi sote—AK na AJ wakiwa watakatifu vile vile—wanaweza kufanywa watakatifu "kukamilishwa" kwa pamoja.

C. Namna ya kuitunza imani yetu (12:1-29)

Sura inaendelea kutoka kwenye maana na mifano ya imani inayovumilia katika sura ya 11 na inatutia moyo jinsi tutakavyoishi imani yetu. Tunafanya hivyo kwa kuelekeza shabaha yetu kwa Yesu Kristo, *"mwanzilishi na mkamilishaji wa imani."* Tunafanya hivyo pia kwa kutambua kwamba hatupo peke yetu. Kanisa ni familia na familia husaidia wa kwao. Matokeo yake, tunatakiwa kukubali kurudiwa na Bwana, hilo hutufanya tufanane na Kristo, kusaidiana kila mtu na mwenzake ili kubaki katika uaminifu, si kurudi nyuma kwenye dhambi, na kwenda nje nje ya "njia iliyonyooka" inayotupeleka kwenye uzima.

Kuna tofauti kadhaa za kufurahisha kati ya sura ya 11 na ya 12: sura ya 11 inahusisha viashiria tu; sura ya 12 inabeba sheria na inatia moyo. Sura ya 11 karibu yote ni kama inaongea na nafsi ya tatu (yeye, wao,); sura ya 12 kwa ujumla ipo katika nafsi ya kwanza (mimi, sisi) na ya pili (wewe, yako). Sura ya 11 ni ya kihistoria zaidi, kuhusu wakati uliopita wa Waisraeli, sura ya 12 inahusu mambo ambaye ambayo wakristo wanakumbana nayo katika wakati uliopo.

1. Ni lazima tuweke kando kila kitu kituzingacho njiani, kukaza mwendo hata mwisho, tukimtazama Yesu (**12:1-3**).

[1] Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, [2] tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. [3] Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu.

"Kwa hiyo," ambayo huanza katika sura hii, inaonesha sura ya 12, ni mwendelezo na imeunganika na sura ya **10:32-39** na sura ya 11. Katika **10:32-39**, wasomaji wanatiwa moyo kukumbuka siku zao za mwanzo za imani yenye kuvumilia na wasirudi nyuma. Sura ya 11 inatoa maana na kuelezea imani na pia inatoa mifano ya imani ya watakatifu wa AK, na wengine wa wakivulia hadi kufa. **11:39-40** kisha inatoa mwelekeo unaotuingiza kwenye sura ya 12, ikijikita katika umakini na kuhama kutoka *"wao"* na kuja kwenye *"sisi"* Sasa, sura ya 12 inatutia moyo, kwa nuru tunayopata kutoka kwenye mifano ya imani inayovumilia ya watakatifu wa AK, kujikita sisi wenyewe katika imani inayovumilia. Hata hivyo, misingi ya imani yetu inayovumilia siyo imani ya watu wengine bali ni mfano wa Yesu Kristo, aliye mmoja mwaminifu kupita wote. Sisi tumezungukwa na *"wingu kubwa la mashahidi."* Haina maana wanatutazama au wanashuhudia kile tunachofanya, kama vile mashabiki uwanjani. Mfano huo unaweza ukawa kwa mtazamo kwamba, kwa kuwa **mst. 1** unaongelea kwa habari ya sisi kukimbia mbio iliyowekwa mbele yetu, kama vile tunashindana kwenye riadha. Hata hivyo neno "mashahidi" ni *marturōv,* kutoka hapo tunapata neno "wafia imani." Kwa hiyo, msisitizo ni kwa tendo la wao kuwa ,mashahidi waaminifu kwa ajili ya kristo. Ushahidi wao wa uaminifu kwetu ni kielelezo na muhimu iwe hamasa kwetu. Lakini kama mstari wa **2** unavyosema, macho yetu ni lazima yawe yameelekezwa, siyo kwa wingu kubwa la mashahidi, lakini kwa YESU. Yeye ni *''shahidi mwaminifu''* wa pekee. (**Ufu 1:5**). Alitupa imani yetu (**Efe 2:8-9**) na ataikamilisha (**Flp 1:6**). Kama tukimshika Yesu—amabaye ni, kile alichofanya, na kile anachokuja kufanya—kama kipaumbele katika fahamu zetu, na kumkaribia kwa neno na kwa Roho wake, tutaweza kuvumilia hadi mwisho. **Mstari wa 2** (*"na kuketi mkono wa kuume wa enzi wa Mungu"*) inahusu **Zab 110:1**. Tunapoelekeza macho yetu kwa Yesu, ni muhimu kwetu kukumbuka kwamba yeye ni *"yupo mkono wa kuume wa enzi ya Mungu,"* kwa sababu *"aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee."* (**Ebr 7:25**). **Mstari wa 2** unatuonyesha kuwa *kushushwa* kwa Yesu ni kielelezo kikuu kwetu sisi cha uvumilivu na kustahimili; Yesu *aliyepo enzini* ni mdhamini wetu mkuu kwa ajili ya kutukuzwa kwetu hatimaye.

Kifungu hiki kimewekwa ili kututia moyo na kutuonya kwa uhalisia tukiwa katika safari ya maisha. Kama **mst. 1** unavyotukumbusha, sisi kwa hakika tunakimbia *"mbio imewekwa mbele yetu"* (na Mungu). Tunatakiwa *"tukimbie kwa uvumilivu,"* kama mifano katika sura ya 11 ya wale ambao imani yao ilivumilia inavyotueleza. Ili

kukimbia kwa uvumilivu, ni lazima *"na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi."* Zingatia kuwa **mst. 1** inaeleza tofauti kati ya "vikwazo" na "dhambi." "Vikwazo" vyetu si lazima viwe dhambi zetu. Vikwazo vinaweza kuwa dhambi, lakini kwa ujumla ni mambo yote ya Maisha mabayo yanweza kuchukua muda wetu mwingi na juhudi zetu na kutupindisha na kutufanya tuache *"kumtazama Yesu."* Hivyo vikwazo vinaweza kuwa kazi zetu, fedha, tamaa zetu za kupata mafanikio, yaani, yote yale ambayo kwayo tunaishi. Yanaweza kuwa *mazuri* na *muhimu* ambayo tunayafanya kuwa ya *muhimu sana* kwetu na kuwa *kipaumbele cha kwanza* kwetu.

Dawa ni *"kumtazama Yesu"* na *"kumzingatia yeye"* kwa sababu *"mwanzilishi na mkamilishaji wa imani."* Msemo huo una uzito sana. Unaonyesha Yesu alitembea kikamilifu safari ya imani yeye mwenyewe, na kuikamilisha, kama ilivyoelezwa katika sehemu iliyobaki ya **mst. 2**. Pia inaonyesha kwamba Yesu alianzisha imani yetu na ataikamilisha, kama ilielezwa katika **Flp 1:6** (*"Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu"*). Lakini kwa kuongezea, inaeleza kuwa hata kwa kupitia Yesu, mashujaa wa imani katika sura ya 11 walipangwa kwa kufuata kronolojia, yeye ndiye aliyehamasisha imani yao. Hiyo ndio maana Ibrahimu alikuwa akitazamia (**Ebr 11:10**) na kama Yesu alivyosema, *"Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi"* (**Yoh 8:56**). Zaidi ya hilo, watakatifu wa AK, ingawa hawakupokea ahadi, *"bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia,"* (**Ebr 11:13**).

Maneno *"tumtazame"* na *"zingatia"* ni muhimu. "Kumtazama" (*aphoraō*) ni muundo wa kitendo wenye uzito "tazama," inamaanisha kutazama "kwa umakini na kumaanisha" na, kwa lugha ya ishara, "kutazama akilini, Kuelekeza akili kwa jambo hilo" (Zodhiates 1993: *aphoraō,* 302). To "zingatia" (*analogizomai*) maana yake "kukumbuka, fikiri. Kuzingatia kwa usahihi na kipekee au tena na tena'' (Zodhiates 1993: *analogizomai,* 154). Kwa kifupi, jinsi tutakavyoweza kuvumilia kwa mafanikio na kupiga mbio ya Maisha yetu ni kuwa na Yesu mara zote kama aliye na thamani kuu na kumwaza kila wakati katika fahamu zetu. Frank Laubach, mmishenari aliyeheshimika sana huko Filipi, aliyeanzisha mpango wa kufundishana wa Kila mmoja, amfundishe mmoja, iimejadiliwa hili litafanyika. Mpango wake una sehemu mbili. Kwanza, tunapaswa kusoma na kusoma tena Maisha ya Yesu yaliyorekodiwa kwenye Injili tena na tena kwa kutafakari sana na kwa maombi saa moja kwa siku. Kwa hiyo tunatembea na Yesu kupitia Galilaya kwa kutembea naye kwenye kurasa zinazoelezea maisha yake ya hapa duniani." Pili, alikuja na "Cheza na Dakika." Ndani yake, tunamfanya Kristo: "Tunajaribu kumwita akilini aingie kwa dakika moja kila baada ya muda. Hatuhitaji kusahau kila kitu, wala kuyaacha kufanya kazi zetu, lakini tunamwalika ashiriki yote tunayofanya, tunayosema na kufikiri" (Laubach 2007: 89) Laubach alisema kwamba, hii shughuli "ni shughuli ya muhimu ambayo hakuna mtu aliyewahi kujaribu"; isifanyike kwa ukamilifu, bali aligunda kuwa, kiwango cha mafanikio, ni, nafikiri kwa urahisi zaidi, na usahaulifu unapungua sana. Mambo niliyofanya hapo zamani kwa kusumbuka sana, Sasa nayafanya kirahisi na kwa nguvu kidogo. . . . Nami ninashuhudia kwa namna ambayo dunia inatoa mwitiko." (Laubach 2007: 35, 32-33) Rebecca Pippert ana mawazo yanayofanana na "kuanza kusoma Biblia kila siku, kila mara na unavyozidi kusoma, kuna kitu bila shaka kitakugonga na hisia zitaanza kuwa sawa. Kwa vyovyote vile, fanya mapema iwezekanavyo" (Pippert 1979: 97) Ni kuanyia kazi kile kitakachoweza kukuamsha na kukufanya uweze kudhihirisha uaminifu na tumaini kwa Yesu.

"Kwa kutomtazama Yesu" na kutomzingatia, na kutofanya hayo *"kuweka" pembeni kila mzigo mzito na dhambi ituzingayo kwa upesi,''* Mwishoni matokeo yanaeleza hivi, **mst. 4**, *"Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi."* Yesu alimwaga damu katika kushindana na dhambi. Alishinda dhambi muda wote mpaka mwisho. Ili kuangaza mwanga wa Kristo sawa sawa, ni lazima kuikaribia nuru ya Kristo, ya mamlaka na nguvu, tukimweka kwenye akili zetu. Tukifanya hivyo, sisi pia tutaweza kukimbia kwa uvumilivu, usichoke, usikate tamaa lakini pia, kimbia pasipo shaka na kwa ushindi.

2. Ni lazima tukubali kurudiwa na Bwana (**12:4-11**).

[4]Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi; [5]tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana, Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, Wala usizimie moyo ukikemewa naye; [6]Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye. [7]Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye? [8]Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali. [9]Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi? [10]Maana ni hakika, hao kwa siku chache waliturudi kama walivyoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. [11]Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani.

Sehemu hii inaweza kugawanywa katika sehemu mbili: **Mistari ya 4-8** unahusu uana. **Mistari ya 9-11** Inatofautisha nidhamu ya kibinadamu na nidhamu ya kiungu. **Mstari wa 4** is ni wa mpito, unamalizia wazo la mstari wa 1-3 kwa kudokeza kuwa imani inayovumilia ina gharama, hata kufikia kiwango cha kumwaga damu. Lakini mstari wa **4** pia unatuongoza kwenye somo la majaribu ya imani, ambayo Mungu hutupatia kwa njia ya majaribu ya imani yetu, ambayo Mungu anatupatia katika mfumo wa nidhamu. Majaribu ni mepesi ukilinganisha na kile ambacho Yesu alivumilia, kwa sababu, tofauti na Yesu—ambaye *"jasho lake likawa damu"* kwenye bustani ya Getsemane (**Lk 22:44**), na aliyemwaga damu yake kwa wingi alipokuwa msalabani—sisi hatujamwaga damu katika kupambana kwetu na dhambi *ile itunasayo kwa wepesi* (**mst. 1**).

Somo la nidhamu ya kiroho inatambulishwa hapo kwenye **mst. 5-6**, ambayo inanukuu **Mit 3:11-12**. Linafafanuliwa tena katika **mst. 7-11: mst. 7-8** inaonesha kwamba nidhamu ya kiroho inatutambulisha sisi ya kuwa tu Watoto wa halali wa Mungu; **mst. 9** unaonesha mwitikio wetu wa nidhamu ni lazima uwe heshima kwa ufalme wa Mungu Baba, kama ambavyo tungefanya kwa baba zetu wa mwili; na **mst. 10-11** unatueleza kusudi la nidhamu ya kiroho ni kutufikisha sisi kwenye utakatifu; nidhamu hiyo inatueleza kwamba Mungu "*hutunidhamisha sisi sisi kwa ajili ya mema yetu, ili tuweze kuwa watakatifu kama yeye na inazaa tunda la amani la haki"* Nidhamu ambayo inaelezwa inaweza ikahusisha aina yoyote ya mateso, magumu, au maumivu. Kipekee kwa kuwa nidhamu imeunganishwa na wazo la kwamba ni riadha (**mst. 1**), inayohitaji mafunzo na nidhamu ya kufanikiwa—kwa kuangazia juu ya nani anatupatia hiyo nidhamu, kusudi na matokeo yake—nidhamu tunayoongelea haihusiki na kuumiza, lakini kazi yake ni kuelimisha na kutufunza. Mateso na magumu, kwa hiyo, siyo lazima iwe ni ishara ya kuadhibiwa au kukosa kwetu imani. Badala yake, ni ishara ya kuhusika kwa Mungu kwenye Maisha yetu kwa njia ya Kristo. Kwa sababu hizo, nidhamu hiyo inaweza pia kufurahiwa (**Rum 5:3-5; Yak 1:2-4; 1 Pet 3:14; 4:14**). Yote haya, tena yanatuonyesha umuhimu wa kumwelekezea Kristo macho yetu, siyo tu kupitia hali zetu za nje tu.

Sote tunajaribiwa kugeuka kutoka kuendelea kujitoa kikamilifu kwa kristo, hasa tunapokuatana na mambo magumu na mateso. Nyakati hizo, tunatakiwa kuelekeza macho yetu kwa Kristo, na kutilia maanani kufufuka kwake na kielelezo alichotupa. Tunatakiwa kuwaza kuhusu uwepo wake ulio ndani yet una mabadiliko makubwa aliyofanya ndani yetu. Tunatakiwa kukumbuka vile mbio yetu ilivyo fupi na furaha kuu isiyo na mwisho na thawabu ambayo ni yetu ikiwa tutabakia waaminifu sasa. Mwisho tunatakiwa kukumbuka mambo hayo hayo—hali zetu, magumu, na mateso—yanataka kutufanya tutamani kugeuka nyuma ni mambo hayo hayo ambayo Mungu huyatumia katika Maisha yetu ili kutukuza na kutufanya tunafanane na Yesu.

3. <u>Ni lazima tuwasaidie ndugu zetu katika Kristo (**12:12-17**).</u>

[12] Kwa hiyo inyosheni mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza, [13]mkaifanyie miguu yenu njia za kunyoka, ili kitu kilicho kiwete kisipotoshwe, bali afadhali kiponywe. Maonyo dhidi ya Kukataa Neema ya Mungu [14]Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao; [15]mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo. [16]Asiwepo mwasherati wala asiyemcha Mungu, kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. [17]Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa (maana hakuona nafasi ya kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi.

Neno "kwa hiyo" inayoanza katika sura hii, inaunganisha sehemu hii na kile kilichosemwa kuhusu kushindana na dhambi hata ikibidi kumwaga damu na kuwa tayari kwa ajili ya kunidhamishwa na Mungu. Inatuambia kwamba sisi kushindana na dhambi siyo jukumu letu wenyewe. Hata kufurahia kurudiwa na Bwana kama ishara ya yeye kuhusika katika Maisha yetu na pia kama kichocheo cha kukuza tabia za kiungu na kukuza ukaribu na Mungu siyo jambo la mtu mwenyewe peke yake. Bali kwa sababu kanisa ni familia sisi tumeunganishwa kwa karibu sana na ndugu zetu kaka na dada katika mwili wa Kristo. Kwa hiyo sehemu moja ya sisi kupingana na dhambi ni kuwatia nguvu na kuwatia moyo wengine katika mapamabano yao dhidi ya kushinda dhambi na kufurahia kurudiwa na Mungu. *"Mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza"* inawakilisha hali ya kukata tamaa katika imani. **Mstari wa 12**, tunapotiwa moyo kwa maneno haya; *"inyosheni mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza,"* ni mwanwi wa maneno ya Elifazi kwa Ayubu katika kitabu cha **Ayu 4:3-4** (*"[3]Tazama, wewe umewafunza watu wengi, Nawe umeitia nguvu mikono iliyokuwa minyonge. [4]Maneno yako yamemtegemeza huyo aliyekuwa anaanguka,*) na **Isa 35:3**, (*"Watie moyo waliochoka [lit. 'mikono iliyolegea], watie nguvu wenye migoti yaliyolegea [lit. 'magoti yanayotetemeka]"*). Maneno ya kutiwa moyo katika **mst. 13** *''fanyia miguu njia iliyonyooka''* ina maana kwamba tunapaswa kuwasaidia ndugu na dada zetu kuchagua njia sahihi na kutulia kwenye njia sahihi, bila kujali ugumu wanaopitia ukoje.

Mstari wa 13 unaturejesha kwenye **Mit 4:26** (*"Ulisawazishe pito la mguu wako, Na njia zako zote zithibitike"*). Baadhi ya ishara za maana ya*"njia zilizoonyooka"* zinapatikana kwenye **mst. 14-16**. Kwenye **mst. 14** tumeambiwa *"tafuteni amani na watu wote" na* kuwa na *"utakatifu ambao pasipo huo hakuna mtu atakayemwona Bwana."* "Amani" tunayotafuta siyo "amani kwa gharama yoyote." Bali ni, amani ambayo inaenda sambamba na utakatifu. Amani haitokei hivi hivi; ni lazima itafutwe. Hiyo ina maana kwamba amani inayoongelewa siyo tu kule kukubaliana tu na adui ili kuepuka ugomvi lakini ni amani ya kweli, amani ya kudumu. Aina hiyo ya amani inaweza kupatikana kwa Kristo (**Yoh 14:27; 16:33; Mdo 10:36; Rum 5:1; 2:14; Kol 3:15**) kwa njia ya Roho Mtakatifu (**Rum 8:6; 14:17; Gal 5:22; Efe 4:3**). Hii ni aina pekee ya amani ambayo inaweza kuwaunganisha watu pamoja katika uhusiano wa kina sana na ni amani pekee ambayo inadumu. Ni kwa kumtazama Kristo tu—kwa kuwa na moyo wake (**Ezek 36:36**), kutumia nia yake (**1 Kor 2:16**), na kutembea kwa Roho wake (**Gal 5:16**)—tunaweza kupata hii amani ya kweli, inayodumu na *"na watu wote"* (**mst. 14**). Zaidi ya hilo, **mst. 15-16** unaongeza, *"Tazameni mmoja wenu asiipungukie neema ya Mungu"* na hakikisheni *"hayupo mtu asiye na maadili au asiye na Mungu kama Esau"* miongoni mwenu. Machozi ya Esau yalionyesha majuto kama matokeo ya kitendo chake cha hamaki, lakini hayakuwa huzuni ya kimungu ambayo inamwongoza mtu kubadilika moyo ambayo husababisha maamuzi ya kugeuka mbali na dhambi na kuwa na Maisha yaliyobadilika yanayodhihirisha matunda ya toba ya kweli (**Mt 3:8; 2 Kor 7:10**). Tena, wanaojadiliwa hapa ni watu ambao, wapo ndani ya Kristo na wamevua utu wa kale na wamevaa utu mpya (**Efe 4:22-24**). Katika mistari hii, maonyo mawili au maneno ya kutia moyo (**mst. 14**) ni "chanya," yaani., ni sifa ambazo mwili wa Kristo unatakiwa uwe nazo na zionekane. Maneno mengine ya kutia moyo (**mst. 15-16**) ni "hasi," yaani., sifa ambazo mwili wa Kristo haupaswi kuwa nazo wala kuzionyesha. Yote mawili chanya na hasi ambayo ni maonyo au tahadhari zinaakisi **Zab 34:14**, inayosema, *"Acha uovu utende mema; tafute amani uifuate."* Maneno ya kututia moyo, kuhimiza kwa mara nyingine tena yanaonyesha kwamba sisi ni mwili, tunahitaji kumtazama Kristo tu na tunahitaji kuwa pamoja katika umoja ili sote tuweze kubakia katika "njia iliyonyooka."

Katika **mst. 15**, *"shina la uchungu"* inarejea **Kum 29:18** (''*Asiwe mtu katikati yenu, mume wala mke, wala jamaa, wala kabila, ageukaye moyo wake leo amwache BWANA, Mungu wetu, kwenda kuitumikia miungu ya mataifa hayo; lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga;")* Muktadha uliopo katika Kumbukumbu la Torati ni Musa anahuisha Agano la Kale kabla ya Waisraeli kuingia nchi ya ahadi. George Guthrie anaeleza, "Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatumia lugha hii ya picha kuwatia changamoto wasikiaji wake wasiliache agano jipya lililo kuu ambalo Kristo ametupatia" (Guthrie 2007: 988). Mara nyingine tena, uaminifu—siyo tu wa watu binafsi bali wa jamii yote—kama ilivyohimizwa na kutiwa moyo.

4. <u>Ni lazima kutambua kuwa tayari tumeufikia mlima Sayuni wa kweli na Yerusalemu ya Mbinguni (**12:18-29**).</u>

[18]Maana hamkufikilia mlima uwezao kuguswa, uliowaka moto, wala wingu jeusi, na giza, na tufani, [19]na mlio wa baragumu na sauti ya maneno; ambayo wale walioisikia walisihi wasiambiwe neno lo lote lingine; [20]maana hawakuweza kustahimili neno lile lililoamriwa, Hata mnyama akiugusa huo mlima atapigwa kwa mawe. 2[1]Na hayo yaliyoonekana jinsi yalivyokuwa ya kutisha, hata Musa akasema, Nimeshikwa na hofu na kutetemeka. [22]Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, [23]mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, [24]na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.

[25]Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni; [26]ambaye sauti yake iliitetemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia. [27]Lakini neno lile, Mara moja tena, ladhihirisha kuhamishwa vile viwezavyo kutetemeshwa, kama vitu vilivyoumbwa, vitu visivyoweza kutetemeshwa vikae. [28]Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; [29]maana Mungu wetu ni moto ulao.

Matukio yanayoelezwa katika **mst. 18-19**, na nukuu za **mst. 20-21** na zinahusiana na Mungu kushuka juu yam lima Sinai kumpa Musa Amri kumi (tazama **Kut 19:12-20; Kum 4:11; 19:19**). Hata hivyo, **mst. 22-24** unatuambia sisi kwamba matukio ya mlima Sinai ni "kivuli" au "nakala" kuwakilisha mlima wa kweli wa Sayuni, *"mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu ya Mbinguni,"* na Maisha halisi na uhalisia wa Kiroho wa Kristo mwenyewe (**Kol 2:16-7; Ebr 8:1—10:22**). Katika huduma yake duniani, na baada ya kufufuka kwake, Yesu aligeuza mwelekeo mzima wa nabii za AK. Katika **Zab 2:6, 8** Mungu alitangaza kuwa, *"Nami nimemweka mfalme wangu*

Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu. . . . Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, Na miisho ya dunia kuwa milki yako..” Mwishoni mwa jibu lake kwa wanafunzi wake walipokuwa wameuliza kuhusu kurejesha Ufalme wa Israeli, Yesu aliwaambia waende *“hata miisho ya dunia”* (**Mtd 1:8**). Hilo inarejea kwenye Agizo Kuu (**Mt 28:18-20**), na inaakisi **Zab 2:8,** inayosema kwamba *“miisho ya dunia”* imepewa Ufalme wa Masihi kama urithi wake. Yesu anachukua mawazo ya AK anayaunda upya na kuonyesha maana yake mpya ya ufalme: “Kwa agizo hili la Yesu la kuwataka wanafunzi waende kwa mataifa yote hadi miisho ya dunia, kuwaona kinabii mataifa wakienda Yerusalemu (Isaya 2:2-5, Mika 4:1-5; Zekaria 8:20-23) inaondolewa na uhalisia wa wamishenari wa kiyahudi kwenda kwa mataifa. Mwondoka uliotarajiwa wa watu kutoka pembezoni kuja katikati umerekebishwa kwa kuwepo utume unaotoka katikati (Yerusalemu, mahali Yesu alikufa na kufufuka kutoka kwa wafu) kwenda pembezoni (miisho ya dunia).” (Schnabel 2002: 47) Wakati Agano la Kale likiwa bado hai, hata wakati wa huduma ya Yesu ya duniani, Yerusalemu ilikuwa inaitwa “mji Mtakatifu” (**Isa 48:2; Dan 9:24; Neh 11:1, 18; Mt 4:4; 27:53**). Hata hivyo baada ya Yesu kufufuka “neno ‘mji mtakatifu’ halitokei tena, kwa kuwa alianza kuishi ndani ya Kanisa siyo Yerusalemu, na siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu hakujaza hekalu wala Yerusalemu bali aliwajaza mitume na wale wote waliotubu na kubatizwa (Mtd 2:1-4, 38-39)” (Kistemaker 2000: 437).

Kuja kwa Yesu mara ya kwanza kulianzisha ufamle wa Mungu wa siku za mwisho. **Ebr 12:18, 22** kwa hiyo inahitimisha kwa kusema kwamba katika Kristo sisi ‘’*hatukufikia mlima usioweza kuguswa…bali tumeufikia mlima Sayuni mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu ya Mbinguni”* (pia tazama **Gal 4:21-31**). Wakati mstari wa **22** unasema kwamba neno *“tumeufikia,”* lipo katika wakati uliotimia. Hiyo inaelezea kwa yote uliokamilika na ambao bado haujakamilika na ambao unaendelea. Rejea kwa *‘’kanisa la wazaliwa wa kwanza”* (**mst. 23**) unaonyesha “mahali pa upendeleo pa watakatifu kama waliotengwa kwa ajili ya Mungu (Kutoka 4:22; 13:2) na warithi wa vitu vyote” (Rayburn 1989: 1147). Kuna jambo la ajabu hapa: Ufalme wa Mungu na Utawla Kristo umeanzishwa rasmi, unatenda kazi kikanuni, na upo sasa (Ufalme ulio “tayari”) hata hivyo, hizo falme mbili hazifunuliwa wazi kikamilifu bado, bali ukamilifu wa utukufu wake wote unangojwa (Ufalme ambao bado) Kwa sasa, mema na mabaya yapo pamoja, lakini utakuja wakati wa mavuno na kutenganishwa kwa mema na mabaya. Baadhi ya mifano ya Yesu, kama mfano wa ngano na magugu (**Mt 13:24-30, 36-43**) na mfano wa nyavu (**Mt 13:47-50**), inaongea kuhusu hali mbili za ufalme. Kwa hiyo waamini wameshafika Yerusalemu ya Mbinguni (**Ebr 12:22**), ulio kamili, usio na upungufu, uwepo wa utukufu wa Yerusalemu mpya utakuwa baadaye (**Ufu 21:10-11**).

Kwenye **mst. 24**, rejea iliyofanywa kwa damu ya Yesu inayonena *“kuliko damu ya Habili,” inaonyesha kwamba* Habili pia alikuwa mfano wa Kristo. **Mstari wa 25** unatuonya kuwa *“usimkatae Yeye anenaye. . . anayeonya kutoka Mbinguni.”* Kimuktadha, hii inasema kuhusu Yesu, kwa kuwa **mst. 24** unasema kwamba yeye ni *“mpatanishi wa Agano Jipya, na damu ya kunyunyizwa, ambayo hunena mema kuzidi damu aya Habili.”* Zaidi ya hayo, **mst. 25** unasema kuhusu Yesu ambaye alianza kutuonya duniani na sasa anatuonya kutoka Mbinguni.*”* Kama **Efe 1:21** inavyotukumbusha. Yesu amekiti mkono wa kuume wa Baba, *“juu sana kuliko falme na mamlaka na ufalme na kila jina liitwalo, si ulimwenguni humu bali na ujao pia* (pia tazama **Zab 110:1; Mdo 2:32-36**).

Mstari wa 26a unaanza, *“Na sauti yake ilitikisa dunia wakati ule.”* Hiyo inawezekana ni maelezo ya kile kilichotokea kwenye mlima Sinai wakati Mungu anashuka mlima Sinai katika **Kut 19,** kama ilivyojadiliwa katika sura hii **Ebr 12:18-21**. **Mstari wa 26**, Mungu akaendelea kusema, *“Mara nyingine tena nitatikisa si dunia tu bali na Mbingu tu.”* Nukuu hii inatoka **mst. 2:6**. Muktadha wa asili wa Kitabu cha Hagai ni ujenzi wa Hekalu baada ya kutoka uhamishoni. Ni mtikisiko aliofanya Mungu ambao unahusisha kuwaita Wana wa Israeli kutoka kwa mataifa na uharibifu wa falme za kidunia kama vile Misri na Wakanani. Yote hayo, hata hivyo, ni kivuli cha hekalu la kweli (Kristo) na ufalme wa kweli wa kiroho (kanisa). Tukiachana na kutiswa kwa dunia na kutikiswa kwa mbingu inaonyesha kwamba mtikisiko huo unaokuja utahusisha kosmiki yaani anga litatikiswa. Maelezo, *‘’Mara nyingine tena’’* katika **mst. 27** unahusu mwishoni. Kwa hiyo, kutikiswa unahusu **mst. 26** utatokea pamoja na tukio la kuja kwa Yesu Kristo kwa mara ya pili. **Ufu 6:12-17; 16:17-21; 19:11-21**; na **20:9-11** yote hueleza kuhusu kutikiswa kwa anga na zoezi lake la kuhukumu mataifa. Katika **Ufu 6:12-14; 16:18-20**; and **20:11** kuharibiwa kwa hali ya anga ipo wazi itatokea. Kwenye **Ufu 19:11-21** ni wazi kabisa kwa sababu ya ‘’hasira’’ ya watu wake (**19:15**; linganisha **6:16; 16:19**). **Mstari wa 27** inaelezea kuwa huu mtikisiko na ile hali unahusu *“kuondolewa kwa viwezavyo kutikiswa, kama vile vitu vilivyoumbwa, ili kwamba vitu vile ambavyo havitikiswa viweze kubaki.”* **Mstari wa 28** unasema kwamba *“tumepokea ufalme ufalme usiotikiswa.” Kwa maneno mengina Ufalme wa Kristo ambao sisi ni sehemu yake* una usalama wote. Ni ufalme wa kiroho, ulio na misingi ya milele, na wenye uhusiano ulio salama pamoja na Mungu ambao unavumilia masumbufu na majaribu ya Maisha. Matokeo yake, waamini ni lazima wasimame imara katika imani yao, wakiunganisha na Kristo kuliko kutegemea usalama wa kidunia. Kama alivyosema Paulo katika **Rum 8:38-39** *“wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.”*

Kwa kutazama yale ambayo Mungu atafanya Kristo atakaporudi, tunatiwa moyo *“na mwe na neema,*

ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho" (**mst. 28**).[32] Shurani zetu kwa Mungu kwa neema kuu aliyotumwagia lazima itupekee kuwa na mtazamo wa *"heshima na kicho"* kwa Mungu, ambayo matokeo yake ni kwa na *"utumishi unaokubalika"* kwa jina la Mungu na kwa Roho wake kwa wengine. Kwa maneno mengine, tunatakiwa kuvumilia kwa imani; imani inayovumilia itajidhihirisha yenyewe tunavyoishi. **Mstari wa 29** unaongeza kwenye hili onyo kama sababu ya zaidi kwa nini tuvumilie katika imani, *"kwa maana Mungu wetu ni moto ulao."* Maelezo hayo ni sawa na **Kum 4:24**. Kama Leon Morris anavyoeleza, "Ni rahisi kubweteka kwa ajili ya upendo wa Mung una huruma zake tukapuuza jinsi anavyopinga kabisa uovu wote. . . . Mwandishi anakazia hili kwa wasomaji wake kwamba wakipuuza hasira ya Mungu ni uangamivu wao." (Morris 1981: 145) Maonyo kipekee ni sahihi kwa kuwa kanisa linakumbana na majaribu yale yale ya uaminifu kama yale ya Waisraeli wa AK wa kimwili. Sisi kama Israeli wa kiroho, mpya na wa kweli, kanisa limeitiwa kuulinda utakatifu wao mbele za Bwana. "Kwa kumtazama Yesu Kristo kama utimilifu wa uhusiano wa kiagano, Agano Jipya linaweza kutatua ule ugumu uliokuwepo kwenye AK kati ya 'ukarimu na ukali wa Mungu', kama Paulo anavyosema katika Rum 11:22. Israeli walikutana na yote mawili: Ukarimu wa Mungu ambao kwa huo wakafanyika Israeli kabisa, na ukali wake kwa huo walibakia kama 'Yakobo' asiyekombolewa. Na sasa kwa kuwa ni Yesu, na wala siyo kanisa anayetimiza uhusiano wa kiagano, kanisa hukumbana na matakwa ya kimaadili yale yale kama Waisraeli walivyokuwa, kufisha chochote cha kidunia kilicho ndani yako, tamaa ya mwili, kutokuwa safi, tamaa, tamaa mbaya, kutamani ambayo ni ibada ya sanamu 'vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu' (Kol. 3:5, tafsiri ya mwandishi). Paulo alijua kwamba dhambi ya ibada ya sanamu iliwasumbua Israeli kwa kanisa inaweza kuwa tatizo pia, unafiki, kama ilivyokuwa mara zote, tamaa inayopitiliza ambayo siyo kwa ajili ya kumpenda Mungu. Kanisa huishi katika mvutano huo kati ya Yakobo na Israeli ndani yao wenyewe mpaka ukombozi wa mwisho utakapokuja (Rum. 8:23, *nk.*)." (Motyer 2000: 596) Tutakapoweka pembeni kila kitu kituzingacho kwenye njia yetu na kukaza mwendo mpaka mwisho, tukimkazia Yesu macho yetu (**12:1-3**), tukikubali kurudiwa na Bwana (**12:4-11**), tukiwasadia kaka na dada zetu katika Kristo (**12:12-17**), na kutambua ya kwamba tumeshaufikia mlima Sayuni wa kweli na Yerusalemu ya Mbinguni (**12:18-29**), tutavumilia katika imani ya kweli na tutakuwa tukimtolea Mungu *"ibada inayokubalika kwa heshima na kwa kicho."*

D. Maelekezo ya mwisho ya kuendea kazi (13:1-19)

Waebrania 12 inamalizia kwa maneno ya kutia moyo, *"na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; maana Mungu wetu ni moto ulao."* **Waebrania 13** sasa inatupatia njia za kiutendaji, *"ibada yetu yenye kupendeza"* inaonekanaje. Inatuonyesha jinsi ya kuiweka imani yetu kwenye matendo katika Maisha ya kila siku katika maeneo yote makuu ya Maisha—Maisha ya kijamii, Maisha yetu ya binafsi, na Maisha yetu ya kidini—ikiwa ni pamoja na mahusiano yet una waumini wengine pamoja na wageni, kuwajali wafungwa, na watu walioonewa, ndoa, fedha, uongozi wa kanisa, uhusiano wetu na Mungu na maombi.

1. <u>Maelekezo kuhusu Maisha ya kijamii (**13:1-3**).</u>

[1]Upendano wa ndugu na udumu. [2]Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua. [3]Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili.

Kristo anatoa muhutasari wa Biblia nzima kwenye amri mbili, *"[37]Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. [38]Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. [39]Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. [40]Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii."* (**Mt 22:37-40**) Paulo alisema kwamba *"sheria yote hutimia katika neno moja, lililopo kwenye sentensi hii, "Mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Gal 5:14**). Matokeo yake **Waebrania 13** inaanza na upendo: upendo kwa ndugu zetu katika Kristo: ukarimu kwa wageni; na kuwajali wafungwa na walioonewa. Hii inaakisi kile Yesu alichosema kuhusu hukumu *"[34]Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, 'Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; [35]kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni,*

[32] Msemo *"na tuwe na neema,"* kiuhalisia ina maana *"tuwe na neema."* Ikitafsiriwa neno kwa neno, maana yake itakuwa tuishike ile neema ambayo Mungu anatupatia, kwa sababu ni kwa neema tunaweza kutumika kama tunavyohitajika. Kwa kutambua ni kwa kiwango sisi tumepokea neema yake, heshima na kicho chetu kwa Mungu itaongezeka.

mkanikaribisha; [36]nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.'" (**Mt 25:34-36**)

Mstari wa 2, neno lilitofasiriwa "ukarimu" ni *philoxenia,* ambalo kiuhalisia maana yake ni "upendo kwa wageni." Kuwakarimu malaika pasipo kujua inatukumbusha juu ya Ibrahimu (**Mwa 18:1-8**) na Lutu (**Mwa 19:1-3**). Ingawa tunaweza kukutana na kaka na dada zetu na wageni kwa bahati tu au katika hali ya kawida ya shughuli za Maisha, wafungwa na waliioonewa kwa ujumla ni lazima kuwafikia walipo au kuwatafuta. Richard Wurmbrand, amabaye yaye mwenyewe alivumilia miaka mingi ya kuwa gerezani katika nchi ya Romania kwa sababu ya imani yake anatukumbusha, "Mara zote unapokutana na mtu aliyepo kwenye mateso, usije ukasema imani yake ni dhaifu. Unatakiwa ustaajabie ya kwamba amewezaje kubaki na imani pamoja na yote anayopitia. China, Laos, Korea ya Kusini, na ulimwengu wa Waislamu, Wakristo wanakaa gerezani mahali ambapo imani inaweza kumomonyolewa na kuzimwa. Wanahitaji uelewa wako na upendo. Watakatifu wa Agano Jipya walihubiri wakiwa wafungwa gerezani. Wakumbuke wafungwa waliopo gerezani leo. "Vaa uhusika wao na uombe kwa ajili yao." (Wurmbrand 1998: 10) Yote yanayodhihirisha huruma ya Kikristo na upendo kwa ajili ya wengine ni mchakato unaohusisha wote kwa vitendo na huo unapaswa kuzingatiwa kwenye maisha yetu na uwe ndio utambulisho wetu.

2. <u>Maelekezo kuhusu maisha ya kibinafsi (**13:4-6**).</u>

[4]Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu. [5]Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, ''Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.'' [6]Hata twathubutu kusema, ''Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; Mwanadamu atanitenda nini?''

Mungu aliiasisi ndoa (**Mwa 2:24; Mt 19:4-6**). Mahusiano katika ndoa, hususan katika kipengele cha kushiriki tendo la ndoa, ni uhusiano wa ndani sana ambao wanadamu wanaweza kuwa nao. Unafananishwa na uhusiano wa Kristo na Kanisa (**Efe 5:31-32**). Kwa hakika, Kristo ''anaitwa bwana arusi'' (**Mt 9:15; 25:1, 5, 6, 10; Mk 2:19-20; Lk 5:34-35; Yoh 2:9; 3:29**), na kanisa linaitwa "bibi arusi" na "mke" wa Kristo (**Ufu 21:2, 9**). Ukaribu uliopo kwenye mahusiano katika ndoa ni taswira ya uhusiano kati ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Matokeo yake, **mst. 4** unaanza kwa kusema *"Ndoa na iheshimiwe na watu wote."*

Kulingana na Biblia, tendo la ndoa linatakiwa kuwa katika muktadha wa uhusiano wa ndoa ya mke mmoja au mume mmoja wa kudumu(yaani, Maisha yote). (tazama **Mwa 2:24; Mt 19:4-6; 1 Kor 7:1-2, 8-14, 36; 1 Tim 3:2; 5:9, 11, 14; Tito 1:6; Ebr 13:4**). Kwa hiyo **mst. 4** unaendelea kusema *"na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu."* Biblia inakataza aina zote za mahusiano ya kingono yaliyo nje ya ndoa (**1 Kor 6:18; 2 Kor 12:21; Gal 5:19; Efe 5:3; Kol 3:5; 1 Thes 4:3-5; Ebr 13:4**). Hii inahusisha: tendo la ndoa kwa wasiooa (uasherati) (**Kum 22:13-21; 1 Kor 7:2, 8-9; 1 Thes 4:3**); tendo la ndoa kwa watu waliopo kwenye ndoa wanaposhiriki na watu ambao si wenzi wao katika ndoa (uzinzi) (**Kut 20:14; Law 18:20; 20:10; 1 Kor 6:9-10; Yak 2:11**); ukahaba (**Law 19:29; Kum 23:17-18**); Kufanya ngono miongoni mwa jinsia moja (**Law 18:22; 20:13; Rum 1:26-27; 1 Kor 6:9-10**; uhusiano wa kingono kwa ndugu wa damu (**Law 18:6-17; Kum 27:20, 22-23; 1 Kor 5:1**); ubakaji (**Kum 22:23-27**); Kufanya ngono na mnyama (**Kut 22:19; Law 18:23; 20:15-16; Kum 27:21**).

Usafi katika ndoa ni muhimu ana kuliko watu wengi wanavyotambua. Kubakia waaminifu katika ndoa na kuacha kabisa mahusiano kingono nje ya ndoa ni njia ya msingi sana ambayo kwa hiyo tunaonyesha uaminifu wetu kwa Mungu. Biblia inatambua umhimu wa kiroho wa tendo la ndoa na usafi katika ndoa kwa kufananisha ibada ya sanamu, kumwacha Mungu, kutokuwa mwaminifu kwa Mungu, na kuabudu miungu mingine na matendo maovu na uzinzi na uasherati. (**Kut 34:14-16; Law 17:7, 20:4-6; Kum 31:16-18; Yer 3:6-10; Ezek 16:15-22; 23:1-20; Hos 2:2; 4:12; Yak 4:4; Ufu 2:18-22; 14:8; 17:1-5; 18:1-3; 19:1-2**). Katika **1 Kor 6:15-18** Paul warns: *"[15]Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! [16]Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, WALE WAWILI WATAKUWA MWILI MMOJA. [17]Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. [18]Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe."* Katika kifungu Paulo anatuambia hatuwezi kufanya jambo katika miili yetu ambayo haiwezi kuathiri roho zetu. Hii ni kweli kwa watu wote, lakini ni hatari zaidi kwa Wakristo. Sababu ni wkaba tumeungwa na Kristo, kimwili na kiroho. Sisi ni mwili wake (**1 Kor 12:12-27**), na miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Kor 6:19-20**, pia tazama **Yoh 14:16-17; 1 Kor 3:16-17; 2 Kor 6:16**). Matokeo yake, tunapojihusisha na matendo ya kingono nje ya ndoa, ni kama tunamshirikisha Kristo katika matendo hayo. Dhambi ya uzinzi au uasherati ina matokeo mabaya ya kiroho. Kwa upande mwingine usafi wa dhidi ya uasherati na uzinzi inafanya uhusiano na Mungu uwe wazi pasipo kufungwa kwa sababu ya dhambi au kuzimwa (tazama **Isa 59:2; Mal 2:13-16; 1 Thes 5:19**).

Kudumisha usafi kwa kuepuka ngono nje ya ndoa pia ni muhimu sana kwa watu wanaweza kuepuka kupata au kueneza magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono (MZ), yakiwepo VVU/UKIMWI (tazama **Mit 3:1-8; 5:1-11; 7:1-27; 1 Kor 7:34**). MZ na VVU/UKIMWI yanaenea sana duniani kote. Kadiri yanavyoenea, ynajenga usugu hata kuwa vigumu hata pale mtu anapotumia dawa zilizoeleka au zilizopo. MZ na VVU/UKIMWI yanaweza kusababisha maumivu makubwa, gharama za matibabu, ugumba, udhaifu, na kifo. Kwa hiyo kufuata maadili ya Biblia kuwa na maadili ya kutoshiriki tendo la ndoa kabisa nje ya ndoa, inasababisha matokeo mazuri ya kimwili na ya kiroho.

Commented [jm2]: STD stands for sexually transmitted disease. Use the Swahili letters instead

Kutoka kwenye mambo muhimu na kuzingatia ya ndoa na tendo la ndoa, mstari wa 5, huongelea juu ya jambo lenye na muhimu la pesa. Kukosa maadili katika ndoa au kujihusisha na uzinzi na uasherati na tamaa vimeunganishwa pamoja katika Agano Jipya. (**Efe 5:5; Kol 3:5**). Sababu ni kwmba fedha ni ya kiroho vile vile sawa na tendo la ndoa na ndoa. Kwa hiyo katika **2 Kor 8-9**, Biblia inatumia misemo ya kiroho kuelezea kuwasaidia maskini na wahitaji. *charis* kimsingi ina maana ya "neema" inatafsiriwa kama "neema" au "kazi ya neema" katika **2 Kor 8:1, 6, 7, 9, 19, 9:8,** na **14**, inatafsiriwa kama "kibali" katika **2 Kor 8:4**, na kutafsiriwa kama "shukrani" katika **2 Kor 8:16** na **9:15**; *koinonia*, kwa kawaida inahusika na "ushirika" au "kushirikiana," inatafsiriwa kama "kushirikiana" katika **2 Kor 8:4** na inatafsiriwa kama "michango" katika **2 Kor 9:13**; *leiturgia*, kutokana na hilo tunapata neno "liturujia," inatafsiriwa kama "ibada au huduma au utumishi" katika **2 Kor 9:12**; na *diakonia,* maana yake ''utumishi" au "huduma," inatafsiriwa kama "huduma" katika **2 Kor 9:1, 12-13**. Tunachofanya kwa kutumia fedha zetu kinatudhuru sisi kiroho sasa na milele **(Zab 41:1-3; 112:5-6; Mit 19:17; 22:9; Mt 6:3-4; 19-21; 19:21; 25:19-30; Lk 12:33-48; 16:9, 19-31; 19:15-26; Mdo 10:4; Flp 4:17; 1 Tim 6:18-19**). Tatizo siyo fedha yenyewe, bali ni mtazamo wetu juu ya fedha. Mtazamo wet una vipaumbele juu ya umiliki wa vitu yaweza kuwa kiashiria cha muhimu sana ya kutujulisha mtazamo wetu na vipaumbele halisi juu ya Mungu. (pia tazama **Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17**). Kupenda fedha ni jambo ambalo linaweza kutugeuza kirahisi zaidi mbali na Bwana zkuliko kingine. Hatari ya jambo imeonyeshwa kwenye **Efe 5:5** and **Kol 3:5**, mahali ambapo tamaa ya fedha inafananishwa na ibada ya sanamu. Maonyo katika **mst. 5** linalotaka tuwe *"huru kutoka hali ya kupenda fedha"* inaakisi **1 Tim 6:10**, *"Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi."*

Mstari wa 5 unaishia na nukuu kutoka **Kum 31:6; Yos 1:5**, na mstari wa 6 unahusisha nukuu kutoka **Zab 118:6** (**Zab 117:6**, LXX). Nukuu inaonekana ni neno la kutia moyo, ambayo inakazia maonyo yaliyopo kwenye mstari wa 5 yaani *"kutosheka na kile ulichonacho."* Yote mawili kutosheka (**mst. 5**) na uhakika (**mst. 6**) ametoka katika uwepo wa Mungu na kumtumaini. Nukuu katika mstari wa 6 inaendana kabisa na Zaburi **117:6**, LXX. Nukuu katika mstari wa 5 imefungwa, lakini siyo kama mfanano uliopo kwenye **Kum 31:6**; **Yos 1:5**, ingawa Philo wa Alexandria (c. 20 BC-AD 50) alitumia katika moja ya uandishi wake. Kwa hiyo, wengine husema swali limetoka kwenye nakala za toleo la Septuagint ambalo leo halipo (Morris 1981: 147; Guthrie 2007: 992).

3. Mafundisho kuhusu Maisha ya kidini (**13:7-19**).

7 Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza
sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao. 8 Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.
9 Msichukuliwe na mafundisho ya namna nyingine nyingine, na ya kigeni; maana ni vizuri moyo ufanywe imara
kwa neema, wala si kwa vyakula, ambavyo wao waliokwenda navyo hawakupata faida. 10 Tuna madhabahu
ambayo wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake. 11 Maana wanyama wale ambao damu yao
huletwa ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa nje ya kambi.
12 Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango. 13 Basi na tutoke
tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake. 14 Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule
ujao. 15 Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo
jina lake. 16 Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo
Mungu.
17 Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama
watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa
ninyi. 18 Tuombeeni; maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema
katika mambo yote. 19 Nami nawasihi zaidi sana kufanya hayo ili nirudishwe kwenu upesi.

Katika **mst. 7-9**, somo linabadilika na kuwa na uaminifu katika fundisho. **Mstari wa 7** unaturejesha **Ebr 2:3** (*"sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia"*). Zingatia hili, siyo tu mafundisho ya kweli ambayo yanaenda sawa na fundisho, bali pia na uaminifu wa tabia. Yaani *"matokeo ya kitabia"* bila shaka ni kuhusu Maisha ya haki ya

viongozi. *"walionena neno la Mungu kwenu."* Maisha ya uaminifu ambayo yanatakiwa yaigwe, wale waliofundisha Waebrania ambao wameandikiwa kitabu hiki walikuwa wanafuata nyayo za Yesu, ambaye ni *"yeye yule, jana na leo na hata milele''* (**mst. 8**). Maneno ya kutia moyo ya *"kuwakumbuka wale waliowaongoza,"* kutazama mwenendo wao na *"kuiga imani yao"* imeunganishwa na maonyo ya *"kutochukuliwa na mafundisho ya namna nyingine nyingine, na ya kigeni;"* (**mst. 9**). Hii inafanan na maelekezo ya Paulo kwa Tim ya *"uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine"* (**1 Tim 1:3**). Rejea hizi juu ya "moyo" na "vyakula" katika **mst. 9**, na msisitizo katika mistari hii juu ya kudumisha uaminifu wa kweli na kutegemea neema ya Mungu kuliko kulenga aina fulani za vyakula inaenda sawa na mafundisho ya Yesu katika **Mk 7:14-23** kwamba kile kitokacho moyoni ni muhimu sana kuliko kile kiingacho mdomoni (pia tazama **Kol 2:16-17**).

Mstari wa 10 unaanza kwa kugusia kuhusu vyakula ili kutoa wazo la muhimu. Hasa hasa **mst. 10-14** unaonyesha kwamba kuendelea kuabudu kwa kufuata namna ya AK kwenye hekalu la kidunia na kumwabudu Yesu *havina uhusiano.* "Yesu ameanzisha mfumo mpya wa hekalu (unaotumia msemo 'madhabahu') ambao unaenda tofauti na mfumo wa hekalu iliyo kwa mfano wa 'hema' ya kuabudia. Kwa hakika mifumo miwili haina uhusiano: ile iliyokuwepo kwenye mifumo ya awali viliondolewa kwenye mfumo huu mpya ('wale waliokuwa wakihudumu kwenye hema hawana haki ya kula': mst. 10); wale ambao sasa wanamwamini Yesu wnapaswa kujihesabu kuwa hawahusiki na ule mfumo wa zamani ('na twende kwake *nje* ya kambi': mstari wa 13). . . . Hii inalazimisha ufahamu mpya ambao ni tofauti. Kifo cha kilikuwa 'nje ya ukuta wa mji' (mst. 12), siyo (kama sadaka za wanyama za wanayama) ndani ya 'hekalu' (mst. 11). Kwa hiyo uchaguzi ulihitajika—au wa kwenda kwa Yesu 'nje ya kambi' (mst. 13) au wa kubaki, ndani ya mji na kuielekea hekalu kama ilivyokuwa. Kutumia lugha mbadala ya kijiografia, kule ambako mtu amejikadhi kwa hekalu lilipo mlimani au mahali pa fuvu lakichwa'? Tofauti ya haya mawili ipo wazi. Mfumo mpya wa kumwendea Mungu ameuanzisha ; lazima uchaguzi ufanyike.'' (Walker 1996: 206-7) Rejea katika **mst. 13** to *"Maana wanyama wale ambao damu yao huletwa ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa 'nje ya kambi'"* imechkuliwa kutoka desturi iliyokuwa sehemu ya ibada ya Siku ya Upatanisho (tazama **Law 16:14-15, 27**). Kama tulivyoona katika **Ebr 2:17; 7:11; 8:3;** na **9:23—10:18**, Siku ya Upatanisho ilikuwa ni mfano wa Kristo naye amekwisha kutimiza hilo kwenye dhabihu yake msalabani. Rejea ya mstariwa 14 ya kutokuwa na "*mji udumuo"* hapa duniani lakini "*tunautafuta mji ule ujao"* inaturejesha kwa Ibrahimu amabye alikuwa akitafuta "*mji amabao misingi mwenye kuibuni na kuujenga ni Mungu"* (**Ebr 11:10**), yaani, mji ambao Mungu ametuandalia (**Ebr 11:16**), *"Yerusalemu ya Mbinguni"* (**Ebr 12:22**).

Tofauti kati ya mfumo wa Agano la Kale na Agano Jipya ipo wazi. Vyakula vya ibada za Agano la Kale vilikuwa vya kidunia na havikuwa vya kudumu; chakula chetu kipya cha Agano ni Yesu mwenyewe, kinadumu milele (**Yoh 6:48-58**). Dhabihu za wanayama za Agano la Kale zilikuwa za muda mfupi na hazikuweza kuwabadilisha watu ndani yao (**Ebr 9:9**); Dhabihu ya Kristo mwenyewe inadumu na hutuosha dhamiri zetu (**Ebr 9:14**). Hema ya Agano la Kale na hekalu ni majengo ya kimwili; Kristo na Kanisa ni madhabahu ya kweli idumuyo milele na ni hekalu la Mungu (**Yoh 1:14; 2:19-22** [Kristo "ameweka makao katikati yetu" naye ni hekalu la kweli]; **1 Kor 3:16, 17a, 17b; 2 Kor 6:16a, 16b; 2 Thes 2:4; Ufu 3:12; 7:15; 11:1, 19** [kanisa ni ''hekalu la Mungu'' la kweli]; **Efe 2:21; 1 Pet 2:5;** and **Ufu 13:6** [kanisa ni *"hema yake"*]). Katika Agano la Kale, dhabihu za wanyama zilitolewa mara kwa mara, lakini hazikuweza kuondoa dhambi (**Ebr 10:11**); Kristo alijitoa mwenyewe kuwa dhabihu moja kwa ajili ya kutupatanisha kwa ajili ya dhambi zetu (**Ebr 10:12**). Sasa, katika Agano Jipya, aina mpya ya dhabihu inahitajika. Nayo ni *"dhabihu za shukrani kwa Mungu"* (**mst. 15**). Hiyo dhabihu ya sifa inatakiwa itolewe "*kwa njia Yake"* na inatakiwa itolewe "daima." Ni *"matunda ya midomo yetu kumtolea shukrani kwa jina lake."* Ukweli kuwa sifa ni "tunda" la midomo inaonyesha kwamba imetokea moyoni mwa mwamini na inaonyesha tabia ya mwamini (ona **Mt 7:17-20; Lk 6:43-45**). **Mstari wa 16** inapanua maelezo kuhusu "dhabihu" kwa kuongezea *"msiache kutenda mema na kushirikiana*." Kanisa la kwanza lilidhihirisha hili. **Mdo 4:32-35** inaeleza, *"[32] Na [x] jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. [33] Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote. [34] Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa [35] wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji."* Kwa kifupi, Maisha yetu kwa ujumla yamewekwa mfumo mpya. Haitakiwa maisha yawe tena chini ya desturi kutoka nje yetu. Badala yake, Maisha yanatakiwa yatawaliwe na desturi zilizo ndani yetu ambazo tunazidhihirisha nje yetu kwa hiari ya mioyo yetu na kudumu kufanya, kwa shukrani na sifa kwa Mungu, kwa midomo yetu na kwa matendo.

Mstari wa 17-19 inamalizia sehemu hii kwa maelekezo ya kitume na ya kibinafsi. Mstari wa **17** unarejea kwenye mada ya viongozi wa kanisa. Wakati mstari wa **7** umeongelea juu ya wale ambao mwanzoni waliwafundisha waumini wa kiebrania, mstari wa 17 unaongelea kuhusu viongozi waliopo wakati huo. Msemo

"wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu" inaakisi **Yak 3:1**, *"Ndugu zangu msiwe waalimu wengi, mkijua ya kuwa mtapata hukumu kubwa zaidi."* Uongozi wa kanisa, ukisimama na wajibu wake mkuu wa kufundisha na kufundisha na kuongoza kwa kuwa vielelezo, ni wa muhimu sana (tazama **Mdo 13:1; Rum 12:6-7; 1 Kor 12:28; Efe 4:11-12**). Kanisa linakuwa na nguvu na uzuri kwa kadiri ya nguvu na uzuri wa uongozi wake. Uongozi ukifanyika vibaya au kwa nia mbaya, viongozi wanaweza kuleta upotofu ndani ya kanisa kuwapotosha wengi. Maonyo kuhusu wajibikaji wa viongozi katika **Ebr 13:17** na **Yak 3:1** yanaendana na kanuni zilizoelezwa na Yesu katika **Lk 12:48**, *"Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi."* Katika **Mk 12:38-40** Yesu alitumia kanuni ile kwa waandishi wa Kiyahudi ambao walikuwa wanahamasishwa na nafasi yao ya mamlaka na kanzu zao ndefu, kupewa salamu za heshima sokoni, na kuketi kwenye viti vya heshima kwenye masinagogi na mahali pa heshima karamuni. Wanatumia nafasi zao *"kula kwenye nyumba za wajane"* Kwa maneno mengine, kama Victor Babajide Cole anavyoeleza, "Waliomba kwa ajili ya wale wasio na hatia, wasio na msaada, waliowakilishwa na wajane wasio na watetezi. Mbaya zaidi, hujaribu kuficha nia yao ovu kwa kuomba maombi marefu ya kinafiki, mbele ya watu (12:40). Yesu alionya kwamba watu watendao mambo kama haya watapata hukumu kali. Kwa bahati mbaya, maonyo haya bado yanapiga kelele hata leo. "Watu wa Mungu na wahudumu wa Injili wawe macho wasiangukie kwenye tabia hizi kwani kwa hakika zitaleta ghadhabu ya Mungu" (Cole 2006: 1193)

Maonyo ya mstari wa 17 ya kwamba kundi lazima wawape viongozi fursa ya kuongoza *"kwa furaha na siyo kwa majuto"* inawekwa wazi zaidi na mtume Paulo kwenye waraka wake kwa Fil. Paulo aliandika kutoka gerezani. Hata hivyo, aliweza kusema kwamba siku zote ana *"sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha"* (**Flp 1:4**); aliona kuwa hata katika kifungo chake aweze *"Lakini, ndugu zangu, nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili"* (**Flp 1:12**), na *"Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote, ikiwa ni kwa hila, au ikiwa ni kwa kweli, Kristo anahubiriwa; na kwa hiyo nafurahi, naam, nami nitafurahi;"* (**Flp 1:18**); na angeweza kusema haya *"hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu, nafurahi; tena nafurahi pamoja nanyi nyote."* (**Flp 2:17**). Kwa maneno mengine, hata kamamazingira ya nje ya kanisa na viongozi wa kanisa yanaweza kuwa magumu na yenye kuleta majaribu, viongozi anapokuwa wameungana na kundi, Roho Mtakatifu anaweza kuleta furaha ya kweli na *"amani ya Mungu ipitayo akili zote"* (**Flp 4:7**).

Maonyo na maneno ya kutia moyo ya kuwa na furaja na ushirikiano katika umoja kati ya viongozi na kundi unahitimishwa kwa ombi katika **mst. 18-19** hili *"Tuombeeni; maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote. Nami nawasihi zaidi sana kufanya hayo ili nirudishwe kwenu upesi."* Maombi ya kundi kwa ajili viongozi wake (na viongozi kuliombea kundi) ni muhimu. Ina saidia kuweka uimara kwenye ushirika na umoja; inasaidia kusababisha tabia ya kuheshimiana; inasaidia kurejesha mahusiano yaliyopata shida.

MASWALI YA MJADALA

1. Ni kwa namna gani uwekaji wa Agano la Ibrahimu na pazia la hekalu ni ishara ya Kristo na ni kwa namna gani na hayo yalitimizwa Katika Kristo?

2. Kwa nini tunaweza kuwa na uhakika mkamilifu wa imani yetu na wokovu ikiwa tupo ndani ya Kristo?

3. Kwa nini kukusanyika kwetu pamoja (Ebr 10:25) kama kanisa ni muhimu?

4. Hali yetu ya kuendelea kutenda dhambi kwa makusudi inatoa ujumbe gani kuhusu hali yetu ya kiroho, na kwa nini *"Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi"* (Ebr 10:26)?

5. Ebr 10:32-39 inalinganisha mateso na ''thawabu kubwa'' tutakayopokea ikiwa tutastahimili katika Maisha haya imani.

- Hata ikiwa Kristo alishinda kifo, na sisi tumefanyika wana katika familia yake, kwa nini unafikiri waumini waaminifu bado wanateseka na wakati hata wanapata mateso makubwa?

- Kifungu kinaunganisha thawabu yetu kuu na kurudi kwake Yes umara ya pili na huonyesha kwamba itatokea ''kitambo kidogo.'' Tunawezaje kutazamia kurudi kwake Kristo kama kitu kitakachotokea kitambo kidogo tu wakati imeshachukua miaka 2000 tangu kifo chake na kufufuka kwake na kupaa kwake.

6. Eleza maana ya imani, kulingana na maana, maelezo, na mifano inayopatikana kwenye Waebrania sura ya 11.

7. Jadili imani ya Habili, Henoko, na Nuhu, kama ilivyojadiliwa katika sura ya 11 ya kitabu cha Waebrania, na jinsi imani yao inavyofanana na imani yako na ya watu unawaona katika kanisa?

8. Nini maana ya kutembea kwa imani na siyo kwa kuona na inatuashiria nini? Je kufanya hivyo ni rahisi au ngumu?

9. Katika Waebrania 11, baadhi "vielelezo" na "vivuli" vya Kristo vimetajwa, akihusika Habili, Safina, na Ibrahimu akimtoa Ibrahimu kama sadaka, unafikri nini kuhusu taipolojia inayopatikana hapo?

- Je taipolojia inaathirije mtazamo wako wa Biblia?
- Taipolojia wakati mwingine inaweza kutumika kwa mambo mengi Zaidi(toa mfano kama unao)?

10. Sehemu ya mwisho ya Waebrania 11 inatoa mifano ya watu waliobakia waaminifu pasipo kujali mateso na majaribu makubwa, magumu n ahata kifo na hata hawakupokea ahadi waliyopewa.

- Kwa nini unafikiri Mungu anatumia vitu hasi katika Maisha yetu?
- Kwa nini mar azote tunafikiri kwamba, tukiwa na imani, hatutakutana na mambo hayo au kama tukikutana nayo, ni ishara kwamba au hatuna imani au kwamba Mungu anatuadhibu?

11. Vikwazo husababishaje kushindwa kuvumilia katika imani na kuacha kuendelea au kuchukua mwelekeo mwingine kutoka kwenye mbio tuliyokuwanayo? Tunawezaje kushinda vikwazo hivyo?

12. Moja ya vitu vinayohimizwa kwenye sura ya 12 ni mwili wa Kristo jinsi tunavyotakiwa kusaidia kaka na dada katika Kristo kukataa dhambi na kusherehekea kurudiwa na Mungu. Tunawezaje kufanya hivyo?

13. Moja ya jinsi ya kushinda dhambi ni kuwa mkweli kuhusu dhambi kwa kaka na dada katika Kristo tunaowaheshimu na kuwaamini. Wakristo wengi hawana uhusiano wa namna hiyo na hawaungamiani dhambi wao kwa wao, hata kama tumeagizwa kufanya hivyo (Yak 5:16). Kwa nini unafikiri hali iko hivyo na tunaweza kufanya nini kukuza uhusiano huo?

14. Jadili asili ya Ufalme wa Mungu "uliotayari, na uliobado" na ukweli kwamba tayari tumekwisha kuufikia Milima Sayuni wa kweli na Yerusalemu ya Mbinguni. Kweli hizi zina matokeo gani kwa Maisha yetu?

15. Mtazamo wa Mungu kuhusu dhambi na uovu ni nini? Hiyo itasababisha tofauti gani kwenye Maisha yetu?

16. Sura ya 13 inaonyesha kazi ya imani kwa maeneo makuu ya imani katika Maisha yetu ya kila siku—ya kijamii, ya kibinafsi, nay a kidini—ikiwa ni pamoja na mahusiano yetu na waumini wenzetu na pia na wageni, kuwajali wafungwa na walioonewa, ndoa, fedha, uongozi wa kanisa, na mahusiano yetu na Mungu na maombi.
Tukijua hili, kwa nini makanisa mengi hawana mpango wa kuwafanya wanafunzi ili kuwasaidia waamini kuelewa na kuweka katika matendo imani yao katika kila eneo la Maisha? Tutafanyaje kuanzisha programu hizo?

17. Tutafanyaje ili kuonyesha upendo kwa Kristo na watu waliopo gerezani?

18. Ndoa ni uhusiano wa karibu na kwa hiyo ni uhusiano wa kiroho. Je sisi mmoja mmoja na kanisa tunaweza kufanya nini kuimarisha ndoa zetu?

19. Fedha pia ni ya kiroho. Je sisi kama mtu mmoja mmoja na makanisa tunaweza kufanya nini kuwasaidia watu wetu (na makanisa) watumie fedha zao kwa hekima zaidi na kibiblia?

20. Kuna tofauti gani kati ya tunachoamini na jinsi tunavyoaishi? Kama hivi viwili vinatofautiana hiyo inatuambia nini?

21. Jadili tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya.

22. Wakristo wote, na hasa viongozi wa kanisa, tutatoa hesabu kwa yale tunayofanya katika Maisha haya. Tutafanyaje sisi kibinafsi na makanisa kuwasaidia watu wetu, hasa hasa watu wetu, Zaidi sana viongozi wetu, ili waishi kibiblia zaidi na kuwa waaminifu kwa mafundisho yao na maisha?

- Sisi kibinafsi na makanisa tufayaje pale viongozi wanapoenda mbali na fundisho sahihi na au Maisha ya utakatifu?

V. <u>Hitimisho (13:20-25)</u>

Hitimisho hili linatoa muhutasari wa maudhui kadhaa ambayo ni muhimu katika kitabu hiki: damu; Agano jipya la milele; Ubwana wa Kristo; na umhimu wa kufanya mapenzi yake. Pia kwa mara ya kwanza, inamwita Yesu *''Mchungaji mkuu wa Kondoo''* kwa wazi inataja kuhusu kufufuka kwake.

A. Baraka (13:20-21)

[20]Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, [21]awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una yeye milele na milele. Amina.

Baraka hizi kimsingi hutoa kwa muhutasari kila ambacho ukristo humaanisha kwa ujumla. Kama tulkivyojadili kuhusu Melekzedeki **Ebr 7:1-10**, wakati Mungu ni *"ni Mungu wa amani,"* Yesu ni *"Mfalme wa Amani"* (**Ebr 9:6**), ambaye hutoa *"Amani yangu . . . siyo kama ulimwengu utoavyo"* (**Yoh 14:27**). **Efe 2:14** inaongeza, *"Yeye mwenyewe ni amani yetu."* Ni Kristo pekee ndiye anayetupa amani hiyo: Amani kati yetu na Mungu; amani na watu wengine; na amani ndani yangu. Hii inasababishwa na ukweli kwamba Mungu *"alimleta kutoka kwa wafu Mchungaji mkuu wa Kondoo,"* Yesu Kristo (tazama **Yoh 10:1-18**). Kristo kufufuka kutoka kwa wafu kumemfanya Yesu awe na thamani na aitwe *"Yesu Bwana wetu"* (yaani., Mungu alikuja duniani kama mtu) na kulifunua kwamba Baba amekubali dhabihu ya Yesu mwenyewe kwa ajili yetu kwa kuwa hajamwacha Yesu kaburini pasipo kumfufua. *"damu ya agano la milele"* inasema kuhusu Agano Jipya, ambalo Kristo alilianzisha msalabani. Na Yesu akasema, alipochukua kikombe katika KaramU ya Mwisho, when he took the cup at the Last Supper, *"Kikombe hiki kilichomwagwa kwa ajili yenu ni agano jipya katika damu Yangu''* (**Lk 22:20**). Agano Jipya ni ya milele kwa kuwa lenyewe linatoa uzima wa milele, na kamwe haitakuwa kuukuu au kukosa thamani au kuzidiwa kama ilivyokuwa na Agano la Kale la Musa (tazama **Ebr 8:8-13**). Tukijua ya kuwa tumewezeshwa *"kufanya kila tendo jema ili kufanya mapenzi yaken,"* tumekwisha kuona kwamba mtu amjiapo Kristo, yeye anapokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), Nia ya Kristo (**1 Kor 2:16**), na Roho kutoka kwa Kristo (**Ezek 36:26; Yoh 14:17**). Kwa maneno mengine, tumewezeshwa kwa njia zote, kwa moyo, nia na Roho wa Kristo mwenyewe, ili kufanya mapenzi yake. Na maelezo kuwa kwamba yeye ana *"anafanya ndani yetu kile kipendezacho machoni pake,''* inaakisi pia **Flp 2:12-13**, amabapo Paulo anaasa *"utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka; kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."* Kristo aliafanya haya yote kwa ajili yetu. Kwa hiyo siyo ajabu kuwa anamalizi baraka namna hiyo kwamba kwake *"uwe utukufu milele na milele. Amina."*

B. Maneno ya Kutia moyo (13:22)

[22]Lakini nawasihi, ndugu, mchukuliane na neno hili lenye maonyo maana nimewaandikia kwa maneno machache.

Msema huu *"neno la kutia moyo"* pia linapatikana katika **Mdo 13:15**, ikiwa na maana ya ujumbe au homilia. Kwa sababu hiyo, wachambuzi wengi huona kitabu cha Waebrania kama ujumbe uliogeuzwa kuwa waraka (k.mf., Marshall, Travis, na Paul 2002: 232-33). Pia ndio maana inaonyeshwa na ukweli kwamba kitabu hakina mwanzo uliozoeleka wa kitume(utambulisho wa mwandishi, mpokeaji, na maeno ya salamu), ingawa ina

hitimisho la kitume. Ingawa kitabu cha Waebrania ni moja ya vikitabu vikubwa vya Agano Jipya, ina "imefupishwa" ikiwa imejaa maudhui mengi inayoshughulika nayo.

C. Salamu Binafsi (13:23-25)

[23]Jueni ya kuwa ndugu yetu Tim amekwisha kufunguliwa; ambaye, akija upesi, nitaonana nanyi pamoja naye. [24]Wasalimuni wote wenye kuwaongoza, na watakatifu wote; hao walio wa Italia wanawasalimu. [25]Neema na iwe nanyi nyote.

Mwandishi wa Waebrania kwa hakika aliwajua wasomaji wake na historia yao: alijua historia yao (**Ebr 6:9-12**); jinsi walivyovumilia mateso na walivyowahurumia wafungwa (**10:32-34**); na hali ya wakati ule ya kiroho chao (**5:11-14; 12:4**). Anawaita "ndugu" (**mst. 22**) inaonyesha mwandishi aliwajua kibinafsi wasomaji wake. Kumtaja Timotheo ya kwamba ametoka gerezani, na maelezo kwamba *"nitawaona pamoja naye atakapokuja tena hivi punde"* (**13:23**) inaonyesha pia mwandishi anamfahamu pia Timotheo. Kitabu hakiweki wazi wasomaji wake wa karne ya kwanza walikuwa mahali gani. Ingawa baadhi wanasema au walikuwa Alekzandria au Yerusalemu kama mahali walipoishi wasomaji wake, viashiria vinaonyesha walikuwa Roma, na maelezo katika **mst. 24** kwamba *"wale waliotoka Italia wawasalimu"* inapendekeza kuwa washirika wake walikuwa kutoka Italia na kwamba alikuwa anawasalimia watu wa nyumbani kwao (Guthrie 1983: 27; Marshall, Travis, na Paulo 2002: 243). Kutajwa kwa "neema" ni hitimisho linalofaa kwa kujau ukweli kwamba waraka umejaa kile ambacho Mungu katika Kristo amefanya kwa ajili ya watu wake na ukweli wake neema ni misingi ya imani yetu na ukristo wenyewe.

MASWALI YA MJADALA.

1. Andika kwa muhutasari umuhimu wa Ukristo na tofauti yake na dini zingine.

2. "Mchungaji Mkuu wa Kondoo" Tunapata matokeo gani kutoka na maelezo hayo kuhusu Yesu na kwetu sisi?

3. Kwa nini kufufuka kwa Yesu Kristo ni jambo lenye umhimu mkubwa?

BIBLIOGRAFIA

"13 Reasons Why Melchizedek Was Actually the Pre-Incarnate Word of God." 2014. *The Christ Plus Zero Movement.* https://christpluszero.wordpress.com/2014/12/13/10-reasons-why-melchizedek-was-actually-the-pre-incarnate-word-of-god/.

Alexander, T. Desmond. 2008. *From Eden to the New Jerusalem: Exploring God's plan for life on earth.* Nottingham, England: Inter-Varsity.

Anselm of Canterbury. 1903. *Cur Deus Homo.* Translated by Sidney Norton Deane. Chicago: Open Court. http://www.ccel.org/ccel/anselm/basic_works.i.html.

"Any non-biblical proof of Melchizedek?" Not dated. Bible Hub. Online: https://biblehub.com/q/any_non-biblical_proof_of_melchizedek.htm.

Archer, Gleason. 1982. *Encyclopedia of Bible Difficulties.* Grand Rapids: Zondervan. http://sent2all.com/Archer-Introduction%20to%20Bible%20Difficulties.pdf.

Augustine. 1950 (reprint). *The City of God.* New York: Random House.

Bauckham, Richard. 1982. "The Lord's Day." In *From Sabbath to Lord's Day: A Biblical, Historical and Theological Investigation,* edited by D. A. Carson, 221–50. Grand Rapids: Zondervan. https://archive.org/details/fromsabbathtolor1982unse.

———. 1998. *God Crucified: Monotheism and Christology in the New Testament.* Grand Rapids: Eerdmans.

Beale, G. K. 2004. *The Temple and the Church's Mission: A Biblical Theology of the Dwelling Place of God* (NSBT 17). Downers Grove, IL: InterVarsity.

Blomberg, Craig. 2007. “Matthew.” In *Commentary on the New Testament Use of the Old Testament,* ed. G. K. Beale and D. A. Carson, 1-109. Grand Rapids: Baker Academic.

Bock, Darrell. 1992. “The Reign of the Lord Jesus Christ.” In *Dispensationalism, Israel and the Church,* ed. Craig Blaising and Darrell Bock, 37-67. Grand Rapids: Zondervan.

Bullinger, E. W. 1979. *Great Cloud of Witnesses.* Grand Rapids: Kregel.

Carson, D. A. 2000. “Reflections on Assurance.” In *Still Sovereign: Contemporary Perspectives on Election, Foreknowledge, and Grace*, edited by Thomas R. Schreiner and Bruce A. Ware, 247-76. Grand Rapids: Baker. https://media.thegospelcoalition.org/documents/carson/2000_reflections_on_assurance.pdf.

_____. “Getting Excited About Melchizedek; Psalm 110.” 2013. In *The Scriptures Testify About Me,* edited by D. A. Carson, 145–74. Wheaton, IL: Crossway.

Carson, D. A., and Douglas Moo. 2005. *An Introduction to the New Testament,* 2nd ed. Grand Rapids: Zondervan.

Clement of Rome. *First Epistle of Clement to the Corinthians.* c.95. http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.i.html.

Clowney, Edmund. 1972-73. “The Final Temple.” *Westminster Theological Journal* 35: 156-89. http://www.beginningwithmoses.org/articles/finaltemple.htm.

Cole, Victor Babajide. 2006. “Mark.” In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1171-1202. Nairobi: WordAlive.

Cross, John. 2014. “Where in the Scriptures does it say that God told Cain and Abel to bring a blood sacrifice?” Online: http://www.goodseed.com/blog/2014/01/02/where-in-the-scriptures-does-it-say-that-god-told-cain-and-abel-to-bring-a-blood-sacrifice/.

Davis, C. Truman. 1982a. “The Anatomical And Physiological Details Of Death By Crucifixion.” *New Wine Magazine.* https://thecatholicmanshow.com/55-meditations-on-the-crucifixion-of-jesus/.

———. 1982b. “A Physician Analyzes the Crucifixion.” *New Wine Magazine.* http://www.thecross-photo.com/Dr_C._Truman_Davis_Analyzes_the_Crucifixion.htm.

Demarest, Bruce. 1997. *The Cross and Salvation*. Wheaton, IL: Crossway.

DeWaay, Bob. 1998. “Hebrews 6:4-8 on Apostasy.” *Critical Issues Commentary* 49. https://cicministry.org/commentary/issue49.htm.

Didache. c.70–110. http://www.ccel.org/ccel/richardson/fathers.viii.i.html.

Dirks, Jerald. 2008. *The Cross & the Crescent.* Riyadh: International Islamic Publishing House. https://islamicbulletin.org/en/ebooks/the_cross_and_the_crescent.pdf.

Dumbrell, William. 2001. “Genesis 2:1–3: Biblical Theology of Creation Covenant.” *Evangelical Review of Theology* 25: 219–30.

Duncan, Ligon. 2013. “Jesus and Melchizedek.” *RTS*. https://rts.edu/resources/jesus-and-melchizedek/.

Eames, Christopher. 2020. “Archaeology Reveals Jerusalem’s Origins.” Armstrong Institute of Biblical Archaeology. Online: https://armstronginstitute.org/226-archaeology-reveals-jerusalems-origins.

Epistle of Barnabas. 1989. In *The Apostolic Fathers,* 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 159–88. Grand Rapids: Baker. http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01/Page_137.html.

Eusebius Pamphilus. 1890. *Ecclesiastical History.* Grand Rapids: Eerdmans. https://ccel.org/ccel/schaff/npnf201/npnf201.i.html.

Finney, Charles. 1878. *Lectures on Systematic Theology.* Edited by J. H. Fairchild. Grand Rapids: Eerdmans (Reprint).

France, R. T. 1971. *Jesus and the Old Testament.* London: Tyndale. https://archive.org/details/jesusoldtestamen0000fran.

Fritsch, Charles. 1947. “Biblical Typology.” *Bibliotheca Sacra* 104: 87–100, 214–22.

Gentry, Peter. 2010. “Daniel’s Seventy Weeks and the New Exodus.” *Southern Baptist Journal of Theology* 14: 26-44. http://www.sbts.edu/resources/files/2010/05/sbjt_v14_n1_gentry.pdf.

Gleason, Randall. 2002. “The Eschatology of the Warning in Hebrews 10:26-31.” *Tyndale Bulletin* 53: 97-120. http://www.tyndalehouse.com/tynbul/library/TynBull_2002_53_1_06_Gleason_Hebrews10Warning.pdf.

Goppelt, Leonhard. 1982. *Typos: The Typological Interpretation of the Old Testament in the New.* Translated by Donald Madvig. Grand Rapids: Eerdmans.

Greidanus, Sidney, 1999. *Preaching Christ from the Old Testament.* Grand Rapids: Eerdmans.

Grudem, Wayne. 2000. “Peerseverance of the Saints: A Case Study from the Warning Passagees In Hebrews.” In *Still Sovereign,* ed. Thomas Schreiner and Bruce Ware, 133-82. Grand Rapids: Baker.

Guthrie, Donald. 1983. *Hebrews* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

Guthrie, George. 2007. “Hebrews.” In *Commentary on the New Testament Use of the Old Testament,* ed. G. K. Beale and D. A. Carson, 919-995. Grand Rapids: Baker Academic.

Hanson, Anthony. 1965. *Jesus Christ in the Old Testament.* London: SPCK.

Hartley, Donald. 2006. “Heb 11:6—A Reassessment of the Translation ‘God Exists.’” *Trinity Journal* 27: 289-307.

Hays, Richard. 1993. “Christ Prays the Psalms: Paul’s Use of an Early Christian Exegetical Convention.” In *The Future of Christology,* edited by Abraham Malherbe and Wayne Meeks, 122–36. Minneapolis: Fortress.

Hoekema, Anthony. 1979. *The Bible and the Future.* Grand Rapids: Eerdmans.

Hurtado, Art. 1999. “Are the Persons Described in Hebrews 6:4-6 Christians?” https://bibleresourceman.wordpress.com/01-hebrews-interpretive-challenge-of-the-bible/are-persons-in-hebrews-64-6-christians/.

Ignatius. 1989. “To the Magnesians.” In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 93–97. Grand Rapids: Baker. http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.iv.html.

Jackson, Wayne. 2002. “Why Does Hebrews 8:13 Use the Present Tense?” *Christian Courier.* https://christiancourier.com/articles/why-does-hebrews-8-13-use-the-present-tense.

_____. 2025a. “Was Melchizedek the Preincarnate Christ?” *Christian Courier.* https://christiancourier.com/articles/was-melchizedek-the-preincarnate-christ.

_____. 2025b. “Was the Sabbath a Divine Requirement from the Time of Creation?” *Christian Courier.* https://christiancourier.com/articles/was-the-sabbath-a-divine-requirement-from-the-time-of-creation.

“Jesus Is Better Than Melchizedek.” 1993–1994. *Israel My Glory.* https://israelmyglory.org/article/jesus-is-better-than-melchizedek/.

Johnson, Luke Timothy. 2006. *Hebrews: A Commentary.* Louisville: Westminster John Knox.

Justin Martyr. 1994a. *Dialogue with Trypho*. In *The Ante-Nicene Fathers,* vol. 1, edited by Alexander Roberts and James Donaldson, revised by A. Cleveland Coxe, 194–270. New York: Christian Literature. Reprint, Peabody, MA: Hendrickson. http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01.viii.iv.html.

———. 1994b. *First Apology*. In *The Ante-Nicene Fathers,* vol. 1, edited by Alexander Roberts and James Donaldson, revised by A. Cleveland Coxe, 159–87. New York: Christian Literature. Reprint, Peabody, MA: Hendrickson. http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01.viii.ii.html.

Kaiser, Walter. 1995. *The Messiah in the Old Testament.* Grand Rapids: Zondervan. https://archive.org/details/messiahinoldtest0000kais.

Kassa, Tesfaye. 2006. “Hebrews.” In *Africa Bible Commentary,* edited by Tokunboh Adeyemo, 1489-1508. Nairobi: Word Alive.

Katz, Jochen. Not dated. “You are my Son, today I have begotten you.” *Answering Islam.* http://www.answering-islam.org/BibleCom/ps2-7.html.

Keller, Timothy. 2008. *The Reason for God.* New York: Dutton.

_____. 2015. *Preaching: Communicating Faith in an Age of Skepticism.* New York: Viking.

Kistemaker, Simon. 2000. “The Temple in the Apocalypse.” *Journal of the Evangelical Theological Society* 43: 433-41. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/43/43-3/43-3-pp433-441_JETS.pdf.

Koehler, Ludwig, and Walter Baumgartner. 2001. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament,* vol 1, translated and edited under the supervision of M. E. J. Richardson. Leiden: Brill. https://archive.org/details/hebrewaramaiclex0001kohl.

Ladd, George Eldon. 1977. “Historic Premillennialism.” In *The Meaning of the Millennium: Four Views,* edited by Robert Clouse, 17-40. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Lane, William. 1991. *Hebrews 1-8* (WBC 47A). Dallas: Word.

Laskaris, Ernie. 2018. “The New Atheist Sledgehammer: Like Epistemological Air Boxing.” *Themelios* 43: 434–47. https://www.thegospelcoalition.org/themelios/article/the-new-atheist-sledgehammer-like-epistemological-air-boxing/.

Laubach, Frank. 2007. *Letters by a Modern Mystic.* Colorado Springs: Purposeful Design.

Lenski, R. C. H. 1966. *The Interpretation of the Epistle to the Hebrews and the Epistle of James.* Minneapolis: Augsburg. https://archive.org/details/interpretationof0000rchl_p0v6/mode/2up.

Lincoln, A. T. 1982. “Sabbath, Rest, and Eschatology in the New Testament.” In *From Sabbath to Lord’s Day: A Biblical, Historical and Theological Investigation,* edited by D. A. Carson, 197–220. Grand Rapids: Zondervan. https://archive.org/details/fromsabbathtolor1982unse.

Lunn, Nick. 2020. *Jesus in the Jewish Scriptures.* Pontypool, Wales: Faithbuilders.

Maier, Paul. 1973. *First Easter.* New York: Harper & Row. https://archive.org/details/firsteastertrueu00maie.

Marshall, I. Howard, Stephen Travis, and Ian Paul. 2002. *Exploring the New Testament: A Guide to the Letters and Revelation.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Martin, Walter. 1985. *The Kingdom of the Cults,* revised and expanded ed. Minneapolis: Bethany.

McKnight, Scot. 1992. “The Warning Passages of Hebrews: A Formal Analysis and Theological Conclusions.” *Trinity Journal* 13: 21-59.

Menn, Jonathan. 2025. *Biblical Theology: The Story of the Christ.* Eugene, OR: Resource.

_____. 2018. *Biblical Eschatology,* 2nd ed. Eugene, OR: Resource.

Meyer, Stephen. 2021. *Return of the God Hypothesis.* New York: HarperOne.

Morris, Leon. 1981. “Hebrews.” In *The Expositor’s Bible Commentary,* vol. 12, edited by Frank Gaebelein, 399-603. Grand Rapids: Zondervan.

Motyer, Stephen. 2000. “Israel (Nation).” In *New Dictionary of Biblical Theology,* ed. T. Desmond Alexander and Brian Rosner, 581-87. Leicester, England: Inter-Varsity.

Mounce, William. 2006. *Mounce’s Expository Dictionary of Old & New Testament Words.* Grand Rapids: Zondervan.

Nelson, Richard. 2003. "'He Offered Himself': Sacrifice in Hebrews." *Interpretation* 57: 251–65.

Nelson, William. 1993. "Melchizedek." In *The Oxford Companion to the Bible,* edited by Bruce Metzger and Michael Coogan, 511–12. New York: Oxford University Press. https://archive.org/details/isbn_9780965072595.

Ngundu, Onesimus. 2006. "Revelation." In *Africa Bible Commentary,* edited by Tokunboh Adeyemo, 1543–79. Nairobi: Word Alive.

Nicole, Roger. 1975. "Some Comments on Hebrews 6:4-6 and the Doctrine of the Perseverance of God with the Saints." In *Current Issues in Biblical and Patristic Interpretation, edited by Gerald Hawthorne,* 355-64. Grand Rapids: Eerdmans.

O'Brien, Peter. 2010. *The Letter to the Hebrews.* Grand Rapids: Eerdmans.

"Original sin." Not dated. *Theopedia.* http://www.theopedia.com/Original_sin.

Owen, John. 1969. *An Exposition of Hebrews*. Marshallton, DE: National Foundation for Christian Education.

Peterson, David. 1979. "The Prophecy of the New Covenant in the Argument of Hebrews." *Reformed Theological Review* 38: 74-81.

Pink, A. W. Not dated. *An Exposition of Hebrews.* https://www.monergism.com/thethreshold/sdg/pink/An%20Exposition%20of%20Hebrews%20-%20A.%20W.%20Pink.pdf.

Piper, John. 1996. "When Is Saving Repentance Impossible?" https://www.desiringgod.org/messages/when-is-saving-repentance-impossible.

_____. 2008. "The New Birth Produces Love." https://www.desiringgod.org/messages/the-new-birth-produces-love.

Pippert, Rebecca. 1979. *Out of the Saltshaker.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Poythress, Vern. 1991. *The Shadow of Christ in the Law of Moses.* Brentwood, TN: Wolgemuth & Hyatt. Online: http://frame-poythress.org/ebooks/the-shadow-of-christ-in-the-law-of-moses/.

Rayburn, Robert. 1989. "Hebrews." In *Evangelical Commentary on the Bible,* edited by Walter Elwell, 1124-49. Grand Rapids: Baker.

Riddlebarger, Kim. 2003. *A Case for Amillennialism.* Grand Rapids: Baker.

Schnabel, Eckhard. 2002. "Israel, the People of God, and the Nation." *Journal of the Evangelical Theological Society* 45: 35-57. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/45/45-1/45-1-PP035-057_JETS.pdf.

Shayesteh, Daniel. 2004. *The Difference is The Son.* Castle Hill, NSW, Australia: Shayesteh.

Sproul, R. C. 1992. *Essential Truths of the Christian Faith.* Wheaton, IL: Tyndale. https://archive.org/details/essentialtruthso0000spro.

_____. 2002. *Saved from What?* Wheaton, IL: Crossway. https://archive.org/details/savedfromwhat0000spro_n6f1.

Stibbs, A. M. 1970. "Hebrews." In *The New Bible Commentary,* 3rd ed., edited by D. Guthrie, J. A. Motyer, A. M. Stibbes, D. J. Wiseman, 1191-1221. Carmel, NY: Guideposts.

Stott, John. 1986. *The Cross of Christ.* Downers Grove, IL: InterVarsity. https://archive.org/details/crossofchrist0000stot/mode/2up.

Sweeney, James. 2003. "Jesus, Paul, and the Temple: An Exploration of Some Patterns of Continuity." *Journal of the Evangelical Theological Society* 46: 605-31. http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/46/46-4/46-4-pp605-631_JETS.pdf.

Taylor, Matt and Rachel. 2020. "The People and Offence of Hebrews 6:4-6." https://seekingourgod.wordpress.com/2020/04/15/the-people-and-offence-of-hebrews-64-6/#_ftnref29.

Taylor, Richard. 1985. *Ethics, Faith, and Reason.* Englewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall.

Verbrugge, Verlyn. 1980. "Towards a New Interpretation of Hebrews 6:4-6." *Calvin Theological Journal* 15: 61-73.

Waldron, Samuel. 2000. "The Eschatological Kingdom." In *Lecture Notes on Eschatology*, no pages. Online: http://www.vor.org/truth/rbst/escatology00.html.

Walker, P. W. L. 1996. *Jesus and the Holy City: New Testament Perspectives on Jerusalem.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

"Was Melchizedek a man or a type of Christ?" Not dated. *Never Thirsty.* https://www.neverthirsty.org/bible-qa/qa-archives/question/was-melchizedek-a-man-or-a-type-of-christ/.

Wells, Tom, and Fred Zaspel. 2002. *New Covenant Theology.* Frederick, MD: New Covenant Media.


Williamson, Paul. 2007. *Sealed with an Oath: Covenant in God's Unfolding Purpose* (NSBT 23). Nottingham, England: Apollos.

Wurmbrand, Richard. 1998. "Remember the Prisoners." *Voice of the Martyrs* (November).

Yarbrough, Robert. 1996. "Biblical Theology." In *Evangelical Dictionary of Biblical Theology,* edited by Walter Elwell, 61-66. Grand Rapids: Baker. http://www.biblestudytools.com/dictionaries/bakers-evangelical-dictionary/biblical-theology.html.

Zodhiates, Spiros. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament.* Chattanooga: AMG.

Mwandishi



Jonathan Menn ni mmwenyeji wa Appleton, WI, USA. Alihitimu B.A. katika Sayansi ya Siasa kutoka kwenye Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, kwa ufaulu wa uliotukuka, mwaka 1974, na kuingizwa kwenye taasisi ya heshima ya Phi Beta Kappa. Kisha akachkua J.D. kutoka Shule ya Sheria ya Cornell, magna cum laude, mwaka 1977, na kuingizwa kwenye jamii ya wanasheria wanaoheshimika wa Order of the Coif. Alitumia miaka 28 iliyofuata akifanya kazi Uwakili kwenye ofisi ya Mwanasheria wa Serikali wa Jimbo la Chicago, na baadaye mshirika katika Menn Law Firm iliyopo Appleton, WI. Aliokoka na kuwa mfuasi wa Yesu Kristo mwaka 1982. Shauku yake ya Theolojia ilimfanya aanze masomo ya Uzamili wa Divinity katika Trinity Evangelical Divinity School in Deerfield, IL. Alipata M.Div. kutoka TEDS, summa cum laude, Mwezi Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa mkurugenzi wa Afrika ya Mashariki waEquipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa Equipping Church Leaders-East Africa (**www.eclea.net**). Masomo ya kina aliyoandika juu ya Biblia yanapatikana kwenye tovuti hii **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kwa anwani hii ya barua pepe: **jonathanmenn@yahoo.com**.